# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

### Kikao cha Kwanza – Tarehe 27 Agosti, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

### KIAPO CHA UAMINIFU

Mbunge afuataye aliapa Kiapo cha Uaminifu:-

1. Mhe. Hamza S. Johari

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Spika inatolewa chini ya Kanuni ya 30(b).

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumapili tarehe 21 Julai, 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 30(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inampa Spika mamlaka ya kumwapisha Mbunge wakati hakuna Mkutano wa Bunge unaoendelea na kisha kutoa taarifa Bungeni kwenye Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge unaofuata. Hivyo, napenda kutoa taarifa kwamba Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo aliapa Kiapo cha Uaminifu siku ya Alhamisi tarehe 25 Julai, 2024 katika Ofisi Ndogo ya Bunge Jijini Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nampongeza sana Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo na kumkaribisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, namtakia heri katika utekelezaji wake wa majukumu aliyoaminiwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri leo hatupo naye hapa Bungeni, kama mnavyofahamu leo ni siku muhimu sana kwa Bunge hili lakini pia kwa Taifa hili, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile yupo kwenye uchaguzi na hivyo yeye ni mmoja kati ya watu ambao wameenda huko kuhakikisha ushindi unarudi nyumbani. Tuwaombee warudi na ushindi huo.

Pia nitumie nafasi hii kumtakia kila la heri Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile katika hiyo nafasi anayogombea ya kuwa

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)* Kanda ya Afrika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo taarifa nyingine pia ambayo inatolewa chini ya Kanuni ya 39(1) ya Kanuni zetu za Kudumu za Bunge kwamba katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ifuatayo: -

(i) Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2024 *(The Appropriation Bill 2024);* na

(ii) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 *(The Finance Bill 2024)*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii napenda kulitaarifu Bunge hili Tukufu kuwa tayari Miswada hiyo miwili imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuwa Sheria za nchi ambazo sasa zinaitwa: -

(i) Sheria ya Fedha za Matumizi Sheria (Na. 5) ya Mwaka 2024 *(The Appropriation Act (No.5) of 2024)*; na

(ii) Sheria ya Fedha, Sheria (Na. 6) ya Mwaka 2024 *(The Finance Act (No. 6) of 2024)*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hiyo ndiyo Taarifa ya Spika.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:** Hati za Kuwasilisha Mezani.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI MAALUM:**

Taarifa ya Kamati Maalum iliyoundwa kuchunguza Mgogoro wa Ardhi kati ya Mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo kikiwemo Kijiji cha Sikaungu katika Jimbo la Kwela.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill 2024)*.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024)*.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

Na. 1

**_NSSF_ Kukamilisha Makusanyo ya Daraja la Nyerere – Kigamboni**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza: -

Je, lini *NSSF* itakamilisha makusanyo ya deni la ujenzi wa Daraja la Nyerere - Kigamboni na kulikabidhi Serikalini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, ambaye sisi Watanzania wote tunaungana kumtakia kila la heri katika uchaguzi unaoendelea na tuna imani Mwenyezi Mungu ataweka mkono wake wa heri na tutashinda.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF)* ulianza rasmi uendeshaji wa Daraja la Nyerere Kigamboni mwezi Mei 2016 ambapo hadi kufikia mwezi Julai 2024 sawa na miaka tisa ya uendeshaji, jumla ya shilingi 102,018,000,000 zimekusanywa kutokana na tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi wakati wa kuanzishwa kwake, mradi utarejesha fedha za mfuko kiasi cha shilingi bilioni 344 hadi kukamilika kwake kwa kipindi cha miaka 30. Fedha hizi ni gharama za uendeshaji pamoja na ulinzi na thamani ya fedha iliyowekezwa. Hivyo, baada ya fedha hizo kurejeshwa, mradi utakabidhiwa Serikalini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, je, *NSSF* haioni ipo haja sasa ya kuendelea kujenga madaraja na barabara kwa kutumia mtindo huu kama ilivyofanya katika daraja la Nyerere? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali haioni sasa ipo haja baada ya *NSSF* kumaliza mkataba wao daraja hili likapitika na wananchi wa Temeke na Mbagala bila kutozwa chochote? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Chaurembo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, *NSSF* itaendelea kuwekeza kwenye miradi yote yenye tija na ile ambayo inaenda kulenga kutoa huduma kwa wananchi na kurahisisha maisha kwa wananchi wote na hasa katika kuangalia pia ulindaji wa thamani ya fedha ya mfuko wa wanachama wa *NSSF*. Kwa hiyo, tutaendelea kuwekeza kwenye maeneo yote ambayo yatakuwa yana tija lakini pia ambayo yatakuwa yanaenda kuhudumia wananchi walio wengi ili kuweza kuleta ule ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusiana na tozo baada ya gharama za mradi kurejeshwa na daraja hili kukabidhiwa Serikalini, hatua nyingine zitafuata na itakuwa ni mali ya Serikali na maamuzi yatafanyika kwa namna ambayo itaruhusu wananchi wote kuweza kulitumia bila kuwa na gharama, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa, lakini swali langu limejibiwa na swali la pili la Mheshimiwa mwenye swali.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukuwa fedha kwenye mifuko na kwenda ku-*invest* maeneo ambayo aidha ulipaji wake, *return* yake inachelewa au kwenye miradi isiyokuwa na tija kabisa kama Mradi wa *Dege Beach* na kuleta usumbufu kwa wastaafu wanapotaka kuchukuwa mafao yao. Ni lini Serikali itafanya tathmini ya kina kwenye miradi yote na kugundua hasara iliyojitokeza kutokana na ku-*invest* kwenye miradi isiyokuwa na tija?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakupa uchaguzi, swali hilo linahitaji majibu ya kina, linaweza kujibiwa kama swali la msingi lakini kama unaona utataka kulijibu sasa nakupa nafasi. Lije kama swali la msingi ama unaweza kulijibu sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naweza kulijibu.

**SPIKA:** Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Ester Bulaya kwa mwongozo au angalizo ambalo amelitoa. Ni kweli tayari Serikali imeshaandaa mwongozo maalum wa namna ya kueleza Mifuko ya Hifadhi za Jamii ikiwemo pia taasisi nyingine za Serikali namna ya kuweza kuwekeza kupitia Benki yetu ya Taifa *(BOT)* na tayari mwongozo huo ndiyo unaotoa kanuni hiyo na hata kabla ya uwekezaji, hufanyika tathmini ya kuangalia mradi, lakini pia maandiko ya mradi na baadaye kwenda kwenye hatua ya kuweza kupitishwa. Kwa hiyo, zile hatua za kwenda kupitisha miradi hii inahitaji pia idhini au ithibati ya *BOT* na tumeendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia suala la *return on investment,* kuna maeneo ambayo yanalenga zaidi katika kutoa huduma na kuleta

nafuu kwa wananchi. Kwa mfano, Daraja la Kigamboni ingekuwa kama tumelenga zaidi katika faida, tungejikuta kwamba wananchi wanapata changamoto na adha ya kuhudumiwa kuliko lile lengo la Serikali la kuhakikisha kuna *social welfare* katika jamii.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea pia kuweka miradi ambayo inaleta tija na miradi yote ambayo tunaendelea nayo imefanyiwa tathmini ukiacha mabadiliko mbalimbali ya hali za kiuchumi na kifedha ambazo zinatokea duniani kote.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu suala la tathmini, tayari tumeendelea kufanya tathmini na tunayo sheria ambayo inaongoza, tunafanya *actuarial evaluation* kila wakati, kila baada ya miaka mitatu. Kwa hiyo, suala la tathmini nalo pia linatupa mwongozo wa kujua changamoto zilizopo au changamoto ambazo zinaweza zikaja kutokea katika uwekezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kuhusiana na kwamba wanacheleweshewa malipo. Sheria ya *NSSF* inaeleza malipo ya mstaafu yatalipwa ndani ya siku 60 na tumeshaanza kulipa hata chini ya siku 10 kwa kupitia mifumo mbalimbali ya TEHAMA. Kwa hiyo, *NSSF* tumeshaboresha mambo mengi na kwa sasa changamoto za ulipaji hazipo tena.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinazowekezwa siyo sehemu ya fedha ambazo zinaenda kulipa wastaafu. Kwa hiyo, mstaafu wakati wowote atakapokuwa tayari amestaafu ndani ya siku 60, sheria inaelekeza tunakuwa tumeshamlipa mafao yake na tumeshafanya hivyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Ujenzi wa Uzio katika Kituo cha Afya Pasua – Moshi**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga uzio katika Kituo cha Afya Pasua Manispaa ya Moshi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi na Mfuko wa Jimbo imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa Kituo cha Afya cha Pasua. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 hadi 2023/2024, jumla ya shilingi milioni 16 zilitolewa na kujenga kipande cha urefu wa mita 65 kati ya urefu wa mita 242 wa uzio huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Manispaa ya Moshi imetenga shilingi milioni 25 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa uzio huo. Aidha, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Moshi itaendelea kutenga bajeti ya ujenzi wa uzio huo hadi utakapokamilika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa, Mfuko wa Jimbo ulipeleka shilingi milioni saba ukaendelea kujenga uzio huo na ikawapa wananchi matumaini makubwa sana kutokana na changamoto iliyopo katika kituo hicho cha afya kwa wagonjwa kuibiwa nguo wakati wameanika, chupa za chai pamoja na simu.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha ili kumaliza changamoto hii ya ujenzi wa kituo hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vituo vyetu hivi vya afya vinakuwa na usalama, ikiwemo kujenga uzio kwa ajili ya kuzuia changamoto ambazo Mheshimiwa Mbunge amezisema.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini kwa kupeleka fedha za Mfuko wa Jimbo pia na Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi kwa kuendelea kupeleka fedha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeshaelekeza Manispaa ya Moshi, wataendelea kutenga fedha kwa awamu na kuhakikisha kwamba uzio huu unakamilika mapema sana iwezekanavyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe maswali yawe mafupi, unaenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Noah Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa uzio katika hospitali ya Wilaya ya Olturumet?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilishapeleka fedha kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa Hospitali ya Halmashauri ya Arumeru kwa maana ya hospitali ya Olturumet na ninafahamu kwamba kuna uhitaji wa ujenzi wa uzio. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunakamilisha kwanza yale majengo kwa ajili ya kutoa huduma za jamii kwa wananchi na baada ya hapo tutakwenda na mpango wa kujenga uzio katika hospitali ile, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Temi kilichopo Arusha Mjini kimezungukwa na makazi ya watu na hivyo kuondoa faragha na usalama wa wagonjwa. Je, ni lini Serikali itajenga uzio katika kituo hiki cha afya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa nchi Ofisi ya TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha kuanza kutenga fedha ya mapato ya ndani kwa awamu, kwa ajili ya kujenga uzio katika kituo hicho cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Serikali mna mpango gani wa haraka wa kujenga uzio kwenye Kituo cha Afya Nkomolo kinachohudumia zaidi ya Kata tano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kujibu katika majibu yangu ya msingi, Serikali iliweka utaratibu wa kujenga vituo hivi vya afya kwa awamu kwa kuanza na ujenzi wa miundombinu ambayo itasaidia kutoa huduma za afya kwa wananchi na baadaye kwenda kwenye hatua za kujenga uzio kwa ajili ya usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunatambua uhitaji wa uzio katika kituo kile cha afya, na kwa sababu tumeshakamilisha

kwa kiasi kikubwa ujenzi wa miundombinu ya huduma, tutakwenda kuanza ujenzi wa uzio huo ili kuongeza usalama wa kituo kile.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Tabora Manispaa, Kata ya Mbugani, wananchi wa Kata hiyo wameanzisha ujenzi wa zahanati. Je, Serikali itakuwa tayari kwenda kuwa-*support* kumalizia boma lao kwa sababu kuna *population* kubwa na hakuna zahanati wala kituo cha afya katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia vituo vya afya na zahanati ikiwemo katika Manispaa ya Tabora. Naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya Kata hiyo ya Mbugani ili tufanye tathmini ya kuona ni kiasi gani cha fedha kinahitajika na kuona kama tunaweza tukapata fedha kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri, mapema iwezekanavyo fedha ipelekwe kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati hiyo. Kama hatutaweza kupata kupitia mapato ya ndani, basi Serikali Kuu tutatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha zahanati hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Je, ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika kila Jimbo ili Kata ya Kiborloni iweze kupata kituo cha afya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali ilishaweka mpango wa kujenga kituo cha afya katika kila Jimbo na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge walioorodhesha maeneo yao ya kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya ikiwemo Jimbo la Moshi Mjini kwa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba dhamira ya Serikali iko pale pale kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vya afya katika Majimbo yote na hatua iliyopo kwa sasa ni kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba Abass, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, kwa kuwa sasa ujenzi wa vituo vya afya na zahanati inaonekana changamoto ni uzio: Je, haioni haja kwamba kuanzia sasa vituo vyote vipya vitakavyojengwa pamoja na zahanati mpya zitakazojengwa sehemu ya uzio iwe ni sehemu ya ujenzi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika michoro na *design* za vituo vya afya, zahanati na hospitali za Wilaya, pamoja na majengo ya huduma za afya, uzio ni sehemu ya mchoro huo. Kwa hiyo, Serikali ilishaweka mpango wa kuhakikisha kwamba tunajenga uzio katika vituo hivyo, lakini tunaweka vipaumbele kipaumbele cha kwanza ni kukamilisha miundombinu ya huduma ili wananchi waweze kupata huduma za afya katika vituo na zahanati hizo na baadaye tunakwenda kwenye hatua ya ujenzi wa uzio.

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tutakwenda kwa awamu baada ya kukamilisha miundombinu ya huduma, tutakwenda kwenye ujenzi wa uzio kwa ajili ya kuongeza usalama, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 3

**Kituo cha Afya Mgombezi –** ***Korogwe TC***

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza: -

Je, lini Kituo cha Afya cha Mgombezi Korogwe *TC* kitapatiwa fedha iliyobaki shilingi milioni 250 ili kumalizia ujenzi wa kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali iliipelekea Halmashauri ya Mji wa Korogwe shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuipandisha hadhi zahanati ya Mgombezi kuwa kituo cha afya. Fedha hizo zimejenga wodi ya wazazi na jengo la upasuaji ambapo jengo la Wazazi tayari limekamilika na linatumika. Jengo la upasuaji lipo katika hatua ya umaliziaji ambapo inahitajika shilingi milioni 36 kulikamilisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mji wa Korogwe itatenga shilingi milioni 36 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la upasuaji na Serikali Kuu itatenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kituo cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Mkomole katika Halmashauri ya Korogwe Vijijini katika Halmashauri ya Korogwe Vijijini na Kata ya Pagwi katika Halmashauri ya Kilindi ni Kata ambazo ziko pembezoni sana na hakuna huduma za afya kabisa. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ambayo wananchi wameshaanza kujenga katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali imeshaweka mpango mkakati wa kujenga vituo vya afya na zahanati katika maeneo ya kimkakati na kipaumbele ikiwa ni maeneo ambayo ni magumu kufikika au maeneo ambayo yako pembezoni zaidi. Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kupokea hoja ya Mheshimiwa Mbunge, lakini nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Korogwe pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilindi kutoa kipaumbele kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ukamilishaji wa maboma hayo, lakini pia kuleta taarifa rasmi Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za wananchi katika ukamilishaji wa vituo hivyo vya huduma, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Kituo cha Afya cha Kipindimbi kitapatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi za wanaume na wanawake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, tumeanza ujenzi wa vituo vya afya kwa awamu ya kwanza ambapo tumeanza

tumejenga majengo matano kwa shilingi milioni 500, lakini awamu ya pili inayofuata ni kwenda kujenga majengo ya kulaza wagonjwa (wodi ya wanaume, wanawake pamoja na wodi ya watoto). Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ndulane kwamba, tutakapoingia awamu hiyo ya pili tutahakikisha pia tunatoa kipaumbele katika kituo hicho cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tunashukuru Serikali imetujengea vituo vya afya viwili; Magazini na Ligela na imetupatia vifaatiba vya milioni 600, lakini vituo hivyo havina watumishi wa kituo cha afya. Je, Serikali iko tayari sasa kutuletea watumishi wa kada ya afya katika vituo vya afya hivyo viwili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, baada ya ujenzi wa vituo hivyo vya huduma za afya na kupeleka vifaatiba, hatua ambayo Serikali inaendelea kuitekeleza sasa ni kupeleka watumishi wa kada mbalimbali ili waanze kutoa huduma za afya katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali inaendelea na hatua za mwisho za watumishi wa sekta ya afya zaidi ya 10,000. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Kawawa kwamba, katika ajira hizo tutatoa kipaumbele katika vituo hivyo vya afya ili watumishi wafike kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nirejee tena, nenda moja kwa moja kwenye swali. Ukileta na shukrani tena, unamaliza na muda wa wenzako kupata nafasi ya kuuliza maswali.

Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali italeta fedha za awamu ya pili kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya Nkwansira na Masama Kati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba Kituo cha Afya cha Nkwansira na Masama Kati katika Jimbo la Hai vilipewa fedha awamu ya kwanza shilingi milioni 250 na Mheshimiwa Mbunge amefuatilia sana. Nikuhakikishie, tuko katika hatua za mwisho za kupeleka fedha hizo shilingi milioni 500 katika vituo hivyo viwili; shilingi milioni 250 kwa kila kituo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatupatia pesa za kumalizia kituo cha afya katika Kata ya Nampungu ili majengo yale yaanze kutumika kabla ya kuchakaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Nampungu kilipokea fedha za Serikali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali na naomba nitumie fursa hii kuchukua hoja ya Mheshimiwa Mbunge, nione tufanye tathmini katika *level* ya Wizara ili kuona majengo yale yanahitaji kiasi gani cha fedha. Vilevile nimwelekeze Mkurugenzi wa Tunduru kutuletea taarifa rasmi kwamba kituo hicho ili kikamilike kinahitaji fedha kiasi gani ili tuweze kuona namna ya kupata fedha hiyo mapema kwa ajili ya kwenda kukamilisha majengo hayo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mansoor.

**MHE. SHARIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Spika, kituo cha Kikubizi kimeshakamilika na leo kina miezi miwili, lakini tunasubiri vifaatiba. Lini *MSD* wataleta vifaatiba kwa kuwa fedha zimeshapelekwa Halmashauri, lakini vifaatiba havijafika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, amepeleka fedha za vifaatiba kwenye Halmashauri zote 184 kote nchini, zaidi ya bilioni 280 ziko katika Halmashauri zetu na baadhi ya vifaatiba vimeshapelekwa kutoka MSD. Pia baadhi ya vifaatiba Bohari Kuu ya Dawa iko katika hatua za mwisho za kupeleka vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge, naomba nimhakikishie kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutafuatilia *MSD* ili kuona mapema iwezekanavyo vifaa vinafika kwa ajili ya kituo hicho cha afya, ahsante.

Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kujenga kituo cha afya Masieda Jimbo la Mbulu Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, maeneo yote ambayo yanahitaji ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati yalishaainishwa. Ikiwa eneo hilo la Masieda ni eneo la kimkakati katika Halmashauri ya Mbulu Vijijini, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwa awamu tunapeleka fedha hizo ikiwa vigezo vya kujenga kituo hicho vinakidhi, lakini ikiwa imewasilishwa jina la Kata hiyo kama ni kipaumbele katika Jimbo lake, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha afya Sangabuye kilipandishwa hadhi mwaka 1999 kutoka zahanati na kuwa kituo cha afya. Kituo hicho mpaka leo kina wodi moja ambayo inatumika na wanawake, wanaume pamoja na watoto. Je, ni lini Serikali itakamilisha miundombinu ya pale ikiwa ni pamoja na kujenga uzio? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Mabula, watoto, wanawake na wanaume wanalazwa kwenye wodi moja?

**MHE. ANGELINA S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Wanawezaje kulazwa wodi moja?

**MHE. ANGELINA S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ndivyo ilivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, napata wasiwasi, wanalazwaje wanaume na wanawake kwenye wodi moja? Yaani wameweka mapazia au ni nini?

**MHE. ANGELINA S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, katika kituo hicho cha afya unaweza ukakuta kitanda hiki amelazwa mwanamke, kitanda kinachofuata kuna mwanaume, kingine kuna mwanamke ana mtoto ndani ya wodi moja. Pia ni toka mwaka 1999 miundombinu hiyo haijakamilika na nilishauliza hilo swali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utaratibu na sera ya Wizara ya Afya, hairuhusiwi kulaza wagonjwa kwa maana ya wanawake na wanaume katika wodi moja. Kwa hiyo, kwa taarifa hii, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunaipokea taarifa kwamba kuna tatizo katika Menejimenti ya hospitali hiyo na Manispaa yenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba niichukue hoja hii mapema iwezekanavyo, kwanza nimwelekeze Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala kwa niaba ya Waziri wa Nchi,

**MBUNGE FULANI:** Halmashauri ya Ilemela.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni Halmashauri ya Ilemela; leo hii afike pale mara moja na atupatie taarifa rasmi Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kuona namna nzuri ya ku-*manage* wagonjwa katika wodi zile kwa sababu haikubaliki kulaza wanaume na wanawake katika wodi moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Manispaa ya Ilemela ina uwezo angalau wa kuanza ujenzi wa wodi. Nimwelekeze Mkurugenzi, kupitia mapato ya ndani kwa dharura, wafanye *reallocation* waanze ujenzi wakati Ofisi ya Rais, TAMISEMI ikitafuta fedha kwa ajili ya kuwaunga mkono, kwa ajili ya ujenzi wa wodi hiyo muhimu, ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu umesema unamwelekeza Mkurugenzi ili upate taarifa na kwa sababu maelezo aliyoyatoa Mbunge wa Ilemela Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula yako kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kwamba watoto, wanawake na wanaume wanalazwa kwenye wodi moja, kwa sababu hapa maswali ya nyongeza nimeshamaliza, waliosimama baadaye siwapi nafasi.

Kwa hiyo, wewe nenda, hebu ukamwulize huyu Mkurugenzi, aende hapo na nitakupa nafasi baadaye ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri. Wanalalaje hao watu wote watatu; yaani watoto, wanawake na wanaume kwenye wodi moja? Tutafutie hizo taarifa halafu mimi nitakupa nafasi ya kutoa ufafanuzi vizuri ili jambo hili likae vizuri kwenye Taarifa zetu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Nachingwea, sasa aulize swali lake.

Na. 4

**Mfumo wa Nafasi za Ajira kwa Kila Jimbo**

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Mfumo utakaowezesha kupata idadi sawa ya nafasi za ajira katika kila Jimbo badala ya mfumo wa sasa?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kwa ruhusa yako, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu katika nafasi hii kama Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nachukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma kwa namna ambavyo amenijalia na leo nimesimama mbele katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kushika nafasi hii. Naomba nitoe ahadi kwake na kwa Watanzania kwamba nitaitumikia nafasi hii nikitanguliza uadilifu, uchapakazi na maslahi ya Taifa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, nakushukuru wewe kwa miongozo yako na namna ambavyo umeendelea kutulea na Waheshimiwa

Wabunge wote kwa namna ambavyo tumekuwa tukishirikiana kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, wananchi wangu wa Jimbo la Kwela ambao wamenifanya niwepo ndani ya Bunge hili niwaahidi nitaendelea kuwatumikia na kutanguliza yale waliyokuwa wamenituma ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi naomba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nijibu swali la Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Jimbo la Nachingwea kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2008 Toleo la pili aya ya 4.2, nafasi za ajira hutolewa kwa ushindani na kwa kuzingatia sifa stahiki kwa mujibu wa miundo ya maendeleo ya utumishi wa kada husika. Vilevile nafasi za wazi za ajira hutolewa kwa kuzingatia ikama ya watumishi katika taasisi husika ambayo imejumuishwa katika mahitaji halisi yaliyopo katika taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hati idhini iliyoidhinishwa kila taasisi mahitaji ya watumishi katika taasisi moja hutofautiana na taasisi nyingine kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukubwa wa taasisi na uwingi wa majukumu. Aidha, idadi ya Taasisi za Umma zinatofautiana kwa kila jimbo; kwa misingi hiyo, idadi ya nafasi za ajira hutofautiana jimbo moja na jimbo lingine.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetoa kibali cha ajira na nafasi 47,404 za ajira mpya kwa waajiri wote ambapo kila mwajiri katika kila jimbo amepata nafasi kwa kuzingatia ikama ya watumishi katika maeneo hayo. Aidha, katika kutekeleza kibali hicho Serikali kupitia Sekretarieti ya Ajira kwa watumishi wa umma imetangaza nafasi kada ya Elimu na afya kimkoa na usaili utafanyika katika ngazi ya mkoa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nipongeze kwanza Serikali, wamesema sasa walau wameshusha kwa ngazi ya mkoa, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza: Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kutambua mahitaji ya nafasi hizi za kazi kwa kila jimbo ili kutoa msawazo sawa na baadaye kuratibiwa kitaifa ili kulinda utaifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wako vijana ambao walihitimu vyuo mbalimbali kuanzia 2015 mpaka 2020 na kwa sasa kwa kutumia mfumo hawa vijana ni kana kwamba mfumo unawakataa. Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kutoa upendeleo maalum kwa hawa vijana ambao kwa sasa kwa sababu ya umri unavyokwenda wanaachwa sasa kwenye mfumo wa ajira? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Amandus kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ametaka kujua kwamba Serikali ina mpango gani wa juu ya kushusha hizi ajira katika ngazi ya majimbo kwa maana hiyo. Bunge lako Tukufu lilitoa maelekezo kwa Serikali kwamba wahakikishe ajira hizi zinashuka katika ngazi za mikoa. Katika kutekeleza hilo na *commitment* ambayo Serikali ilitoa ndani ya Bunge hili, tayari utekelezaji huo umeanza ambao tumeanza katika ngazi ya mkoa na usaili utafanyika katika ngazi ya mkoa ambapo utahusisha Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, baadaye kwa kuwa safari ni hatua, tayari Serikali itaendelea kujipanga kwa namna ya kushuka katika ngazi ya wilaya. Kwa hiyo, nimwondolee shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekuwa ikisikiliza maelekezo ya Bunge na ushauri

wa Waheshimiwa Wabunge na ushauri wake tunaupokea, tutaingiza katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ameuliza habari ya kwamba ni namna gani Serikali imejipanga sasa kuangalia wale waliohitimu kwa miaka ya nyuma. Ni kweli katika nyakati mbalimbali Serikali imetumia hiyo *approach* ya kuchukua wale wa miaka ya nyuma na ndani ya Bunge humu tulipata ushauri huo, lakini kiukweli ukiangalia wale wanaohitimu na namna ambavyo Serikali imekuwa ikitoa ajira nafasi zinakuwa ni chache. Kwa hiyo, ukienda kwa mtindo huo unaweza ukakuta tunakaa ndani ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka mmoja, kwa mfano waliohitimu 2015 tunakaa tunaajiri ndani ya miaka sita, kwa hiyo, tatizo litakuwa pale pale, ndiyo maana tumerejea kufuata kwenye Sera ya Ajira na Utumishi kwamba sasa waende kwenye ushindani na katika ushindani ili kuzingatia pia waliomaliza kwa miaka ya nyuma, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kwamba kama endapo waliokuwa kwenye ushindani wamefungana kwa *marks* na yule ambaye ana umri mkubwa atapewa kipaumbele, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majibu haya yamejibiwa kwa kirefu, lakini naona bado mmesimama. Mheshimiwa *Eng.* Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kumekuwa na taratibu zile kwa mfano nafasi za majeshi na vitu vingine ambavyo watoto wanapatikana kwenye maeneo yetu ya majimbo. Baada ya usaili kutoka kwenye wilaya, anafika mkoani mkoa wanawarudisha, wanaambiwa huyu ana kovu, sijui ana nini, kumekuwa na vigezo vingi sana watu wa mkoa wanadhulumu watu wa wilaya.

Mheshimiwa Spika, sasa tulikuwa tunaomba nafasi zipelekwe wilayani hasa zile ambazo hazihitaji vigezo zaidi ya *Form Four*. Wakishatoka wilayani waende moja kwa moja kwenye *training* kwa

sababu wanapofika mkoani, watu wa mkoani wanakuwa na nafasi za kuchomeka watu wao na watu wetu waliotoka kwenye wilaya wanaachwa. Tulikuwa tunaomba hilo lizingatiwe, ni hilo tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nadhani huo ulikuwa ni ushauri, kwa hiyo, utachukuliwa halafu wakaupime kwa sababu hapo mwishoni umemaliza vizuri, lakini vigezo lazima vizingatiwe. Tukisema kutakuwa hakuna vigezo kwa sababu tu watu wametoka mahali, itakuwa changamoto, ila mwishoni umemaliza kwamba unatoa ushauri wa namna ambavyo wafanye hili zoezi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri naamini umeupokea huo ushauri.

Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilitaka nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba je, wapo tayari kutoa hadharani vigezo wanavyotumia kwa vijana kupata ajira ili kuondoa usumbufu wa vijana wanaoomba ajira, kusumbua Wabunge wakidhani kwamba ukituma *message* kwa Mbunge atakuombea ajira ili wajue kwamba ajira inatolewa kwa haki na mtu atakayeomba ana sifa atapata nafasi hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ni wazi kwamba kupitia Sekretarieti ya Ajira, vigezo vyote viko wazi na kwa namna ambavyo tunafanya usaili, matokeo yanatoka wazi na wale ambao wanatokea kukosa wanapewa sababu. Hata hivyo, tumetoa fursa ya kwamba yule ambaye anadhani hakutendewa haki, amepewa fursa ya kukata rufaa. Kwa hiyo, vigezo vyote viko wazi na kila Mtanzania yuko wazi kuomba kwa kadri ya nafasi anayotaka, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tulikuwa tunajadili suala la wale vijana ambao wanajitolea kwenye shule zetu kufundisha au kutoa huduma kwenye vituo vya afya. Serikali imekuwa inaahidi kwamba itatoa kipaumbele wakati wa kutoa ajira kwa hawa wanaojitolea. Je, Serikali imechukua hatua gani angalau kuchukua kuunda kanzidata ya hawa vijana wanaojitolea? Mimi najua kwamba watu wa Jimbo la Vunjo iliwasilisha orodha ndefu tu ya vijana wanaojitolea, naomba kupewa jibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali hilo la Mheshimiwa Dkt. Kimei kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu mzuri katika ajira safari hii. Kweli vijana wanaojitolea katika sehemu zetu huko katika Serikali ni wengi, tumechukua kanzidata na tukaona kwamba suala la wanaojitolea halitakuwa *automatic,* nao wataingia kwenye mfumo wa ushindani, lakini mwishoni yule aliyejitolea atakuwa na *added advantage* ukilinganisha na yule asiyejitolea.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali inaandaa mfumo mzuri ambao tutawabaini kwanza namna ya kuwapata hao wanaojitolea na pia hawa wanajitolea wamekuwa wakifanya kazi pia kuona namna hata ya kuwapatia stahiki ili waweze kupata morali ya kuweza kujitolea. Kwa hiyo, Serikali ina utaratibu mzuri na tumeshauandaa hivi karibuni tutau-*submit*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu tatizo la ajira mpya kuhama kwenye Halmashauri zile za pembezoni limekuwa ni kubwa sana, nini kauli ya Serikali juu ya watumishi hawa ambao wanaajiriwa baada ya miaka mitatu wote wanakuwa wameondoka kabisa kwenye vituo vyao vya kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweka utaratibu mzuri kwamba mtumishi anapoajiriwa anatakiwa kukaa kwenye kituo cha kazi miaka isiyopungua mitatu. Hata hivyo, kuna taratibu mbalimbali ambazo ni miongozo kwamba hata kuomba uhamisho na sasa hivi tumeanzisha mfumo mzuri ambao waajiri wanaomba uhamisho kupitia kwenye mfumo unaitwa e-Uhamisho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge na hata katika ajira hizi tulizotangaza zimetangazwa kimkoa. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baadhi ya kada za afya hasa mikoa ile ya pembezoni zimekosa wanaoomba, nafasi ni nyingi lakini wanaoomba wamekuwa wachache hasa mikoa ya pembezoni mfano Mtwara, Kigoma na Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa waombaji wasikimbilie tu kuomba nafasi hizi sehemu za mijini kwa sababu huko kuna ushindani mkubwa. Niwaase pia waombe huko kwa sababu pia Serikali imeweka vizuri miundombinu kama vile maji na huduma nyingine za kijamii. Kwa hiyo, wasihofu kuomba ajira katika sehemu za mikoa ya pembezoni, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 5

**Serikali Kuanza Miradi Mingi Mipya**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, faida gani Serikali imepata kwa kuanzisha miradi mingi kwa wakati mmoja bila kusubiri mingine ikamilike ili kuanza mipya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiibua na kutekeleza miradi/programu mbalimbali za maendeleo kwa kuzingatia malengo na shabaha za Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Ili kuhakikisha kasi ya utekelezaji wa programu na miradi inafikia malengo na shabaha ya Mpango, katika mwaka 2024/2025 msukumo mkubwa umewekwa kwenye kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo pamoja na kukamilisha utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo hususan katika sekta wezeshi ambayo ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, miradi mipya itakayojumuishwa kwenye Mpango ni ile inayolenga kuleta matokeo ya haraka ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kuongeza wigo wa ujumuishi wa Watanzania, kuongeza uwiano wa mapato ya ndani na pato la Taifa, kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma za nje ili kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na kuongeza ajira hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali langu, kipi kimekuwa kipaumbele cha Serikali katika kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo kwa sababu miradi mingi imekuwa inaanzishwa lakini haikamiliki, lakini pengine mingine inatelekezwa na ku-*attract interest*. Mfano mdogo ni mradi wa masoko ya

kimkakati ulioko Kyerwa, Mulongo pia Nankwenda umetelekezwa kwa zaidi ya miaka 10 bila kuguswa na kufanya chochote ikiwa imefikia linta.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza. Katika miradi ambayo inachukua muda mrefu na ku-*attract interest,* lakini mingine imetelekezwa na ikiwa imekopewa fedha, ni ipi thamani ya fedha katika miradi ya namna hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, miradi hii ya kipaumbele nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mipango yote ambayo inakwenda kutekelezwa na Serikali inazingatia mambo mengi. Moja, kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi ni kuangalia ile miradi wezeshi ambayo inakwenda kuchochea maendeleo katika sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, miradi yote inayoanzishwa inakuwa imefanyiwa *study* na ina umuhimu wake na ndiyo maana imeanzishwa kwa kila eneo. Kwa hiyo, kwa mfano hili la Kyerwa nadhani labda tulifanyie ufuatiliaji wa karibu, tujue tatizo nini? Pia kuwepo na soko katika eneo la Kyerwa ni mahali pazuri kwa wafanyabiashara na wakulima kupelekeza mazao yao kwa ajili ya kwenda kuuza na wale wanaonunua kama ni jumla, basi waende wakauze rejareja katika maeneo mengine. Hii yote ni katika mnyororo wa thamani katika kuongeza thamani na kuweza kuongeza uchumi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika swali la pili, Mheshimiwa Mbunge anasema miradi imetelekezwa. Inawezekana kweli unasema imetelekezwa kwa sababu ya mtazamo unaoona, lakini hakuna mradi hata mmoja uliotelekezwa, miradi yote inategemea upatikanaji wa fedha. Sasa inapotokea kwamba kuna changamoto ya upatikanaji wa fedha, miradi hiyo inaonekana kama imesuasua au imetelekezwa lakini upatikanaji wa fedha unapopatikana basi miradi hiyo inaendelea kutekelezwa na inakwenda ku-*service* au

yale makusudi yaliyokusudiwa inapokuwa imekamilika, basi maendeleo yanakuwa yanaendelea kutokana na mahitaji ambayo yamepangwa katika mradi huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Halima James Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, moja kati ya miradi mingi ambayo inaanzishwa kwa pamoja ni miradi ya barabara. Ninavyozungumza sasa hivi barabara mbalimbali wakandarasi wameondoka *site* kwa sababu ya madeni. Hadi mwezi Machi, wakandarasi washauri waelekezi walikuwa wanaidai Serikali shilingi bilioni 913 ikiwa ni pamoja na riba ya shilingi bilioni 79.5. Kamati ya Bunge ya Bajeti ilishaishauri Serikali...

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima ni kwenye swali siyo uchangiaji, uliza swali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Serikali inadaiwa na wakandarasi kiwango cha fedha nilichokitaja pamoja na *interest* imesababisha barabara nyingi zimekwama. Ni lini mtajenga barabara kutokana na uwezo wa Serikali wa kibajeti? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mdee kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tunapitisha bajeti katika Bunge lako Tukufu na tunapopitisha bajeti, lengo la Serikali ni kwenda kutekeleza miradi yote ambayo imepitishwa katika bajeti. Hata hivyo, tatizo linapotokea kwamba kuna wakati labda fedha zinachelewa kutoka au kwa sababu moja au nyingine aidha ni ya kimfumo au sababu nyingine yoyote inasababisha miradi hiyo kusuasua na kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali tumejipanga na Serikali iko tayari kupitia Wizara ya Fedha tunakwenda kutoa fedha kwa ajili ya kulipa madeni na kwenda kuzuia yale maongezeko ya riba katika miradi mbalimbali. Kwa hiyo, tutakwenda kutoa fedha kwa wakati ili kuweza kuzuia ongezeko la riba katika mikataba mbalimbali ya wakandarasi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko makini na tunakwenda kuhakikisha miradi hiyo inakwenda kukamilika.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimeshawakumbusha kwamba maswali yawe mafupi. Waheshimiwa Mawaziri yale ya kwa niaba tulishayafuta kwenye Bunge lililopita. Ukija tu hapa mbele inajulikana umekuja kwa niaba, kwa hiyo, huna haja ya kusoma hayo, nenda moja kwa moja kwenye majibu ya swali ili kukomboa wakati wa maswali ambao tunautumia hapa ndani.

Wizara ya Nishati Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 6

**Kusambaza Vituo vya Gesi ya Magari Nchini**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza vituo vingi vya nishati ya gesi ya magari nchini baada ya Wananchi kuhamasika kutumia nishati hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kuna vituo vitano vya *CNG* vinavyofanya kazi katika Mikoa ya Dar es Salaam (Ubungo Maziwa, *TAZARA* na Uwanja wa Ndege), Pwani (Mkuranga) na Mtwara (Dangote). Aidha, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali kupitia *TPDC* inajenga vituo viwili vya *CNG* katika maeneo ya Dar es Salaam (*UDSM* na Hospitali ya Taifa Muhimbili) na Pwani kituo kimoja (*Kairuki Pharmaceuticals*, Kibaha Zegereni).

Mheshimiwa Spika, aidha, *TPDC* inaendelea na Ununuzi wa Vituo Vidogo vya kujaza *CNG* kwenye magari vinavyohamishika *(Mobile CNG Filling Stations)* ambavyo vitasimikwa katika maeneo ya Dar es Salaam vitatu; Morogoro kimoja na Dodoma viwili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta binafsi, Kampuni ya *TAQA-Dalbit* inaendelea na Ujenzi wa Kituo cha *CNG* katika Mkoa wa Dar es Salaam (barabara ya Sam Nujoma) eneo la Posta. Pia Kampuni ya *Energo* inaendelea na ujenzi wa kituo cha *CNG* eneo la Mikocheni – Dar es Salaam na Kampuni ya *BQ* inaendelea na ujenzi wa kituo cha *CNG* katika eneo la Goba – Dar es Salaam, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza: Je, Serikali kwa kuonyesha mfano ina mpango gani sasa wa kubadilisha magari ya Serikali kutoka matumizi ya mafuta kwenda gesi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili: Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kusambaza karakana ya kubadilisha mfumo wa matumizi ya mafuta kwenda kwenye matumizi ya gesi katika mikoa yote Tanzania? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusiana na mkakati wa Serikali kubadilisha magari ya Serikali kwenda kwenye mifumo ya gesi, kama Serikali kwa kweli jambo hili tunalihitaji sana kwa sababu lina manufaa makubwa sana ikiwemo kupunguza gharama na matumizi. Tumeshatafuta mtaalamu mshauri ambaye kwa sasa hivi atatusaidia kufanya *study* za kimazingira pamoja na kuweka michoro ya kihandisi ili kufanya tathmini kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma pamoja na vituo vya *GPSA* ili kujua tunaongezaje suala hili ili magari haya yakishabadilishwa mfumo yaweze kujaziwa gesi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari Serikali tumeanza kulifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusiana na karakana, kwa kweli kwa kushirikiana na sekta binafsi tunao mkakati mahsusi wa kuhakikisha mpaka itakapofika Disemba, 2025 tutakuwa na zaidi ya vituo 30.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli jambo hili kama Serikali tumelibeba kwa dhati kwa ajili ya kuendeleza jitihada za Mheshimiwa Rais za kutumia nishati safi, si tu ya kupikia bali pia katika maeneo mengine kwa ajili ya manufaa kwenye mazingira yetu na manufaa mengine ya kiuchumi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari tumeanza kwa Dar es Salaam kwa ajili ya vituo na karakana na tutafanya vivyo hivyo kwa kadiri muda unavyokwenda kwa ajili ya mikoa mingine, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge mlioko kwenye sehemu kuu ya Mawaziri waacheni Mawaziri wasikilize maswali kwanza. Kipindi cha maswali kikiisha mtaruhusiwa kuja huku, kwa sasa tulishatoa hilo katazo. Kwa hiyo, wapeni nafasi ili waweze kusaidiana kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kasi ya usambazaji wa vituo hivi ni ndogo sana ukilinganisha na hamasa iliyopo. Je, Serikali inatuambia nini...

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes, subiri.

Mheshimiwa Waziri keti, anayeuliza yuko nyuma yako, Mheshimiwa Agnes Marwa.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, kasi ya usambazaji wa vituo hivi ni ndogo sana ukilinganisha na hamasa iliyopo, je, Serikali inatuambia nini katika hili hasa katika Mkoa wa Mara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kasi ya usambazaji, ni kweli hili tuliliona na tulianza kwa kurahisisha vigezo vya kupata vibali kwa ajili ya wawekezaji binafsi ili waweze kuwekeza kwa urahisi. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tumebadilisha mifumo na kuongeza kasi kwenye kutoa leseni kwa ajili ya kuanzisha vituo ili kuzialika sekta binafsi ziweze kushiriki katika uwekezaji huu kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi kwa ajili ya kutatua changamoto ambayo tunayo, tumeagiza vituo vya kuhamishika vya gesi *(Mobile CNG Stations)* kwa ajili ya kutatua changamoto hii kwa uharaka. Vilevile tunajenga vituo zaidi ya vitano pale Dar es Salaam kwa ajili ya kuhakikisha kuwa watu wanaendelea kupata huduma hii kwa uharaka.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli tumeongeza kasi kwenye kutoa leseni kwa haraka na kwenye kujenga, sisi Serikali pia kwa kushirikiana na sekta binafsi, ili tuweze kutoa huduma kwa haraka, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, sasa aulize swali lake.

Na. 7

**Kuondoa Kero ya Umeme Visiwa vya Ukara na Ilugwa – Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa kuondoa kero ya kutokuwa na umeme wa uhakika na wa gharama kubwa kwenye Visiwa vya Ukara na Ilugwa – Ukerewe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kero ya kutokuwa na umeme wa uhakika na kupunguza gharama ya umeme katika Visiwa vya Ukara na Ilugwa, Serikali kupitia Mradi wa Gridi Imara unaotekelezwa na *TANESCO* imeanza kujenga njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovolti 132 pamoja na kujenga kituo cha kupokea na kupoza umeme chenye mashineumba mbili zenye uwezo wa *MVA* 120 katika eneo la Nansio Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa kituo hicho, visiwa vya jirani kikiwemo Kisiwa cha Ukara vitaungwa na umeme wa Gridi ya Taifa. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* imeendelea kutoa ruzuku kwa wazalishaji binafsi wa umeme wanaohudumia visiwa hivyo ili kuwapunguzia gharama za uendeshaji. Kupitia ruzuku hiyo wazalishaji hao wataweza kuboresha hali ya upatikanaji umeme katika visiwa hivyo na kuweza kupunguza bei ya kuuza umeme kwa wananchi wanaowahudumia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Visiwa vya Ilugwa na Ukara wananchi wananunua umeme kwa shilingi 1,800 kwa *unit,* mbaya zaidi wanapata umeme huo kwa saa 10 pekee, kuanzia saa tano asubuhi hadi saa tano usiku, je, Serikali ina kauli gani kuhusu kuwarahisishia maisha wananchi wa visiwa hivi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mradi wa kutoa umeme Bunda na kuongeza nguvu kuelekea Nansio, mkandarasi anachelewa kwa sababu wananchi wanaopaswa kupisha mradi huu hawajalipwa fidia, je, ni lini Serikali italipa fidia ili mkandarasi huyu aweze kuendelea na kazi yake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Visiwa vya Ukara na Ilugwa vina umeme jua ambao unapelekwa na Kampuni ya JUMEME na ni kweli wanalipa wastani wa shilingi 750 mpaka 800 kwa *unit.* Hii ni kutokana na kwamba mwekezaji yule mchana anatumia *solar* na usiku anatumia jenereta na *diesel* kuzalisha umeme. Kwa hiyo, gharama zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi ndiyo maana changamoto ya muda mrefu ni hii ya kujenga kituo cha kupooza umeme ambapo Serikali tunatumia takribani shilingi bilioni 132.5 kujenga njia ya kusafirisha umeme na kituo cha kupooza umeme Ukerewe ili kuweza kutatua changamoto ya umeme Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kipindi hiki cha muda mfupi, Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* anafanya jitihada za kuweza kutoa ruzuku ya mifumo midogo *(solar pannels)* za nyumbani ili wananchi waweze kununua kwa nusu bei na waweze kupata umeme usiku wakati tunasubiria kujenga kituo cha kupooza umeme na hii njia ya kusafirisha umeme ili viweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la fidia, tunaendelea kuwasihi wananchi waweze kuachia maeneo yao ili kuweza kutekeleza miradi wakati tunasubiri kulipwa fidia.

Niwahakikishie wananchi wote ambao wako katika miradi hii, kwamba watalipwa fidia zao na tuko katika mchakato huo ili kuweza kukamilisha fidia zao.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuwasihi wananchi, miradi hii ni kwa manufaa ya wote, waiamini Serikali, watupishe tupitishe miradi na fidia tunaendelea kuzifanyia kazi na watalipwa kwa wakati, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Visiwa vya Maisome, Kaserazi pamoja na Yodzu wana changamoto kutoka kwa mzalishaji wa umeme (JUMEME) ambapo hivi sasa nimeongea nao wananunua umeme kwa *unit* moja shilingi 2,200. Ahadi ya Serikali ilikuwa ni kupitisha umeme wa *cable* mpaka Kisiwani. Je, ahadi hiyo itatimizwa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa maeneo haya ya visiwa ambavyo amevisema Mheshimiwa Mbunge, kwa yale maeneo ambayo yako kilometa mbili kutoka pale ambapo umeme upo tutajitahidi kuanzia sasa hivi tuweze kuyafikishia umeme wa *cable*. Yale yaliyokuwa mbali kwa hatua hii ya muda mfupi tutaendelea kutoa hizi *solar pannels* za ruzuku ili wananchi waweze kupata umeme wa uhakika huku tukiendelea na mikakati ya muda mrefu ya kuwafikishia umeme, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Rex Energy* inafanya kazi ya kusambaza umeme katika visiwa vidogo vidogo saba katika Jimbo la Ukerewe, lakini mpaka sasa mradi huu unasuasua kwa sababu mkandarasi hajalipwa ruzuku. Nini kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Mkandarasi *Rex Energy* ni mkandarasi binafsi na amepewa leseni na halmashauri kwa ajili ya kufikisha umeme kwenye maeneo hayo. Utoaji wa ruzuku una vigezo na moja ya kigezo ni uwezo mzuri wa mwekezaji katika kutoa huduma. Tutajiridhisha juu ya vigezo hivi na kama mwekezaji huyu ana vigezo basi tutampatia ruzuku kwa vigezo ambavyo tunavyo, lakini kama hatakidhi vigezo tunataka tuwahakikishie kwamba tutatafuta mkandarasi mwingine ambaye ana uwezo wa kufikisha umeme katika maeneo haya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini kituo cha kupozea umeme kinachojengwa eneo la Uhuru, Wilayani Urambo kitakamilika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Kupoza Umeme cha Uhuru kimeshafikia zaidi ya 97% na kwa sasa hivi tupo katika hatua za kufanya *test* kwa kutumia jenereta huku tukisubiri *line* ya kusafirisha umeme inayojengwa na *ITDCO* ambayo imeshafikia ziadi ya 67% iweze kukamilika. Kwa hiyo, kituo kile kwa kweli kimekamilika kwa zaidi ya 97%. Tunachosubiria ni *line* ya umeme ambapo pia tunategemea hivi karibuni itakamilika na kituo hiki kuanza kufanya kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kukamilisha usambazaji wa umeme vijiji vyote 62 Wilaya ya Nyang'hwale, lakini kuna changamoto, *tranformer* hizo zimeanza kuzidiwa kwa sababu wananchi wengi wamefungua viwanda vidogovidogo, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kumwelekeza

Meneja wa *TANESCO* Wilaya ya Nyang'hwale afanye tathmini kwenye *transformer* ambazo zimezidiwa na kubadilishwa tuwekewe nyingine kubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, niwape pole wananchi wa Nyang'hwale kwa changamoto hiyo. Ninamwelekeza meneja sasa hivi wafanye tathmini kuweza kuona maeneo ambayo yanahitaji kubadilishiwa *transformer* ili wananchi wa Nyang'hwale ambao ni wazalishaji wazuri sana waweze kupata huduma na kuwasaidia katika shughuli zao za kiuchumi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swali lake.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi hii. Naomba sasa swali langu namba nane lipate majibu ya Serikali...

**SPIKA:** Subiri kidogo, Mheshimiwa Mbunge, muuliza swali yuko nyuma yako huko. Kwa hiyo, tafuta kiti upande wako uketi.

Haya, Mheshimiwa Ally Kassinge.

Na. 8

**Fidia kwa Wananchi Wanaopisha Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa Masoko**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali italipa fidia kwa wananchi 447 wanaopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa Masoko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga fedha katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi 447 wanaopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa Masoko. Taratibu za maandalizi ya malipo haya zinaendelea na pindi zitakapokamilika malipo haya yataanza kulipwa mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, suala hili nimelizungumza hapa Bungeni hii ni mara ya saba, ikiwa maswali ya msingi matatu, ya nyongeza mawili na nimechangia mara moja. Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anahitimisha Mpango na Bajeti wa mwaka 2024/2025 alizungumza masuala ya fidia kuwa yatakuwa kipaumbele. Mwaka wa fedha umeanza na hii ni robo ya kwanza: -

(a) Je, ni lini wananchi wangu hawa watalipwa fedha hizi kiasi cha shilingi bilioni 6.2?

(b) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari baada ya Bunge hili aambatane na mimi kwenda Kilwa Masoko ili tukakutane na wananchi wangu hawa tukawape majibu ya Serikali yenye matumaini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili, mara tu baada ya Bunge niko tayari niongozane na Mheshimiwa Mbunge twende huko.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, kwamba ni lini; ni mwaka huu wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake.

Na. 9

**Maboresho ya Mitaala ya Elimu**

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR** aliuliza:-

Je, maboresho mangapi ya mitaala ya elimu yamefanyika katika vipindi tofauti na nini matarajio ya mitaala mipya katika ubunifu na uvumbuzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya mitaala nchini yamefanyika katika vipindi sita tangu tupate Uhuru. Aidha, kutokana na dira na malengo ya elimu katika ngazi mbalimbali, maboresho ya mitaala ya mwaka 2023 yamejikita katika ujenzi wa umahiri wa msingi katika kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijitali, maadili na uzalendo. Hizi zote ni stadi za karne ya 21 kwa kuzingatia falsafa ya elimu ya kujitegemea. Hivyo, maudhui ya ngazi mbalimbali ya elimu yamejikita pamoja na masuala mengine kujenga ubunifu na uvumbuzi miongoni mwa wanafunzi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, swali la nyongeza.

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waiziri kwa ridhaa yako

naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Elimu ndiyo chemchem na chimbuko la wataalamu katika fani/stadi mbalimbali za kiuchumi na kwa kuwa Serikali imetumia gharama kubwa kufanya maboresho ya mabadiliko haya ya mitaala mipya.

(a) Je, ni kwa namna gani na kwa kiasi gani maboresho ya mitaala haya mapya yataleta mabadiliko katika kupunguza idadi ya utegemezi wa wataalamu wa stadi mbalimbali kutoka mataifa mbalimbali nchini?

(b) Je, ni kwa kiasi gani maboresho haya ya mitaala yatatusaidia katika kupunguza ule mfumo wa wahitimu wetu wa vyuo mbalimbali kuweza kujiajiri badala ya kuajiriwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ameir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi, kwanza kipekee tumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye amekuwa chanzo cha mabadiliko haya makubwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa maboresho ya mitaala haya ya mwaka 2023 katika ngazi mbalimbali za elimu yamezingatia mahitaji ya soko la sasa na baadaye. Kwa muktadha huo kozi mbalimbali zenye uhitaji mkubwa katika soko la ajira zimeweza kuanzishwa na Serikali hutoa mikopo katika maeneo hayo kwa vyuo vya kati na vyuo vikuu nchini. Kwa kufanya hivyo tunaamini kabisa itaweza kupunguza utegemezi wa wataalamu katika sekta mbalimbali kwenye miradi yetu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili, maboresho ya mitaala ya mwaka 2023 yamelenga kutoa elimu ya ujuzi kwa kuanzisha mkondo wa elimu ya mafunzo ya amali ambapo katika ngazi ya elimu mhitimu atakuwa amepata maarifa, stadi na ujuzi utakaomwezesha kujiajiri au kuajiriwa. Kwa hiyo, dhana kubwa katika mfumo wetu huu na mitaala yetu ya sasa inalenga hasa kumwandaa kijana au mhitimu kuhakikisha kwamba anaweza kujiajiri au akaajiriwa mahala popote, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 10

**Gharama za Kusafisha Figo**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza gharama za kusafisha figo kupitia Bima ya Afya kwa Wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bohari ya Dawa *(MSD)* inafanya jitihada za kununua vitendanishi na vifaa vinavyotumika kusafisha figo moja kwa moja kutoka viwandani ili kupunguza gharama za huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa wananchi mara utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote utakapoanza waweze kujiunga kwani ni njia pekee ya kuweza kuwasaidia kuepuka gharama za matibabu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa... aaa, naona ameketi, kwa hiyo hana swali. Mheshimiwa Mbona umesimama tena?

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru...

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naishukuru Serikali kwa hatua inayochukua. Kwa kuwa sasa Watanzania wengi wanakabiliwa na kadhia hii, je, Serikali haioni kuwa ni wakati mwafaka wa kutazama upya gharama hii ambayo kwa wiki pengine ni kati ya shilingi 600,000 mpaka shilingi 800,000 na ukifikiria kwa mwaka mzima wenye majuma 52 gharama hii hailingani kabisa na mapato ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali ina mkakati gani sasa wa kwenda kwenye ngazi ya vituo vya afya tulivyojenga ili kupunguza gharama hii na kuweza kununua vifaa pamoja na kuwaandaa wataalamu ili kupunguza gharama hii kwa Watanzania wanaopitia wakati huu mgumu wa matibabu kwa gharama hizi kubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kutizama eneo hili muhimu ambalo linawagusa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, moja, Serikali imeshaanza na ndiyo maana kama mlisikia juzi moja ya hospitali sasa hivi wameshusha zile gharama ulisikia kwamba unakuta shilingi 250,000 mpaka shilingi 300,000 kwenye maeneo mengine, sasa hivi ukienda kwenye Hospitali ya Temeke, Dar es Salaam ni shilingi 150,000. Kwa hiyo, gharama inaendelea kushuka kutokana na hatua hizi ambazo zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, kwamba twende kwenye ngazi ya zahanati na mambo mengine, kwanza suala hilo linahitaji *investment* kubwa na utaalamu. Sasa hivi tuko kwenye ngazi ya mkoa. Tutaendelea kujipanga kwa namna ya kushuka kwenye ngazi ya wilaya jinsi muda unavyokwenda, lakini kwanza tujenge uwezo kwenye ngazi ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, pia namuomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wenzangu, suala siyo tunatibuje figo mara matatizo yatakapotokea, lakini tujikite kuzingatia yale ambayo Profesa Janabi na wataalamu wengine wanasema ili tusiweze kupata matatizo ya figo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mbona unataka kutupeleka sehemu siyo. Saa hizi ni kipindi cha maswali, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Kwa kuwa magonjwa haya yasiyoambukiza ikiwemo figo, Naibu Waziri amezungumza kwamba Hospitali ya Temeke inafanya matibabu kwa shilingi 150,000/=: Kwa nini isipungue kwa Taifa zima ili na watu wa mikoa mingine waweze kuhudumiwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mwakagenda. Ni kweli lengo ni kwenda nchi nzima, lakini kwa sababu tunaendelea kwa maana ya kubadilisha vifaa kwenda kwenye vitendanishi, tuna-*rollout* nchi nzima. Bado naendelea kusisitiza, suala la magonjwa ambukizi tuzingatie maelekezo ya Profesa Janabi na wataalam wengine, hapo ndipo tutakapoweza kutoka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Madini. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 11

**Wanawake Wanaomiliki Migodi ya Madini Nchini**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Je, ni Wanawake wangapi wanaomiliki Migodi ya Madini nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, kabla sijajibu hili swali, naomba sekunde 30 tu niweze kutoa pole kwa wananchi wangu wa Jimbo la Longido wanaoishi katika Tarafa ya Enduimet, Kata ya Olmolok ambao Shule yao ya Sekondari ya Enduimet iliungua moto jana na watoto wa kike 345 sasa hawana makazi na hawana chochote. Nawahakikishia kwamba, ninashirikiana na Serikali yetu sikivu kuanzia ngazi ya Wilaya na Mkoa, tutahakikisha huduma hizo muhimu za kupata mablanketi, vitanda na magodoro zinafanyiwa kazi ili waendelee kusoma kwa amani katika shule hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pole hizo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shughuli za madini zimekuwa zikifanyika kupitia watu binafsi na kampuni ambazo ndani yake kuna wanawake na wanaume. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ilibainika kuwa, nchini kuna takribani wanawake milioni tatu wanaoshiriki katika mnyororo wa thamani wa madini.

Mheshimiwa Spika, tafiti ndogo iliyofanywa na *TAWOMA* kwa kushirikiana na Shirika letu la *STAMICO* kwa wanawake 992 katika Mikoa ya Shinyanga, Geita, Mara na Simiyu, ilibainika kuwa, wanawake 17 sawa na asilimia 1.7 wanamiliki migodi, wanawake 67 sawa na asilimia 6.8 wanamiliki maeneo ya uchimbaji. Yaani maduara katika leseni za uchimbaji madini na wanawake 855 sawa na asilimia 86.2 wanajishughulisha na kazi zinazohusiana na uchimbaji pamoja na uchenjuaji wa madini huku wanawake 53 sawa na asilimia 5.3 wanatoa huduma maeneo ya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwasimamia na kuwapatia leseni wanawake wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini ili kuongeza mchango wao kwenye sekta hii na kuimarisha uchumi wao. Wizara inaamini kuwa mwanamke akiwezeshwa, jamii nzima imewezeshwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, idadi ya wanawake milioni tatu ni ndogo sana. Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhamasisha wanawake wengi zaidi waweze kushiriki katika sekta hii?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa mikoa ambayo ina madini mengi ya kimkakati. Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuifanya Dodoma kuwa ni miongoni mwa vivutio vya wawekezaji wa madini ili kusudi wananchi wake waweze kufaidika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Fatma Toufiq kwa maswali yake mazuri sana ambayo yanalenga kuwahamasisha wanawake waingie katika sekta hii ya madini yenye kuleta tija kwa Taifa. Kwanza, kwa swali lake hili la kwanza, sisi Wizara ya Madini kupitia Taasisi ya

*STAMICO* na Tume ya Madini tumekuwa na mkakati mahususi wa kuhamasisha jamii nzima ya Watanzania wakiwemo wanawake kwa kutoa elimu na kuendelea kutenga maeneo mahsusi, kwa ajili ya vikundi vya wachimbaji wakiwemo wanawake nchini. Kwa hiyo, naendelea kumwomba awahamasishe wanawake wa Mkoa wa Dodoma nao wajiunge katika vikundi na waje Wizarani kwa sababu, tunaendelea kutenga maeneo kwa ajili yao.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, mkakati tulionao sisi kama Wizara kwa sasa hivi, kwanza ni Mheshimiwa Rais ameendelea kututuma nje katika makongamano ya kimataifa kwenda kutangaza fursa za uwekezaji katika sekta hii ya madini mkakati. Tumeendelea kuongezewa fedha, kwa ajili ya kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali nchini kubaini madini haya kwa kutumia sayansi na tekenolojia ya kisasa kama jiofizikia kupitia ule mfumo wa ndege zisizo na rubani na helikopta.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna mpango mkakati wa kuanza *high resolution airborne survey* katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Mkoa wa Dodoma ili kubaini madini hayo. Tayari Mkoa wa Dodoma unajulikana kwamba una *lithium* na shaba kwa wingi na tafiti hizi zinavyoendelea kufanyika ndivyo tutakavyozidi kubaini maeneo ili Watanzania wote wajihusishe na biashara hii yenye tija.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 12

**Kuboresha Zao la Korosho Wilaya ya Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha uzalishaji wa zao la korosho katika Wilaya ya Nanyumbu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa zao la korosho kwa uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla, Serikali imeendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya kuboresha uzalishaji wa zao la korosho nchini ikiwemo Wilaya ya Nanyumbu kwa kusimamia huduma za ugani ambapo Maafisa Ugani wote 16 wamepatiwa pikipiki ili kuhakikisha wakulima wanafikiwa kwa wakati na kupatiwa elimu stahiki, ikiwemo kanuni bora za kilimo cha korosho ikijumuisha matumizi sahihi na salama ya viuatilifu.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuendelea kuboresha kanzidata ya wakulima wa korosho na kutoa ruzuku ya pembejeo kwa lengo la kuhakikisha kipato cha wakulima kinaongezeka kwa kupunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa mipango hiyo, uzalishaji wa korosho katika Wilaya ya Nanyumbu unaendelea kuongezeka kutoka tani 15,735 mwaka 2021/2022 na kufikia tani 16,735.027 mwaka 2023/2024 na korosho zote ziliuzwa kwa daraja la kwanza.

Mheshimiwa Spika, malengo yaliyopo ni kuhakikisha uzalishaji katika Wilaya ya Nanyumbu unafikia tani 71,600 ifikapo mwaka 2030 na kuendelea kulinda ubora wa korosho hizo kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza; katika kuboresha zao la

korosho ni pamoja na kutoa bei nzuri kwa wakulima wa korosho. Je, lini Serikali itatoa bei elekezi ya zao la korosho, hasa ukizingatia kwamba msimu wa korosho unaanza tarehe 01 Septemba, mwaka huu 2024?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili: Kwa kuwa, uzalishaji wa zao la korosho ndani ya Wilaya ya Nanyumbu umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka, na hivyo kusababisha Chama Kikuu cha Ushirika kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi: Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba wakati umefika Wilaya ya Nanyumbu ikaanzisha Chama chake Kikuu cha Ushirika, ili kuwa karibu zaidi na wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, mfumo utakaotumika katika ununuzi wa korosho ni mfumo wa *TMX,* yaani soko la bidhaa kupitia *TMX*. Ukweli ni kwamba, safari hii hatutakuwa na bei elekezi isipokuwa tutakuwa na *base price,* yaani bei ya msingi ambayo itakuwa inajumuisha gharama zote ambazo mkulima alizitumia katika kuzalisha kilo moja ya korosho. Kwa hiyo, mnunuzi hatanunua chini ya hiyo *base price* kupitia mfumo wa *TMX*. Bei hiyo tutaitoa mwezi Septemba, 2024 kwa sababu, nimeshajadili na kuzungumza na Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho na amenihakikishia kwamba, atalifanya hilo mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzisha Chama cha Msingi cha Nanyumbu, maana yake inajiondoa katika Chama cha *MAMCU*. Sisi kama Wizara hatuna pingamizi na jambo hilo, isipokuwa Wilaya ya Nanyumbu wanapotaka kuanzisha chama hicho wafuate taratibu zote ikiwemo kuita Mkutano Mkuu wa Wanachama wote wajadiliane. Jukumu letu kama Wizara litakuwa ni kuwaongoza ili kufikia lengo ambalo wanalihitaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 13

**Ukarabati wa Barabara ya Masasi – Liwale Kupitia Nachingwea**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya kutoka Masasi kwenda Liwale kupitia Nachingwea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa *Eng*. Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale yenye urefu wa kilometa 175 ni miongoni mwa miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa utaratibu wa *EPC+F*. Kutokana na mabadiliko ya uchumi duniani, eneo linalohusu fedha limekuwa na changamoto ya upatikanaji. Ili kuepuka kuchelewa zaidi kwa utekelezaji wa miradi hii, Serikali imeanza kuangalia utaratibu mbadala ili mikataba iliyopo ifanyiwe mapitio yatakayowezesha miradi hii kujengwa kwa utaratibu wa kawaida wa "*design and build*" na ujenzi wake ufanyike kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kando ya barabara hiyo ya kutoka Masasi – Nachingwea – Liwale kuna nyumba zimewekewa alama za '*X*' za kijani na nyekundu: Ni nini maana ya '*X*' hizo mbili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kama kuna '*X*' moja inahitaji malipo, ni lini wananchi watapata malipo hayo kwa sababu, barabara ile wamebomolewa nyumba kwa zaidi ya miaka 10? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwenye miradi mingi ambayo tunatekeleza kuna alama za aina mbili. 'X' ya kijani maana yake ni kwamba huyu mtu ambaye ataathirika na ujenzi utakaofuata anastahili kulipwa fidia kwa sababu, ama barabara imemfuata au yuko kwenye maeneo ambayo hakuifuata barabara na kwa hiyo, anastahili kulipwa. Kama amewekewa '*X*' nyekundu maana yake yuko kwenye hifadhi ya barabara na kwa hiyo, sheria inamtaka aondoe hiyo nyumba na hastahili malipo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Kuna swali lingine na Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, swali langu moja halijajibiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, samahani. Nimejibiwa swali moja, swali la pili sijajibiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umejibu yote mawili au umejibu moja?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, aliuliza maana ya alama mbili, lakini pia, nimekumbuka alisema nyumba zimebomolewa muda mrefu.

**SPIKA:** Ndiyo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, kama kuna alama za kijani, hatuna utaratibu wa kubomoa nyumba mpaka tuwe tumemlipa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge…

**SPIKA:** Ngoja. La kwanza aliuliza zile alama zina maana gani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** La pili ni, wale waliowekewa alama wakabomolewa, nadhani kuna hoja ya fidia. Kama wana fidia, wanalipwa lini? Sasa ndiyo maana nimekuuliza, umejibu maswali yote mawili au umejibu moja? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, lile la wanalipwa lini kwa kweli, nilikuwa sijalijibu.

**SPIKA:** Haya, basi mjibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza Serikali kama mtu analipwa, hatubomoi nyumba kabla hatujamlipa na kama hilo limetokea, kama watu wamebomolewa, lakini hawajalipwa namwomba Mheshimiwa Mbunge tuweze kuonana. Ninachofahamu watakuwa wamewekewa alama '*X*' ya kijani, lakini Serikali bado haijapeleka fedha.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia kabla ya mradi kuanza tutawapelekea fedha na hatutabomoa kabla ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nassor kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 14

**Ukarabati wa Barabara ya Kongowe Hadi Mjimwema**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Barabara ya Kongowe hadi Mjimwema?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya ukarabati wa maeneo korofi katika Barabara ya Kongowe – Mjimwema – Kivukoni yenye urefu wa kilometa 25.01, hasa yale yaliyoharibika sana katika kipindi cha mvua. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 500, kwa ajili ya ukarabati wa maeneo yote yaliyoharibika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, barabara hiyo ni ya muda mrefu sana na ukarabati unaofanyika wa vipande vipande umesababisha barabara hiyo kuwa mbovu zaidi, je, Serikali haioni haja sasa ya kuijenga upya barabara hiyo, kipande cha kutoka Kongowe – Mjimwema?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Changamoto ya barabara pia, inaikumba Ilala kipande cha kutoka Mvuti – Dondwe – Magereza – Kiwamwi, Mkoa wa Pwani. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuikamilisha barabara hiyo ili kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Ukonga wanaotoka Mvuti waweze kufika Dondwe pamoja na wanafunzi wa shule za sekondari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya Kongowe – Mjimwema ni barabara ya muda mrefu na imechoka, lakini kwa sasa wakati tunatafuta fedha, moja ni kuifanyia usanifu na kuipanua kwa sababu sasa imekuwa ni barabara ambayo imekuwa na *traffic* kubwa kwa maana ya magari mengi. Kwa hiyo, tunafanya usanifu ili kuipanua, lakini wakati tunatafuta fedha hiyo, ni lazima sasa hivi tuhakikishe kwamba magari yanapita kwa kuifanyia hayo matengenezo ya kawaida ambayo ni ya lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Mvuti – Dondwe, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa sisi Wizara ya ujenzi na hasa *TANROADS*, tukitoka Chanika – Mvuti barabara yetu hasa tunayoihudumia ni ile inayoenda Mbagala. Kuanzia Mvuti – Dondwe – Magereza inahudumiwa na wenzetu wa TAMISEMI. Kwa hiyo, nina uhakika tutawasiliana ili waweze kuona namna ya kuiboresha na pengine kuiweka katika mipango ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 15

**Kuhamisha Gereza la Kihesa Mgagao, Iringa**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itahamisha Gereza la Kihesa Mgagao ili kubadili matumizi kama yalivyo maeneo mengine yaliyokuwa Makambi ya Wakimbizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Magereza itaanza kuchukua hatua za awali zikiwemo za kupima upya eneo la Magereza kwa kutenganisha eneo kwa ajili ya shule ya sekondari na gereza la Mgagao, ambapo majengo yanayotumika kama gereza yatabaki kutumika kama shule ya sekondari na gereza litajengwa katika sehemu nyingine itakayotengwa. Aidha, Serikali itatenga fedha baada ya kumaliza kupima kwa ajili ya ujenzi wa Gereza la Mgagao, ili kupisha majengo yaliyokuwa makambi ya wakimbizi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana kwa swali letu hili la leo. Je, ni kwa nini sasa hilo eneo Serikali isilikabidhi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii ili kiwe chanzo kizuri sana cha mapato na kuleta tija kwa wananchi wa eneo hilo ambao mara nyingi sana hata barabara zao hazipitiki wakati wa mvua?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuambatana nami twende mpaka Kilolo katika hilo eneo la kambi hiyo ili akajionee uhalisia wa maombi yangu ambayo yamekuwa ya muda mrefu ili wananchi waweze kupata moto kwa majibu mazuri ambayo umewapatia siku ya leo?

**SPIsKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali la kwanza ni kwamba kwa sasa mpango wa Serikali ni kuhakikisha inapima eneo hili na kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule pamoja na Gereza la Mgagao. Pia Mheshimiwa Mbunge ameleta mapendekezo na sisi kama Serikali tunayachukua tukayachakate tuone kama eneo hili litafaa kwa ajili ya kuhamia kwenye Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kwenda eneo hilo alilotaja, mimi niko tayari, baada ya Bunge tutaongozana naye kwenda kwenye eneo hilo na kuliangalia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Kudhibiti Wimbi la Wahamiaji Haramu**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kudhibiti wimbi la Wahamiaji haramu katika Mipaka ya nchi yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Serikali katika kudhibiti wimbi la wahamiaji haramu katika mipaka ya nchi ni kuimarisha doria na misako katika maeneo ya mipaka, kufanya kaguzi kwenye vizuizi mbalimbali katika barabara kuu zinazounganisha mikoa kwa mikoa, kuendesha operesheni za kuwabaini wahamiaji haramu na kuwachukulia hatua stahiki za kisheria, kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Mipaka *(e-border)* ambao unasaidia kudhibiti wageni wasio na sifa kabla hawajaingia nchini na tunaendelea kufanya vikao vya kimataifa, kikanda na ujirani mwema, kwa lengo la kupanga mipango ya pamoja ya kudhibiti uhamiaji haramu na matukio mengine ya kihalifu yanayovuka mipaka, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Othman Hija, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wahamiaji haramu bado wamekuwa wakionekana wanaingia nchini na wanapopatikana wanapelekwa katika Magereza yetu ambako wanaongeza gharama za bajeti katika Magereza yetu: Je, Serikali haioni haja ya kuwarejesha kwao mara tu wanapowakamata? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Othman, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wapo wahamiaji haramu ambao wanapokamatwa hurejeshwa kwenye nchi zao, lakini wapo ambao wakati tunafanya mawasiliano na nchi zao, huwekwa Magerezani na wapo wanaofungwa kutokana na aina ya makosa waliyoyatenda, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete, sasa aulize swali lake.

Na. 17

**Sababu Kutosafiri Nje ya Nchi Baada ya Kupata *Visa***

**MHE. OMAR ALI OMAR** aliuliza: -

Je, sababu gani zinazosababisha Wananchi ambao wamepatiwa *Visa* kwenda nje ya nchi kutosafiri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiwaruhusu wananchi kwenda nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali baada ya kukamilisha taratibu zote za kuondoka nchini. Hata hivyo, baadhi ya

wananchi wamekuwa wakizuiliwa kuondoka nchini kutokana na sababu kadha wa kadha ikiwemo sababu za kiusalama kutokana na mazuio yanayowekwa na taasisi za kiusalama, kuwa na *Visa* isiyo halali, kuwepo viashiria vya uhusika katika usafirishaji haramu wa binadamu hasa watoto wadogo na wanawake, kwa wale wanaoenda kufanya kazi nje ya nchi kushindwa kukidhi vigezo vilivyowekwa na Wizara ya Kazi na Ajira na mwisho ni kutokufuatwa kwa taratibu za kusafiri nje ya nchi kwa watumishi wa umma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Ali Omar, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha umakini katika kutoa haki ya msingi kwenye *Visa* ambazo zinatolewa na Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ipo makini sana katika eneo hilo, itaendelea kuwa makini na ninawaomba wale wote wanaoomba *Visa* kwa ajili ya kusafiri nje ya nchi, wazingatie sheria na taratibu za nchi yetu na wasijihusushe na vitendo ambavyo vitawazuia kutokusafiri nje ya nchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake; naona Waheshimiwa Wabunge wawili mmesimama, kwa hiyo, mwenye majibu ya Mheshimiwa Mbunge ni yupi kati yenu?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Tabora.

**SPIKA:** Hoja siyo Tabora, yule kule kanyoosha mkono kwamba anayo majibu ya Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

Na. 18

**Kuanzisha Kombe la Michezo la Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. AZIZA S. ALLY** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kuanzisha Kombe Maalum la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa anajitoa sana kwenye Sekta ya Michezo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sekta ya michezo nchini. Katika kuenzi mchango huo, tayari tumeelekeza vyama na mashirikisho ya michezo nchini kuona namna bora ya kuwa na kombe maalum la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ukubwa zaidi kwa michezo wanayoisimamia, lengo likiwa ni kuwa na mashindano makubwa ya Kitaifa yatakayohusisha michezo mbalimbali yatakayofahamika kama *Samia Taifa Cup* kuanzia ngazi za chini na tayari Wizara imegawa vifaa katika mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa wadau tofauti wameanzisha mashindano mbalimbali yanayotumia jina la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo ni pamoja na Ligi ya *Mama Samia Mshikamano Cup* (Mbeya Mjini); *Dr. Samia Katambi Cup* (Shinyanga); *Simiyu Samia Marathon*; *Dkt. Samia Cup* (Same); *Chato Samia Cup* (Chato); na *Samia Afya Cup* ambayo ni mashindano yanayoandaliwa na Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili *(MOI)* na kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma na binafsi na mashindano mengine mengi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa michezo iko mingi na hivi juzi tumeshuhudia Yanga imechukua shilingi milioni 30 uwanjani, je, ni mchezo gani kati ya michezo hiyo hasa ambapo Kombe la Mama litakuwa limetengewa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mama Shally hakuwa na sababu ya kuitaja Yanga, angeuliza tu moja kwa moja, lakini siyo neno. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuko katika hatua za mwishoni za mazungumzo na Kampuni ya *1xBet* ambapo tunakwenda kupata ufadhili kwa ajili ya mashindano na timu zetu mbalimbali zikiwemo Timu za Taifa. Miongoni mwa mambo ambayo tumeamua ni kwamba Ligi ya Taifa ya *Netball*, itakwenda kuitwa Ligi ya Mpira wa Pete ya *Samia Suluhu Cup*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa kwa sababu swali hili walikuwa wamesimama Waheshimiwa Wabunge wawili kuuliza, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, swali la nyongeza.

Aah, Mheshimiwa Mbunge wa nyuma yako sijui alitaka kuuliza kwa niaba yako ama! Kwa niaba ya Mheshimiwa Hawa, ahaa, haya, naambiwa umempa nafasi Mheshimiwa Esther Matiko aulize kwa niaba yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, ni kwa nini Serikali isianzishe kliniki za michezo mbalimbali ambazo zitafanyika kila mwaka kwenye wilaya zote nchini ili kuweza kuibua vipaji na kuviendeleza na kupata vijana mahiri ambao watashiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa kama vile *Olympic*? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, Serikali inazo namna kadhaa kwa ajili ya kupata vijana kwa ajili ya kuliwakilisha Taifa ikiwemo mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA, lakini wazo la Mheshimiwa Mbunge siyo baya, naomba nilichukue twende tukalifanyie kazi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Dhana ya Ushindani na Kuwalinda Watumiaji**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenganisha dhana ya ushindani na dhana ya kuwalinda watumiaji wa bidhaa na huduma nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Jafo, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kimsingi dhana ya ushindani na kumlinda mlaji zina uhusiano mkubwa kwa sababu ushindani wenye afya katika soko ni mojawapo ya njia bora ya kumlinda mlaji. Kupitia ushindani, mteja hunufaika kwa kupata unafuu wa bei, kuongezeka kwa wigo wa upana, bidhaa bora na chaguo sahihi kwa mlaji, kukuza ubunifu wa uzalishaji wa bidhaa na kudhibiti ukiritimba katika soko.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusimamia ushindani wa haki na kuwalinda watumiaji wa bidhaa na huduma hapa nchini kwa kutumia Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003 ambayo inatarajiwa kufanyiwa marekebisho katika Mkutano huu wa Bunge kwa lengo la kuongeza tija kwa watumiaji kwa kumlinda mlaji, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini hata hivyo soko letu limejaa bidhaa nyingi hafifu zisizofaa kwa watumiaji na nyingi zinatokana na udhaifu wa Sheria ya Ushindani tuliyonayo. Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa kuleta hapa Bungeni, tukatunga sheria mahsusi ya kumlinda mtumiaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namba mbili, kuzagaa kwa bidhaa hafifu hasa vinywaji, sekta ya dawa na sekta ya ujenzi, huoni kwamba Sheria ya Ushindani tuliyonayo, aidha imeelemewa au ni ya zamani sana hivyo Serikali kutunga Sheria na kutenganisha hizi dhana mbili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana kwa sababu suala la kulinda bidhaa au kumlinda mteja ni jambo la msingi, lakini hata hivyo, ombi lake la kwamba tuone namna gani ya kulinda sheria, bahati nzuri siyo muda mrefu katika Bunge hili tutakuja na sheria ambayo mwisho wa siku ni kwamba sheria hii itaona jinsi gani ya kushughulikia mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati mwingine katika suala zima la bidhaa, ukienda bidhaa za ujenzi na mambo mengine, hata

upande wa vyakula imekuwa ni changamoto kubwa. Ni imani yetu Waheshimiwa Wabunge katika mjadala wa sheria utakaokuja hivi karibuni katika Bunge hili, tutakuwa pamoja kuhakikisha kwamba tunatengeneza sheria mahsusi kabisa ambayo itasaidia kuwalinda Watanzania hasa katika kuhakikisha kwamba tunapata bidhaa zilizokuwa sahihi kwa ajili ya watumiaji, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kuna swali lingine la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 20

**Kasi ya Uboreshaji Bandari ya Dar es Salaam**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza: -

Je, Wizara ya Viwanda na Biashara imejipanga vipi kuendana na kasi ya uboreshaji Bandari ya Dar es Salaam?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara, pamoja na majukumu mengine iliyonayo, ina majukumu mahsusi ya kusimamia maendeleo ya viwanda na biashara, kuendeleza miundombinu ya viwanda na kukuza mauzo ya bidhaa nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Kuimarisha na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mahitaji ya usafirishaji wa bidhaa za mazao kwenda sehemu mbalimbali nchini na nje ya nchi;

(ii) Kuimarisha Kamati za Pamoja Mpakani na Asasi za Wafanyabiashara ili kurahisisha ukaguzi wa pamoja wa bidhaa na mazao;

(iii) Kutoa usaidizi kwa wafanyabiashara wadogo wanaonufaika na itifaki ya Soko la *EAC, SADC* na *AfCFTA* ili kuharakisha ufanyaji biashara mipakani; na

(iv) Kuanza maandalizi ya Mpango Kabambe wa Ujenzi wa Viwanda kwa Mwaka 2025/2026 hadi 2030/2031 wenye lengo la kuhamasisha uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zitasaidia kuharakisha ufanyaji wa biashara kupitia usafirishaji na kuhakikisha kwamba uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam pamoja na miundombinu mingine ikiwemo Reli ya *SGR* italeta faida kubwa za kiuchumi na kijamii hapa nchini, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali na naishukuru kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, bado kuna changamoto kubwa ya ucheleweshwaji wa mizigo bandarini. Kuna wakati unakuta zaidi ya meli 20 ziko zinasubiri kushusha mzigo. Je, Wizara hii kwa kuwa inahusika na wafanyabiashara, haioni kama kuna haja ya kukaa na *TPA* na mwekezaji kuona namna nzuri ya kutatua hii changamoto ya ucheleweshaji wa mizigo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunaipongeza sana Serikali kwa uboreshaji wa Bandari. Ukanda wa Ziwa Tanganyika tunaona kuna Bandari ya Kalema, tunaishukuru sana Serikali, lakini Wizara hii haioni kuna haja ya kuwa na mpango maalumu wa kuwaandaa wafanyabiashara vijana, wakulima na wavuvi ili kuitumia Bandari hii

ya Kalema kufanya biashara ili kuingiza pato kwa Taifa na pato la mtu mmoja mmoja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la dada yangu Mheshimiwa Sylvia Francis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hivi karibuni baada ya kupata uteuzi, niliamua kukaa na wafanyabiashara kubaini changamoto zao. Miongoni mwa jambo ambalo walibainisha ni suala hilo kwamba mizigo sasa hivi inachelewa. Hata hivyo, Serikali hivi sasa ina mchakato mpana, hili ni jambo la mpito tu, siyo muda mrefu watu wataona kuna *transformation* kubwa sana inafanyika na shughuli za usafirishaji mtaona zimeboreka sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hata juzi nilipotembelea Bandari ya Tanga, wengine wanaanza kusema sasa hivi kuna mabadiliko makubwa yanapitia katika Bandari ya Tanga. Kwa hiyo, naomba kuwahakikishia Watanzania kwamba kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Uchukuzi na Serikali kwa ujumla, siyo muda mrefu mtaona mapinduzi makubwa katika suala zima la usafirishaji wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala zima la Kalema kwamba ni jinsi gani tutahamasisha vijana kuletewa utaratibu mzuri, ni jukumu letu hili. Naomba niwaombe Watanzania kwamba, hivi karibuni tumeamua sasa kuja na mpango mkubwa sana na hasa mpango huu utahusisha makundi mbalimbali ikiwemo makundi ya vijana. Kwanza, suala zima la kuweka programu kwanza ya viwanda, lakini kuhakikisha kurahisisha mchakato wa kusafirisha mizigo maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Watanzania, hili jambo tutalibeba kwa nguvu zote na muda siyo mrefu sana mtaona tunakuja na kazi kubwa sana ya kuwasaidia Watanzania. Lengo letu

ni kwamba tufanye *reform* katika maeneo mbalimbali ambayo itawasaidia Watanzania katika viwanda na halikadhalika katika biashara na hasa katika hii milango yetu ya bandari tulizokuwanazo za baharini na katika maziwa yetu tuliyokuwanayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali, na sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele. Tutaanza na tangazo la wageni.

Tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika, kwanza ni wageni watatu wa Mheshimiwa Hamza Johari ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na hii ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, yupo Ndugu Neema Grace Johari ambaye ni mke wake, karibu sana; yupo Ndugu Saritha Johari ambaye ni mtoto wake, ahsante sana na pia yupo Ndugu Tamika Johari, naye ni mtoto wake, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hawa ni Ndugu Samwel Maneno ambaye ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, yupo Ndugu Onorius Njole ambaye ni Mwandishi Mkuu wa Serikali, yupo Ndugu Leonard Tumua, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Ndugu Buji Pambebuye, Mkurugenzi wa Mipango na Ndugu Prosper Rwegerela, Kaimu Mkurugenzi wa Uratibu na Ushauri wa Kisheria. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Sunday Hyera, Mkurugenzi wa Mikataba, Ndugu Francis Adolf, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Ndugu Leyla Muhaji, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ndugu Regina Mtagurwa, Mhasibu Mkuu, Ndugu Alfred Nyaronga, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Ndugu Proscovia Ichekweleza, Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi na Manunuzi. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine, sijui kama na wao wako Jukwaa la Spika, lakini wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria na hawa ni viongozi kutoka taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria; yupo Ndugu Eliakim Maswi ambaye ni Katibu Mkuu - Wizara ya Katiba na Sheria, ahsante sana na pia yupo Dkt. Thomas Masanja, Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ahsante sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Japhace Daudi, Mkuu wa Kitengo cha Tathmini ya Sheria Tume ya Kurekebisha Sheria, ahsante sana, yupo Ndugu Jenipher Kaaya, Mwakilishi wa Wakili Mkuu wa Serikali Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ndugu Emmanuela Mwingira, Mwakilishi wa Kabidhi Wasii *(RITA),* Ndugu Victor Kategere, Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Ndugu Bibiana Kileo, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ndugu Anjela Anatory, Mkurugenzi wa Sheria Wizara ya Katiba na Sheria, ahsanteni sana na karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, kwanza ni wageni watatu ambao ni wadau wa sekta ya utalii kutoka Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 11 wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini *campus* kuu ya Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 20 na walimu nane wa Shule ya *Kinder World Daycare and Preschool* iliyopo Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. Haya, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Lipo tangazo lingine ambalo linatoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba *TWPG* siku ya leo tarehe 27 Agosti, 2024, mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge saa 7.00 mchana kutakuwa na mafunzo ya Wabunge Wanawake wote. Kikao hicho kitafanyika Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tunaendelea na ratiba yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, naona umesimama.

## JAMBO LA DHARURA

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54 ya Kanuni zetu za Bunge. Kwa ajili ya muda naomba nisiisome.

Mheshimiwa Spika, kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio ya utekaji, upoteaji na mauaji yanayoendelea kwa watoto, wanaharakati, viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa na makundi mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili limeshazungumzwa na taasisi mbalimbali ambazo wameshafanya tathmini, Tume ya Haki za Binadamu, *TLS* pamoja na Vyama vingine vya Siasa ikiwemo CHADEMA; na kwa kuwa jambo hili lina maslahi na linaumiza Watanzania; na Bunge hili tupo kwa ajili ya hawa Watanzania; kulingana na umuhimu wake, naomba nitoe hoja hii Wabunge wenzangu waniunge mkono, Bunge hili lijadili na kutoa maelekezo kwa Serikali ili angalau Watanzania waendelee kupata haki yao ya kuishi kuliko wasiwasi ambao unaendelea hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**SPIKA:** Haya umetoa hoja kabla. Hata hivyo waliosimama hawajafika kumi.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, wametosha.

**SPIKA:** Ndiyo utaratibu wetu Waheshimiwa Wabunge. Ndiyo utaratibu wetu ulivyo kwa Kanuni za Kudumu za Bunge. Mheshimiwa Aida Khenani amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54 akieleza kwamba kuna mambo ambayo yanatokea kwenye jamii na Kanuni ya 54 inazungumzia Bunge kupata nafasi ama fursa ya kujadili jambo la dharura linalokuwa limejotokeza kwenye jamii na ambalo haliwezi kufanyiwa kazi katika utaratibu wa kawaida na kwa hivyo Bunge kutakiwa kulijadili jambo hilo ambalo linakuwa ni la dharura ili iweze kutoa aidha Bunge litoe ushauri kwa Serikali au likiazimia, basi liwe limetoa maelekezo kwa upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, wakati huo huo Kanuni ya 55 inatoa masharti ya jambo ambalo linaweza kutolewa ambapo Mheshimiwa Spika anatakiwa kuyapitia hayo masharti aone jambo lililotolewa ikiwa linakidhi hayo masharti ya Kanuni ya 55 au la.

Waheshimiwa Wabunge, mambo aliyoyataja Mheshimiwa Aida Khenani hapa, kwa ujumla wake ni mambo mazito, kwa sababu ukiongelea kupotea mtu, kutekwa mtu, kuuawa kwa mtu ni mambo mazito. Hapa ametaja kwamba kuna taasisi mbalimbali zimesema.

Mimi taasisi hizo sijazisikia, sijapitia hizo taarifa zao kuona wameeleza kwa sura ipi na hata kama ningekuwa nimezipitia ni jambo ambalo Kanuni yetu ya 55 inaeleza kwamba yale ambayo yanaweza kufanywa kwa utaratibu wa kawaida kwa sababu ni mambo ya utekelezaji, Serikali huwa inabidi ifanye kazi yake. Ni yale ambayo yanakuwa yako nje ya ule utaratibu wa kawaida ama Bunge linaona Serikali haifanyi chochote, basi inaweza kuchukua hatua hizo.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba Mheshimiwa Aida alitoa hoja kabla ya masharti ya Kanuni ya 54, acha ya Kanuni ya 55 hayajatimia, lakini nilimwacha afanye hivyo kwa sababu niliona na Wabunge wengine nao wameunga mkono, lakini Kanuni ya 54 inataka atoe maelezo, nikishajiridhisha na hii Kanuni ya 55 ndiyo nimpe nafasi atoe sasa maelezo kwa kina ili Bunge liweze kumuunga mkono kwa Wabunge 10 kusimama au la.

Hata hivyo, jambo hilo alilolieleza kuhusu utekaji, kuhusu mauaji ni mambo ambayo kama ni uchunguzi umefanyika, basi unapaswa kuwa uchunguzi umefanywa siyo na mtu kama mimi kwamba nimesimama nikasema kuna mtu sijamwona, ama nikasema kwamba kuna mtu ameuawa, kwa hiyo simjui aliyeuawa. Sasa Bunge litakuwa linaielekeza nini Serikali katika mazingira kama hayo?

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hizi nilizozisema, pamoja na uzito wa mambo haya, Serikali ichukue hatua zile zinazochukua kama zile za kawaida zinashindikana, basi iweze kuongeza nguvu kwenye kuhakikisha raia wanakuwa salama; lakini kwa maana ya kwamba ni hoja ya dharura ambayo Bunge inaweza kuijadili, Hapana, haijakidhi masharti ya Kanuni ya 55. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ester Bulaya.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba sasa hivi zoezi la uandikishaji au uboreshaji wa daftari la wapiga kura, aidha maeneo mengine yanaendelea au maandalizi yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa Jimbo la Bunda Mjini ni tofauti. Tayari vituo vya uandikishaji kwenye Kata 13 vimetoka, lakini Kata ya Nyatwali vituo vyake saba vimeondolewa. Wale wananchi hawajui

hatma yao ya msingi ya haki yao ya kikatiba ya kupiga kura, wananchi zaidi ya 7,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 walikaa kikao cha wadau wa uchaguzi pamoja na Mwandikishaji Mkuu wa Jimbo. Alichowaambia ni kwamba hawa watu wanatakiwa kuhamishwa, lakini mpaka sasa hivi hatma ya fidia yao hawajui. Hawajui Serikali watawapeleka wapi na hayo yote yamesababishwa na Serikali wenyewe, sasa wanataka kuwapoka haki yao ya kikatiba ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, hata kama wanahamishwa, itatolewa *notes* zaidi ya miezi mitatu, lakini hawa watu pia hawajalipwa na hata hiyo miezi mitatu pia ikija hata ile haki ya msingi ya kupiga kura kwenye Serikali ya Mitaa hawataweza kufanya, vile vile hawatahakiki vitambulisho vyao, na hawajui wanaenda wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, hili jambo ni *serious,* hatuhitaji wananchi wa Mara nao wagome kama Ngorongoro ili ndiyo muwape haki yao. Naomba kiti chako…

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, kwanza ni haki hawa watu kukosa haki yao ya kikatiba kwa ajili ya maandalizi ya uandikishaji wa daftari la wapiga kura kwa kuondolewa vituo vyao kwenye Kata nzima? Pili, naomba kiti chako kielekeze Serikali itoe majibu ya kina ya haki za msingi ya wananchi wa Nyatwale kwenye jambo hili. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Ester Bulaya, hakuwa amesema Kanuni lakini alivyosema Mwongozo wa Spika maana yake anasimama chini ya Kanuni ya 76 inayomruhusu Mbunge kusimama na kuomba mwongozo juu ya jambo ambalo linakuwa limetokea hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hii Kanuni ya 76 inatoa nafasi hiyo kwa sababu Spika hana uwezo wa kutoa mwongozo kwenye

kila jambo ila anao uwezo wa kutoa mwongozo kwa mambo yanayotokea hapa Bungeni, na ndiyo muktadha wa hii Kanuni ya 76. Hata hivyo, jambo alilolieleza Mheshimiwa Ester Bulaya linahusu haki ya wananchi kushiriki katika uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hili ni jambo ambalo Serikali iko hapa ndani na wamelisikia, walifuatilie kama wale wananchi watakuwa wameondoka kabla, basi waruhusiwe kule wanakopelekwa ndiyo wajiandikishe huko ili waweze kushiriki katika hii haki yao. Kama watakuwa hawajaondoka kabla ya uchaguzi, maana yake washiriki kwenye kuchagua viongozi watakaowaongoza katika kipindi hiki.

Kwa hiyo, Serikali imesikia Mheshimiwa Ester Bulaya, lakini kwenye hilo kwa mujibu wa Kanuni zetu, mimi siwezi kutoa mwongozo wowote, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu, Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati Maalum iliyoundwa Kuchunguza Mgogoro wa Ardhi kati ya Mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na Vijiji Vinavyolizunguka Shamba hilo Kikiwemo Kijiji cha Sikaungu katika Jimbo la Kwela

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wetu wa Kamati Maalum, Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya aje awasilishe taarifa ya Kamati Maalum. Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA - MWENYEKITI WA KAMATI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha muhtasari wa Taarifa ya Kamati Maalum ya Bunge ya Kuchunguza Mgogoro wa

Ardhi kati ya Mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na Wananchi wa Vijiji vinavyozunguka Shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka uliyonayo chini ya...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana, kwa taarifa hii inayosomwa hapa ikiwa ni lazima kuzungumza, basi tunaruhusiwa milango iko sita, mnatoka kidogo pale nje mnaenda kusemezana ili tusikilize maana wakati mwingine tutaanza kuzungumza mambo ambayo hayajasemwa hapa. Tumsikilize Mwenyekiti, anachosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba nianze.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha muhtasari wa Taarifa ya Kamati Maalum ya Bunge ya Kuchunguza Mgogoro wa Ardhi kati ya Mwekezaji katika Shamba la Malonje na Wananchi wa Vijiji vinavyozunguka Shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 144 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Tarehe 27 Mei, 2024 uliunda Kamati Maalum ya Bunge ya Kuchunguza Mgogoro wa Ardhi kati ya Mwekezaji katika Shamba la Malonje na wananchi wa vijiji vinavyolizunguka shamba hilo ili kushauri hatua za utatuzi. Kamati ilifanya kazi kuanzia tarehe 15 Julai, 2024 hadi tarehe 5 Agosti, 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi ya Kamati imekamilika, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu matokeo ya uchunguzi na tathmini ya mgogoro wa ardhi katika Shamba la Malonje pamoja na mapendekezo ya kutatua mgogoro huo.

Pamoja na taarifa hii, maelezo ya kina kuhusu Matokeo ya kazi ya Kamati ya kuchunguza mgogoro huu yameambatishwa.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Taarifa. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya utangulizi kwa madhumuni ya kubainisha muktadha wa kazi iliyofanyika; sehemu ya pili inabainisha matokeo ya uchambuzi ambayo ni msingi wa mapendekezo ya Kamati. Aidha, sehemu ya tatu inatoa mapendekezo ya utatuzi wa mgogoro ambayo ndiyo lengo kuu la kuundwa kwa Kamati hii na sehemu ya nne itakuwa inatoa hitimisho la taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, muktadha wa kazi iliyofanywa na Kamati, inagusa mambo makuu matatu. Jambo la kwanza ni historia fupi ya mfumo wa umiliki, usimamizi na upatikanaji wa ardhi nchini na Jambo la pili ni msingi wa Bunge kuchunguza mgogoro wa ardhi katika Shamba la Malonje. Jambo la tatu ni chimbuko la Kamati hii na njia zilizotumika katika uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Bunge Kuchunguza Mgogoro wa Ardhi katika Shamba la Malonje. Kama ilivyo kwa migogoro mingi ya ardhi, mgogoro baina ya Mwekezaji katika Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo una madhara makubwa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, mgogoro huo una athari hasi kwa Mwekezaji mwenyewe na wananchi kwa ujumla. Kwa ujumla, athari hizo zinazuia ustawi wa wananchi na Mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, linategemewa kusimamia shughuli za umma kwa namna inayozingatia maslahi ya wananchi ambao ndiyo msingi wa mamlaka nchini. Serikali inao wajibu wa kuhakikisha kuwa, shughuli zote zinalenga ustawi wa wananchi wakiwemo wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka Shamba la Malonje na wanaohusika katika uwekezaji kwenye shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Kamati Maalum. Taarifa Rasmi za Bunge zinaonesha kuwa kwa nyakati tofauti, taarifa kuhusu

mgogoro huu zimejitokeza Bungeni, wakati wa michango ya wawakilishi wa wananchi au katika maswali na taarifa za Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa kina kuhusu kujitokeza kwa taarifa juu ya mgogoro huu unapatikana katika matokeo ya kazi ya Kamati ambayo ni Kiambatisho cha Taarifa hii. Kwa ujumla, tangu mwaka 2012 hadi 2024 suala la mgogoro huu limejitokeza Bungeni zaidi ya mara 20.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande wake imekuwa ikitoa majibu na ahadi mbalimbali kuhusu kushughulikia mgogoro huu lakini kwa zaidi ya miaka 13 suluhisho halijapatikana. Mnamo tarehe 7 Novemba, 2023, Mbunge wa Jimbo la Kwela, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, aliwasilisha Bungeni hoja ya dharura akilitaka Bunge lijadili mgogoro huu, Mheshimiwa Sangu alieleza madhara yaliyowapata wananchi kutokana na mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hoja hiyo, tarehe 01 Februari, 2024, Kanisa la Efatha lilikuandikia barua kuwasilisha utetezi wake kuhusu tuhuma zilizodaiwa kutolewa na Mheshimiwa Sangu dhidi yake. Tuhuma hizo zilihusu mgogoro wa ardhi kati ya Mwekezaji kwenye Shamba la Malonje ambao ndiyo Kanisa la Efatha na Vijiji vinavyolizunguka shamba hilo. Kwa busara zako, ulilielekeza suala hili kwa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Mei, 2024 Kamati hiyo iliwasilisha kwako Taarifa ya Matokeo ya kikao chake. Kutokana na mapendekezo ya taarifa hiyo, tarehe 27 Mei, 2024 uliunda Kamati Maalum kwa ajili ya kushughulikia mgogoro wa ardhi katika shamba la Malonje. Kamati hiyo uliipa hadidu za rejea tano kama zifuatazo: -

(i) Kubaini eneo la Shamba la Malonje lilipoanzia;

(ii) Kubaini mipaka halisi ya Shamba la Malonje na vijiji vinavyozunguka shamba;

(iii) Kubaini iwapo taratibu za uongezaji wa eneo zilifuatwa katika ongezeko la ukubwa wa shamba la Malonje;

(iv) Kubaini iwapo kuna dalili za vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu vinavyodaiwa kufanywa na walinzi wa shamba la Malonje na iwapo vitendo hivyo vinatokana na miongozo ya wamiliki wa shamba; na

(v) Kubaini jambo lingine lolote linalohusiana na mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, hatua uliyoichukua ni muhimu sana na kwa kufanya hivyo, wananchi na wadau wa amani, usalama na ustawi wa wananchi wamekupongeza kwa dhati kwa kuwa uamuzi wako unaonesha kujali na kutamani wananchi wapate ufumbuzi kwa matatizo yao. Kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati hii, nitumie fursa hii kukushukuru kwa imani kubwa uliyoionesha kwetu. Pia, niungane na wananchi na wadau mbalimbali kukupongeza kwa kujali umuhimu wa kutatua mgogoro huu uliodumu kwa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mgogoro huu, wananchi wanalalamikia shamba la Mwekezaji kujumuisha maeneo ya vijiji vyao wakikosa ardhi ya kilimo na ya kuchungia mifugo yao, huku mwekezaji akilalamikia wananchi kuingilia mipaka ya shamba lake lililopimwa na akauziwa na Serikali. Ikiwa hatua za kutatua mgogoro huu hazitapatikana mapema, madhara zaidi yanaweza kutokea ikiwemo kuathiri maisha na mali za watu na kuzuia azma aliyonayo mwekezaji katika shamba hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, njia zilizotumika katika kutekeleza majukumu yake, kwanza Mapitio ya Sera, Sheria na Miongozo inayohusu masuala ya ardhi na Mapitio ya Nyaraka mbalimbali zinazohusiana na Shamba la Malonje;

Mheshimiwa Spika, pili, mahojiano na wadau mbalimbali waliobainika kuwa na taarifa, uelewa na maoni yanayoweza kufanikisha kazi ya Kamati. Wadau hawa walijumuisha walalamikaji

ambao ni wananchi wa vijiji na viongozi wao, Mwekezaji (Bodi ya Wadhamini wa Efatha), Viongozi wa Mkoa wa Rukwa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, katika *screen* ni mikutano iliyofanywa katika vijiji vinavyozunguka Shamba la Malonje.

Mheshimiwa Spika, tatu, ziara kwenye Shamba la Malonje pamoja na vijiji sita kati ya nane vinavyozunguka shamba hilo. Vijiji vilivyotembelewa ni Sikaungu, Msanda Muungano, Songambele Azimio, Mawenzusi, Ulinji na Isesa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya taarifa ni kuhusu uchambuzi na maelezo ya matokeo; Mapitio ya sera, sheria na nyaraka yalifanyika ili kufanikisha matokeo ya uchunguzi na tathmini ya Kamati. Mahojiano na ziara uwandani zililenga kupata matokeo kamili na mapendekezo yanayokidhi utatuzi wa mgogoro wa shamba la Malonje. Sera zilibainika kutoa miongozo muhimu huku sheria zikionekana kuwa na masharti ya kisheria yanayohitajika katika utatuzi wa mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa hadidu za rejea, Hadidu ya kwanza ni Kubaini Eneo la Shamba la Malonje Lilipoanzia. Kamati katika uchambuzi wake ilizingatia kuwa kusudio katika hadidu hii ni historia ya kuanzishwa kwa shamba la Malonje kwa kuhusianisha na mgogoro kati ya mwekezaji na vijiji vinavyozunguka shamba hilo. Uchambuzi umeonesha mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu umiliki na matumizi ya awali ya shamba la Malonje, nyaraka mbalimbali zinaonesha kuwa tangu mwaka 1930 wakati wa Utawala wa Kikoloni, shamba la Malonje lilimilikiwa na mwekezaji Mlowezi aliyeitwa George Damm na baadaye lilimilikiwa na mkewe aliyejulikana kwa jina la Bi. Isle Damm. Wakati huo lilikuwa na ukubwa wa ekari 300 likitumika kwa

kilimo na baadaye ufugaji. Aidha, matokeo ya mahojiano na wazee wa vijiji hivyo vilithibitisha historia hiyo.

Mheshimiwa Spika, umiliki wa shamba hili ulihama kutoka kwa Bi. Isle Damm na kuwa chini ya Serikali, mwaka 1967. Kuhama kwa umiliki huo kulitokana kutelekezwa kwa shamba hilo na Bi. Isle Damm kufuatia Azimio la Arusha. Mwaka 1971 Serikali ilichukua shamba hilo na baadaye likakabidhiwa kwa taasisi mbalimbali za Serikali, ikiwemo Kampuni ya Taifa ya Kilimo *(NAFCO),* ambayo nayo ilirithisha shamba hilo kwa Kampuni za Ranchi za Taifa *(NARCO),* ambayo nayo ilirithisha kwa Kampuni ya Ufugaji wa Ng'ombe wa Maziwa *(DAFCO)*. Hadi wakati huu, shamba lilikuwa na ukubwa wa ekari 47,520.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi kutumia shamba kabla ya mwaka 2007. Nyaraka muhimu na matokeo ya mahojiano kwa pamoja vinaonesha kwamba, tangu enzi za Bi. Isle Damm, wananchi walikuwa wakitumia sehemu ya shamba hilo kwa makazi, kilimo na ufugaji. Mwaka 1977, Serikali iliunda Kamati ndogo ya Wilaya iliyopendekeza kuwa *NARCO* ipunguze ekari 10,007 kwa ajili ya vijiji vinavyozunguka shamba hilo na jambo hilo liliridhiwa na *NARCO*.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikupata uthibitisho wa utekelezaji kamili wa mapendekezo hayo. Uhakika ni kwamba, wananchi waliendelea kutumia sehemu ya shamba hilo na ni ushahidi kwamba wananchi waliendelea kuhitaji ardhi tangu wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utatuzi wa migogoro kabla ya shamba la Malonje kubinafsishwa, uchunguzi umeonesha kwamba, migogoro ya shamba hilo ilikuwepo tangu enzi za umiliki wa Bi. Damm na wakati likiwa chini ya *NAFCO* na likiwa chini ya *NARCO*. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kutatua migogoro hiyo, ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu kutojihusisha na uvamizi wa mashamba na kumega sehemu ya shamba ili kuwagawia wananchi. Hata hivyo, hatua hizo hazikuzaa matunda.

Mheshimiwa Spika, hadidu ya pili ni Kubaini Mipaka Halisi ya Shamba la Malonje na Vijiji Vinavyozunguka. Shamba la Malonje limezungukwa na vijiji mbalimbali tangu enzi za Mkoloni. Vijiji kama Malonje, Kaoze, Ntuki na Sikaungu vilikuwepo tangu miaka ya 1960. Barua ya tarehe 15 Januari, 1964 kutoka kwa *Division Executive Officer Local Court Sumbawanga* kwenda kwa *Area Secretary District Office Sumbawanga* inathibitisha uwepo wa vijiji jirani na Shamba la Malonje.

Mheshimiwa Spika, naomba nifanye nukuu ya barua hiyo. Nukuu: "Ni kweli nimekuta watu wa miji ifuatayo wameshagawana shamba hilo na kuanza kulima kama ifuatavyo: Kwa upande wa Kaskazini wa shamba ni Kaoze Village, kwa upande wa Kusini wa shamba - Ntuki Village na kwa upande wa mashariki wa shamba ni Sikaungu village." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ramani ya shamba ya mwaka 1997 iliyosajiliwa kwa tarehe 8 Desemba, 1997 inaonesha hali ya sasa ambapo shamba hilo linapakana na vijiji vinane. Kwa Upande wa Kaskazini - Kijiji cha Kinamwanga, Kaskazini Mashariki - Kijiji cha Mawenzusi, Kusini - Kijiji cha Sikaungu, Kusini Mashariki - Kijiji cha Msanda Muungano, Mashariki - Kijiji cha Songambele Azimio, Magharibi - Gereza la Mollo na Malonje, Kusini Magharibi - Vijiji vya Ulinji na Isesa kama inavyoonekana katika mchoro ambao umeambatishwa.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya wazee wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo yanaonesha kuwa vijiji hivyo vimekuwepo tangu zamani japo upimaji wa ardhi ya vijiji hivyo ulifanyika mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, ni dhahiri kwamba ongezeko la watu kwenye vijiji vinavyozunguka shamba hilo limeongeza mahitaji ya ardhi inayofaa kwa uzalishaji. Hali hii inachangia mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na wananchi hao na ikizingatiwa kuwa baadhi ya wananchi walizaliwa na kukuta wazazi wao wakitumia shamba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipaka ya shamba na vijiji vinavyozunguka, Kamati ilichambua Ramani ya Shamba la Malonje ya mwaka 1997, Ramani ya Shamba la Mwekezaji ya Mwaka 2008 na Ramani ya Vijiji vya Sikaungu, Songambele Azimio na Msanda Muungano za mwaka 2009. Kwa kutumia wataalamu wa ramani na upimaji, Kamati ililinganisha ramani hizo kwa kuzingatia *coordinate*. Hatua hiyo ilitoa picha halisi ya mipaka ya shamba na vijiji vinavyozunguka shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, kwenye *screen* utaona mwingiliano wa vijiji hivyo kwamba ramani inaonekana vipo ndani ya shamba la mwekezaji, lakini shamba la mwekezaji pia mipaka yake ipo ndani ya vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kielelezo hicho, sehemu ya ardhi inaonekana ndani ya maeneo ya vijiji ya mipaka ya Sikaungu, Msanda Muungano pamoja na Songambele Azimio, inaingiliana na mipaka ya Shamba la Malonje na Shamba la Magereza kwa jumla ya hekta 3,357. Hekta 2,844 zinaingiliana na Shamba la Malonje wakati hekta 512 zinaingiliana na Shamba la Gereza la Mollo. Ili kujiridhisha zaidi, tulipokuwa uwandani Wajumbe wa Kamati waliweza kuona *beacons* zinazoingiliana baina ya Shamba la mwekezaji pamoja na vijiji vinavyozunguka shamba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Kamishna wa Ardhi walifafanua kwa Kamati kwamba, ramani za ardhi ya vijiji zinatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114 na kwamba, ni kwa ajili ya kuweka mipaka ya utawala wa vijiji na siyo kumilikisha ardhi hiyo kwa vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonesha kwamba mwekezaji naye anatafsiri mwingiliano huo wa mipaka kama ilivyofafanuliwa na Waziri na Kamishna wa Ardhi. Hata hivyo, wananchi wao wanasema kwamba mipaka hiyo ya vijiji inatumia alama za asili na mito zilizopo kwenye ramani na wameendelea kuamini kuwa sehemu hiyo ya shamba iliyo ndani ya mipaka ni ardhi ya vijiji vyao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahitaji ya ardhi kwa vijiji vinavyozunguka Shamba la Malonje, Kamati ilifanya uchambuzi wa nyaraka zilizowasilishwa kutoka mamlaka mbalimbali za Serikali, maelezo ya mashahidi na marafiki waliofika mbele ya Kamati, ziara ya Kamati uwandani, maelezo ya mwekezaji na maelezo ya wananchi kwa baadhi ya vijiji waliyoyatoa mbele ya Kamati. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Ongezeko la ukubwa wa ardhi ya Shamba la Bi. Isle Damm mwaka 1946 hadi 1955 na Kampuni ya *NAFCO* mwaka 1968 hadi 1974 lilisababisha vijiji kukosa ardhi kwa ajili ya makazi, kilimo na malisho hali iliyozua mgogoro kwa wakati huo;

(ii) Ongezeko la watu katika vijiji vinavyozunguka shamba hilo limeongeza mahitaji ya ardhi, jambo linalochangia mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na mwekezaji;

(iii) Sehemu ya ardhi ya shamba la mwekezaji ipo ndani ya mipaka ya vijiji hivyo kusababisha changamoto ya kisheria kuhusu umiliki wa ardhi;

(iv) Wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo wamekuwa wakitumia ardhi ya Shamba la Malonje kwa kilimo na makazi, ingawa kuna tofauti ya tafsiri kuhusu mipaka kati yao na Serikali; na

(v) Mwekezaji amekuwa akikodisha sehemu ya shamba kwa wanavijiji na wananchi wengine kwa kulipia kati ya shilingi 10,000 na shilingi 50,000 kwa ekari na kwenye *screen* ni risiti inayoonesha kukodishwa kwa wananchi kwa shilingi 10,000 kwa ekari moja wanapotaka kutumia eneo la mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, pamoja na kutozwa kodi ya shilingi 10,000 kwa ekari hadi shilingi 50,000 wananchi pia hupaswa kutoa

gunia moja la mazao kwa kila ekari ambayo ni fungu la kumi kama linavyotolewa na mwekezaji kwa wananchi wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suluhu ya kudumu ni lazima izingatie uhalisi wa hali ya ardhi na mahitaji ya wananchi wa vijiji hivyo bila kupora haki yao ya ardhi na ndiyo maana wanalazimika kukodi ili waweze kupata mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadidu ya tatu ni Taratibu Zilizofuatwa Kuongeza Ukubwa wa Shamba la Malonje. Namna Shamba lilivyoongezeka kwa nyakati tofauti; nyaraka zinaonesha kwamba, ukubwa wa Shamba la Malonje umebadilika mara kadhaa ikiwa chini ya umiliki wa Bi. Isle Damm na baadaye Taasisi za Serikali kutokana na utwaaji wa maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1955 shamba liliongezeka kutoka ekari 100 hadi ekari 6,248 chini ya Bi. Isle Damm. Mwaka 1973 liliongezeka tena kutoka ekari 2,541 hadi ekari 47,520 chini ya *NAFCO* na mwaka 1980 ukubwa ulipunguzwa na ukabaki ekari 37,513. Ramani ya mwaka 1997 ilionesha ukubwa wa ekari 45,692.5. Mwaka 2004 Wizara ya Mifugo ilipokuwa inakabidhi shamba hili kwa Mkoa wa Rukwa ilikadiriwa kwamba shamba hili lina ukubwa wa ekari 37,500. Katika uhakiki wa mwaka 2017 ilibainika kuwa wala siyo 37,500 badala yake ni 34,370.

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonesha kwamba, mabadiliko haya ya ukubwa hayaelezeki kwa uhakika na hutofautiana kati ya nyaraka na nyaraka. Ni maoni ya Kamati kuwa, maamuzi kuhusu eneo la shamba yamekuwa hayazingatii taratibu sahihi na hii ni sababu ya mgogoro unaoendelea na vijiji vinavyozunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu taratibu zilizotumika kuongeza ukubwa wa shamba. Hakuna uthibitisho wa misingi ya njia zilizotumika katika mabadiliko ya ukubwa wa shamba tangu kabla ya uhuru na hata likiwa chini ya mwekezaji wa sasa. Hakuna nyaraka yoyote inayothibitisha kuzingatia taratibu za kuongeza ukubwa huo na tathmini hiyo inaonesha kuwa kukosekana kwa

uthibitisho wa misingi ya ongezeko la shamba hadi sasa ni jambo ambalo limerithiwa na likaendelea na hata wakati wa sasa shamba hilo lilipouzwa na Manispaa ya Sumbawanga kwa mwekezaji wa sasa.

Mheshimiwa Spika, kutoka mwaka 1968 hadi 1974 *NARCO* iliongeza ukubwa wa shamba kutoka ekari 2,800 hadi ekari 47,520, lakini hakuna nyaraka zinazoonesha kufuatwa kwa utaratibu, bali upo waraka mmoja tu unaoonesha kwamba watu tisa walistahili kulipwa fidia lakini hata katika waraka huo ni watu watatu peke yake walioonekana kusaini. Kwa jinsi hiyo, fidia inaonekana haikuwa inalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo hayo yanaleta mashaka kuhusu kufuatwa kwa taratibu za uongezaji wa ukubwa wa shamba. Dosari hizo za kumbukumbu ni miongoni mwa viashiria vya tatizo la kuongezeka kwa eneo la Shamba la Malonje kihistoria. Mashaka kuhusu utaratibu uliotumika kuongeza ukubwa huo, yanachangia kwa kiasi kikubwa kuendelea kuwepo kwa mgogoro wa ardhi katika Shamba la Malonje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe maelezo ya mauzo hekta 10,000 za Shamba la Malonje. Mwaka 2007 Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilitangaza kuuza hekta 3,000 na zilikuwa na miundombinu ya ufugaji. Tangazo lilikuwa la kuuza ekari 3,000 lakini mwekezaji alipendekeza kununua hekta 10,000 kwa shilingi milioni 600. Jambo hili lilikubalika bila umma kutangaziwa, wala kufanyika uthamini wa shamba kinyume na taratibu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba wa mauzo unaonesha kuwa Manispaa ya Sumbawanga ilimuuzia mwekezaji wa shamba hekta 10,002. Aliomba 10,000 akauziwa 10,002 zikazidi mbili pale katika 10,000 lakini mipaka yake haikuhakikiwa kabla ya mauzo. Hali hii inaashiria kuwa taratibu za upatikanaji wa shamba hilo hazikuzingatiwa ipasavyo na zoezi hilo limechangia mgogoro kati ya mwekezaji na wananchi wa vijiji jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonesha kuwa, uuzaji wa hekta 10,002 bila umma kutangaziwa, bila shamba kupimwa na bila kushirikisha wadau muhimu ni miongoni mwa sababu zinazochochea mgogoro huo. Wananchi wanahisi mwekezaji ameongeza ukubwa wa shamba hadi kwenye ardhi yao ya kilimo na malisho, jambo linalozidisha mgogoro. Suluhu ya kweli inahitaji kurekebisha madhara hayo ya kihistoria ya ukiukwaji wa taratibu.

Mheshimiwa Spika, uuzaji wa shamba hilo bila uthamini unaashiria kwamba, shamba liliuzwa kwa bei ndogo kuliko thamani halisi. Uuzaji wa shamba hilo bila uthamini kuwa umefanyika kabla ya mauzo, unaashiria kwamba shamba liliuzwa kwa bei ndogo kuliko thamani halisi. Kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inathibitishwa kuweka dhamana shamba hilo la mwekezaji na kukopa shilingi 3,001,905,000 mwaka mmoja baadaye, ongezeko la thamani ya asilimia 400, hali inayozua maswali kuhusu uuzwaji wa shamba hilo kwa shilingi milioni 600.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa mauzo na mgawanyo wa hekta zilizobaki baada ya mwekezaji kuwa ameuziwa zile hekta 10,002; baada ya mwekezaji kuuziwa hekta 10,002, zilibaki hekta 3,748 ambazo zilikusudiwa kuuzwa kwa wafugaji wadogo wa vitalu vya hekta 50 kwa mfugaji mmoja. Mapitio ya nyaraka muhimu na matokeo ya mahojiano yanaonesha kwamba, kati ya hekta hizo 1,139 zilienda Gereza la Mollo na zilizobaki 2,609 ndizo zilizokwenda katika vitalu 51 ambavyo viliuzwa kwa wananchi kutoka maeneo mbalimbali wakiwemo wafanyabiashara, viongozi wa kisiasa, viongozi wa Serikali ngazi ya mkoa na wilaya pamoja na familia ya mwekezaji. Aidha, bei ya vitalu hivi ilikuwa shilingi 2,500,000.

Mheshimiwa Spika, wananchi walionesha juhudi za kutaka kununua vitalu hivi kwa ajili ya kilimo. Hata hivyo, lengo lao halikufanikiwa kwa kuwa masharti ya uuzaji wa vitalu hivyo yalitaka ununuzi uwe kwa ajili ya ufugaji pekee ilhali wao wamezoea kilimo. Kwa tathmini ya jumla kuhusu masharti hayo, uhalisia haukuzingatiwa wakati wa uuzaji wa vitalu. Ushahidi wa masharti

haya kukosa uhalisia ni kuwepo kwa waliouziwa vitalu kwa masharti ya kufuga lakini kwa leo wanavitumia kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu ushirikishwaji wakati wa mchakato wa mauzo ya Shamba la Malonje umebaini kuwa mchakato wa mauziano na upimaji wa Shamba la Malonje haukushirikisha wadau muhimu kama Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Iliyouza ni Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga lakini wenzao *DC* (Halmashauri ya Wilaya) hawakushirikishwa, na vijiji ambavyo vinazunguka, vikiwemo vya Sikaungu, Msanda Muungano na Songambele Azimio.

Mheshimiwa Spika, baada ya mauzo ya shamba kufanyika ndipo ikagundulika kwamba sehemu ya shamba hilo iko ndani ya mipaka ya utawala wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Kwa jinsi hiyo, ikaazimiwa kwamba, katika zile shilingi milioni 600, basi wale wa Halmashauri ya Sumbawanga wapewe shilingi milioni 200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa mujibu wa maelezo ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Sumbawanga na ushahidi wa nyaraka zilizowasilishwa, hata katika zile shilingi milioni 200 walizopaswa kupewa bado walipokea shilingi milioni 50 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hiyo imekuza uhusiano mbaya kati ya vijiji, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na hivyo kuleta changamoto katika utatuzi wa mgogoro huo. Aidha, sintofahamu kuhusu mgao wa fedha za mauzo ya shamba inaashiria matumizi mabaya ya fedha za umma zinazotokana na mauzo ya Shamba la Malonje.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye maelekezo ya Baraza la Mawaziri kuhusu mgawanyo na matumizi wa Shamba la Malonje. Baraza la Mawaziri lilielekeza Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kusimamia ubinafsishaji wa Shamba la Malonje kwa kuligawa katika vipande vya hekta 50, 50 kwa wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa.

Mheshimiwa Spika, katika maelekezo hayo ofisi ya mkoa ilielekezwa pia kwamba iwapo watapata changamoto ya kubinafsisha basi waweze kurejea kule maelekezo yalikotolewa. Uchambuzi unaonyesha kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa ilikiuka maelekezo hayo ikiwemo kuuza hekta 10,002 kwa mwekezaji huku zile zilizobaki zikigawiwa kwa wananchi na Gereza la Mollo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa mahojiano Mheshimiwa Balozi Daniel Ole Njoolay alidai kwamba hakuwahi kuona barua ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo bali alielezwa na wasaidizi wake kuwa ofisi yake imepewa mamlaka ya kusimamia mauzo ya shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya uuzaji wa shamba yalionesha kuwa Mkuu wa Mkoa alikuwa na ufahamu wa barua hiyo, ikizingatiwa aliongoza vikao vya majadiliano na mwekezaji na kutoa maelekezo kwa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kuhusu uuzaji kama vile kupima eneo lililobaki na kuliuza kwa wafugaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipomhoji Waziri wa Mifugo na Uvuvi kuhusu kutosimamia ubinafsishaji, alieleza kuwa Wizara haikuwa na wajibu huo kwani shamba lilikwishakabidhiwa kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Kamati ina mtazamo kuwa Wizara haikutekeleza majukumu yake ipasavyo, kwani ilikuwa na maelekezo kutoka Baraza la Mawaziri na ilipaswa kutoa mrejesho kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchunguzi ulionesha kuwa Serikali ilifahamishwa kuhusu ukiukwaji wa maelekezo ya Baraza la Mawaziri na viongozi wa mkoa lakini hatua hazikuchukuliwa. Hali hii inaongeza mashaka kuhusu juhudi za Serikali katika kutatua mgogoro huu. Iwapo Serikali haitachukua hatua madhubuti, mgogoro utaendelea na wananchi wa vijiji vinavyohusika wataendelea kuhisi kuwa Serikali haiwasaidii katika kutatua mgogoro huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadidu ya nne ni Dalili za Vitendo vya Uvunjifu wa Haki za Binadamu. Hadidu hii ya nne iliongoza Kamati kwenye kubaini iwapo kuna dalili za vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu vinavyodaiwa kufanywa na walinzi wa Shamba la Malonje na iwapo vitendo hivyo vinatokana na miongozo ya wamiliki wa shamba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu vurugu katika Shamba la Malonje Kamati ilibaini kuwa katika nyakati tofauti kumekuwepo vurugu kati ya walinzi wa mwekezaji na wananchi wa vijiji vinavyozunguka Shamba la Malonje. Mathalani, kumekuwepo na matumizi ya nguvu kupita kiasi ikihusisha silaha za moto upande wa walinzi wa mwekezaji na silaha za jadi kwa upande wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya vurugu hizo yalisababisha mmoja wa walinzi wa mwekezaji kuuawa, lakini pia wananchi kujeruhiwa kwa risasi. Kamati ilishuhudia alama za wananchi kujeruhiwa kwa risasi ambapo ushahidi ulithibitishwa kwa nyaraka za hospitali zilizothibitisha majeraha ya risasi. Wananchi waliopigwa risasi walithibitisha kwa Kamati kwamba wamepigwa risasi hizo na walinzi wa mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili mtu aliyekuja mbele ya Kamati wakati iko uwandani, mmoja anaitwa Ndugu Festo Kamwanga. Kwenye *screen* ni yeye aliyepigwa risasi kifuani, shavuni na mguuni.

Mheshimiwa Spika, mbili, mwingine aliyekuja mbele ya Kamati anaitwa Ndugu Elius Cosmas Kauzeni. Yeye alipigwa risasi kichwani na begani, ndiye anayeonekana kwenye *screen* na anaendelea kuishi na risasi hizo kichwani hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, mwingine aliyekuja mbele ya Kamati anaitwa Ndugu Dickson Charles Simkonde aliyepigwa risasi tumboni kama inavyoonekana kwenye *screen;* na mwingine aliyekuja mbele ya Kamati yeye anaitwa Ndugu Nuru Togwa, yeye alikatwa masikio yote mawili kama anavyoonekana kwenye *screen*.

Mheshimiwa Spika, mwingine aliyekuja mbele ya Kamati anaitwa Martin Kazikupenda Mpisi, huyo anayeonekana kwenye *screen*. Yeye alivunjwa miguu na hadi sasa amekuwa na ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, vurugu hizi zinaashiria uvunjifu wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi na kumiliki mali. Aidha, tatizo la uhaba wa ardhi kwa ajili ya uzalishaji ikilinganishwa na mahitaji linachangia mivutano isiyokoma baina ya wananchi pamoja na mwekezaji na hatimaye kutokea vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake Kamati ilibaini kuwepo kwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake katika Vijiji vya Sikaungu, Msanda Muungano, Mawenzusi, Isesa na Ulinji. Wanawake saba walieleza kutendewa vitendo hivyo kwa vipindi tofauti na walinzi wa mwekezaji. Aidha, wanawake hao walieleza kuwa walikamatwa na kupelekwa katika eneo ambalo kule uwandani linaitwa Majumba Mawili ambayo ni kama korokoroni ya muda ya mwekezaji. Walipokuwa katika Majumba hayo Mawili walitendewa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia ikiwemo kubakwa. Hata hivyo, wanawake hao walikiri kutoripoti matukio hayo Polisi kutokana na aibu na hofu ya kuachwa na waume zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kumhoji msimamizi wa kitengo cha ulinzi wa shamba la mwekezaji ambaye alikiri kwamba wanawakamata watu wanapopita shambani bila ruhusa na kuwahifadhi katika eneo hilo la Majumba Mawili. Pia, Kamati ilipata fursa ya kufika eneo hilo la Majumba Mawili.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Kamati kwa maelezo ya wananchi pamoja na mazingira ya eneo husika ni kwamba, upo uwezekano wa tuhuma hizo za wananchi kuwa na ukweli, jambo linalohitaji kuthibitishwa zaidi na vyombo vya dola vinavyohusika.

Mheshimiwa Spika, niende kwa matumizi ya njia za asili zinazokatisha shambani. Kamati imebaini kuwa wananchi wamekuwa wakizuiwa kupita kwenye njia za asili zinazokatiza shamba la mwekezaji bila kibali cha Serikali ya Kijiji. Njia hizo zimekuwa zikitumiwa kwa muda mrefu kwenda maeneo mbalimbali kupata huduma muhimu tangu enzi za ukoloni.

Mheshimiwa Spika, aidha, wananchi walieleza kuwa wamekuwa wakitozwa faini ya shilingi 50,000 kwa ng'ombe mmoja, pindi anapopita katika shamba la mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kuwa shamba la mwekezaji ni kubwa na njia za asili zinazopita katika shamba hilo zinarahisisha mawasiliano baina ya kijiji na kijiji kingine. Kuzuiwa kutumia njia hizo na kulazimishwa kupita njia ndefu ni unyanyasaji na uvunjifu wa haki za binadamu. Aidha, kuzuiwa na kufunga njia hizo za asili kunachangia uhasama na uhusiano mbaya kati ya mwekezaji na wananchi wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu iwapo vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu vinatokana na miongozo ya wamiliki wa shamba hilo. Kamati ilibaini kuwa shamba la mwekezaji linalindwa na Kampuni ya *Funguka Security Company Limited* inayomilikiwa na Bodi ya Wadhamini wa *Efatha Church* na *Efatha Foundation Limited*.

Mheshimiwa Spika, msimamizi wa kitengo cha ulinzi alieleza kuwa alipatiwa mafunzo ya ulinzi na kampuni hiyo na baadaye kupewa kazi ya ulinzi. Kamati iliona kuwa, kwa kuwa shamba linamilikiwa na mwekezaji, Bodi ya Wadhamini wa Efatha na Kampuni ya Ulinzi ya *Funguka Security* iko chini ya kanisa hilo, hali hii inaweza kutafsiriwa kuwa vitendo vya walinzi vinafanywa kwa miongozo ya wamiliki wa shamba.

Mheshimiwa Spika, hadidu ya tano ni Mambo Mengine Kuhusiana na Mgogoro wa Shamba la Malonje. Hatua zilizowahi kuchukuliwa kutatua mgogoro baina ya mwekezaji na wananchi wanaozunguka Shamba la Malonje; Kamati imebaini kuwa hatua

mbalimbali zimechukuliwa na Serikali katika kutafuta suluhu za mgogoro wa Shamba la Malonje.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa iliunda timu ya wataalamu kuchunguza mgogoro huo na kutoa mapendekezo kwa *RCC*. Mwenyekiti, wa *RCC* alimjulisha Mheshimiwa Rais kuhusu mgogoro na hatua zinazopendekezwa. Aidha, mwaka 2017 pia Mkuu wa Mkoa aliunda timu nyingine na kuwasilisha mapendekezo Serikalini.

Mheshimiwa Spika, moja ya matokeo ya kazi ya timu hizo ni mwekezaji kukubali kutoa hekari 3,000 ili kupunguza tatizo la ardhi kwa Vijiji vya Sikaungu, Msanda Muungano na Songambele Azimio. Hata hivyo, pamoja na kutoa ekari 3,000 hatua hii haikutatua mgogoro huo kwani wananchi wa Kijiji cha Sikaungu waliamini kuwa ardhi hiyo ni sehemu ya ardhi yao na hivyo hawakupokea hizo hekari 1,000 walizopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine iliyochukuliwa na Serikali ilikuwa ni kutoa Ilani ya siku 90 mwaka 2015 ili kufuta umiliki wa Shamba la Malonje. Hatua hii ililenga kurejesha amani kwa wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo lakini haikufanikiwa, na haikufanikiwa kwa sababu za kisheria ambazo zilikuwa na changamoto na zinahitaji tafakuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonyesha kuwa kulikuwa na makosa ya kitaalamu yaliyosababisha Serikali kushindwa kufikia azma hii ya kulichukua shamba hili mwaka 2015. Makosa hayo yako hivi; yalihusu usimamizi mbovu wa Shauri Na. 7 la Mwaka 2015 lililofunguliwa na mwekezaji dhidi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga katika Mahakama Kuu ya Masijala ya Sumbawanga. Shauri hilo lilimalizika kwa kusainiwa Hati ya Maridhiano mwaka 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umebainisha kuwa, Kamishna wa Ardhi ndiye aliyepaswa kushtakiwa na wala sio Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga. Aidha, masharti ya hati ya maridhiano

hayakuzingatia masharti ya mkataba wa mauziano ya shamba ambayo yalimruhusu mwekezaji kutumia shamba kwa shughuli yoyote kinyume na makubaliano ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, katika shauri hili kuna uwezekano wa saini ya Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwenye hati ya maridhiano kuwa ilighushiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzingatiaji wa masharti ya mkataba wa mauzo ya Shamba la Malonje uchambuzi wa Kamati umeonesha kwamba mwekezaji hazingatii masharti ya mkataba wa mauziano wa shamba na hati ya umiliki. Mkataba ulimtaka mwekezaji aweze kufanya ufugaji wa kisasa lakini mwekezaji anatumia zaidi kiasi kikubwa kwa kilimo zaidi ya ufugaji na asilimia ndogo ya matumizi kwa mujibu wa masharti.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa Serikali haikuwa na mikakati madhubuti ya kuhakikisha masharti hayo katika mkataba yanatekelezwa ipasavyo na matokeo yake yamemfanya mwekezaji aweze kupata hatimilki nyingine mwaka 2021; na hati hiyo sasa, kwa sababu alikuwa amepewa kufuga na yeye akawa analima, mwaka 2021 akapata hati nyingine kutoka Serikalini iliyobadili matumizi ya shamba kutoka kufuga tu na sasa ikaongeza ufugaji, kilimo cha miti pamoja na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, badiliko hilo halikufuata taratibu za mabadiliko au nyongeza ya matumizi ya shamba, kwa maana ya kwamba hakukuwa na tangazo kwa wadau linaloelekeza kufanya mabadiliko au nyongeza katika shamba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kasi ndogo ya uwekezaji katika shamba; ni miaka takribani 17, tangu mwaka 2007 hadi leo mwekezaji alipouziwa shamba, na kwa kadri ya taarifa zake alizowasilisha, anasema shamba limeendelezwa kwa 41.9%. Hata hivyo, maelezo yaliyotolewa na Kamishna wa Ardhi kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliposhughulikia suala hili tarehe 3 Mei, yanaonesha kwamba kiasi kilichoendelezwa ni asilimia nne tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutofautiana kwa takwimu kuhusu kiasi kilichoendelezwa kati ya mwekezaji na Kamishna wa Ardhi ni ishara ya kutoendelezwa ipasavyo kwa shamba hilo, ikizingatia kuwa baadhi ya mazao yaliyopo shambani ni ya watu mbalimbali waliokodishwa na wala siyo ya mwekezaji. Kwa ujumla uchunguzi umebainisha kwamba sehemu kubwa ya shamba hilo hata tulipokuwa uwandani haijaendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende sehemu ya tatu ya mapendekezo ya utatuzi wa mgogoro.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuundwa kwa Kamati hii ni kupata mapendekezo kuhusu ufumbuzi wa mgogoro uliopo kati ya mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na wananchi wanaozunguka shamba hilo. Kwa namna mgogoro huu ulivyo, dhana ya ardhi kuwa msingi wa uhai kwa wananchi inafifia na dhana ya ardhi kuwa na thamani au msingi wa uzalishaji mali inapoteza maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inahitaji kurekebishwa kwa kuondoa mizizi ya mgogoro uliopo. Utatuzi huo unapaswa kutegemea matokeo ya uchunguzi uliofanyika kwa muono wa Sera na Sheria zilizopo na kuzingatia ustawi wa maisha ya watu kama inavyotaka Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo: Pendekezo la Kwanza, Umiliki wa Shamba la Malonje.

Kwa kuwa, masuala mbalimbali katika mgogoro unaohusu umiliki wa Shamba la Malonje, yanajumuisha:-

(1) Kubadilika ukubwa wa shamba mara kadhaa na kuwepo kwa vipimo vinavyotofautiana kuhusu ukubwa wake, jambo linalochangia kuendelea kwa mgogoro;

(2) Kutozingatiwa kwa dhamira na maelekezo ya Baraza la Mawaziri, yaliyohusu matumizi ya Shamba la Malonje kuwa ufugaji, hata hivyo uuzaji wa shamba hilo ukiwa na kasoro;

(3) Kutofuatwa kwa taratibu za uuzaji wa mali za umma wakati wa kuuza Shamba la Malonje na hivyo, kusababisha sintofahamu na mashaka ya uhalali miongoni mwa wadau;

(4) Kutoshirikishwa kwa wadau muhimu, ikiwemo wananchi, viongozi wa vijiji pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga katika mchakato wa ubinafsishaji wa shamba na hivyo uwekezaji katika shamba hilo kutokubalika;

(5) Mwekezaji kutotekeleza masharti yaliyo katika mkataba wa mauziano na hati ya umiliki wa shamba ya mwaka 2009, hivyo, kutokufikiwa kwa malengo yaliyotazamiwa na wasiwasi wa wananchi kuhusu uzingatiaji wa maslahi yao;

(6) Kubadilika kwa matumizi ya shamba pasipo kuzingatia taratibu, hivyo badiliko hilo kutokukubalika miongoni mwa wananchi na kukiuka dhamira ya ubinafsishaji wa shamba hilo;

(7) Kutokuwa na usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba wa mauziano ya Shamba la Malonje kwa upande wa Serikali na hivyo kutoa fursa ya mwekezaji kuamua atakavyo na kuwakwaza wananchi;

(8) Kuingiliana kwa mipaka ya shamba na mipaka ya baadhi ya vijiji, hivyo kusababisha mgogoro wa matumizi ya eneo la ardhi lenye mwingiliano;

(9) Baadhi ya vijiji kutokuwa na ardhi ya kutosha kwa ajili ya kilimo na ufugaji ilhali kuna eneo la ardhi ya Malonje

halitumiki na hivyo kuwavutia kuendesha shughuli zao kwa kukodishwa na kujikuta katika mgogoro na mwekezaji;

(10) Sehemu kubwa ya shamba kutotumiwa na mwekezaji badala yake kukodishwa kwa wanakijiji na wananchi wengine;

(11) Mwekezaji kupendekeza hekta 10,000 badala ya 3,000 zilizotangazwa kwa bei ya shilingi milioni 600 na Serikali kukubali bila kufanya uthamini wa shamba na mifugo iliyokuwepo wakati wa kutangaza kusudio la kuuza hekta 10,000 jambo linalosababisha mashaka miongoni mwa wananchi;

(12) Uwepo wa uhusiano mbaya kati ya mwekezaji na wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo kunakosababishwa na mvutano wa mgongano wa matumizi ya shamba na hivyo kusababisha mapigano na uvunjifu wa amani kwa mwekezaji na wananchi hao.

Na Kwa kuwa, masuala haya kwa ujumla wake yanaathiri manufaa ya shughuli za uzalishaji kwa mwekezaji na yanatofautiana na dhana ya ardhi kuwa msingi wa uhai kwa wanavijiji;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ibatilishe umiliki wa shamba lote la Malonje. Serikali ibatilishe umiliki wa shamba lote la Malonje likihusisha shamba la *Efatha* na mashamba yanayolizunguka ikiwemo vitalu 51 kwa kuzingatia sheria na maslahi ya umma. *(Makofi)*

(b) Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji nane vinavyozunguka shamba pamoja na Gereza la Mollo, utakaobainisha mahitaji ya ardhi pamoja na matumizi ya ardhi hiyo. *(Makofi)*

(c) Serikali ilipime shamba hilo na kuligawa upya kwa wahusika ambao ni wanavijiji, Gereza la Mollo, mwekezaji *Efatha Church* na wenye vitalu kwa kuzingatia mahitaji halisi ya ardhi kwa wanavijiji, uwezo wa mwekezaji, uwezo wa wenye vitalu na mahitaji ya Gereza la Mollo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili: Shauri la Ardhi Na. 7 la mwaka 2015 kati ya Bodi ya Wadhamini wa *Efatha* dhidi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga:-

Kwa kuwa msingi wa Shauri la Ardhi Na. 7 la 2015 lililofunguliwa Mahakama Kuu ya Masijala ya Sumbawanga ni *notice* ya kubatilisha umiliki wa shamba katika shamba la mwekezaji iliyotolewa na Afisa Ardhi Mteule kwa niaba ya Kamishina wa Ardhi;

Na kwa kuwa, katika shauri hilo aliyeshitakiwa ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa badala ya Kamishna wa Ardhi ambaye ndiye aliyetoa *notice* na ndiye mwenye mamlaka hayo kisheria:-

(a) Shauri hilo liliishia kwa njia ya maridhiano ambapo ilisainiwa hati ya maridhiano baina ya pande mbili ambapo upande wa Serikali alisaini Mkurugenzi wa Manispaa na Mstahiki Meya; na

(b) Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga alieleza kwamba, saini yake imeghushiwa na hivyo, kuibua wasiwasi wa uhalali kuhusu hati hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ichukue hatua za kisheria ikiwemo kuomba marejeo kuhusu maamuzi hayo ya Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye uchunguzi ili kuwabaini na kuwachukulia hatua wale wote watakaothibitika kughushi saini ya Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tatu; utekelezaji wa Maagizo ya Baraza la Mawaziri:-

Kwa kuwa, Maagizo ya Baraza la Mawaziri kuhusu uuzaji wa shamba hilo yalikusudia ardhi ya shamba hilo itumike kwa ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa; na kwamba, wananchi wauziwe vitalu kuzunguka shamba hilo ili waweze kujifunza ufugaji bora, lakini utekelezaji ulikiuka maagizo hayo, jambo lililokwamisha tija iliyokusudiwa; hayakuwahi kubadilishwa kipindi chote mgogoro ukiendelea, jambo linaloendeleza tofauti ya mtazamo kati ya Baraza la Mawaziri na watumiaji wa ardhi ya shamba hilo na hayakuwahi kutekelezeka miongoni mwa wananchi na kusababisha wananchi kushindwa kununua vitalu, jambo linalochangia upungufu wa ardhi kwa shughuli hizo;

Na kwa kuwa, mambo haya yanaathiri mustakabali wa wananchi wanaozunguka shamba hilo, manufaa aliyotarajia mwekezaji na tija iliyokusudiwa na Serikali kisera na ustawi wa wananchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itathmini msingi na malengo ya uamuzi wake kupitia Baraza la Mawaziri kuhusu Shamba la Malonje ili kubaini iwapo kuna tija inayopatikana na kuchukua hatua stahiki kulingana na azimio la kwanza.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la nne; usimamizi wa Sheria inayoweka ukomo wa kumiliki ardhi nchini:-

Kwa kuwa, idadi ya watu inaongezeka siku hadi siku na mahitaji ya ardhi yamekuwa yakiongezeka licha ya ardhi kutokuongezeka huku kukiwa hakuna mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo mengi nchini;

Na kwa kuwa, hakuna ufanisi katika utekelezaji wa kanuni za mwaka 2001 zinazohusu ukomo wa kumiliki kiasi cha ukubwa wa ardhi ya kawaida na ardhi ya vijiji; na kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina mipango ya usimamizi wa ukomo wa kiasi cha

ukubwa wa kumiliki ardhi katika maeneo yao, hali inayochangia kutokuwa na usawa katika umiliki ardhi miongoni mwa wananchi, ilhali mahitaji ya ardhi kwa wananchi ni makubwa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali isimamie utekelezaji wa kanuni zinazoweka ukomo wa wananchi kumiliki ardhi nchini na Serikali isimamie kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007 kwa kupima ardhi ya nchi nzima na kuiwekea mipango na matumizi ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya ardhi, kuwezesha umiliki unaotambulika, jambo litakalowezesha ardhi ndogo kutumika kwa manufaa ya watu wengi na kupunguza migogoro ya mipaka na umiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tano; hatua dhidi ya vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu:-

Kwa kuwa, uchunguzi umebainisha dalili za kuwepo kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu katika Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo, lakini waliohusika katika tuhuma za vitendo hivyo hawajachukuliwa hatua za kisheria hadi sasa;

Na kwa kuwa, hatua hizo zinahitaji kufanyika kwa uchunguzi ili kubaini hatua zinazostahili kuchukuliwa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na uendeshaji wa kesi za jinai nchini zifanye uchunguzi na kuchukua hatua stahiki kulingana na matokeo ya uchunguzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la sita; Usimamizi wa kampuni za ulinzi nchini:-

Kwa kuwa, walinzi wa Kampuni ya Ulinzi ya *Funguka Security Company Limited* inayolinda shamba la mwekezaji wamekuwa wakituhumiwa kufanya vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu; na kwamba, imebainika kuwa, walinzi hao wamekuwa wakipewa

mafunzo ya ulinzi kutoka kwenye kampuni hiyo yakiwemo mafunzo ya kutumia silaha za moto kwa kufungamanishwa na imani ya wamiliki wa shamba;

Na kwa kuwa, Kamati katika kupitia masharti yanayotolewa na mamlaka za usimamizi wa kampuni binafsi za ulinzi haijaona sharti linalohusu kampuni binafsi kutoa mafunzo kwa walinzi wake na kuwafungamanisha na imani zao, hali ambayo Kamati inaamini kwamba inasababisha walinzi hao kukosa weledi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itazame na kufanya tathmini juu ya taratibu zinazotumika kwa sasa kutoa vibali kwa kampuni za ulinzi ili kuona kama vigezo vinavyotumika kutoa vibali kwa kampuni hizo vinakidhi mahitaji ya sasa kiusalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye uchunguzi juu ya uhalali na weledi wa walinzi wa mwekezaji kwa vitendo vinavyodaiwa kufanyiwa wananchi wa vijiji vinavyozunguka Shamba la Malonje. Serikali ichunguze vitendo vya walinzi wa Kampuni ya Funguka kujeruhi wananchi kwa kutumia silaha za moto na kuchukua hatua dhidi ya watakaobainika kukiuka sheria na taratibu katika kutumia silaha za moto.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifungue upya majalada ya kesi za uchunguzi zinazohusu matukio yote ya uvunjifu wa haki za binadamu zilizotokana na mgogoro wa Shamba la Malonje na kuchukua hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Wajumbe wa Kamati Maalum ya Kuchunguza na Kutathmini Mgogoro katika Shamba la Malonje kati ya Mwekezaji na Wananchi Wanaozunguka Shamba Hilo wanakushukuru kwa dhati kwa uongozi wako, maono na juhudi za kuliwezesha Bunge kushughulikia changamoto za wananchi katika utekelezaji wa shughuli za umma.

Mheshimiwa Spika, Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, linatarajiwa kuendelea kusimamia na kuishauri Serikali ili iweze kutimiza lengo la kuwezesha ustawi wa maisha ya watu. Chini ya uongozi wako, Bunge limeendelea kutimiza wajibu huo na litaendelea kufanya hivyo kwa kuwa, ni chombo cha uwakilishi wa wananchi na ni Bunge lao. Hivyo, haliwezi kuacha kufanya juhudi inayowezesha kutatuliwa kwa migogoro.

Mheshimiwa Spika, kamati pia inamshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa kusimamia vyema uratibu wa shughuli za Kamati. Usimamizi wake umewezesha uratibu bora wa Sekretarieti uliofanikisha kazi ya Kamati kwa misingi ya uratibu madhubuti wa Kibunge.

Mheshimiwa Spika, napenda ku-*register* shukurani zangu za dhati kwamba, Sekretarieti uliyotupatia ilifanya kazi bora sana. Aidha, shukurani zinatolewa kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Serikali ya Mkoa wa Rukwa kwa ushirikiano mkubwa walioipatia kamati kiasi cha kufanikisha kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inawashukuru wadau mbalimbali waliofika kwenye Kamati na kutoa taarifa muhimu zilizowezesha uchambuzi wa Kamati. Miongoni mwao ni Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, viongozi wa Kanisa la *Efatha*, Wakurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa na Wilaya ya Sumbawanga na wadau wengine wote waliowasilisha taarifa kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inawashukuru wananchi wa Vijiji vya Sikaungu, Msanda Muungano, Songambele Azimio, Mawenzusi, Ulinji na Isesa kwa ushirikiano wao kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, tunawashukuru wote walioipatia Kamati taarifa muhimu ambazo ziliisaidia kupata uelewa na kuzichakata, hatimaye kupata mapendekezo. Kwa hakika wote walioipatia Kamati taarifa maoni na ushirikiano uliostahili tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama ilivyoelezwa, lengo la Kamati hii lilikuwa ni kutoa ushauri unaowezesha utatuzi wa mgogoro kati ya mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo. Mgogoro huo umetokana na sababu zilizoelezwa ambazo zote zinapaswa kuangaliwa kwa mtazamo wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji Sura 114.

Mheshimiwa Spika, mtazamo huo izingatiwe pia lengo la Serikali la kuwezesha ustawi wa wananchi na kwamba, ardhi ni msingi wa maisha ya wananchi wakiwemo wananchi wa vijiji vinavyolizunguka Shamba la Malonje. Kwa msingi huo, kwa kadiri itakavyoonekana inafaa, mapendekezo yaliyotolewa yafanyiwe kazi. Muhimu zaidi ni kuwa, mgogoro huu usipotatuliwa mwekezaji hataweza kufanikiwa katika uwekezaji wake na wala wananchi hawataweza kuwa na matumizi ya ardhi inayohusika kwa namna ya kupata ustawi wao.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali haitafanikiwa katika kustawisha maisha ya wananchi wa vijiji hivyo na wala Bunge halitakuwa limesaidia kupatikana kwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI MAALUM YA BUNGE YA KUCHUNGUZA MGOGORO WA ARDHI KATI YA MWEKEZAJI KATIKA SHAMBA LA MALONJE NA WANANCHI WA VIJIJI VINAVYOZUNGUKA SHAMBA HILO – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 144 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, tarehe 27 Mei, 2024 uliunda Kamati Maalum ya Bunge ya

Kuchunguza Mgogoro wa Ardhi kati ya Mwekezaji katika Shamba la Malonje na Wananchi wa Vijiji vinavyolizunguka shamba hilo ili kushauri hatua za utatuzi. Kamati hii ilifanya kazi kuanzia tarehe 15 Julai, 2024 hadi tarehe 05 Agosti, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa kazi ya Kamati imekamilika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Matokeo ya Uchunguzi na Tathmini ya Mgogoro wa Ardhi katika Shamba la Malonje pamoja na mapendekezo ya kutatua mgogoro huo. Pamoja na taarifa hii, maelezo ya kina kuhusu Matokeo ya kazi ya Kamati ya Kuchunguza Mgogoro huu yameambatishwa.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu nne: Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya utangulizi kwa madhumuni ya kubainisha muktadha wa kazi iliyofanyika na Sehemu ya Pili inabainisha matokeo ya uchambuzi ambayo ni msingi wa mapendekezo ya Kamati. Aidha, Sehemu ya tatu inatoa mapendekezo ya utatuzi wa mgogoro ambayo ndiyo lengo kuu la kuundwa kwa Kamati hii na Sehemu ya nne inahitimisha Taarifa.

### 1.3 Muktadha wa Kazi iliyofanywa na Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kazi iliyofanywa na Kamati inagusa mambo makuu matatu. Jambo la kwanza ni historia fupi ya mfumo wa umiliki, usimamizi na upatikanaji wa ardhi nchini na Jambo la pili ni msingi wa Bunge kuchunguza mgogoro wa ardhi katika Shamba la Malonje. Jambo la tatu ni chimbuko la Kamati hii na njia zilizotumika katika uchunguzi.

#### 1.3.1 Historia Fupi ya Mfumo wa Umiliki na Usimamizi wa Ardhi

**Mheshimiwa Spika,** historia inaonesha kuwa, kabla ya uhuru ilikuwepo mifumo ya umiliki, usimamizi na upatikanaji wa ardhi ambayo misingi yake iliendana na mahitaji ya wakati huo. Misingi hiyo ilibadilika baada ya uhuru ambapo ardhi ilitambulika kuwa nguzo kuu ya uzalishaji mali (*major means of production*) na hivyo kuwa

msingi wa uhai. Serikali iliendelea kufanya juhudi mbalimbali za kuimarisha misingi ya umiliki, usimamizi na matumizi ya ardhi kwa namna isiyosababisha migongano na migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya juhudi mbalimbali za Serikali, migogoro ya ardhi imekuwa ikiibuka miongoni mwa watumiaji wa ardhi. Mgogoro wa Shamba la Malonje ni miongoni mwa migogoro iliyoibuka.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 1991, Serikali iliunda Tume ya Rais ya Uchunguzi wa masuala ya ardhi nchini iliyoongozwa na Profesa Issa Shivji. Tume hiyo ilizunguka nchi nzima na kuhojiana na wananchi na ikatoa mapendekezo ambayo ndiyo sehemu ya chimbuko la Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 na Sheria kuu zinazohusu sekta ya Ardhi nchini. Sera hiyo iniatambua ardhi kama rasilimali ya msingi katika kufikia maisha bora kwa kila Mtanzania. Kwa msingi huo, ardhi ni rasilimali inayotegemewa kwa maisha ya watanzania waishio mijini na vijijini wakiwemo wananchi wanaoishi vijiji vinavyolizunguka Shamba la Malonje.

**1.3.2 Msingi wa Bunge Kuchunguza Mgogoro wa Ardhi M katika Shamba la Malonje**

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyo kwa migogoro mingi ya ardhi, mgogoro baina ya Mwekezaji katika Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo una madhara makubwa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, mgogoro huo una athari hasi kwa Mwekezaji na wananchi kwa ujumla. Athari hizo zinasababisha ugumu katika kuendesha shughuli za kiuchumi kwa Mwekezaji na kwa wananchi wa vijiji hivyo. Kwa ujumla, athari hizo zinazuia ustawi wa wananchi na Mwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, linategemewa kusimamia

shughuli za umma kwa namna inayozingatia maslahi ya wananchi ambao ndio msingi wa mamlaka nchini. Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa shughuli zote zinalenga ustawi wa wananchi wakiwemo waishio katika vijiji vinavyozunguka Shamba la Malonje pamoja na Mwekezaji.

### 1.3.3 Chimbuko la Kamati Maalum

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuwezesha mtiririko wa ufuatiliaji wa maudhui na mwelekeo wa uchunguzi, naomba kurejea chimbuko la kuundwa kwa Kamati hii. Ili kufanikisha hilo mambo makuu mawili yanahusika. La kwanza ni kujitokeza Bungeni kwa taarifa zinazoeleza kuwepo kwa mgogoro katika shamba la Malonje na jambo la pili ni matokeo ya kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii yaliyowasilishwa kwako tarahe 09 Mei, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa Rasmi za Bunge zinaonesha kuwa kwa nyakati tofauti, taarifa kuhusu mgogoro huu zimejitokeza Bungeni wakati wa michango ya wawakilishi wa wananchi au maswali na taarifa za Kamati za Bunge. Ufafanuzi wa kina kuhusu kujitokeza kwa taarifa juu ya mgogoro huu unapatikana katika Matokeo ya Kazi ya Kamati ambayo ni Kiambatisho cha Taarifa hii. Kwa ujumla, tangu mwaka 2012 hadi 2024 suala la mgogoro huu limejitokeza Bungeni zaidi ya mara 20.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikitoa majibu na ahadi mbalimbali kuhusu kushughulikia mgogoro huu lakini kwa zaidi ya miaka 13 suluhisho halijapatikana. Mnamo tarehe 7 Novemba 2023, Mbunge wa Jimbo la Kwela, Mhe. Deus Clement Sangu, aliwasilisha Hoja ya Dharura Bungeni akitaka Bunge lako tukufu lijadili mgogoro huu kutokana na athari zilizowapata wananchi wa vijiji vinavyolizunguka shamba la Malonje na Mwekezaji

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia hoja hiyo, tarehe 01 Februari, 2024, Kanisa la Efatha lilikuandikia barua kuwasilisha utetezi wake kuhusu tuhuma zilizodaiwa kutolewa na Mhe. Sangu, dhidi ya kanisa la Efatha. Tuhuma hizo zilihusu mgogoro wa ardhi kati ya Mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na wananchi wa vijiji vinavyolizunguka shamba hilo. Kwa busara zako, ukalielekeza suala hili lijadiliwe na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 9 Mei, 2024 Kamati hiyo iliwasilisha kwako Taarifa ya Matokeo ya kikao chake. Katika taarifa hiyo mambo makuu yaliyobainishwa ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Mgogoro wa Shamba la Malonje ni wa muda mrefu na kwamba umekuwa ukizungumzwa Bungeni kwa nyakati tofauti;

(ii) Licha ya kumbukumbu za mawasiliano kati ya Waziri wa Ardhi na Mwekezaji kuonesha mgogoro umekwisha, bado mgogoro huo upo.

(iii) Hatua za Waziri wa Ardhi hazikurejea kumbukumbu zilizopo Bungeni kuanzia mwaka 2012 hadi 2015.

(iv) Wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje hawaridhiki na namna Wizara ilivyoshughulikia mgogoro huo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo, tarehe 27 Mei, 2024 uliunda Kamati Maalum kwa ajili ya kushughulikia mgogoro wa ardhi katika shamba la Malonje. Aidha na kuipa Kamati hiyo Hadidu za Rejea zifuatazo:-

(i) Kubaini eneo la shamba la Malonje lilipoanzia;

(ii) Kubaini mipaka halisi ya shamba la Malonje na vijiji vinavyozunguka shamba;

(iii) Kubaini iwapo taratibu za uongezaji wa eneo zilifuatwa katika ongezeko la ukubwa wa shamba la Malonje;

(iv) Kubaini iwapo kuna dalili za vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu vinavyodaiwa kufanywa na walinzi wa shamba la Malonje na iwapo vitendo hivyo vinatokana na miongozo ya wamiliki wa shamba; na

(v) Kubaini jambo lingine lolote linalohusiana na mgogoro huo.

**Mheshimiwa Spika**, hatua uliyoichukua ni muhimu na kwa kufanya hivyo, wananchi na wadau wa amani, usalama na ustawi wa wananchi wamekupongeza kwa dhati kwa kuwa uamuzi wako unaonesha kujali na kutamani wananchi wapate ufumbuzi wa matatizo yao. Kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati hii, nichukue fursa hii kukushukuru kwa imani kubwa uliyoionesha kwetu. Lakini pia niungane na wananchi na wadau mbalimbali kukupongeza kwa kujali na kuonesha umuhimu wa kutatua mgogoro huu uliodumu kwa miaka mingi bila utatuzi.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mgogoro huu, wananchi wanalalamikia shamba la Mwekezaji kujumuisha maeneo ya vijiji vyao na hivyo kukosa ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji na kwa upande wa mwekezaji akilalamikia wananchi kuingilia mipaka ya shamba lake alilouziwa na Serikali.Ni maoni ya Kamati kwamba ikiwa hatua za kutatua mgogoro huu hazitapatikana mapema, madhara zaidi yanaweza kutokea ikiwemo kuathiri maisha na mali

za watu na kuzuia azma aliyonayo mwekezaji katika shamba hili.

### 1.3.4 Njia Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** desturi za Taarifa za Kamati za Bunge zimetambua umuhimu wa kuainisha njia zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi inayoripotiwa. Kwa msingi huo, naomba kubainisha njia zilizotumika wakati wa uchunguzi na tathmini ya mgogoro huu.
Njia hizo ni:-

(i) Mapitio ya Sera, Sheria na miongozo inayohusu masuala ya ardhi nchini na Mapitio ya Nyaraka mbalimbali zinazohusiana na Shamba la Malonje;

(ii) Mahojiano na wadau mbalimbali waliobainika kuwa na taarifa, uelewa na maoni yanayoweza kufanikisha kazi ya Kamati. Wadau hawa walijumuisha walalamikaji (Wananchi wa vijiji na viongozi wao), Mwekezaji (Bodi ya Wadhamini wa Efatha), Viongozi wa Mkoa wa Rukwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na
Waziri wa Mifugo na Uvuvi; na

(iii) Ziara kwenye shamba la Malonje pamoja na vijiji sita kati ya vinane vinavyozunguka shamba hilo. Vijiji hivyo ni Sikaungu, Msandamuungano, Songambele Azimio, Mawenzusi, Ulinji na Isesa.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI NA MAELEZO YA MATOKEO

### 2.1 Maelezo

**Mheshimiwa Spika,** Mapitio ya Sera, Sheria na Nyaraka yalifanyika ili kufanikisha matokeo ya uchunguzi na tathmini ya Kamati. Mahojiano na ziara uwandani vililenga kupata

utoshelevu wa matokeo kiasi cha kuwa na mapendekezo yanayokidhi utatuzi wa mgogoro katika shamba la Malonje. Sera zilibainika kutoa miongozo muhimu katika utatuzi wa mgogoro huu. Sheria zimeonekana kuwa na masharti ya kisheria yanayofaa kuzingatiwa ili kutatua mgogoro katika shamba la Malonje.

### 2.2 Uchambuzi wa Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa urahisi wa mtiririko, naomba kubainisha uchambuzi na matokeo kwa kila hadidu ya rejea kama ifuatavyo:-

#### 2.2.1 Kubaini Eneo la Shamba la Malonje Lilipoanzia

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchambuzi wake ilibaini ilizingatia kuwa kusudio katika hadidu hii ni historia ya kuanzishwa kwa shamba la Malonje kwa kuhusianisha na mgogoro kati ya Mwekezaji na vijiji vinavyozunguka shamba hilo. Kwa kuzingatia hadidu hii, Kamati ilichambua nyaraka mbalimbali kutoka kwa Serikalini na kwa Mwekezaji, ilipokea maelezo ya mashahidi na marafiki wa Kamati na vilevile ilitembelea shamba hilo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umeonesha mambo mbalimbali kama ifuatavyo:-

**(a) Umiliki na Matumizi ya Awali ya Shamba la Malonje**

**Mheshimiwa Spika**, nyaraka mbalimbali zinaonesha kuwa, tangu mwaka 1930 wakati wa utawala wa kikoloni, Shamba la Malonje lilimilikiwa na mwekezaji Mlowezi aliyeitwa George Damm na baadaye mkewe Bi. Isle Damm. Wakati huo, shamba lilianza kwa ukubwa wa **ekari 300** na kuongezwa ukubwa katika nyakati tofauti tofauti likitumika kwa kilimo na baadaye ufugaji. Aidha, matokeo ya mahojiano na Wazee wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo yanaendana na kumbukumbu hizo. Kufanana kwa kumbukumbu na

maelezo ya pande hizi mbili kuhusu historia hiyo, ni dalili ya uthabiti wa historia iliyoelezwa.

**(b) Umiliki wa Shamba kuanzia Mwaka 1967**

**Mheshimiwa Spika,** umiliki wa shamba hili ulihama kutoka kwa mtu binafsi, Bi. Isle Damm na kuwa chini ya Serikali, mwaka 1967. Kuhama kwa umiliki huo kulitokana na aliyekuwa mmiliki kulitelekeza shamba hilo kufuatia Azimio la Arusha. Mwaka 1971 Serikali ililichukua shamba hilo na baadaye likakabidhi kwa taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo Kampuni ya Taifa ya Kilimo (NACO) ambayo ililirithisha shamba hilo kwa Kampuni za Ranchi za Taifa (NARCO) ambayo nayo ililirithisha kwa na Kampuni ya Ufugaji wa Ngombe wa Maziwa (DAFCO). Hadi wakati huu, shamba lilikuwa na ukubwa wa ekari 47,520.

**(c) Wananchi Kutumia Shamba Kabla ya kuuzwa kwa Mwekezaji Mwaka 2007**

**Mheshimiwa Spika,** nyaraka muhimu na matokeo ya mahojiano kwa pamoja vinaonesha kwamba, tangu enzi za Bi Isle Damm, wananchi walikuwa wakitumia sehemu ya shamba hilo kwa makazi, kilimo na ufugaji. Mwaka 1977, Serikali iliunda Kamati ndogo ya Wilaya ajili ya iliyopendekeza kuwa NARCO ipunguze ekari 10,007 na zigawiwe kwa baadhi ya vijiji vinavyozunguka shamba hilo, jambo ambalo liliridhiwa na NARCO.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika uchambuzi wake haikupata uthibitisho wa utekelezaji kamili wa mapendekezo hayo. Uhakikia ni kwamba, wananchi waliendelea kutumia sehemu ya shamba hilo. Hali hii ni ushahidi kuwa wananchi walihitaji ardhi katika shamba hilo tangu wakati huo.

**(d) Utatuzi wa Migogoro Kabla ya Shamba la Malonje Kubinafsishwa**

**Mheshimiwa Spika,** uchunguzi umeonesha kwamba, migogoro ya shamba hilo ilikuwepo tangu enzi za umiliki wa Bi Damm na wakati wa NACO na NARCO. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kutatua migogoro hiyo, ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu kutovamia au kumega sehemu ya shamba hilo. Hata hivyo, hatua hizo hazikuzaa matunda na wananchi waliendelea kutumia shamba hilo kwa shughuli za kilimo na ufugaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hatua za Serikali za kuelemisha wananchi kutofanikiwa kuzuia mgogoro ni ishara kwamba, hazikuwa na uhalisia au hazikugusa kiini cha msingi cha tatizo (*root cause*), Hivyo, kufanya mgogoro kuendelea kuwepo.

**2.2.2 Kubaini Mipaka Halisi ya Shamba la Malonje na Vijiji Vinalivyozunguka**

**Mheshimiwa Spika,** hadidu ya pili iliitaka Kamati kubaini mipaka halisi ya shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka. Kamati katika uchambuzi wake ilibaini kuwa lengo la hadidu hii ni kupata uhalisia wa madai kwamba, sehemu ya ardhi ya vijiji inaingiliana na mipaka ya shamba la Malonje. Kwa kuongozwa na hadidu hiyo, Kamati imepitia nyaraka zilizowasilishwa kutoka Serikalini na kwa Mwekezaji na kuoanisha na matokeo ya mahojiano na ziara uwandani. Uchambuzi wa yote hayo ulijumuisha kutumia ufafanuzi wa kitaalam kuhusu ramani na uchoraji ili kupata picha halisi ya mipaka na shida inayojitokeza katika mgogoro huu.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchunguzi huo yanaonesha kama ifuatavyo:-

**(a) Shamba Kuzungukwa na Vijiji**

**Mheshimiwa Spika**, Shamba la Malonje lilikuwa linazungukwa na vijiji mbalimbali tangu enzi za mkoloni. Vijiji vya Malonje, Kaoze, Ntuki na Sikaungu ni miongoni mwa vijiji vilivyokuwepo tangu miaka ya 1960. Barua ya tarehe 15 Januari, 1964 kutoka kwa *Division Executive Officer Local Court* Sumbawanga kwenda kwa *Area Secretary District Office* Sumbawanga ni ushahidi wa kuwepo kwa vijiji jirani na Shamba la Malonje. Sehemu ya barua hiyo inaeleza:-

**Nukuu**: "*… ni kweli nimekuta watu wa miji ifuatayo wameshagawana shamba hilo na kuanza kulima kama ifuatavyo: - kwa upande wa Kaskazini wa shamba ni Kaoze Village, kwa upande wa kusini wa shamba - Ntuki Village na kwa upande wa mashariki wa shamba ni Sikaungu village*." **Mwisho wa kunukuu**.

**Mheshimiwa Spika**, ramani ya shamba ya mwaka 1997 iliyosajiliwa kwa Na. 30573 ya tarehe 8/12/1997 inaonesha uhalisia wa sasa ambapo shamba hilo linapakana na vijiji nane. Upande wa Kaskazini - Kijiji cha Kinamwanga, Kaskazini mashariki - kijiji cha Mawenzusi, Kusini - Kijiji cha Sikaungu, Kusini Mashariki - kijiji cha Msandamuungano, Mashariki - kijiji cha Songambele Azimio, Magharibi - gereza la Mollo na Kijiji cha Malonje, na Kaskazini Magharibi - Vijiji vya Ulinji na Isesa.


**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya baadhi ya wazee wa vijiji vinavyozunguka shamba, yalionesha kuwepo kwa vijiji hivyo kwa miaka mingi licha ya kwamba upimaji wa ardhi ya vijiji hivyo ulifanyika mwaka 2009. Uchambuzi unaonesha kuwa, vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje si vipya bali vilikuwepo tangu shamba lilipokuwa likimilikiwa na familia ya Damm. Aidha, vijiji hivyo vimeendelea kuongezeka ukubwa kutokana na ongezeko la watu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, ni wazi kwamba, ongezeko la watu kwenye vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje limekuza msukumo wa mahitaji ya ardhi inayofaa kwa uzalishaji kwenye vijiji hivyo. Hali hii inachangia kuwepo kwa mgogoro wa ardhi kati ya Mwekezaji kwenye shamba la hilo na wananchi wa vijiji hivyo ikizingatiwa kuwa, wengi wa wananchi hao ni wazawa wa vijiji hivyo na waliwakuta wazazi wao wakitumia shamba hilo.

**(b) Mipaka ya Shamba na Vijiji Vinalivyozunguka**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa ramani ya Shamba la Malonje ya mwaka 1997, ramani ya shamba la Mwekezaji ya mwaka 2008 na ramani ya ardhi ya vijiji vya Sikaungu, Songambele Azimio na Msandamuungano za mwaka 2009. Kwa kutumia wataalam wa Ramani na upimaji, Kamati ililinganisha ramani hizo kwa kuziweka pamoja na kuzingatia kodineti za ramani *(coordinate points*). Kwa hatua hiyo Kamati ilipata picha halisi ya mipaka ya shamba na mipaka ya vijiji vinavyozunguka shamba hilo na mwingiliano wa mipaka hiyo. Kwa rejea ya muonekano huo, Kielelezo Na. 01 kinaonesha ramani hiyo.

**Kielelezo NA. 1: Ramani ya Shamba Sikaungu, Msandamuungano na**




**Chanzo:** ***Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa kielelezo hicho, sehemu ya ardhi ya shamba inaonekana ipo ndani ya maeneo ya vijiji. Kwa mfano, sehemu ya shamba la Mwekezaji inaonekana kuwa ndani ya eneo la kijiji cha Sikaungu. Hali hiyo pia imeonekana kwa vijiji vya Msandamuungano na Songambele Azimio. Mipaka ya vijiji vya Sikaungu, Msandamuungano na Songambele Azimio inaingiliana na mipaka ya Shamba la Malonje na Shamba la Magereza kwa jumla ya **hekta 3,357.16**.

**Mheshimiwa Spika**, jumla ya **hekta 2,844.75** za ramani ya ardhi ya vijiji zinaingiliana mipaka na shamba la Malonje na **hekta 512.41** ya ramani ya ardhi ya vijiji zinaingiliana mipaka na shamba la gereza la Mollo. Kwa kuzisoma ramani kwa pamoja, Kamati imeweza kutathmini madai ya wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje kuwa sehemu ya ardhi yao imejumlishwa kwenye ardhi ya shamba hilo. Aidha, ili kujiridhisha zaidi, Kamati ilifika uwandani ambapo ilijionea alama za mipaka (Beacons) za shamba la Mwekezaji zikiwa ndani ya eneo la kijiji cha

Sikaungu na alama za mipaka ya kijiji cha Sikaungu zikiwa ndani ya shamba la Mwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi aliieleza Kamati kwamba, ramani za ardhi ya vijiji inayotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114 ni kwa ajili ya kuweka mipaka ya utawala wa vijiji na si kumilikisha vijiji hivyo ardhi inayohusika. Maelezo kama hayo yalitolewa pia na Kamishna wa Ardhi mbele ya Kamati mnamo tarehe 20 Julai, 2024 kama ifuatavyo:-

**Nukuu**: "*… ile ni ardhi ya jumla na ina usimamizi tofauti, lakini haiwezi kuwa sehemu ya ardhi ya kijiji kwa sababu yenyewe imekuwepo kabla hata ya Sheria ya Ardhi ya Kijiji haijaja. Mhe. Mwenyekiti kwa hiyo, niseme tu kwamba, mipaka ya kijiji imewekwa kwa ajili ya kuwapa mamlaka viongozi wa vijiji kujua mipaka ya vijiji vyao na waweze kusimamia maslahi yaliyoko ndani ya kijiji chao. Lakini haioneshi kwamba, kuna muingiliano wa upimaji juu ya upimaji…*" **Mwisho wa Kunukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, tathmini inaoensha kwamba, Mwekezaji anatafsiri mwingiliano huo wa mipaka sawa na tafsiri iliyotolewa na Waziri na Kamishna wa Ardhi. Pamoja na hivyo, ni ukweli kwamba, wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba vikiwemo vijiji vya Sikaungu, Songambele Azimio na Msandamuungano kwa muda mrefu wanatambua mipaka ya vijiji vyao kwa kutumia alama za asili kama vile mito ambayo ipo kwenye ramani zilizosajiliwa mwaka 2009. Kwa msingi huo, wameendelea kuamini na kutambua kuwa sehemu ya shamba iliyo ndani ya mipaka ya kijiji ni ardhi ya vijiji vyao.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7(1) (a - e) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114 kinaeleza kuwa, ardhi ya vijiji ni ardhi yote iliyo ndani ya mipaka ya kijiji kilichosajiliwa

ambayo si ardhi ya akiba au ardhi ya jumla. Aidha, kifungu cha 2 cha sheria hiyo kimetafsiri ardhi ya jumla kuwa ni ardhi ya umma ambayo si ardhi ya akiba au ardhi ya kijiji. Kwa msingi huo, uelewa tofauti wa tafsiri ya ardhi ya kijiji na mipaka ya kiutawala ya vijiji umechangia mgogoro uliopo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(6) cha Sheria hiyo, Kamishna wa Ardhi anayo mamlaka ya kutoa vyeti vya ardhi ya vijiji kwa kuzingatia mipaka iliyoainishwa ya ardhi ya kijiji au mipaka iliyokubalika kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji au sheria nyingine au kwa taratibu za kiutawala zinazotambulika.

**(c) Mahitaji ya Ardhi kwa Vijiji Vinavyozunguka Shamba la Malonje**

**Mheshimiwa Spika,** uelewa kuhusu mipaka unategemea mtazamo unaotokana na mambo mbalimbali. Serikali kwa upande wake inatekeleza sera na kusimamia sheria na wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba kwa upande wao wanatafsiri mipaka kulingana na mahitaji waliyonayo pamoja na sheria zilizopo. Ili kuzingatia mambo hayo yote, Kamati ilihitaji kubaini mahitaji ya ardhi kwa vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi wa nyaraka zilizowasilishwa kutoka mamlaka mbalimbali za Serikali, maelezo ya mashahidi na marafiki waliofika mbele ya Kamati, ziara ya Kamati uwandani, maelezo ya Mwekezaji na maelezo ya wananchi wa baadhi ya vijiji waliyoyatoa mbele ya Kamati, yamebainika mambo yafuatayo:-

(i) Ongezeko la ukubwa wa ardhi katika shamba la Bi. Isle Damm mwaka 1946 hadi 1955 na Kampuni ya NACO kati ya mwaka 1968 hadi 1974 kutoka ekari 300 hadi ekari 47,520 mtawalia lilisababisha baadhi ya vijiji kukosa ardhi kwa ajili ya makazi, kilimo na

kuchungia mifugo. Tathmini ya Kamati imeonesha kuwa ongezeko hilo la ardhi lilijumuisha maeneo yanayotumiwa na wananchi. Hali hiyo ilisababisha mgogoro kati ya Mwekezaji na wananchi wa vijiji vinavyolizunguka shamba hilo, hali inayoendelea hadi sasa.

(ii) Ongezeko la watu kwenye vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje limeongeza mahitaji ya ardhi kwa ajili ya makazi, kilimo, na kuchungia mifugo. Uchunguzi ulionesha kuwa ongezeko hilo la watu limechangia kwa kiasi kikubwa mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na Mwekezaji.

(iii) Sehemu ya ardhi inayotambuliwa kuwa ndani ya shamba la Mwekezaji ipo ndani ya mipaka ya baadhi ya vijiji vinavyolizunguka shamba jambo linalosababisha changamoto ya kisheria kuhusu umiliki na matumizi ya ardhi hiyo. Katika baadhi ya maeneo katika vijiji vya Sikaungu, Songambele Azimio na Msanda muungano, alama za mipaka ya shamba la Mwekezaji zimewekwa ndani ya mipaka ya vijiji na alama za mipaka ya vijiji zimewekwa ndani ya shamba la Mwekezaji na hivyo kusababisha muingiliano wa mipaka.

(iv) Kwa miaka mingi, wananchi katika vijiji vinavyozunguka shamba wamekuwa wakitumia ardhi ya shamba la Malonje inayodaiwa kuwa sehemu ya vijiji hivyo. Shughuli kubwa wanazozifanya katika ardhi hiyo ni kilimo na makazi na si rahisi kuelewa tafsiri ya mipaka ya ardhi ya vijiji na ardhi ya jumla inayotolewa na Mwekezaji na wataalamu wa Serikali.

(v) Mwekezaji amekuwa akikodisha sehemu ya shamba kwa wanavijiji na wananchi wengine. Wananchi

hupaswa kutoa shilingi elfu kumi kulipia fomu ya maombi ya kukodi shamba na baada ya mavuno kutoa gunia moja la mazao yao kwa kila ekari.

**Mheshimiwa Spika,** jambo kubwa la kuzingatia ni kuwa mwenye haki ya ardhi hapaswi kuporwa haki hiyo na wananchi kwa ujumla wanastahili kuwezeshwa kutumia nguzo kuu ya uzalishaji mali kwa namna inayowezesha ustawi wao. Hivyo, suluhu ya kudumu inayozingatia uhalisia wa hali ya ardhi ya shamba la Malonje na mahitaji ya ardhi kwa wananchi wa vijiji vinavyolizunguka shamba hilo ni jambo la lazima.

### 2.2.3 Taratibu Zilizotumika katika Kuongeza Ukubwa wa Shamba la Malonje

**Mheshimiwa Spika,** hadidu ya tatu iliitaka Kamati kubaini iwapo taratibu za uongezaji wa eneo zilifuatwa katika ongezeko la ukubwa wa shamba la Malonje. Kwa madhumuni ya kuifanyia kazi hadidu hii, Kamati ilizingatia uwezekano wa ongezeko la ukubwa wa shamba kuwa miongoni mwa sababu za mgogoro unaoendelea. Ili kufanikisha azma hiyo, Kamati ilipitia nyaraka mbalimbali zinazohusu ongezeko la ukubwa wa eneo la shamba la Malonje. Mapitio ya nyaraka hizo yalifanyika kwa kuzingatia historia ya kuongezeka kwa shamba ambayo inayoonesha kama ifuatavyo:-

#### (a) Namna Shamba Lilivyoongezeka kwa Nyakati Tofauti

**Mheshimiwa Spika,** nyaraka zinaonesha kwamba, ukubwa wa shamba la Malonje umekuwa ukibadilika kwa vipindi mbalimbali tangu likiwa chini ya umiliki wa Bi. Isle Damm na badaye Taasisi za Serikali. Njia zilizotumika katika za ongezeko la ukubwa wa shamba hilo imeelezwa ni pamoja na utwaaji wa maeneo ya vijiji au ya wanavijiji katika awamu tofauti tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** mara ya kwanza shamba hilo liliongezeka ukubwa kati ya mwaka 1946 hadi mwaka 1955 kutoka **ekari 100** hadi **ekari 6,248** likiwa chini ya umiliki wa Bi. Damm. Mara ya pili, sehemu ya shamba hili liliongezeka ukubwa mwaka kati ya mwaka 1968 hadi 1973 kutoka **ekari 2,541** hadi **ekari 47,520** likiwa chini ya umiliki wa NACO.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 1980 shamba lilipunguzwa ukubwa kutoka **ekari 47,520** hadi ekari **37,513**. Aidha, ramani ya mwaka 1997 ilionesha shamba lina ukubwa wa **ekari 45,692.5**. Mwaka 2004 wakati Wizara ya Mifugo inalikabidhi shamba kwa Serikali ya mkoa wa Rukwa ilieleza kuwa ukubwa wa shamba hilo ni **ekari 37,500.** Kwa mujibu wa uhakiki uliofanyika mwaka 2017, ukubwa wa shamba ulikuwa **ekari 34,370**.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kwamba, mabadiliko ya ukubwa wa shamba kwa nyakati tofauti hayaelezeki kwa uhakika. Ukubwa wa eneo uliokuwa ukiongezeka unatofautiana kati ya nyaraka moja na nyaraka nyingine na hivyo kukosekana kwa uhakika na uhalisia uwandani. Uchambuzi umeonesha kwamba, hali hii ni dalili kuwa uamuzi kuhusu maeneo ya shamba hilo umekuwa ukifanyika bila misingi ya uhalisia. Jambo hilo nalo ni miongoni mwa sababu za uwepo wa mgogoro kati ya shamba la Mwekezaji na vijiji vinavyolizunguka.

**(b) Taratibu zilizotumika katika kuongeza ukubwa wa shamba la Malonje**

**Mheshimiwa Spika,** hakuna uthibitisho wa kufuatwa kwa taratibu katika ongezeko la ukubwa wa shamba kabla ya uhuru, wakati wa umiliki wa Taasisi za Serikali na hata likiwa chini ya Mwekezaji wa sasa. Kwa ujumla nyaraka hazithibitishi njia zilizotumika na wala matokeo ya mahojiano hayatoi ushahidi wa uhakika. Mathalani, mwaka 1955, Bi. Isle Damm aliongeza shamba kutoka

**ekari 100** hadi **ekari 6,248** lakini hakuna nyaraka yoyote inayothibitisha kuzingatiwa kwa taratibu za kuongeza ukubwa wa shamba. Kwa tathmini hiyo, kukosekana kwa uthibitisho wa misingi ya ongezeko la shamba hadi sasa ni jambo lililorithiwa na likaendelea hata kwa ongezeko lilijitokeza tangu kuuzwa kwa shamba hilo na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

**Mheshimiwa Spika,** kutoka mwaka 1968 -1973 NACO iliongeza ukubwa wa shamba kutoka **ekari 2,807** hadi kufikia **hekari 47,520**, lakini hakuna nyaraka zinazoonesha kufuatwa kwa utaratibu, bali upo waraka mmoja unaoonesha idadi ya watu 9 wa kijiji cha Mawenzusi waliostahili kulipwa fidia. Watatu kati ya hao walisaini na watu sita hawakusaini. Halikadhalika, taarifa hiyo haielezi ukubwa wa eneo lillilotwaliwa kwa kila mwanakijiji wala maelezo kuhusu fidia na ukubwa wa maeneo yaliyotwaliwa katika vijiji vingine vinavyozunguka shamba hilo.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo hayo yanaleta mashaka kuhusu kufuatwa kwa taratibu za uongezaji wa ukubwa wa shamba. Dosari hizo ni miongoni mwa viashiria vya kutokufuatwa kwa taratibu katika kuongezeka kwa ukubwa wa shamba la Malonje. Mashaka kuhusu utaratibu uliotumika kuongeza ukubwa wa shamba yanachangia kuendelea kuwepo kwa mgogoro wa ardhi kwenye shamba la Malonje.

**(c) Mauzo ya Hekta 10,000 za Shamba la Malonje**

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 2007 Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilitangaza kuuza **hekta 3,000** ambazo zilikuwa na miundombinu ya ufugaji pamoja na mifugo. Kwa mujibu wa maelezo ya marafiki na mashahidi katika vijiji vinavyozunguka shamba, eneo hili lilikuwa limezoeleka kwa wananchi kuwa ndio shamba la Malonje. Hata hivyo Mwekezaji alipendekeza kununua

**hekta 10,000** kwa bei ya shilingi **milioni 600** na kukubaliwa na Mkoa pasipo umma kutangaziwa wala kufanya uthamini wa shamba.

**Mheshimiwa Spika**, mkataba wa mauzo ya shamba hilo unaonesha kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilimuuzia mwekezaji shamba lenye ukubwa wa hekta 10,002 kabla ya mipaka yake kuhakikiwa jambo ambalo ni kinyume na taratibu za ununuzi na uuzaji wa ardhi ya umma.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo inaonesha kuwa upatikanaji wa shamba hilo kwa ukubwa uliotajwa kwenye mkataba wa mauziano haukuzingatia ipasavyo taratibu stahiki. Aidha, namna zoezi la uuzaji wa shamba lilivyoendeshwa imechangia kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa mgogoro kati ya Mwekezaji na wananchi wa vijiji vinavyolizunguka shamba hilo. Mathalani, kwa shamba hilo kutokuwa limepimwa ili kubaini iwapo lina ukubwa wa **hekta 10,000** na kwamba mipaka yake ni halisi, inasababisha wasiwasi mkubwa wakati wa matumizi yake baada ya kuuzwa na hivyo kuchangia mgogoro wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, tathmini inaonesha kuwa, uuzaji wa **hekta 10,002** pasipo umma kutangaziwa, kutozingatiwa kwa umuhimu wa kulipima kabla ya kuuza na kutokushirikisha wadau muhimu wakiwemo wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo, ni miongoni mwa mambo yanayosababisha wananchi kuwa na mtazamo unaodumisha mgogoro baina yao na Mwekezaji. Wananchi wamekuwa na imani kwamba, Mwekezaji amejiongezea ukubwa wa shamba hadi kwenye ardhi ya vijiji vyao waliyokuwa wakiitumia kwa kilimo na mifugo kwa miaka mingi.  Kwa hali hiyo, suluhu ya kweli ya mgogoro huo inahitajika namna ili kurekebisha madhara ya kutokuzingatiwa kwa taratibu stahiki.

**Mheshimiwa Spika**, uuzaji wa shamba hilo pasipo kufanya uthamini ni kiashiria kwamba, shamba liliuzwa kwa bei ndogo kuliko thamani halisi. Hali hiyo, inaongeza wasiwasi wa wananchi kuhusu kuzingatiwa kwa maslahi ya umma wakati wa uuzaji. Ushahidi wa bei ndogo unadhihirishwa na uamuzi wa Mwekezaji kuweka dhamana shamba hili na kukopa **shilingi 3,001,905,000** ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya kupata hati miliki ya shamba alilolinunua kwa shilingi **milioni 600**. Mkopo aliochukua Mwekezaji kwa kipindi cha mwaka mmoja baadaye, una thamani iliyoongezeka kwa **asilimia 400** ikilinganishwa na mauzo. Bila shaka, jambo hili linaleta wasiwasi iwapo kuuza shamba kwa **shilingi milioni 600** kulizingatia thamani halisi ya shamba hilo.

**(d) Utaratibu wa Mauzo na Mgawanyo wa Hekta 3,748**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Mwekezaji kuuziwa hekta 10,002, zilibaki hekta 3,748 ambazo zilikusudiwa kuuzwa kwa wafugaji wadogo kwa vitalu vya hekta 50 kwa mfugaji mmoja. Mapitio ya nyaraka muhimu na matokeo ya mahojiano yanaonesha kuwa katika hekta hizo 3,748, Gereza la Mollo liligawiwa hekta 1,139 na hekta 2,609 zilizobaki ziligawanywa katika vitalu 51 ambavyo viliuzwa kwa wananchi kutoka maeneo mbalimbali wakiwemo wafanyabiashara, viongozi wa kisiasa, viongozi wa Serikali ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na familia ya Mwekezaji. Aidha, bei ya vitalu hivi ilikuwa ni **shilingi 2,500,000**.

**Mheshimiwa Spika,** wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba walionesha juhudi za kununua vitalu hivi kwa ajili ya kilimo. Hata hivyo, lengo lao halikufanikiwa kwa kuwa masharti ya uuzaji wa vitalu hivyo yalitaka ununuzi uwe kwa ajili ya ufugaji pekee ilhali wananchi hao wamezoea shughuli za kilimo. Kwa tathmini ya jumla kuhusu masharti hayo, uhalisia wa shughuli za wananchi hao haukuzingatiwa wakati wa uuzaji wa vitalu. Ushahidi wa

masharti haya kukosa uhalisia ni uwepo wa watu wengine waliouziwa vitalu kwa masharti ya kufuga kisasa lakini wanavitumia kwa ajili ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa kuuza vitalu vilivyotokana na shamba la Malonje, ulipuuza maazimio ya kikao cha tarehe 13 Juni, 2008 cha Kamati ya Fedha na uongozi cha Baraza la Madiwani wa Manispaa ya Sumbawanga. Madiwani waliazimia wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba wapewe bure vitalu vilivyopo kwenye maeneo yao, lakini utekelezaji haukufanyika.

**(e) Ushirikishwaji Wakati wa Mchakato wa Mauzo ya Shamba la Malonje**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa nyaraka zilizowasilishwa pamoja na maelezo ya baadhi ya mashahidi na marafiki wa Kamati umebainisha kuwa mchakato wa mauziano na upimaji wa shamba la Malonje haukushirikisha wadau muhimu wakiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na vijiji vinavyozunguka shamba vikiwemo Sikaungu, Msandamuungano na Songambele Azimio. Baada ya mauzo ya shamba kufanyika, iligundulika kuwa sehemu ya shamba inaangukia katika mipaka ya utawala ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Hivyo, iliazimiwa kwamba halmashauri hiyo ipate mgao wa fedha **shilingi milioni 200.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa maelezo ya Manispaa ya Sumbawanga na ushahidi wa Mkuu wa Mkoa Mstaafu Balozi Daniel Ole Njoolay, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilipewa **shilingi milioni 200**, lakini nyaraka za fedha zilizowasilishwa zinaonesha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilipokea **Shilingi milioni 50** tu badala ya **milioni 200** kama ilivyoahidiwa. Tathmini inaonesha kwamba, kutoshirikiswa kwa Halmashauri ya wilaya ya Sumbawanga na vijiji vinavyozunguka shamba

hilo kulisababisha kupuuzwa kwa mahitaji ya ardhi kwa vijiji hivyo wakati shamba la Malonje linauzwa.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo inachangia uhusiano mbaya baina ya vijiji, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na hivyo kuleta changamoto katika utatuzi wa migogoro inayoibuka kuhusiana na shamba hilo. Vievile, sintofahamu ya mgao wa fedha za mauzo ya shamba ni ishara kwamba kuna matumizi mabaya ya fedha za umma zilizotokana na mauzo ya shamba la Malonje.

**(f) Maelekezo ya Baraza la Mawaziri kuhusu Mgawanyo na Matumizi ya Shamba la Malonje**

**Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mawaziri lilielekeza iliyokuwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kusimamia ubinafsishaji wa shamba la Malonje kwa kuligawa katika vipande vya hekta 50 kwa wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa. Wizara hiyo ilikabidhi shamba hilo kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa kupitia barua rasmi kwa ajili ya ubinafsishaji kwa kuzingatia maelekezo ya Baraza la Mawaziri.

**Mheshimiwa Spika,** barua hiyo iliitaka Ofisi ya Mkoa kuwasiliana na Wizara ikiwa kutatokea changamoto katika utekelezaji wa maagizo yake. Hata hivyo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Rukwa haikuwahi kufanya hivyo licha ya kukabiliana na changamoto ya ubinafsishaji wa shamba kwa mgawo wa hekta 50 kwa wafugaji.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonesha kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa ilikiuka maelekezo hayo na badala yake iliamua kuuza hekta 10,002 kwa Mwekezaji na hekta 3748 zilizobaki ziliuzwa mbalimbali na kugawiwa kwa Gereza la Mollo. Wakati wa mahojiano na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa wakati huo, Mhe. Balozi Daniel Ole Njoolay, aliulizwa kama alizingatia maelekezo ya

barua ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, ambayo ilikuwa na maelekezo ya Baraza la Mawaziri. Mhe. Daniel ole Njoolay alieleza kwamba, hakuwahi kuiona barua hiyo bali alitaarifiwa na wasaidizi wake kuwa Ofisi ya Mkoa imepewa mamlaka ya kusimamia uuzaji wa shamba hilo kutoka Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mazingira ya uuzaji wa shamba hilo yalivyokuwa, ikiwemo Mkuu wa Mkoa kuongoza vikao vya majadiliano na Mwekezaji na kutoa maelekezo mbalimbali kwa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kuhusu uuzaji wa shamba hilo kama vile kuelekeza eneo lililobaki lipimwe katika vitalu vyenye ukubwa wa hekta 50 na kuviuza kwa wafugaji wadogo, inaashiria kwamba Mkuu huyo wa Mkoa alikuwa anafahamu barua hiyo tofauti na maelezo yake kuwa hakuwa anaifahamu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipomhoji Waziri wa Mifugo na Uvuvi kuhusu kutokusimamia ubinafsishaji wa shamba la Malonje, alieleza kuwa Wizara yake haikuwa na wajibu huo kwa kuwa ilikabidhi shamba hilo kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa. Mtazamo wa Kamati ni kwamba, Wizara haikutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuwa ndiyo iliyopewa maelekezo na Baraza la Mawaziri na ilipaswa kupeleka mrejesho kuhusu suala hili.

**Mheshimiwa Spika**, uchunguzi ulionesha kuwa, Serikali ilifahamishwa kuhusu viongozi wa Mkoa wa Rukwa na wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kukiuka maelekezo ya Baraza la Mawaziri lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Serikali. Hali hii inaongeza mashaka kuhusu uthabiti wa hatua na juhudi za Serikali katika kutatua mgogoro huu. Iwapo Serikali haitatoa msukumo madhubuti katika utatuzi huu, mgogoro utaendelea kuwepo na wananchi wa vijiji vinavyohusika

wataendelea kuamini kuwa Serikali haijaweza kuwasaidia kutatua mgogoro baina yao na Mwekezaji.

### 2.2.4 Dalili za Uwepo wa Vitendo vya Uvunjifu wa Haki za Binadamu

**Mheshimiwa Spika**, hadidu ya nne iliongoza Kamati kwenye kubaini iwapo kuna dalili za vitendo vya uvunjifu wa Haki za Binadamu vinavyodaiwa kufanywa na walinzi wa shamba la Malonje, na iwapo vitendo hivyo vinatokana na miongozo ya wamiliki wa shamba hilo. Ili kutekeleza jukumu lake kulingana na hadidu hiyo, Kamati ilichunguza matamko, maazimio na mikataba ya kimataifa inayohusu haki za binadamu pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Nia ilikuwa ni kujenga msingi wa matokeo ya kuifanyia kazi hadidu hiyo.

#### (a) Tafsiri ya Haki za Binadamu

**Mheshimiwa Spika**, Tafsiri ya haki za binadamu ilihitaji kuzingatiwa ili kujielekeza kwenye ukweli kuhusu madai yaliyotolewa kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu. Umoja wa Mataifa umetafsiri haki za binadamu kuwa ni haki za asili kwa kila binadamu bila ubaguzi wa rangi, jinsia, utaifa, lugha, dini au hadhi yoyote. Haki hizi zimegawanyika katika makundi matatu: haki za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Mwaka 1984, haki za binadamu ziliingizwa na kuwa sehemu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inatambua haki za binadamu na usawa katika Sehemu ya Tatu kuanzia Ibara ya 12 hadi ya 24.

#### (b) Vurugu katika Shamba la Mwekezaji

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa katika nyakati tofauti, kumekuwepo vurugu kati ya walinzi wa mwekezaji na wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje. Mathalani, kumekuwepo na matumizi ya nguvu kupita kiasi ikihusisha matumizi ya silaha za moto upande wa

walinzi wa Mwekezaji na silaha za jadi kwa upande wa wananchi. Matokeo ya vurugu hizo ni mlinzi mmoja wa mwekezaji kuuawa na wananchi kujeruhiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishuhudia alama za majeraha kwa wananchi ambapo pia ushahidi huo ndiyo risasi. Wanavijiji:-

(i) Ndg. Festo Kamwanga aliyepigwa risasi kifuani, shavuni na mguuni;

(ii) Ndg. Eliud Cosmas Kauzeni aliyepigwa risasi kichwani na begani na anaendelea kuishinazo kichwani hadi sasa;

(iii) Ndg. Dickson Charles Simkonde aliyepigwa risasi tumboni;

(iv) Ndg. Nuru Togwa aliyekatwa masikio yote mawili; na

(v) Ndg. Martin Kazikupenda Mpisi aliyevunjwa miguu na sasa amekuwa na ulemavu wa kudumu uliothibitishwa kwa nyaraka za hospitali.

Wanavijiji waliopigwa risasi walithibitisha kuwa walinzi wa Mwekezaji waliowapiga waliotoa ushahidi mbele ya Kamati ni pamoja na:-

**Mheshimiwa Spika,** Vurugu hizi zinaashiria uvunjifu wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi na kumiliki mali. Aidha, tatizo la uhaba wa ardhi kwa ajili ya uzalishaji ikilinganishwa na mahitaji linachangia mivutano na misuguano baina ya wananchi na Mwekezaji, hatimaye kutokea kwa vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu.

**(c) Vitendo vya Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia kwa Wanawake**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwepo kwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake katika vijiji vya Sikaungu, Msandamuungano, Mawenzusi, Isesa, na Ulinji. Wanawake 7 walieleza kutendewa vitendo hivyo kwa vipindi tofauti na walinzi wa mwekezaji. Aidha, wanawake hao walieleza kuwa walikamatwa na kupelekwa katika eneo la majumba mawili ndani ya shamba hilo na kufanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia ikiwemo kubakwa. Hata hivyo, wanawake hao walikiri kutoripoti matukio hayo polisi kutokana na aibu na hofu ya kuachwa na waume zao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kumhoji Msimamizi wa kitengo cha ulinzi wa shamba la Mwekezaji ambaye alikiri kwamba, huwakamata watu wanaopita shambani bila ruhusa na kuwahifadhi katika eneo lao maarufu kwa jina la majumba mawili. Kamati ilipata fursa pia ya kufika katika eneo hilo la Majumba Mawili. Tathmini ya Kamati kwa maelezo ya wananchi pamoja na mazingira ya eneo husika ni kwamba upo uwezekano wa tuhuma hizo za wananchi kuwa na ukweli, jambo linalohitaji kuthibitishwa zaidi na vyombo vya dola vinavyohusika.

**(d) Matumizi ya Njia za Asili Zinazokatisha Shambani**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa wananchi wamekuwa wakizuiwa kupita kwenye njia za asili zinazokatiza kwenye shamba la Mwekezaji bila kibali cha Serikali ya kijiji. Njia hizo zimekuwa zikitumiwa kwa muda mrefu kwenda maeneo mbalimbali kupata huduma muhimu tangu enzi za ukoloni. Aidha, wananchi walieleza kuwa wamekuwa wakitozwa faini ya **shilingi 50,000** kwa ng’ombe mmoja pindi wanapopitisha mifugo yao katika shamba la Mwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliona kuwa shamba la Mwekezaji ni kubwa na njia za asili zinazopita katika shamba hilo zinarahisisha mawasiliano baina ya kijiji kimoja na kingine. Kuzuiwa kutumia njia hizo na kulazimishwa kutumia njia ndefu ni unyanyasaji na uvunjifu wa haki za binadamu. Aidha, kuzuiwa au kufunga njia hizo za asili kunachangia uhasama na uhusiano mbaya kati ya mwekezaji na wananchi wa vijiji hivyo, jambo ambalo ni mojawapo ya kichocheo cha mgogoro.

**(e) Iwapo Vitendo vya Uvunjifu wa Haki za Binadamu Vinatokana na Miongozo ya Wamiliki wa Shamba Hilo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa shamba la mwekezaji linalindwa na kampuni ya Funguka Security Co. Ltd., inayomilikiwa na Bodi ya Wadhamini wa Efatha Church na Efatha Foundation Ltd. Msimamizi wa kitengo cha ulinzi alieleza kuwa alipatiwa mafunzo ya ulinzi na kampuni hiyo na baadaye kupewa kazi ya ulinzi. Kamati iliona kuwa kwa kuwa shamba linamilikiwa na mwekezaji (Bodi ya Wadhamini wa Efatha Church) na kampuni ya ulinzi ya Funguka Security Co. Ltd iko chini ya kanisa hilo, hali hii inaweza kutafsiriwa kuwa vitendo vya walinzi vinafanywa kwa miongozo ya wamiliki wa shamba.

### 2.2.5 Mambo Mengine Kuhusiana na Mgogoro wa Shamba la Malonje

**Mheshimiwa Spika**, hadidu ya tano na ya mwisho iliitaka Kamati ibaini jambo lingine lolote linalohusiana na mgogoro wa shamba la Malonje iwapo litakuwepo. Katika kuichambua hadidu hii ya rejea, Kamati ilizingatia kuwa lengo la hadidu hii ni kuiwezesha Kamati kutosheleza uchunguzi kwa kuangalia masuala yote yanayohusika katika mgogoro wa shamba la Malonje kwa lengo la kutoa ushauri kamili unaowezesha utatuzi wa mgogoro au hatua za kuchukuliwa ili mgogoro kama huu usijitokeze tena.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekutana na masuala mengine muhimu yanayohusiana na mgogoro huo. Masuala hayo yametokana na uchambuzi wa nyaraka zilizoifikia Kamati pamoja na maelezo ya marafiki na mashahidi wa Kamati. Yaliyojitokeza katika uchunguzi ni kama ifuatavyo:-

**(a) Hatua zilizowahi kuchukuliwa katika kutatua mgogoro baina ya Mwekezaji na Wananchi wanaolizunguka shamba la Malonje**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa hatua mbalimbali zilizowahi kuchukuliwa na serikali katika kutafuta suluhu za mgogoro wa Shamba la Malonje. Mwaka 2012, Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa iliunda Timu ya Wataalamu kuchunguza mgogoro huo na kutoa Mapendekezo. Timu hiyo ilitoa mapendekezo mbalimbali ya utatuzi kwa RCC, ambayo chini ya Mwenyekiti wake, ilimwandikia Mheshimiwa Rais kumjulisha kuhusu kuwepo kwa mgogoro huo na hatua zinazopendekezwa kuchukuliwa. Hali kadhalika, mwaka 2017 Mkuu wa Mkoa wa wakati huo aliunda timu nyingine ambayo nayo ilitoa mapendekezo mbalimbali. Mkuu wa Mkoa huyo aliwasilisha Serikalini mapendekezo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** mojawapo ya matokeo ya kazi ya timu hizo, ni Mwekezaji kukubali kutoka ekari 3000 kwa ajili ya kupunguza tatizo la ardhi kwa vijiji vya Sikaungu, Msandamuungano na Songambele Azimio. Hata hivyo, hatua hii haikufanikiwa kutatua tatizo lililokuwepo kwa kuwa bado wananchi kutoka Kijiji cha Sikaungu wanaamini ardhi hiyo iliyotolewa ni mali yao tangu zamani.

**Mheshimiwa Spika,** hatua nyingine iliyowahi kuchukuliwa ni Serikali kukusudia kufuta umiliki wa shamba la Malonje kwa kutoa ilani ya siku 90 kwa Mwekezaji. Hatua hii ilichukuliwa mwaka 2015 na ililenga kuzingatia maslahi ya

umma kwa kurejesha amani na utulivu kwa wananchi wa vijiji vinavyolizunguka shamba. Hata hivyo mafanikio hayakupatikana kutokana na changamoto za kisheria ambazo zinavuta tafakuri ya kina.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonesha kuwa kulikuwa na makosa ya kitaalam ambayo yalisababisha kutokufikiwa kwa azma ya Serikali. Makosa hayo yalihusu usimamizi mbovu wa Shauri Na. 7 la Mwaka 2015 lililofunguliwa na Mwekezaji dhidi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Shauri hilo lilimalizika kwa pande zinazohusika kusaini Hati ya Maridhiano mwaka 2017 ambayo ilisajiliwa katika Mahakama Kuu Masijala ya Sumbawanga.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi huo, imebainika kuwa aliyepaswa kushtakiwa ni Kamishna wa Ardhi na si Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga. Aidha, masharti ya Hati ya Maridhiano hayakuzingatia masharti ya mkataba wa mauziano ya shamba kwa kueleza kuwa **Mwekezaji asisumbuliwe kuhusu umiliki na matumizi ya shamba**. Kwa dosari hiyo, shamba linaweza kutumika kwa shughuli yoyote na sio kwa ufugaji tu kinyume na makubaliano ya mauziano. Vilevile, ulibainika uwezekano wa saini ya Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga iliyopo kwenye hati ya maridhiano kuwa ya kughushi.

**(b) Uzingatiaji wa Masharti ya Mkataba wa Mauzo ya Shamba la Malonje**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umeonesha kwamba, Mwekezaji hazingatii masharti ya mkataba wa mauziano ya shamba na Hati ya umiliki. Mkataba ulitaka matumizi ya shamba yawe kwa ajili ya ufugaji wa kisasa, lakini Mwekezaji alitumia kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya kilimo zaidi ya ufugaji. Aidha, hali ya shamba inaonesha asilimia ndogo ya matumizi kwa mujibu wa masharti.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa Serikali haikuwa na mikakati madhubuti ya kuhakikisha masharti ya mkataba yanatekelezwa ipasavyo. Ushahidi wa wa matokeo hayo ni hatua ya Serikali kumpatia Mwekezaji hati miliki nyingine mwaka 2021. Hati hiyo ilibadili matumizi ya shamba kutoka kufuga tu na kuwa kilimo, ufugaji na kilimo cha miti bila ya kufuata taratibu za mabadiliko au nyongeza ya matumizi ya shamba.

**(c) Kasi Ndogo ya Uwekezaji Katika Shamba**

**Mheshimiwa Spika,** ni miaka takriban kumi na saba tangu Mwekezaji auziwe shamba hilo na taarifa alizoziwasilisha kwenye Kamati zinaeleza kuwa eneo alililoendelezwa ni **asilimia 41.9**. Hata hivyo, maelezo yaliyotolewa na Kamishna wa Ardhi kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ililiposhughulikia suala hili tarehe 3 Mei, 2024 yalionesha kwamba, kiasi kilichoendelezwa ni **asilimia 4.1**.

**Mheshimiwa Spika,** kutofautiana kwa takwimu kuhusu kiasi kilichoendelezwa kati ya Mwekezaji na Kamishna wa ardhi, ni ishara ya kutokuendelezwa ipasavyo kwa shamba hilo ikizingatiwa kuwa baadhi ya mazao yaliyopo shambani ni ya watu waliokodi shamba hilo na si ya Mwekezaji. Kwa ujumla, uchunguzi umebainisha kwa uhakika kwamba, sehemu kubwa ya shamba hilo haijaendelezwa ipasavyo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAPENDEKEZO YA UTATUZI WA MGOGORO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la kuundwa kwa Kamati hii ni kupata Mapendekezo kuhusu ufumbuzi wa mgogoro uliopo kati ya Mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na wananchi wanaozunguka shamba hilo. Kwa namna ulivyo mgogoro huu,

dhana ya ardhi kuwa msingi wa uhai kwa wananchi inafifia na dhana ya ardhi kuwa na thamani au msingi wa uzalishaji mali inapoteza msingi. Hali hiyo inahitaji kurekebishwa kwa kuondoa mizizi ya mgogoro uliopo. Utatuzi huo unapaswa kutegemea matokeo ya uchunguzi uliofanyika kwa muono wa Sera na Sheria zilizopo na kuzingatia ustawi wa maisha ya watu kama inavyotaka Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 3.2 Mapendekezo

### 3.2.1 Umiliki wa Shamba la Malonje

**KWA KUWA,** masuala mbalimbali katika mgogoro unaohusu umiliki wa shamba la Malonje yanajumuisha:-

(i) Kubadilika ukubwa wa shamba mara kadhaa na kuwepo kwa vipimo vinavyotofautiana kuhusu ukubwa wake, jambo linalochangia kuendelea kwa mgogoro;

(ii) Kutozingatiwa kwa dhamira na Maelekezo ya Baraza la Mawaziri yaliyohusu matumizi ya shamba la Malonje, hivyo uuzaji wa shamba hilo kuwa na kasoro;

(iii) Kutofuatwa kwa taratibu za uuzaji wa mali za umma wakati wa kuuza shamba la Malonje, hivyo kusababisha sintofahamu na mashaka ya uhalali miongoni mwa wadau;

(iv) Kutoshirikishwa kwa wadau muhimu ikiwemo wananchi, viongozi wa vijiji pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga katika mchakato wa ubinafshaji wa shamba, hivyo, kutokuukabali uwekezaji katika shamba hilo;

(v) Mwekezaji kutotekeleza masharti yaliyo katika mkataba wa mauziano na hati ya umiliki wa shamba

ya mwaka 2009, hivyo kutokufikiwa kwa malengo yaliyotazamiwa na wasiwasi wa wananchi kuhusu uzingatiaji wa maslahi yao;

(vi) Kubadilika kwa matumizi ya shamba pasipo kuzingatia taratibu, hivyo mabadiliko hayo kutokubalika miongoni mwa wananchi na kukiuka dhamira ya ubinafsishaji wa shamba hilo;

(vii) Kutokuwa na usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba wa mauziano ya shamba la Malonje, hivyo kutoa fursa kwa mwekezaji kuamua atakavyo na kuwakwaza wananchi;

(viii) Kuingiliana kwa mipaka ya shamba na mipaka ya baadhi ya vijiji, hivyo kusababisha mgogoro wa matumizi ya eneo la ardhi lenye muingiliano;

(ix) Baadhi ya vijiji kutokuwa na ardhi ya kutosha kwa ajili ya kilimo na ufugaji ilhali kuna eneo la ardhi ya Malonje halitumiki, hivyo kuwavutia kuendesha shughuli zao na kujikuta katika mgogoro na mwekezaji;

(x) Sehemu kubwa ya shamba kutotumiwa na Mwekezaji, badala yake kukodishwa kwa wanakijiji na wananchi wengine;

(xi) Mwekezaji kupendekeza kuuziwa hekta 10,000 badala ya 3,000 zilizotangazwa kwa bei ya **Shilingi milioni 600** na Serikali kukubali bila kufanya uthamini wa shamba na mifugo iliyokuwepo wala kutangaza kusudio la kuuza hekta 10,000, jambo linalosababisha mashaka miongoni mwa wananchi;

(xii) Kumekuwepo na uhusiano mbaya kati ya Mwekezaji na wananchi wa vijiji vinavyolizunguka shamba hilo

kunakosababishwa na mvutano na mgongano wa matumizi ya shamba hilo na hivyo kusababisha mapigano na uvunjifu wa amani kwa Mwekezaji na wananchi wa vijiji hivyo.

**NA KWA KUWA,** masuala haya kwa ujumla wake yanaathiri manufaa ya shughuli za uzalishaji kwa mwekezaji na yanatofautiana na dhana ya ardhi kuwa msingi wa uhai kwa wana vijiji,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**: -

(a) Serikali ibatilishe umiliki wa Shamba lote la Malonje (Shamba la Efatha) na mashamba yanayolizunguka ikiwemo vitalu 51 kwa kuzingatia sheria na Maslahi ya Umma;

(b) Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote nane vinavyozunguka shamba pamoja na Gereza la Mollo utakaobainisha mahitaji ya ardhi pamoja na matumizi ya ardhi hiyo; na

(c) Serikali ilipime shamba hilo na kuligawa upya kwa wahusika ambao ni wanavijiji, gereza la Mollo, Mwekezaji (Efatha Church) na wenye vitalu kwa kuzingatia:-

(i) Mahitaji halisi ya ardhi kwa wanavijiji;

(ii) Uwezo wa Mwekezaji;

(iii) Uwezo wa Wenye vitalu; na

(iv) Mahitaji ya gereza la Mollo.

**3.2.2 Shauri la Ardhi Na. 7/2015 kati ya Bodi ya Wadhamini wa Efatha dhidi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga**

**KWA KUWA,** msingi wa Shauri la Ardhi Namba 7/2015 lililofunguliwa Mahakama Kuu Masijala ya Sumbawanga ni Notisi ya kubatilisha umiliki wa Mwekezaji katika Shamba la Malonje iliyotolewa na Afisa ardhi Mteule kwa niaba ya Kamishna wa Ardhi;

**NA KWA KUWA,** katika shauri hilo:-

a) Aliyeshtakiwa ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga badala ya Kamishna wa Ardhi ambaye ndiye aliyetoa Notisi na ndiye mwenye mamlaka hayo kisheria;

b) Liliisha kwa njia ya maridhiano ambapo ilisainiwa Hati ya Maridhiano baina ya pande mbili ambapo upande wa Serikali alisaini Mkurugenzi wa Manispaa na Mstahiki Meya; na

c) Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga alieleza kwamba saini yake imegushiwa na hivyo kuibua wasiwasi wa uhalali kuhusu hati hiyo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ichukue hatua za kisheria ikiwemo kuomba marejeo kuhusu maamuzi hayo ya mahakama; na

(b) Serikali ifanye uchunguzi ili kuwabaini na kuwachukulia hatua watu wote watakaothibitika kughushi saini ya Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

**3.2.3 Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza la Mawaziri**

**KWA KUWA,** Maagizo ya Baraza la Mawaziri kuhusu uuzaji wa Shamba hilo –

(i) Yalikusudia ardhi ya shamba lote itumike kwa ajili ya ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa na kwamba wananchi wauziwe vitalu kuzunguka shamba hilo ili waweze kujifunza ufugaji bora, lakini utekelezaji ulikiuka maagizo hayo, jambo lililokwamisha tija iliyokusuidwa;

(ii) Hayakuwahi kubadilishwa kipindi chote mgogoro ukiendelea, jambo linaloendeleza tofauti ya mtazamo kati ya Baraza la Mawaziri na watumiaji wa ardhi ya shamba hilo;

(iii) Hayakuwahi kutekelezeka miongoni mwa wananchi na kusababisha wananchi kushindwa kununua vitalu, jambo lililochangia upungufu wa ardhi kwa shughuli zao;

**NA KWA KUWA,** mambo hayo yanaathiri mustakabali wa wananchi wanaozunguka shamba hilo, manufaa aliyotarajia Mwekezaji na tija iliyokusuidiwa na serikali kisera na ustawi wa wananchi,

**KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba**, Serikali itathmini msingi na malengo ya uamuzi wake kupitia Baraza la Mawaziri kuhusu shamba la Malonje ili kubaini iwapo kuna tija inayopatikana na kuchukua hatua stahiki kulingana na Azimo la kwanza.

### 3.2.4 Usimamizi wa Sheria inayoweka Ukomo wa Kumiliki Ardhi Nchini

**KWA KUWA,** idadi ya watu inaongezeka siku hadi siku na mahitaji ya ardhi yamekuwa yakiongezeka licha ya ardhi kutokuongezeka huku kukiwa hakuna mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo mengi nchini;

**NA KWA KUWA,** hakuna ufanisi katika utekelezaji wa Kanuni za mwaka 2001 zinazohusu ukomo wa kumiliki kiasi

cha ukubwa wa ardhi ya kawaida na ardhi ya vijiji; na kwamba mamlaka za serikali za mitaa hazina mipango ya usimamizi wa ukomo wa kiasi cha ukubwa wa kumiliki ardhi katika maeneo yao; hali inayochangia kutokuwa na usawa katika kumiliki ardhi miongoni mwa wananchi, ilhali mahitaji ya ardhi kwa wananchi ni makubwa.

**KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;**

(a) Serikali isimamie utekelezaji wa Kanuni zinazoweka ukomo wa wananchi kumiliki ardhi nchini; na

(b) Serikali isimamie kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007 kwa kupima ardhi ya nchi nzima na kuiwekea mipango na matumizi ili–

(i) Kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya ardhi;

(ii) Kuwezesha umiliki unaotambulika, jambo litakalowezesha ardhi ndogo kutumika kwa manufaa ya watu wengi; na

(iii) Kupunguza migogoro ya mipaka na umiliki.

### 3.2.5 Hatua Dhidi ya Vitendo vya Uvunjifu wa Haki za Binadamu

**KWA KUWA,** uchunguzi umebainisha dalili za kuwepo kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu katika Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo, lakini waliohusika katika tuhuma za vitendo hivyo, hawajachukuliwa hatua za kisheria;

**NA KWA KUWA,** hatua hizo zinahitaji kufanyika kwa uchungzi, ili kubaini hatua zinazostahili kuchukuliwa;

**KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba**, Mamlaka zinazohusika na uendeshaji wa kesi za jinai nchini zifanye

uchunguzi na kuchukua hatua stahiki kulingana na matokeo ya uchunguzi huo.

### 3.2.6 Usimamizi wa Kampuni za Ulinzi Nchini

**KWA KUWA,** Walinzi wa Kampuni ya Ulinzi ya Funguka Security Co. Ltd inayolinda shamba la Mwekezaji wamekuwa wakituhumiwa kufanya vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu na kwamba, imebainika kuwa walinzi hao wamekuwa wakipewa mafunzo ya ulinzi kutoka kwenye kampuni hiyo yakiwemo mafunzo ya kutumia silaha za moto kwa kufungamanishwa na imani ya wamiliki wa shamba;

**NA KWA KUWA,** Kamati katika kupitia masharti yanayotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Kampuni binafsi za ulinzi; haijaona sharti linaloruhusu kampuni kutoa mafunzo kwa walinzi wake na kuwafungamanisha na Imani; hali ambayo Kamati inaamini inasababisha walinzi hao kukosa weledi;

**KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba**;

(a) Serikali itizame na kufanya tathmini juu ya taratibu zinazotumika kwa sasa kutoa vibali kwa kampuni za ulinzi ili kuona kama vigezo vinavyotumika kutoa vibali kwa Kampuni hizo vinakidhi mahitaji ya sasa kiusalama;

(b) Serikali ifanye uchunguzi juu ya uhalali na weledi wa walinzi wa mwekezaji kwa vitendo wanavyodaiwa kuwafanyia wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje;

(c) Serikali ichunguze vitendo vya walinzi wa Kampuni ya Funguka kujeruhi wananchi kwa kutumia silaha za moto na kuchukua hatua dhidi ya watakaobainika kukiuka sheria na taratibu katika kutumia silaha za moto; na

(d) Serikali ifungue upya majalada ya kesi za uchunguzi zinazohusu matukio yote ya uvunjifu wa haki za binadamu zilizotokana na mgogoro wa shamba la Malonje na kuchukua hatua za kisheria.

### 3.3 Majumuisho ya Sehemu ya Tatu

**Mheshimiwa Spika**, mgogoro katika shamba la Malonje umekuwepo kwa muda mrefu sasa. Jitihada kadhaa zimefanyika katika kujaribu kutatua mgogoro huo. Pamoja na jitihada hizo, bado mgogoro umeendelea kuwepo. Tathmini ya Jumla ya matokeo ya uchambuzi wa Hadidu zote zilizotolewa kwa Kamati inaweza kujumuishwa kwa kuelezea kasoro mbalimbali kama chanzo cha mgogoro wa shamba la Malonje.

**Mheshimiwa Spika,** Kasoro hizo zimebainika kwa pande zote, Serikali, Mwekezaji na Wanavijiji. Suala kuu likiwa kujielekeza katika kuzingatia haki za raia katika matumizi ya ardhi, Kamati imependekeza kuanza upya kwa kufuta umiliki wa shamba lote la Malonje na kulipima upya pamoja na kuvipima upya vijiji vinavyozunguka shamba hilo kwa maslahi mapana ya nchi. Lengo ni kufanya mgawanyo mpya kwa kuzingatia mahitaji halisi na kurekebisha kasoro mbalimbali zilizojitokeza awali. Ni matarajio ya Kamati kwamba, hatua hii itatamatisha migogoro katika shamba hilo na kurejesha amani na utulivu kwa wanakijiji pamoja na Mwekezaji.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wa Kamati Maalum ya kuchunguza na kutathmini mgogoro katika shamba la Malonje kati ya Mwekezaji na wananchi wanaozunguka shamba hilo, wanakushukuru kwa dhati kwa uongozi wako, maono na juhudi za kuliwezesha Bunge kushughulikia changamoto za wananchi

katika utekelezaji wa shughuli za umma. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linatarajiwa kuendelea kuisimamia na kuishauri Serikali ili iweze kutimiza lengo la kuwezesha ustawi wa Maisha ya watu. Chini ya uongozi wako, Bunge limeendelea kutimiza wajibu huo na litaendelea kufanya hivyo kwa kuwa ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi na ni Bunge lao, hivyo haliwezi kuacha kufanya juhudi inayowezesha kutatuliwa kwa migogoro.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inamshukuru pia Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa kusimamia vema uratibu wa shughuli za Kamati. Usimamizi wake umewezesha uratibu bora wa Sekretarieti uliofanikisha kazi ya Kamati kwa misingi ya utaratibu madhubuti wa Kibunge. Aidha, shukrani zinatolewa kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Serikali ya Mkoa wa Rukwa kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati kwa kiasi cha kufanikisha khii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawashukuru wadau mbalimbali waliofika kwenye Kamati na kutoa taarifa muhimu zilizowezesha uchambuzi wa Kamati. Miongoni mwao ni Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Viongozi wa Kanisa la Efatha, Wakurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa na Wilaya ya Sumbawanga na wadau wengine wote waliowasilisha taarifa kwa Kamati. Kamati pia inawashukuru wananchi wa vijiji vya Sikaungu, Msandamuungano, Songambele Azimio, Mawenzusi, Ulinji na Isesa kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla tunawashukuru wote walioipatia Kamati taarifa muhimu ambazo ziliisaidia kupata uelewa na kuzichakata hatimaye kupata mapendekezo. Kwa hakika wote walioipatia Kamati taarifa, maoni na ushirikiano uliostahili tunawashukuru sana.

## 4.2 Mwisho

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelezwa, lengo la Kamati hii lilikuwa ni kutoa ushauri unaowezesha utatuzi wa mgogoro kati ya Mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na Vijiji vinavyozunguka Shamba hilo. Mgogoro huo umetokana na sababu zilizoelezwa ambazo zote zinapaswa kuangaliwa kwa mtazamo wa Sera ya Taifa ya Ardhi, ya Mwaka 1995, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Sheria Ardhi ya Kijiji, Sura ya 114. Mtazamo huo uzingatie pia lengo la Serikali la kuwezesha ustawi wa wananchi na kwamba Ardhi ni msingi wa Maisha ya Wananchi wakiwemo wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, kwa kadiri itakavyoonekana inafaa mapendekezo yaliyotolewa yafanyiwe kazi. Muhimu zaidi ni kuwa mgogoro huu usipotatuliwa muwekezaji hataweza kufanikiwa katika uwekezaji wake na wananchi hawataweza kuwa na matumizi ya ardhi inayohusika kwa namna ya kupata ustawi wao. Aidha, Serikali haitafanikiwa katika kustawisha maisha ya wananchi wa vijiji hivyo na wala Bunge halitakuwa limesaidia kupatikana kwa ufumbuzi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Prof. Shukrani E. Manya, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI MAALUM YA BUNGE KWA AJILI YA KUCHUNGUZA MGOGORO WA ARDHI KATIKA SHAMBA LA MALONJE**

27 AGOSTI, 2024

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge. Kama kanuni zetu zinavyotutaka, Mwenyekiti ameshawasilisha taarifa hii ya Kamati Maalum na baadhi ya Wabunge wameomba kwa ajili ya kuchangia. Sasa tutaanza na hawa wachangiaji, na baada ya hapo, kwa utaratibu wetu, ndiyo Bunge litahojiwa.

Sasa ninayo majina hapa ya Wabunge walioomba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ajiandae.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa ya kuchangia asubuhi ya leo. Awali ya yote narejesha shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, aliyetujalia uhai, na aliyetuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa wazima wa afya.

Mheshimiwa Spika, pili, nakupa shukurani Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ya kuwa Mjumbe wa Kamati hii na kazi yetu haikuwa rahisi sana, lakini kwa uhakika, kwa namna ulivyokuwa umeweka mchanganyiko mzuri kwenye Kamati, haikutushinda. Tumeifanya kazi hiyo kwa weledi wa hali ya juu, na kwa uaminifu na uzalendo uliopitiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mapendekezo yote yaliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati yetu na ninaomba niwashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu waunge mkono mapendekezo hayo kama yalivyo ama wayaboreshe zaidi, kama watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu ili kutia msisitizo tu kwamba pendekezo la kwanza ambalo tumelitoa mbele ya Bunge lako Tukufu linazingatia maslahi ya kila mdau kwenye eneo husika. Sababu ya kupendekeza hivyo ni ukweli na uhalisia wa kwamba kumekuwa na *gaps* ambazo zimetufikisha kwenye mgogoro huu kutoka kila upande. Kuna matobo upande wa Serikali

ambayo ndiyo mengi zaidi, lakini pia kuna matobo upande wa wananchi, lakini pia kuna matobo upande wa mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, sasa bila kurudi kwenye *drawing board* na kuanza upya mchakato wa namna ya kukidhi maslahi ya kila mdau katika eneo lile hatuwezi kutatua mgogoro huo. Ndiyo maana Kamati baada ya kutafakari kwa kina, lakini pia baada ya kuangalia taarifa mbalimbali kufika uwandani tuliona tuisaidie Serikali kwa kuipa ushauri kwamba ianzie kwanza kwa kufuta umiliki wa shamba hilo kwa kila mwenye umiliki katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji anamiliki eneo lake lifutwe, baadhi ya watu waliopewa *blocks* wanamiliki hati zao zifutwe, Gereza la Mollo linamiliki hati yake ifutwe, vijiji vimepimwa juu ya ardhi ya kawaida *(general land)* navyo hizo hati zifutwe ili sasa upimaji ufanyike upya bila makosa kwa kuzingatia mahitaji, uwezo wa uwekezaji, shughuli wanazofanya watu na pia kwa kuzingatia maslahi ya watu wote waliopo katika eneo hilo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumetenda haki, lakini pia tutakuwa tumetatua mgogoro kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika upungufu mkubwa uliopo pale kwa upande wa Serikali, kwa mfano, shamba limekuwa likiongezeka ukubwa kutoka mwaka hadi mwaka kutokea enzi za aliyekuwa mwanzishaji wa hilo shamba alikuwa anaitwa Bwana George Damm, Mzungu huyu Mlowezi mwaka 1930. Akaja mke wake akaongeza ukubwa mwaka 1955, wakaja *NACO* ambao ni Shirika la Serikali mwaka 1967 wakaongeza ukubwa, wakaja tena *NARCO* wakaongeza ukubwa mwaka 1973. Shamba limekuwa likikua kwa kiasi kikubwa sana mpaka likafikia ekari 47 na ushee.

Mheshimiwa Spika, katika hatua zote hizo za kuongeza ukubwa wa shamba na kubadilisha ardhi ya vijiji vya asili kutoka kubwa ardhi ya vijiji kwenda kuwa *general land* hakukuwahi kuwa na ushirikishwaji wa wananchi, hakukuwahi kufuatwa taratibu za kubadilisha ardhi ya kijiji kwenda kuwa ardhi ya kawaida *(general*

*land)*. Sasa kama taratibu hazikuwahi kufuatwa toka awali uhalali hauwezi kupatikana leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa hata ukitazama wanafalsafa mbalimbali wanaozungumzia kuhusu haki za binadamu wanasema hata siku moja matokeo hayawezi kuwa halali kama mchakato wa kuyatengeneza hayo matokeo hakuwa halali. Hapa napenda kumnukuu Tom Taylor ambaye ni mbobezi wa Falsafa ya Sheria anazungumzia kuhusu msingi wa uwepo wa haki. Kwa hiyo, Kamati kwa kutafakari kwa kina, tulifikia kushauri kwamba kwa kuwa mchakato wa kulianzisha shamba lenyewe pale awali na hii inatokana na hadidu rejea ya kwanza uliyotupa hakukuwa halali, basi matokeo yote yanayokuja huku mwisho hayawezi kupata uhalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, ndiyo maana tukapendekeza pale kwenye maazimio kwamba basi turudi kule mwanzo tutengeneze kwanza uhalali wa shamba lenyewe. Baada ya kutengeneza uhalali, sasa basi watu wote kwa kuzingatia mambo yaliyotokea, uwekezaji walioweka na uendelezaji walioufanya wapatiwe vipande vipande katika shamba husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadaye vilikuja vikapimwa Vijiji vya Sikaungu, Msanda Muungano na vingine vinavyozunguka pale na vikapewa hati vimekuja kupewa hati juu ya ardhi ya *general* (ardhi ya shamba) shamba tayari lina hati ambayo ni *general land* ama ardhi ya kawaida. Vijiji vikaja vikapimwa juu vikawa *super reimposed* juu ya *general land* ambayo haikubaliki kisheria na hivyo mgogoro tena wa kisheria unatokea.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana wananchi wa Sikaungu hata walipogawia eka zile 1,000 walikataa. Wakasema hizi eka 1,000 zipo kwenye ardhi ya kijiji chetu kwa sababu wana hati. Sasa mtu ana hati ya kijiji, kijiji kimesajiliwa, kijiji kimepimwa na hilo shamba limo katika ardhi yake ya kijiji. Yeye anasema ni eneo lake kwa nini agawiwe tena wakati ni eneo lake. Kwa hiyo, huwezi kutatua mgogoro katika mazingira hayo. Ni lazima ufute hati inayosajili kijiji,

hati inayotoa mipaka ya Kijiji, na pia ufute hati inayoweka mipaka ya shamba. Ukishafanya hivyo sasa ndio utapima useme kijiji kitaishia hapa na shamba litaanzia hapa, ukifanya hivyo sasa utatua mgogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo leo hii wananchi wanaamini eneo ni la kwao lipo ndani ya kijiji na kweli wana hati na wana usajili wa kijiji chao halali kabisa. Mbali na hivyo wananchi hawa wana haki nyingine ya msingi ya kiasili *(customary rights)* za kumiliki hilo eneo kwa sababu ni nyumbani kwao ni mahali pa asili yao.

Mheshimiwa Spika, siku zote tunafanya makosa makubwa sana katika nchi hii kuamini kwamba tunaweza tukaenda sehemu tu, tukapima ardhi, tukaanzisha hifadhi ama tukapima ardhi tukaanzisha shamba kwa maendeleo sawa. Sawa kabisa hakuna anayekataa, lakini hatupati haki ya kuchukua ardhi ya asili ya wananchi. Hatupati hiyo haki. Tutaipata hiyo haki kama tutafuata taratibu na taratibu zimewekwa na sheria na sheria inataka kwanza Mheshimiwa Rais, apewe atoe ridhaa yake kwamba tunabadilisha ardhi ya kijiji kuwa ardhi ya *general* kwa shughuli za maendeleo…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa dakika 10 zimeshaisha.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, sawa namalizia.

Mheshimiwa Spika, pili, tunapata uwezekano wa kufanya hivyo baada ya hiyo ridhaa ya Mheshimiwa Rais, kutolewa, itolewe *notice* ya siku 90, wananchi wakubali ardhi yao kuchukuliwa ama isichukuliwe. Wananchi nao wakitoa ridhaa, sasa ndiyo unabadilisha ardhi. Sasa hili shamba toka enzi za George Damm mpaka miaka hii mchakato wa namna hiyo hakuwahi kufanyika. Hivyo, hakukuwahi kuwa na ridhaa ya mamlaka zinazopaswa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Ahsante sana.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa natazama hapa mapendekezo ya Kamati. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa anatusomea kwenye ile taarifa yake ambayo ameieleza kwa kifupi, lakini taarifa ndefu ipo. Kwenye ile taarifa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kuna mahali unasema kwenye kufuta wakati nakusikiliza, umetaja pia kwamba vijiji vifutwe ili na vyewewe vipimwe upya, kwa ajili ya kuondoa sintofahamu ama kuzua taharuki.

Mapendekezo yaliyoletwa hapa na Kamati yanataja kuhusu Serikali kubatilisha umiliki wa shamba. Sasa kwamba wakatavyokuwa wanapima watapima kwa sura ipi na namna gani, nadhani vijiji sasa tusiviingize hapa kuhusu kufutwa hati zao. Kwa sababu linaweza likaleta taharuki huko kwamba kumbe siyo tu shamba linafutwa na vijiji vinafutwa! Pendekezo lililoletwa hapa na Kamati ni Serikali ibatilishe umiliki wa Shamba lote la Malonje. *(Makofi)*

Halafu sasa kwenye mapendekezo kuhusu vijiji, hapa naona wanasema iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote nane vinavyozunguka shamba. Kwa hiyo, hoja ya kufuta vile vijiji kwenye hii taarifa haipo, ili tukae sawa kule vijijini wasije wakaanza kupata taharuki kwamba halizungumziwi shamba, vinazungumziwa na vijiji pia. *(Makofi)*

Kwa maana ya ile tafsiri uliyoisema Mheshimiwa ambayo na huku imetajwa, ile inayochanganya ya kwamba ardhi ya kijiji na ardhi ya jumla sasa yale ni mambo ambayo tunaweza tu kubishana kisheria na tafsiri zake, lakini kwa maana ya haya mapendekezo yaliyoletwa na Kamati, zile hati za vijiji tuzitoe pembeni tubaki na

hoja ya shamba ili tusilete taharuki kwa wananchi. Kwa hiyo, kwa maelezo haya natarajia wachangiaji wengine pia tuchangie kwa sura hiyo tusilete taharuki kule kwa wananchi wanaotoka kwenye hivi vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mezani. Kwanza, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa Mjumbe wa hii Kamati Maalum kwa ajili ya kutatua mgogoro pale Shamba la Malonje. Pili, nampoongeza sana Mwenyekiti kwa kusoma vizuri na kwa kueleweka sana kwenye hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Spika, mimi nilipata nafasi ya kushiriki kwenye Kamati hii na imenipa fursa ya kujifunza mambo mengi sana kwenye *issue* ya uwekezaji nchini. Kwenye hili jambo la Malonje kwanza niunge mkono maazimio yote ya Kamati na niliombe Bunge na niombe Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono hiki ambacho tumekizungumza na kukipendekeza kama Kamati kuhusu namna ya kuendea hili jambo ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, watu wanaongezeka, idadi ya watu na inaongezeka kila siku…

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, ngoja utaanzia hapo kwenye "watu wanaongezeka."

Kuna wageni ambao wanapaswa kutoka humu ndani, ngoja niwatangaze. Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Anna Lupembe, ambao ni Watumishi wa Mungu kutoka *Calvary Assemblies of God* ya Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Mchungaji Tony Kapola, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 40 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Kwaya ya *Macedonia Voice* kutoka Kanisa la *Calvary Assemblies of God* Kisasa, Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 41 na walimu watatu wa Shule ya *King Vision Pre and Primary School* iliyopo Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sanga, endelea.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwenye hili jambo la Malonje idadi ya watu nchini inaongezeka na mahitaji ya ardhi yanazidi kuongezeka kila siku. Kwa jinsi ambavyo tumeenda kuona uwandani kwa maana ya *site* uhitaji wa ardhi kwa wananchi ni mkubwa sana. Kutokana na kuwepo kwa uhitaji mkubwa wa ardhi kuna haja ambacho tumekipendekeza kwamba umiliki wa lile shamba ubatilishwe ili tuweze kwenda kwenye mchakato wa kuligawa upya ili wananchi na wenyewe waweze kupata haki.

Mheshimiwa Spika, ukienda *site* na ukafanya mikutano na wale wananchi utagundua umuhimu wa maeneo mbalimbali wawekezaji kuwa na mahusiano mazuri na wananchi. Lile jambo lililopo pale tukiliacha leo, tukiliacha kesho, tukiliacha mwakani mwisho wa siku itakuja kuwa na bomu kubwa sana kwa sababu *generation* (kizazi) kinachozidi kuzaliwa pale kinazaliwa na chuki dhidi ya mwekezaji kwa sababu anaona kuna matukio ambayo yametokea kwenye maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili twende kwenye mwanzo mzuri na tuweze kuweka mahusiano mazuri kati ya wananchi wa vile vijiji vinavyozunguka Shamba la Malonje, haya mapendekezo ni muhimu sana na yataleta mustakabali mzuri sana kuhakikisha kwamba mahusiano kati ya mwekezaji, lakini pili mahusiano kati wananchi na eneo la shamba yanaimairishwa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukodishwaji wa lile shamba na kufungamanisha suala la kiimani kwamba ili uweze kukodishwa utoe fungu la 10 ufanye, nini ni vitu ambavyo vimekuwa vikivunja sana mahusiano na ukizingatia katika nchi yetu ni nchi ambayo wakulima siyo wakristu tu, wakulima pia wapo wenzetu ambao hawafungamani na ile imani na wangetamani kutumia hilo shamba.

Mheshimiwa Spika, pia, siyo kusudio la Serikali kuona lile shamba linatumika kwa mfumo huo. Kusudio la Serikali lilikuwa ni uwekezaji wa kisasa. Kutokutumika katika uwekezaji wa kisasa maana yake ni kwamba tumekiuka miiko na taratibu za kimkataba ambazo Serikali ilikuwa imejiwekea. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana kuona Serikali inalisimamia hili ambalo tumelipendekeza kama Bunge na tutafikia muafaka kwenye hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nchi kama nchi yawezekana wakati tunaenda kwenye maono ya uwekezaji kwenye Taifa letu tulikuwa na maono mazuri sana kwamba tunahitaji kubinafsisha maeneo ya Serikali kadha wa kadha ili Watanzania au sekta binafsi iweze ku-*take off* na kuweza kufanya uzalishaji mkubwa. Kwa hiki kinachoendelea Malonje kinatupa maswalli kuna maeneo ambayo tumewezeza viwanda nchini, kuna maeneo ambayo mashamba tumewekeza nchini kama haya maeneo hayafanyiwa tathmini…

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, kuna Taarifa. Nani anatoa taarifa? Mheshimiwa Festo Sanga, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

## TAARIFA

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nimpe Taarifa mzungumzaji kwamba hili analolizungumza hapa linatoa taswira njema ya Taifa kwa ujumla kuangalia maslahi na ustawi wa wananchi wake. Pia, nimfahamishe kwamba kule kwangu Eneo la Momela mipaka ilikuja

ikawekwa kwa ajili ya kupisha uhifadhi, lakini mpaka ule ukawa umepita kwenye milango ya wananchi. Kwa hiyo, akitoka asubuhi anaingia kwenye hifadhi, matunda yake wanaumizwa au wanachukuliwa hatua za kinidhamu na Mamlaka ya Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, pia, kuna Kijiji pale Kata ya Maroroni ambacho kilikuwa kimeshaandikishwa, lakini mpaka wa *KIA* wakaenda kukifuta. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea taarifa ya mzee wangu kwa sababu kile nilichokuwa nakizungumza kwamba ningependekeza kama nchi, lazima tuliangalie suala la uwekezaji kwenye Taifa letu limefikia hatua gani? Kuna maeneo mengi ambayo tumeyawekeza. Huu mgogoro wa Malonje ni mmoja tu, ukienda Handeni kuna mgogoro na ukienda maeneo mbalimbali kuna migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii kama Serikali haitachukua tathmini kufuatilia kila mtu aliyemkabidhi shamba, waliyemkabidhi kiwanda katika sekta ya uwekezaji amefanyia nini kile? Hii migogoro itaendelea kujirudia na kujirudia. Kwa hiyo, kuna haja Serikali ipo hapa ndani inatusikiliza, kuna viwanda ambavyo tuliwapa watu, vimekufa haviendelei kufanya kazi. Kuna mashamba watu wameyakumbatia na uhitaji wa watu bado ni mkubwa ila watu wameyakumbatia.

Mheshimiwa Spika, kuna haja Serikali kuunda timu ya watu wenye uzalendo, ya watu ambao watatanguliza maslahi mbele kuhakikisha tunafanya tathmini kwa sababu nchi yetu kuzaliana kumekuwa ni kwa kiwango kikubwa. Kuna haja ya kuangalia kwamba maeneo mengine ya uwekezaji pia tunayaangalia kwa kina ili kulinda maslahi ya nchi yetu Taifa letu, ni hili hili Tanzania ardhi haiongezi ila idadi ya watu inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa watu waliokumbatia maeneo ya watu ambayo hayazalishi ni muhimu Serikali ikafanya tathmini ili tuweze kuisadia nchi yetu. Mathalani kwenye *issue* ya viwanda ambavyo tumekuwa tukivipigania kelele kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hili suala la Malonje, tumeenda *site,* yaani unaenda sehemu kutafuta uthibitisho mathalani kwenye vituo vya Polisi kuhusu mtu aliyepigwa risasi unakosa *PF3*. *PF3* haipo na wao wanaonesha kwamba hawana taarifa na hilo jambo. Sasa sisi tunaona kabisa kwamba pia hata hizi mamlaka (vyombo vya dola) ni muhimu kabisa kusimama na wananchi. Kwa sababu wananchi wanapoendelea kukosa imani dhidi yao, hawaendi kuripoti *cases* ni kitu ambacho kinakuwa ni kibaya kwenye mustakabali wa kusimamia haki kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana na niombe Jeshi la Polisi wakaangalia pale Rukwa watoe takwimu na mamlaka zipo hapa waangalie nini mchakato wa hawa watu? Watu wengi wamekuwa wakifanyiwa matukio mengi lakini wanaogopa kwenda kwenye vituo vya Polisi kutoa ripoti kwa sababu wanajua mwekezaji ana nguvu, mwekezaji ana mkono mrefu ambao wao wananchi watakuwa wamekosa haki yao. Kwa hiyo, kuna haja pia ya Serikali kuchunguza hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niunge mkono hoja ambayo ipo mezani na nilishawishi Bunge kwamba, leo hili lipo Malonje, lakini kesho itakuwa eneo lingine. Hii ndiyo iwe *basement* yetu au tu-*set bar* kupitia hili ili na maeneo mengine ya nchi tuweze kufanyia tathmini katika suala la uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu ambao wanakumbatia mashamba au viwanda tuanze kuwaangalia kwa jicho lingine ili twende kujenga nchi yetu ambayo ina uchumi imara, nchi ambayo ina uzalishaji, nchi ambayo ina amani, nchi ambayo wawekezaji hawashiki ardhi kubwa na baadaye wanageuka kuwa maadui na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninakushukuru kwa kuniamini kuwa Mjumbe wa Kamati hii Maalum kwa ajili ya Ardhi ya Malonje na mgogoro ule. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nami naungana na wenzangu kukushukuru kwa kunipa fursa ya kutumika ndani ya Kamati hii ambayo taarifa yake imewasilishwa leo.

Mheshimiwa Spika, naungana kabisa na Mwenyekiti kwa taarifa aliyoisoma na mapendekezo aliyoyatoa pamoja na wachangiaji wenzangu ambao wametangulia.

Mheshimiwa Spika, pendekezo kubwa la kwanza la kubatilisha umiliki wa shamba hili la Malonje kama ambavyo nitaeleza, ni pendelezo *or rather* ni maamuzi ambayo Serikali ilishayafikia mwaka 2015 lakini ikafika mahali kukatokea mkwamo ambao nitauelezea huo mkwamo ulitokana na kitu gani.

Mheshimiwa Spika, kishindo ambacho tumekiona uwandani ambako tulikuwa na maeneo mengine wakati wa Kamati hii ni vizuri sana kuelezea mambo machache ambayo ni vizuri tukayaona, mambo yenye utata katika mchakato huu mzima wa kubinafsisha shamba hili kwa mwekezaji huyu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa aliyeomba kununua shamba, kampuni iliyoomba kununua shamba ni Kampuni inayoitwa *Efatha Foundation Limited* kwa barua ya tarehe 24 mwezi wa Machi, 2007. Mchakato ukaendelea na kwa mujibu wa barua ya *RAS* kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo ya tarehe 17 mwezi wa Januari, 2008, aliyeshinda ile zabuni na kupewa kununua lile shamba na kwa mujibu wa ile barua ilisema aliyesaini mkataba ni huyo huyo *Efatha Foundation Limited,* lakini uhalisia wa mambo ni kwamba

mkataba wenyewe wa tarehe 28, mwezi wa Agosti, 2007 ulisainiwa na *Registered Trustees of Efatha Ministry*.

Mheshimiwa Spika, kisheria hawa ni watu tofauti kabisa na tulijaribu kufuatilia kama kuna uhaulishaji wa huo mkataba kutoka kwa yule ambaye alipewa *originally Efatha Foundation Limited* kwenda *Registered Trustees of Efatha Ministry*, hapakuwa na kitu kama hicho.

Mheshimiwa Spika, hati ya kumiliki ardhi ikatolewa kwa *Registered Trustees of Efatha Ministry*, ambao ndio waliosaini mkataba, lakini kwa sasa hawa *Registered Trustees* wa *Efatha Ministry* wamebadilisha jina na kuwa *Registered Trustees of Efatha Church,* lakini mpaka Kamati ikiwa kazini bado hati ilikuwa inasomeka vilevile *Registered Trustees of Efatha Ministry*. Kwa hiyo, utakuta kwamba aliyepewa shamba, aliyesaini mkataba na anayeendesha shamba kwa sasa tena ni kampuni nyingine inayoitwa *Efatha Heritage*.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi siamini kabisa kwamba huu utata ni wa bure bure tu. Huu utata una sababu yake, nami nasema kwamba tunapoingia katika mambo makubwa kama haya, ni vizuri tukawa na uhakika kwamba tuna-*deal* na kampuni gani, inaitwaje, Wakurugenzi ni akina nani na kadhalika. Tusiruhusu hii kubadilisha badilisha kunakofanyika kinyume na mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi ni kwamba, ule mkataba uliosainiwa haujatekelezwa kwa sababu kifungu cha (6) na Kifungu cha (7) cha mkataba huo kinaweka masharti ya dhahiri kabisa kwamba eneo lile litumike kwa ajili ya ufugaji na mambo ya chakula cha mifugo, lakini matumizi kwa sasa ni mengine na hatujaona kwamba kuna *addendum* yoyote ya mkataba au mabadiliko yoyote yale ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, sasa haya mambo yenye utata ni vizuri hata tunapotekeleza marekebisho haya tunayokusudia kuyafanya tuzingatie mambo kama haya. Kwa sasa shamba linalindwa na

Kampuni inaitwa *Funguka Security*. Kwa wanaojua lugha nyingi wanafahamu kwamba Funguka maana yake ni *Efatha* na kwenye *official search* inaonesha kwamba wanaomiliki kampuni hii ni *Efatha Foundation Limited* na *Registered Trustees of Efatha Church.* Kwa hiyo, ni mtu yule yule anazunguka huku na huku.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna swali la msingi kabisa kwamba ni kwa kiasi gani hizi taasisi zisizo za kiserikali, taasisi za kidini na vyama vya siasa, vinaruhusiwa kumiliki makampuni ya ulinzi yanayobeba silaha za moto? Hili jambo kuna haja ya kuliangalia vizuri kwa sababu litatuletea matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sababu mojawapo ya ushahidi wa mdomo ambao tuliupata kwa wahusika wenyewe wa hii kampuni ni kwamba, yule Meneja wa pale anasema, hawaajiri mtu ambaye amepita JKT wala Mgambo, wala mstaafu wa jeshi lolote lile. Kwa maana kwamba, wanaajiri watu wapya na *training* wanaifanya wao wenyewe. Sasa hii ndiyo inayoleta vitendo kama hivyo vya uvunjifu wa haki za binadamu ambavyo kama ingekuwa ni watu ambao ni *trained* vizuri, wangeweza wakavi-*manage* tu kwa utaratibu ule ule kulingana na wananchi walivyo, lakini hawa wanatumia nguvu kubwa kupita kiasi, matokeo yake haya mambo ndiyo yanatokea kwa sababu ya kukosekana kwa weledi kwa hawa watu ambao wanahusika.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa ajili ya haya makando kando yote na mambo ya uvunjifu wa haki za binadamu, Serikali iliazimia kwamba ifute. Haya maamuzi tunayopendekeza leo mwaka 2015 tayari Serikali ilishasema yafanyike, ikatoka ile *notice of revocation* na ilitoka sahihi kabisa, imetolewa na Afisa Ardhi Mteule kwa niaba ya Kamishna wa Ardhi, sasa changa la macho likaanzia hapo.

Mheshimiwa Spika, *Registered Trustees of Efatha Ministry* wakaenda Mahakamani wakaishtaki Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, watu ambao sio wahusika, sio wanaomiliki wa ile Hati na siyo waliotoa ile *notice*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nawachekesha watu, nikasema ni sawasawa na mimi nikupangishe nyumba yangu halafu ukashindwa kulipa kodi, nikakupa *notice* ya kuhama, halafu unaenda unamshitaki mwanangu, halafu mnakwenda Mahakamani mnakubaliana. Ndiyo sasa ikafanyika *Deed of Settlement* kwamba huyu atakaa mpaka afe, asibughudhiwe na mtu yeyote, na yeye ndiyo mmiliki halali, lakini walioko Mahakamani ni Mwekezaji na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ambao sio waliompa shamba na siyo waliotoa *notice of revocation,* lakini kesi ikaendelea hivyo hivyo na hiyo *settlement* ikapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa yale maamuzi yamekuwa yakitumika kama hirizi. Akiguswa kidogo, aah, mimi nina amri ya Mahakama hii inanitambua. Thubutu! Amri ipi hiyo ambayo wala haipo! Mimi nasema hata sasa hivi Kamishna wa Ardhi akiamua kufuta ile miliki, anaweza kwa sababu hakuwepo kwenye kesi na wala amri haimhusu na amri iko *very clear* inamhusu yule aliyekuwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukiacha hiyo, bado sasa *signatories* waliosaini ile *Deed of Settlement,* upande wa mdaiwa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Mstahiki Meya anasema mimi sikuwahi kusaini na hii *signature* imeghushiwa, anasema yeye mwenyewe. Upande wa mdai, *Efatha Ministry* aliyesaini ni mdhamini mmoja tu, yule mwingine alieyesaini ni *District Church Pastor*, ambaye kwa *search* ambayo tumefanya kule *RITA* hayupo katika *trustees* na pale walitakiwa wasaini wadhamini wawili waweke na lakiri ndiyo ule mkataba uwe halali. Kwa hiyo, amri hii ya Mahakama ambayo imekuwa ikitumika kama hirizi, mimi nasema siyo, yaani ni amri ya Mahakama inayohusu watu ambao wala hawamo kwenye mchakato huu kihalali na wala haizuii chochote kufanyika, labda tu kwa taratibu za utawala bora, basi kuwe na utaratibu tu wa kuiondoa ile amri ndiyo hilo lingine lifanyike.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo ripoti imeeleza, shamba lile liko ndani ya Halmashauri mbili. Liko Halmashauri ya Manispaa na Halmashauri ya Wilaya, lakini mchakato wote kuanzia mapatano

yale na kusaini mkataba na malipo, vyote vimeenda kwenye Halmashauri ya Manispaa. Halmashauri ya Wilaya ambako hasa ndiyo tatizo kubwa liliko hawakuhusishwa, wao wameshangaa tu mtu ameingia amekaa hapo, ndiyo baadaye ikatoka amri kwamba na wao wagawiwe fedha kidogo. Laiti wangeshirikishwa leo hii wangejua kwamba kuna Mwekezaji anakuja katika eneo hili, lakini wao wameshangaa tu mtu anaingia pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, pendekezo lile la kwanza ni muafaka kabisa kwamba mchakato huu umevurugika kuanzia mwanzo. Ni *null and void ab initio,* yaani kuanzia kule mwanzo kabisa ulishavurugika huu mchakato. Kwa hiyo, leo hii mimi nalishawishi Bunge lako kwamba lisione wala lisisite kuunga mkono pendelezo hili kwamba miliki hii ya shamba la Malonje ibatilishwe na kazi ianze upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nami nakushukuru kwa kunipa heshima ya kuwa kwenye Kamati hii maalum.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kuunga mkono hoja ya Kamati iliyowasilishwa na Mwenyekiti makini kabisa, mzalendo na anayejiamini, aliyetuongoza vema Wajumbe wake kuitenda hii kazi mpaka usiku wa manane bila kuchoka na tulikuwa tukianza kwa sala na kumaliza kwa sala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni Tanzania peke yake ndiyo inaweza kuendelea kuwa na mwekezaji anayekiuka taratibu, anavunja haki za binadamu na bado akaendelea kuwa na eneo akajiita mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aliyemaliza kuchangia, Mwanasheria nguli, Wakili Msomi, Mheshimiwa Tadayo amesema kabisa, mchakato huu uliharibika tangu mwanzo, hivyo Serikali haina kigugumizi chochote cha kwenda kubatilisha hii hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilikuwa *clear,* maelekezo ya Baraza la Mawaziri, Baraza lililopewa mamlaka kwa mujibu wa kifungu 54 (3) cha Katiba yetu, lilitoa maelekezo mahsusi, maana Baraza la Mawaziri linaweza likatoa maelekezo ya ujumla na maelekezo mahsusi. Moja ya maelekezo mahsusi ni kuuzwa kwa hekta 3,000 kwa ajili ya shughuli ya mifugo, na maelezo hayo yalikuwa yanataka mwekezaji akiwekeza kwa ajili ya mifugo kwa zile hekta 3,000 atawasaidia wananchi wa vijiji vinavyozunguka eneo lile kufuga kisasa. Lengo ilikuwa mwekezaji awekeze kwenye mifugo, afuge kisasa ili wananchi wa vijiji vinavyozunguka eneo lile waweze kunufaika na ufugaji wa kisasa na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, sasa maelekezo ya Wizara husika ambayo walipewa na Baraza la Mawaziri yalikuwa *very clear* na msisitizo kuwa mkishindwa kutekeleza agizo hilo mrudi mfanye *consultation* lakini hawakufanya hivyo. Matokeo yake enzi hizo akiwa Mkuu wa Mkoa, Mzee ninayemheshimu sana Ole Njoolay, aliamua tu kuuza hekta 10,000. Hekta 10,000 ni sawa na ekari 25,000 ndiyo maana nimesema ni Tanzania peke yake ndiyo bado tunaweza tukasema eti hili ni shamba halali la mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi kilichoendelezwa, ameendeleza hekari 900 tu. Hapa walikuwa wanasema wameendeleza asilimia nne kwa miaka zaidi ya 17. Tujiulize, mwekezaji alikuwa na dhamira ya kuendeleza au alikuwa na dhamira ya kopoka kwa kuchukua ardhi. Alikuwa ana dhamira ya kuendeleza au alikuwa ana dhamira ya kuchukua ardhi?

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, wananchi wa vijiji vile hawana sehemu ya kulima, hawana sehemu ya kufuga na ardhi hii haiongezeki lakini wananchi wanaongezeka. Basi sawa

amefanya aliyoyafanya; amebadilisha matumizi ya ardhi, sisi tumeenda, hata ukienda kuangalia kwenye ufugaji, ni vibanda tu vya kawaida ambavyo Mtanzania mwingine anaweza kujenga. Ng'ombe pale hawafiki hata 200. Kwa zaidi ya miaka 17 bado anajiita ni mwekezaji! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, mwekezaji huyu amekuwa akibadilisha matumizi mwaka hadi mwaka. Tumeenda tumekuta kuna mahindi pale yanalimwa, sijui kuna maua kidogo sijui ekari mbili, sijui kuna mkong,e lakini hakuna uwekezaji *tangible* unaompa mamlaka ya kuendelea kumiliki ekari 25,000 wakati wananchi wa vijiji vinavyozunguka wanapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshangaa tumeenda pale Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa anasema yeye haoni hao wananchi wenye shida ya ardhi. Hao watu wanaomsaidia Mheshimiwa Rais wanafanya kazi gani? Anasema, hakuna watu ambao wamejeruhiwa na risasi wala haki za binadamu zinazovunjwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako tumeshuhudia, wakati tunawahoji baadhi ya watu wa kule walisema, kulikuwa kuna mazingira ya rushwa, kuna baadhi ya viongozi wanalimiwa mle, na wananchi wanasema hatuna pa kwenda kutoa malalamiko yetu kwa sababu tunaoenda kuwapa malalamiko wana manufaa kwenye lile shamba la mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya lazima tuyaseme, tuweke misingi ya utawala bora. Hatukatai uwekezaji kwenye nchi yetu, na tunapenda sana tupate wawekezaji wazawa, lakini hawa wawekezaji wazawa wasirudi kwenye kauli ya Baba wa Taifa kwamba Mkoloni mweusi anaweza akawa hatari kuliko mkoloni mweupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni nadra sana kwenye Taifa letu akajitokeza Mama wa miaka 76 akalia amebakwa na mjukuu wake. Ni nadra sana. Nchi hii tuna mwekezaji ambaye mama ameenda kulima apeleke watoto shule, anakamatwa na walinzi wa mwekezaji

kinachomwa kiroba halafu yale maji yake anamiminiwa bibi wa miaka 70 mwilini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeyaona haya, tumeyaona halafu leo kuna viongozi kabisa wanasema ooh, yule mwekezaji ana haki. Tunahitaji wawekezaji watakaowanufaisha wananchi wanaozunguka maeneo hayo. Tunawahitaji wawekezaji wenye utu, wanaofuata misingi ya utawala bora, wanaofuata misingi ya haki za binadamu, na pia tunamhitaji mwekezaji ambaye atakuwa rafiki na sio adui wa wananchi wanaozunguka eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanabakwa, watu wanateswa na wanapigwa risasi kwenye nchi yetu ambayo kimataifa inasifika kuwa ni nchi ya amani. Halafu kuna viongozi wanawatetea, na bado wako kwenye hizo nafasi. Kuna wengine walishindwa kutimiza wajibu wao, lakini wapo, wamekuja kuhojiwa wanakwambia, tulifanya haya maamuzi, hatukuyafanya kwa sababu tulikuwa tunataka kukusudia kufanya makosa. Kweli!

Mheshimiwa Spika, umepewa maelekezo ya Baraza la Mawaziri kuuza hekta 3,000 halafu unaenda kuuza hekari 25,000, hekta 10,000 bila kufanya tathmini ya kujua gharama halisi ya eneo lako? Bila kutangaza *tender* kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu, unauza hekari 25,000 kwa shilingi milioni 600 halafu mwekezaji anaenda kukopea kwa zaidi ya shilingi bilioni tatu. Tanzania hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya nchi yetu, kwa maslahi ya wananchi wa Mkoa wa Rukwa na kwa maslahi ya kuhakikisha Taifa hili lina wawekezaji wanaoweza kukuza uchumi wa nchi yetu, tubatilishe hati hii, twende tukapange upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati na Kamati imekuwa na huruma hapa ya kwamba katika mgao tena anakuwepo, lakini ningekuwa mimi siwezi kuipangia Serikali, inaweza ikatafuta mwekezaji mwingine vilevile. Kama mtu amepewa shamba tangu mwaka 2007 hajaweza kuliendeleza, matokeo yake

kuna migogoro na anafanya vitendo vya udhalilishaji na ukiukwaji wa haki za binadamu, Serikali ina mamlaka ya kuweka mwekezaji yeyote, sio lazima awe yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa heshima ya kuwa Mjumbe wa Kamati Maalum na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya. Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Taarifa hii ya Kamati yako Maalum. Kipekee kabisa kama kijana, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuwa kwenye Kamati hii. Hakika nimejifunza, na nikwambie haukunipeleka kimakosa, nimeiva. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani zangu hizo, dhumuni la shamba kugawanywa kwa mwekezaji ama kubinafsishwa kwa mwekezaji, taarifa yetu imejieleza vizuri sana na nimshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuwasilisha taarifa kwa niaba yetu. Lengo lilikuwa ni jema sana na dhamira ilikuwa ni njema sana juu ya ubinafsishaji ama uwekezaji wa shamba lile. Taarifa imeshiba, imejitosheleza.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika ni mwekezaji kuchukua shamba na kutokwenda kwenye malengo na dhamira lililodhamiriwa kupitia Wizara ya Mifugo ambalo lilipeleka Baraza la Mawaziri na Waheshimiwa Mawaziri wakaridhia shamba lile madaraka yakasimishwe kwa Mkoa wa Rukwa ili waweze kubinafsisha na baadaye mrejesho urudi kwenye Baraza la Mawaziri, na ninaamini likiwa limekamilika kwa kuhakikisha kwamba limetenda haki.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda Rukwa, tumekwenda uwandani, tumewasikiliza wahusika. Tunaujua vizuri ubinafsishwaji, ugawanywaji na haki ambayo haitendeki ndani ya Mkoa wa Rukwa kupitia shamba la *Efatha*. Madhumuni yalikuwa ni ufugaji ambao utawasaidia vijiji vya jirani ama wananchi wanaolizunguka shamba kufanya Mkoa wa Rukwa kupitia Shamba la Malonje kuwa ni kitovu cha kiuchumi kupitia mwekezaji, na wananchi katika ufugaji wa nyama pamoja na maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati shamba lile linakwenda kubinafsishwa wakati mwekezaji anatafutwa, wananchi pia walipewa fursa, lakini walipewa masharti maalum kwamba sharti ni ufugaji na siyo kilimo. Wananchi nao walitafuta fedha za kuweza kulimiliki shamba lakini walikataliwa kwa kigezo kwamba hawaruhusiwi kulima, ni suala la ufugaji peke yake. Jambo la kushangaza na cha ajabu mwekezaji amekuja kupewa ambaye amekidhi vigezo, lakini kwa 99% amekwenda kulima na siyo kufuga jambo ambalo wananchi walikataliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko, wakati tunawaita viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Rukwa, ni ukweli usiyopingika kwanza wamekuwa ni wafichaji wa taarifa, lakini ni waonevu hasa kwa upande wa wananchi. Inasikitisha na inashangaza Mheshimiwa *RC* anasema yeye alipokea maagizo kutoka kwa sekretarieti yake kwa maana ya Katibu Tawala na timu nzima kwamba linatakiwa liuzwe shamba kwa shilingi milioni 600, lakini *RC* hakuwa na nafasi ya kujua na kutaka kwamba barua hiyo aione, aipitie ili aweze kupata mamlaka.

Mheshimiwa Spika, kitu cha ajabu, tulipokutana na Mwanasheria wa Mkoa wa Rukwa alikiri kwamba halifahamu wala hakushirikishwa katika uuzaji wa shamba hili. Katika uuzwaji wa shamba hili hata hizo shilingi milioni 600 bahati mbaya sana kwamba Manispaa ya Sumbawanga ilitakiwa ipate shilingi milioni 400, lakini manispaa ya vijijini ilitakiwa ipate shilingi milioni 200. Tulitumia nguvu na jasho kutafuta uhalali wa hizo fedha na *account* zilizopitia. Tulinyimwa takribani siku mbili taarifa za fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri tulipopata hizo fedha katika Manispaa ambayo ilitakiwa ilipwe shilingi milioni 400, tulipata risiti ya shilingi milioni 50. Halmashauri ya vijijini ambayo tumeambiwa imegawanywa shilingi milioni 200 hatukupata risiti ya shilingi milioni 200, tulipata risiti ya shilingi milioni 50 peke yake. Fedha hizi zimeenda wapi? Mimi na wewe nadhani hatujui, lakini lipo vyombo vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda uwandani, risasi wananchi walizopigwa, matukio yote yaliyofanyika, cha ajabu na kushangaza kuna taarifa za mwekezaji, lakini taarifa za wananchi kwenye Jeshi la Polisi hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kijana, Jeshi la Polisi kupitia Mkoa wa Rukwa linapaswa lijitafakari mara mbili. Jambo hili kule uwandani wananchi hawana haki ya kwenda kushtaki Kituo cha Polisi, hukuti taarifa hizi kwenye kata, hukuti wilayani, taarifa hizi zipo Jeshi la Polisi Mkoa peke yake. Ameeleza hapa Mjumbe aliyepita, wale wananchi kwenye lile shamba, shamba lile lilikuwepo enzi na enzi na lilikuwa lina barabara za asili.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana yupo mama mmoja tulipata historia yake pale ambaye alikuwepo na alikuwa ana mtoto mdogo, walimkamata yule mama wakambaka. Walivyomaliza wakamfungia kwenye majumba mawili, lakini yule mtoto mdogo walimtelekeza shambani.

Mheshimiwa Spika, yule mama alipelekwa Magereza na hapa ni kwa sababu ya muda, tungekuonyesha risiti za siku alipotoka Magereza, risiti ipo lakini mtoto alitekelezwa na baadaye mtoto aliokotwa akaenda kupelekwa kijijini. Mtoto amekaa bila mama yake mpaka mama alipotoka Magereza. Haivumiliki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kuuliza Halmashauri ya Manispaa itakwambia taarifa nyingine; ukienda kuuliza vijijini watakwambia jambo lingine. Tunakubali uwekezaji, mwekezaji huyu sawa tumekubali alime shamba, lakini shamba hili kwa zaidi ya 80% linakodishwa na wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati unakodisha shamba unakodisha kwa shilingi 10,000, lakini mwisho kuna fungu la 10. Nje ya fungu la 10 wapo wananchi wanaokodishwa shamba kwa shilingi 100,000 au shilingi 200,000. Ikitokea kuna kiongozi mkubwa ameshafika pale, anapewa lile shamba na wewe mwananchi wa chini hupewi shilingi 100,000 yako; hurudishiwi shilingi 200,000 yako na wala haulimi shamba na utaondoka kwa kipigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 ya mwezi wa Saba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikwenda Mkoa wa Rukwa, alipofika alikutana na hii changamoto. Hata hivyo, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu alisema ipo Kamati ambayo imeundwa na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge anaisubiri ifanye kazi yake. Ahsante Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, jambo hili limekuwa la miaka mingi lakini Mama ulifika na ulijibu kwa kutulia, tunakushukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania una haki ya kuwa Rais wa Mabunge Duniani Mungu amekuchagua. Unatosha. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anatosha. Watendaji wachache ambao hawana nia njema na Serikali yetu hawamwelewi Mheshimiwa Rais nia yake na dhamira yake kwa wananchi wake. Hatutakubali waendelee kutia doa Serikali kwa uzembe wao.

Mheshimiwa Spika, unamwuliza Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, hajui; unamwuliza *RPC,* hajui; unamwuliza mtendaji wa Serikali, hajui; unamwuliza nani, hajui. Wamewekwa kwa sababu gani? Kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja shamba hili lichukuliwe na lirudi kwenye utaratibu. Hatuna shida na mwekezaji, hatuna shida na wananchi, tunachokihitaji ni haki ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Nami niungane na wenzangu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, pili, nakushukuru wewe mwenyewe kwa kuniamini na kuniweka katika Kamati hii japo kwangu mwanzo ilikuwa ni jambo gumu sana ikizingatiwa kwamba nami niliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na baadhi ya mambo niliwahi kuyaona toka kipindi hicho na nikaja kushtuka kuona kwamba mambo hayo bado yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wote humu ndani tumeapa kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba yetu mpaka leo haijabadilika kwamba sisi ni wananchi tunaofuata misingi mojawapo ikiwa ni misingi ya ujamaa inayozingatia udugu na amani. Nikisema ujamaa wengine wanashtuka. Msishtuke, ndiyo misingi iliyotujenga na ndiyo maana hata mpaka leo tunapofanya mambo yetu tunazingatia huyu mwananchi ana hali gani? Anapata nini? Tupange mambo yetu kwa haki ili wote tuweze kunufaika na tuwe na nchi moja yenye amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mwenyekiti wetu kwanza tunampongeza kwa taarifa ambayo ameisoma kama tulivyoshaurina, lakini kwa unyenyekevu mkubwa na kwa kutoa taarifa za wale wananchi kukushukuru wewe kwa kuthubutu kuunda Kamati hii ili iweze kuchunguza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi nimewahi kuwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Kwa hiyo, nathamini kabisa uwekezaji na hasa Mtanzania au Watanzania wanapothubutu kuwekeza. Tunatarajia sasa uwekezaji wa hawa Watanzania uwe ni mfano na alama ya uwekezaji tunaoutaka katika nchi yetu kwa sababu wanafahamu vizuri shida za Watanzania wenzao, wanafahamu vizuri mazingira yetu, wanafahamu vizuri nini maana ya ardhi na kila linalotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu kama ilivyosemwa Ibara ya nane inazungumzia lengo la Serikali ni kuleta ustawi wa wananchi. Ibara ya tisa ndiyo imefafanua kwa kirefu mno mambo mbalimbali tunayopaswa kufanya. Hapa ningependa kuinukuu hii 9(i) inayosema kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yatilie mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada ya kuondoa umaskini, ujinga na maradhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala haya yanayoendelea pale Rukwa, kuna wenzetu tunawaacha waendelee kuwa kwenye dimbwi la umaskini, wataendelea kuwa na changamoto nyingi, kwa hiyo, hao maadui wakuu watatu hawataondoka. Hili jambo lina muda mrefu. Kama ni mtoto amezaliwa mpaka ameenda shule, tufikie mahali liishe.

Mheshimiwa Spika, nafahamu wengine wanakuwa na hofu, Serikali italipa hela nyingi sana, Serikali itakuwaje? Jamani hawa mbona wanaamua tu hiyo hawaangalii! Hakuna gharama katika kuondoa shida za wananchi na hakuna gharama katika kutoa haki kwa wananchi. Tumesema haki haikujengwa katika misingi sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni yetu, na kama ni yetu lazima wote tunufaike nayo kwa uzuri kabisa. Nisingependa nizungumze zaidi, lakini tukumbuke, Taifa hili sasa hivi lina vijana wengi kuliko sisi watu wazima. Pale Sikaungu kote tulipopita vile vijiji ni vijana wenye nguvu wanaotakiwa kupata ajira zao kwa kutumia rasilimali msingi ambayo ni ardhi. Hawana ajira nyingine, lakini wapo. Hata watoto

wameshajenga roho ile ya uadui, ya chuki, ya kuhuzunika kwamba hapa tunanyanyaswa. Kwa hiyo, ni kizazi kinaendelea kukua katika misingi kwamba hatuwasikilizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yawezekana kuna gharama zitahitajika, lakini Serikali hii imeshawahi kulipa fidia za barabara ili tupate barabara, Serikali hii imeshawahi kulipa fidia kwa mambo mbalimbali ya msingi ilimradi wananchi wake wawe na ustawi. Katika hili, Serikali isimame pamoja na Bunge kuhakikisha mgogoro huu unaisha kwa kutatua tatizo hili kama ilivyopendekezwa, iwe ni mwanzo na mwisho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wangu mpendwa Mheshimiwa Mzee Lukuvi leo ni Waziri wetu wa Sera, Bunge na Uratibu, tunashukuru kurudi tena kwenye nafasi hiyo na tunampongeza. Tuliongozana wote tukaenda kule Rukwa na alikuwa ameanza vizuri. Kama siyo kesi ile kusimamishwa, alikuwa ana nia njema. Basi Mungu amemrudisha, amalizie tena jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba wawekezaji wamepitia na wenyewe changamoto nzito nyingi kwa sababu jambo hili hata hili la kubaka na vitu gani siyo kwamba vyote vimefanyika leo, ni hatua za safari yote hii tunayoizungumza.

Mheshimiwa Spika, sasa mambo kama hayo, watu wanaongea na tunazo hata video zao ila hatuwezi kuziweka hadharani. Kwa hiyo, ni mambo ambayo ni mazito, siyo nchi hii ya Tanzania. Tanzania haina tabia hii. Hatuwezi kuendelea kuishi kama hivi.

Mheshimiwa Spika, pia kuna wadau wamenifuata hapa wanasema, mama sema tena basi waangalie na mengine. Mimi nasema hii iwe ni mfano na iwe ni kutukumbusha tufanye vipi masuala yetu ya kiuwekezaji? Tunajali vipi wananchi wetu? Tuangalie na maeneo mengine ambayo pengine yana changamoto kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii kuweza kuchangia ripoti ya Kamati Maalumu ya Shamba la Malonje. Kwa namna ya kipekee kwanza nikupongeze kwa maamuzi yako ya kuunda Kamati ili kuweza kufuatilia mgogoro huu. Mwenyezi Mungu aendelee kukupa maono, aendelee kuwa nawe ili uweze kuona mambo makubwa ya nchi yetu ambayo tunaweza kuendelea kulisaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza nikiwa kwenye Kamati kwa jambo ambalo limeweza kutokea kwenye Kamati, Kamati yako kwa mara ya kwanza wakati tunaelekea kwenye Kijiji cha Malonje, tulipata shinikizo la kutoka na viongozi wa Serikali. Walisema nendeni, kama mtayakuta, basi tuleteeni, lakini muda huo Kamati inakwenda huko inaambiwa maneno hayo kwa dhihaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wanaambiwa maneno hayo kwa dhihaka tunakwenda kule tukaanza kuulizana, hivi kweli hilo suala lipo? Mbona viongozi wa Serikali wanatuambia hivi? Tukaanza kupata wasiwasi, tukasema hili suala tuna wasiwasi halipo. Wakati tunakwenda kule tulivyowakuta vijana ambao wamepigwa risasi na wanawake ambao wamedhalilishwa, sikuwahi kumwona Mheshimiwa Mbunge wa kiume akilia, lakini kwa mara ya kwanza nikiwa ndani ya Bunge zaidi ya miaka 10 niliona Waheshimiwa Wabunge wako wakidondosha machozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walishindwa kuvumilia namna manyanyaso, wananchi wa vijiji hivyo walivyokuwa wakielezea wanavyovipata kwa uwekezaji huu. Tukwambie kwamba umetenda haki kuiteua Kamati kusema wakashughulikie suala hili. Wakati kijana anayeishi

na risasi kichwani anakwenda pembeni, nilikuwa na miongoni mwa Katibu wa Kamati nikasema mbona huyu kijana kama ana shida nyingine? Nikawa na wasiwasi labda ana shida ya akili. Kumbe tatizo lililokuwa likimsumbua, anaishi na risasi kichwani.

Mheshimiwa Spika, tufikirie kama Waheshimiwa Wabunge tumekaa hapa tukiisaidia Serikali, lakini kuna mwananachi ananyanyasika na uwekezaji, anaishi na risasi toka alipopigwa risasi mpaka leo. Hili tusilimalize kuzungumza. Kama itahitaji mchango kwa Waheshimiwa Wabunge, basi tuwaombe Waheshimiwa Wabunge tumchangie na risasi ile atolewe ili aweze kuishi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la wanawake ambao tulishindwa kuwahoji hadharani, tukawaita pembeni kuwahoji. Kati yao kuna mwanamke alituelezea amebakwa na wanaume watatu lakini mwingine amebakwa na vijana wawili ambao ni walinzi wa Shamba la *Efatha*.

Mheshimiwa Spika, wakati hawa akina mama wamebakwa, wakati wanatoa maelezo mmoja aliyebakwa ana mimba ya miezi mitatu, anasema ilibidi akimbie kijiji kwenda nyumbani kwao kwa mama yake. Alipomweleza mama yake akampa dawa za Kiswahili ili mimba itoke kwa sababu ya imani zao, kwamba lile tendo lililofanyika kwake mtoto atakayezaliwa hataishi vizuri. Sisi tukiwa kama Wabunge wanawake hatuwezi kuvumilia hali hii ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa naishi Zanzibar nilikuwa nikisikia na mpaka leo tupo tukijua habari za ukoloni, lakini kwa mara ya kwanza habari ya ukoloni kwenye kichwa changu nimeanza kupata picha yake kwenye Shamba la Malonje lililoko Rukwa. Kilichopo kule ni ukoloni. Leo mfikirie mwanamama ambaye ni mjamzito anataka kwenda hospitali anatengenezewa masafa marefu, lakini njia ipo kwenye shamba hapa mpaka pale unafika hospitali, lakini hawezi. Hatuwezi kukaa kimya kwenye hili.

Mheshimiwa Spika, wanawake, wananchi wanaoishi kwenye yale maeneo wananyanyasika na wanapata shida.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa, Kunambi.

**SPIKA:** Inatokea wapi?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, niko hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida Cassian kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Kunambi.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tauhida anachosema ni sahihi kabisa na hili shamba ni mfano tu wa matukio yanayoendelea nchini kwa mashamba ya namna hii. Matatizo ya namna hii yako katika maeneo mengi nchini. Hata pale Mlimba kuna Shamba la Kambenga wananchi wamekuwa wakinyanyasika kama walivyonyanyasika wale wengine. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili na Bunge lako litende haki pale Waheshimiwa Wabunge wanapoleta malalamiko kama haya, liendelee kutenda haki.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo ambalo pia lilijitokeza, kuna suala la utozwaji wa wananchi wanaokodi maeneo yale kutozwa fungu la kumi. Tanzania watu wake wanaishi wakiwa na dini, lakini Serikali haina dini. Unapozungumzia fungu la kumi linahusu upande mmoja wa imani, kuna baadhi ya imani haiishi kwenye fungu la kumi, leo unashurutisha?

Mheshimiwa Spika, nilimuuliza mhusika, nikamuuliza unapotoza fungu la kumi hudhani kama unahusisha imani? Unamshurutishaje Hamisi Kigwangala na suala la fungu la kumi? Akanijibu, hatukuwaita, wamekuja wenyewe. Haiwezekani wananchi wa Tanzania washurutishwe kwa sababu ya kutafuta kula yao. Haiwezekani washurutishwe kuishi ndani ya nchi yao kwa sababu ya kutafuta tonge lao, anachokitafuta ni mahindi kwa ajili ya kusonga ugali, huwezi kumshurutisha. Kama Serikali yetu haiwezi kushurutisha watu wake kwenye masuala ya imani, hatuwezi kukaa kimya kuwaacha wawekezaji wakashurutisha watu kwenye masuala ya imani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili wakati ulipotupa hii kazi, tulipokwenda kuripoti kwa wenzetu wa Serikali, walitupa picha kutuonesha kwamba ni suala la kisiasa. Hata leo watu wanaweza kukwambia kwamba hili suala ni la kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kwenye masuala ya maslahi ya wananchi hakuna suala la kisiasa na nikuthibitishie kwa kuwa ni mjumbe wa *NEC* nilifanya kujiridhisha, Mbunge aliyekuwepo pale kati ya vijiji vinavyolalamika ni Mbunge wa CCM, lakini wakati tunaenda kuhoji, Mheshimiwa Ester Bulaya atathibitisha, vijana na viongozi wa CHADEMA walikuwa wakija kumsalimia. Niliwauliza, nikawaambia, vipi mbona mko hapa na hili suala tunaambiwa ni la kisiasa? Wakasema kwenye hili hatuna siasa, wananchi tunataka haki kwa wote. Kati ya watu waliofanya kuandika ripoti, mmoja aliyekuwa anazungumza ni mtu wa CHADEMA, ndiye aliyeandika, anasema wakati wanaandika ripoti, sasa siasa hii ni ya chama gani? Siasa hii ni ya chama gani?

Mheshimiwa Spika, Mbunge anafikia kudharaulika na viongozi wenzie wanaotawala, anasema anatafuta kura. Nafuu Mbunge ukubali kushindwa Ubunge lakini wananchi wapate kuishi vizuri. Wabunge wako hatuwezi kuwa waoga, hatuwezi kuwa Wabunge wa kununuliwa, hatuwezi kuwa Wabunge tulioweza kukaa kuishi ndani ya fedha…*(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**TAARIFA**

**MHE.ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naongezea taarifa kwa Mheshimiwa Tauhida kwamba Mbunge huyu pale mkoani ametengwa, anaonekana mchochezi na wakati tumefika hata Mkuu wa Mkoa alilisema hivyo, lakini tunamshukuru Mheshimiwa Rais amemteua kuwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, nimepokea kwa sababu kwenye suala la kujenga nchi ni lazima twende hivyo.

Mheshimiwa Spika, tumshukuru Rais wetu kwa namna anavyoiongoza Tanzania na kupenda watu wake. Tunakushukuru na wewe kwa kumsaidia Rais kwa kiti ambacho umekikalia, unakitendea haki, unastahili pongezi na unastahili sifa.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwa Wabunge waoga, hatuwezi kuwa Wabunge tunaingia kwenye Bunge lako kuogopa kuzungumza kwa sababu kuna watu wanamiliki fedha, hicho kitu hakiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha ajabu ndani ya mkoa kutoka juu mpaka chini, hakuna kiongozi anayeyaona madhaifu hayo, hayupo. Ni kitu ambacho kama Kamati ya Bunge tumeshangaa, kwamba haiingii akilini, hakuna hata kiongozi mmoja na Mbunge anathubutu kupaza sauti yake, lakini anaonekana kiroja.

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru, tuendelee kusema tunashukuru kwa mambo makubwa ambayo unatusimamia ndani

ya Bunge na kwa hayo, naomba kuunga mkono hoja ya Kamati, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikiri kwamba kuzungumza baada ya wazungumzaji wazuri kama hawa huwa ni changamoto kidogo, lakini najua Roho Mtakatifu atanisimamia na nitasema kile ambacho nataka kusema.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kukushukuru wewe mwenyewe kwa uamuzi wako wa kuona nafaa kuwemo kwenye hii Kamati. Kwangu mimi hii ni *privilege*, ni heshima kubwa na nataka nikuhakikishie kwamba kazi yako imefanyika vizuri, imani yako haijapotea bure, nimekuwakilisha nilivyotakiwa, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kuunga mkono yote ambayo yamesemwa na Mwenyekiti wangu pamoja na wajumbe wengine wote. Nilichokikuta kule ni kwamba wananchi wa vijiji vile hawana ardhi ya kulima, huo ni ukweli wa kwanza ambao nimeukuta. Sehemu kubwa ya ardhi yao imechukuliwa na mwekezaji. Sasa kwa sababu hiyo, nakubali kabisa shamba hili libatilishwe na shamba hili liweze kugawanywa tena upya na wananchi wapate sehemu kubwa zaidi ya mwekezaji kama atapata.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba huwa ni mtetezi sana wa wawekezaji wa ndani, nimeshasimama mara nyingi hapa nikasema nitawatetea sana wawekezaji wa ndani ili waweze kumiliki uchumi wa nchi yao. Wajumbe wa Kamati watakumbuka, nilipokuwa natoa mchango wangu mwanzoni nilikuwa nasema, bwana huyu ni mwekezaji wa ndani lazima tumsaidie na yeye aweze kukua. Tukafunga safari kwenda Sumbawanga, kilomita nyingi.

Mheshimiwa Spika, nilipofika kule, niliyoyakuta, niliyoyaona nilibadilisha mtazamo wangu kuhusu wawekezaji wa ndani. Nimekuta umaskini uliopindukia wa watu wa vijiji vile. Hawana mahali pa kulima. Watu wa Sikaungu mwaka huu hawajalima kabisa, hata chakula kinakuwa tabu kukipata.

Mheshimiwa Spika, nimekutana na watu wamekatwa masikio, nimekutana na akinamama wengine wenye umri mkubwa kabisa wamebakwa. Nimekutana na kijana amepigwa risasi ziko kichwani.

*Naomba nikiri nimeokoka na nampenda Yesu, lakini nilipoyaona yale nilijiuliza swali moja, huyu Mwingira, naomba niseme jina, huyu Askofu, na najua ananitazama hivi sasa, hivi huyu ni Askofu kweli? Haya mambo yanaweza yakafanywa na mtumishi wa Mungu kweli? Neno la Mungu kwenye Mithali 14:30 linasema, amuoneaye maskini amdharau Mungu na amhurumiaye maskini amheshimisha Mungu. (Makofi)* **[Maneno Haya Si Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, baada ya haya niliyoyashuhudia, nilibadili msimamo wangu kabisa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Shigongo, ngoja tuliweke sawa, jambo hili.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, tuliweke sawa.

**SPIKA:** Kwa sababu katika wale wawekezaji, zimetajwa kama taasisi. Kwa hiyo, Bodi ya Wadhamini wa Kanisa la Efatha nadhani na *Efatha Foundation* na kuna mahali nafikiri imetajwa *Efatha Heritage*. Sasa akitajwa mtu mmoja kwa jina lake atakuwa hajatendewa haki na Bunge kwa sababu zimetajwa taasisi. Yeye anaweza kuwa ni mkuu wa mojawapo ya taasisi hizo, lakini kwa maana ya hapa, mwekezaji ni hizo taasisi. Kwa hiyo, yeye kuwa kiongozi wa dini na hiyo nafasi yake ya uaskofu lazima *somewhere* atakuwa anaitendea haki hiyo nafasi ya uaskofu, kwa sababu kilichofanya uwekezaji sio Askofu, aliyefanya uwekezaji ni taasisi. Sasa huenda taasisi ziko chini yake, yeye ndiye Mwenyekiti na

mambo kama hayo, mimi sijui kwa sababu sijazipitia. Sasa ili twende vizuri kwenye hoja hii, haya maneno hapa tunayaondoa ili yasilete mkanganyiko baadaye ili sisi tushughulike na mwekezaji. Wewe nenda na mwekezaji na hayo makampuni ambayo ndiyo yametajwa kama wawekezaji. Huyu aliyetajwa jina hapa kwa maana ya Askofu hajatajwa yeye kama ndiye mwekezaji. Ahsante sana Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nikubali, lakini sasa nirekebishe kauli yangu iwe hivi, hivi huyu Efatha kweli huyu Efatha, Huyu Efatha kweli ni mwakilishi wa Mungu duniani? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimeondoa jina la mtu, huyu Efatha. Huyu Efatha amenibadilisha kabisa mtazamo wangu. Nimeokoka nasema nampenda Yesu na Biblia imetamka wazi ya kwamba amuoneaye maskini amdharau Mungu. Kwa matendo haya yaliyofanywa kama kweli ni maelekezo ya huyu Efatha *image* ya kanisa langu inaingia kwenye utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ngoja nielekee kwenye hoja, wananchi hawa ni maskini. Mimi nimezaliwa familia maskini sana na kuingia hapa ndani ya Bunge ni *privilege*. Mimi peke yangu kufika hapa kuna maskini wengine wengi sana wako nyuma wanaohitaji ardhi iwatoe kwenye umaskini wao.

Mheshimiwa Spika, sio mimi tu miongoni mwa wanasheria wako mmojawapo anaitwa Praisegod Lukio anatoka huko Sumbawanga, jirani kabisa na maeneo yale, amesoma shule kimaskini. Elimu imemsaidia kuwa mwanasheria. Tunahitaji kuwasaidia wananchi wa vijiji hivi ili wapate ardhi hii iweze kuwasaidia kusomesha watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haitawezekana katika Taifa hili ninalolifahamu mimi kukaa na watu ambao wako juu ya sheria. Hakuna mtu ambaye yuko *above the law*; wote tunaheshimu Katiba ya nchi yetu, tunaheshimu sheria ya nchi yetu. Haiwezekani mtu

mmoja anafanya vitendo vya kinyama kiasi hiki, taasisi moja inafanya vitendo vya kinyama kiasi hiki halafu hakuna hatua inayochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanafanyiwa yote haya, mtu hafikishwi hata polisi. Mimi kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitasimama na wananchi wa nchi hii, nitasimama na upande wa haki siku zote za maisha yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme, shamba hili ni kubwa sana. Nilitembea shamba lile unaenda umbali mrefu sana uko ndani ya shamba moja. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge. Namwomba sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa, hapa Mheshimiwa Jacqueline.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamsimamisha anayekuwa anazungumza ni kwamba sentensi yake anakuwa hajamaliza. Kwa hiyo na akirejea kwenye kuzungumza hataweza kumaliza ile sentensi yake. Kwa hiyo, ukisema taarifa, nakuwa nimeshasikia, akimaliza akifika mahali nakunyanyua, usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Shigongo, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

**TAARIFA**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa mchango mzuri wa Mheshimiwa Shigongo.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba kutokana na hoja nzuri ambayo anaizungumza kwamba hakuna sheria yoyote wala hatua zozote zinazochukuliwa dhidi ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia unaofanyika, maana tumesikia kuna kubakwa, kuna watu kulawitiwa, kuna kukatwa masikio. Sasa naomba kwa niaba ya

Serikali Waziri mwenye dhamana ya ukatili wa kijinsia Mheshimiwa Gwajima akaishtaki Efatha kwa niaba ya Serikali.  Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ili kesi iweze kufika Mahakamani ni lazima uchunguzi ufanyike na nadhani kwenye mapendekezo ambayo Kamati Maalum imeyaleta mbele ya Bunge hiyo ni sehemu kwamba uchunguzi wa kina ukafanyike ili ikijulikana hayo matendo yamefanywa na watu fulani basi watu hao wachukuliwe hatua za kisheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa Gwajima yeye hawezi kwenda kushtaki lazima ule utaratibu wa kisheria tuliouweka ufuatwe.

Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya dada yangu Mheshimiwa Jacqueline Msongozi. Sasa nimalizie kwa kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nafahamu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Rais mwenye huruma, ni Rais ambaye anafikiria sana maisha ya watu wake. Katika hili naomba sana aliunge mkono Bunge lake Tukufu na kama ni kubadilisha hati ibadilishwe hati mara moja na wananchi waweze kupata maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Spika, umaskini ni kitu kibaya sana. Naongea habari ya mwanasheria wako Lukio, anatoka maeneo yale yale, amekulia kwenye umaskini ule ule. Wazazi wake wameuza mahindi wamempeleka shule, leo ni mwanasheria. Tunahitaji watu wengine wengi katika nchi hii watoke familia maskini wawe kama sisi. Hawawezi kufika tukiendelea kuwanyang'anya ardhi na kumpa mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, nisiseme mengi sana, naomba niunge mkono hoja na ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Thomasi Mayenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kutoa mawazo yangu. Nianze kwa kusema, kabla sijasahau kwamba, naunga mkono hoja ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kuniamini kuwepo kwenye Kamati hii Maalum ya Uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu, Rais Mkapa aliwahi kusema maneno yafuatayo; *"lakini uongozi ni kuonesha njia, kuonesha njia ni kuwafanya watu waridhike kukuona wewe uko mbele na wao wako nyuma wanakufuata, wanakufuata si kwa jambo lolote bali kwa matendo yako, uwajibikaji wako, kauli zako na kadhalika."*

Mheshimiwa Spika, kwa hiki ambacho umekifanya…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge keti, anayezungumza unamkata pale, ahsante.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa hili ambalo umelifanya umeonesha kwamba wewe ni kiongozi. Matatizo haya, niseme sakata hili, suala hili limekuwepo kwa zaidi ya miaka hamsini, lakini sasa hivi tunaona chini ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, chini yako tunaamini wanawake wanaweza, wanawake wana huruma, wanawake ni watu ambao utendaji wao unaonekana kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hili mimi nilikuwa naomba kusema yafuatayo; baada ya pongezi hizo, mimi nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Rais awawajibishe pale kwenye ule mkoa kuanzia vyombo vya dola na watendaji wake wote. Uzuri ninafahamu kwamba Kamati hii ilivyoundwa, ulivyotuteua Mheshimiwa Rais wetu

anafahamu na anafuatilia. Niwatoe mashaka kwenye jambo hili hakuna mtu atapona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu kuna watu ambao kwenye haya maisha wakishakuwa kwenye nafasi za uongozi wanajisahau sana. Tumekwenda pale, tunaambiwa kwamba taarifa za Efatha zipo Polisi, taarifa za wananchi yale madhila yote ambayo wanafanyiwa taarifa hazipo, inauma sana. Wenzangu waliotangulia wameelezea kwa ujumla wake, lakini mimi nataka kusema kitu kimoja.

Mheshimiwa Spika, siku moja niliwahi kusema kwamba, hii nchi kuna baadhi ya watu na baadhi ya vingozi ambao hata kama wamestaafu au wapo huko nje wanaweza kupigwa mawe ukielezewa waliyoyafanya kwa sababu, haiingii akilini. Kwenye hili nampongeza sana Mwenyekiti wetu wa Kamati Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya amefanya kazi kubwa, *lobbing* ya hawa watu ilikuwa ni ya kiwango cha juu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati, ambao hatukukubali kushikwa kwamba, hiki msikifanyie kazi, hiki msikifanyie kazi. Wale wa mkoani pale walionunuliwa wanajijua wenyewe. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakaa unamwita mtu alikuwa ni kiongozi pale kwenye mkoa, unamuuliza hili jambo ilikuwaje? Anaishia tu kusema, jamani kusema ukweli naomba mnisamehe, hili jambo ilikuwa tu ni bahati mbaya, inauma sana. Leo watu pale wanashindwa kulima, leo watu pale wanashidwa kufanya shughuli zao za maendeleo na amewahi kutoka kiongozi mmoja akasema kwamba, wale wananchi pale ile ardhi ni kubwa sana. Kwamba, maeneo ya wao kulima yanatosha kufanya shughuli zao. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekwenda tumeona hali halisi, haipo hivyo. Mimi nilikuwa na wazo lingine pia, miaka ya zamani, miaka ya nyuma huko kwenye hii Serikali ilikuwa mtu akiwa mkurugenzi, pengine labda viongozi wengine wakubwa kwa nafasi mbalimbali,

moja kati ya adhabu zao ilikuwa ni mtu akifanya makosa, alikuwa Mkurugenzi Dar es Salaam, wanasema huyu tunakwenda kumtupa Sumbawanga huko. Nadhani Watanzania mtakuwa mnakumbuka.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa kuna baadhi ya maeneo yanaonekana kama vile mtu ukitolewa sehemu nyingine ukapelekwa kule ndiyo umekwenda kutupwa. Ninaomba Serikali iangalie imetupa watu wa aina gani huko tunawaletea watu matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu, haiingii akilini mnakaa mnaongea na baadhi ya viongozi, *RPC* yupo pale, Mheshimiwa *IGP* najua unanisikia, *RPC* yupo pale unamuuliza hili jambo limekaa-kaa vipi? Anasema mimi bahati mbaya ndiyo nimeingia mgeni, nina muda fulani. Baadhi ya viongozi pale Mkoani, wanaweza kusema sisi wakati mambo haya yanatokea, wakati madhila haya yanatokea tulikuwa wageni, lakini ulivyokuwa mgeni baada ya kufika hujawahi hata kusikia?

Mheshimiwa Spika, kiongozi mmojawapo pale akasema, mimi sikupata nafasi ya kwenda kuongea na wananchi kusikia matatizo yao na mateso yao, ila nilipata nafasi ya kwenda kuongea na huyu mwekezaji nikanywa naye chai. Roho inauma, hiyo chai ilikuwa imetiwa nini?

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema ifuatavyo, maana hizi chai hizi watu huwa wanapewa chai huko wanajisahau wanasaini vitu vya ajabu. Watu huwa wanapewa chai hata huko nje wanatuingiza kwenye matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ya Efatha, naiomba Serikali kwa ujumla wake ifanye uchunguzi maalumu kwake, lakini pia, vilevile na kwa taasisi zote za uwekezaji Tanzania, aidha ziwe za kidini au wawekezaji wa kawaida na nashukuru sana kwamba kwenye Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ameingia kaka yangu Mheshimiwa Jafo ambaye namwamini sana. Naomba Mheshimiwa Jafo, huu mwavuli wa uwekezaji, *in bracket,* huu unatutia kwenye

matatizo makubwa. Yapo maeneo mengi nchini baadhi ya watu wanalalamika, mashamba yao, maeneo yao ardhi zao, zimechukuliwa na kadhalika. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifanye tathmini kwa ujumla wake kwenye suala la uwekezaji, lakini kwa huyu mwekezaji huyu, ameshaonesha kwamba, hana roho ya huruma wala hana msamaria mtume. Kwa hiyo, naiomba Serikali huyu mwekezaji imwangalie kwa jicho la kipekee. Maeneo yote ambayo amewekeza nchini, Serikali iweze kuangalia.

**SPIKA:** Kuna Taarifa, Mheshimiwa Lucy. Inatokea wapi?

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa kwa nani tena jamani? Mimi hizi Taarifa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Francis.

**TAARIFA**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ili tuweke Taarifa za Bunge vizuri, uwekezaji haupo tena Viwanda na Biashara, upo kwenye Wizara ya Uwekezaji kuna Wizara yake. Kwa hiyo, nampa Taarifa hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana ni sahihi ipo chini ya Mheshimiwa Profesa Kitila, lakini na yeye pia, namuamini ni Profesa mzuri, mtendaji mzuri, kwa hiyo, nina uhakika kwamba, mambo yatakwenda sawa sawa, lakini ninachoomba pia, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na masuala ya Uwekezaji na yeye pia, anaingia humo kwa njia moja au nyingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jafo hili pia na yeye yumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba, taasisi hii iweze kuangaliwa upya. Taasisi hii imechukua maeneo mengi sana kwenye hii nchi. Ukiangalia maeneo ya Kilolo taasisi hii ipo, ukiangalia maeneo sijui ya Handeni taasisi hii ipo, lakini katika haya maeneo yote unakuta kila sehemu kuna mgogoro. Kuna kitu gani?

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukasema kwamba, baadhi ya hao wenzetu wengine ni taasisi za kidini, kuna baadhi ya mambo labda pengine tuweze kuyanyamazia nyamazia, lakini wanaoumia ni wananchi wetu na wako wengi sana. Nchi za jirani wameshaanza kuchukuwa hatua huko kufungia baadhi ya makanisa, kufungia baadhi ya taasisi za kidini. Wanaamua kufanya namna hiyo kwa sababu, ukilinganisha kinachofanyika na faida kwa wananchi ni mambo ambayo hayaendi katika uwiano unaofaa.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Deus Sangu, kwa jinsi ulivyoweza kusimama bila uwoga katika suala hili. Unapokuwa kwenye jambo kubwa kama hili, hii ilikuwa ni vita maana alishaambiwa kwamba, hatapita, alishaambiwa kwamba, utawekewa watu, alishaambiwa kwamba hutafanikiwa kwenye hili jambo kwa sababu, watu wanawajua wanaokula nao, lakini nampongeza Mheshimiwa Deus Sangu kwa kusimamia hili bila uoga na huu ndiyo uongozi unaotakiwa. Kiongozi ukiwa muakilishi wa wananchi, usipokubali kununuliwa, hakuna jambo litashindikana hata Mwenyezi Mungu atakuwa upande wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu yupo hapa, Mheshimiwa Dotto Biteko, kwa niaba ya wale wengine ambao hawapo hapa. Naomba na naomba pia, na Mheshimiwa Rais afanye uchunguzi kuhusu viongozi ambao wanafaidika na yule mwekezaji pale Sumbawanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tumefika pale, mtu anaanza kukuita, unajua hili jambo lipo hivi na hivi, unajua hili jambo lipo hivi na hivi. Kuna watu wanafaidika pale, wanalimiwa. Inauma pale ambapo mtu amekaa yupo Wizarani halafu kuna watu wanamlimia kule,

wanakuja kumwambia kuna mzigo wako wa magunia 500 ya mahindi, *this is not fair and this can only happen somewhere else not in Tanzania.*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, naomba Waheshimiwa Wabunge waunge mkono, tumefanya kazi nzuri bila kumwonea mtu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda sana kwa hivyo, wale mnaoleta vikaratasi sasa hivi basi, majina yapo mengi bado hapa.

Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani na Mheshimiwa Condester Sichalwe ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye kamati hii muhimu. Kwanza nakushukuru kwa kuniamini kuwemo kwenye Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mungu aliyekuongoza kuweza kuunda Kamati hii. Nasema hivi kwa sababu, hawa wananchi inaonesha wamepata shida, wamepata mateso muda mrefu, sasa Mungu ameamua, kupitia wewe, aweze kumaliza mgogoro huu na naamini utaisha.

Mheshimiwa Spika, kama walivyochangia watangulizi wenzangu, kwa kweli ukifika kule *site* ukawaona wale wananchi mateso ambayo wameyapata, umaskini walionao, namna ambavyo wananchi wamepigwa na kunyanyaswa, kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha sana. Tunapenda wawekezaji, lakini wawekezaji wa namna hii kwa kweli, Serikali iwaangalie kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linasikitisha, niseme nimeokoka na naamini hapa Bungeni hakuna mtu ambaye ana mashaka na wokovu wangu.

**MBUNGE FULANI:** Wacha wee.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, lakini taasisi za namna hii ambazo tulitegemea zivutie watu kumjua Mungu, watu waache uovu, ndizo zinazofanya uovu, ni jambo ambalo linaumiza. Wakati mwingine sisi ambao tunatamka tumeokoka unaposikia mwenzako, taasisi inatangaza wokovu, halafu inafanya vitendo vya namna hii ni masikitiko makubwa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, taasisi za namna hii kuna haja ya kuchunguzwa. Tulisikia Uganda alijitokeza mtu mmoja anaitwa Kibwetere akawakusanya watu mwisho wa siku akawaangamiza, haya ndiyo tunayoyaona ya namna hii. Wanajificha kwenye mgongo wa kumtaja Mungu ili watu wajue hawa watu wana Mungu kumbe nia yao ni mbaya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate, hoja iliyoko Mezani inahusu Shamba la Malonje. Waheshimiwa Wabunge lazima tuelewane vizuri, ili isije ikaonekana ni dini fulani inayojadiliwa humu ndani, ili isije ikaonekana ni imani fulani ndiyo inayojadiliwa humu ndani. Kwa hiyo, muelewe tu Bunge ni lazima lifanye kazi yake Kikatiba na kazi tuliyopewa Kikatiba ninyi nyote mnaifahamu, leo sitakuwa na maneno mengi sana hapa mbele. Kwa hivyo, ni lazima Mheshimiwa Mbunge aongozwe kuelekea huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Bilakwate mjadala kuhusu imani pengine siku nyingine tutakapokuwa na hoja Mezani inayohusu hilo, tutaijadili vizuri, lakini kwa maana ya mjadala uliopo Mezani sasa hivi imani ya wale watu, tuwaache na imani yao, tushughulike na huu uwekezaji ambao upo kwenye Shamba la Malonje ambao umeleta changamoto. Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nafikiri ujumbe umefika.

Mheshimiwa Spika,Jambo lingine ambalo linasikitisha ukija kuangalia namna shamba hili lilivyoanza kutangazwa mpaka

linafikia hatua hii kuna mazingira ambayo yanaonesha kulikuwa na rushwa. Kwa sababu gani nasema kuna mazingira? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Baraza la Mawaziri kama yangefuatwa, lakini na jambo lingine la shamba hili ni kitendo cha kuuzwa bei ndogo na baada ya mwaka mmoja hajawekeza kitu chochote cha kupandisha shamba hili akaenda kukopa zaidi ya shilingi bilioni mbili, bilioni tatu na zaidi. Jambo lingine ni uongozi wa mkoa ungechukuwa hatua juu ya vitendo hivi ambavyo vilikuwa vinaendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linanipa mashaka na kuamini kuwa, kuna mazingira ambayo sio mazuri maana Biblia inasema, "rushwa hupofusha hata haki isitendeke". Kitendo cha Uongozi wa Mkoa kuidanganya kamati na kutengeneza mazingira ya kutushawishi tuamini kuwa, kule hakuna mgogoro ni mazingira ambayo kwa kweli, yanatia mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipofika tukaamua kwenda kwenye Uongozi wa Mkoa, lakini tulivyoelezwa tulifika sehemu tukasema mmh, ina maana hiki kitu kilichoundwa kuna uwongo? Yaani tuliingia kwenye wakati mgumu, lakini tukasema aah, ngoja twende na *site* tuone hali ilivyo. Kufika *site,* mnaambiwa hakuna mtu aliyepigwa risasi, mnakuta watu wamepigwa risasi, tukaambiwa na Uongozi wa Mkoa kuwa, hawa wanaolalamika wametoka Mkoa wa Mbeya, lakini tulipofika kule tukawauliza wananchi, hawa watu wanaosema wamepigwa risasi, hawa wakina mama wanaodai wamebakwa ni wa eneo lipi? Wakasema ni wa hapahapa na nyumbani kwao tunaweza kuwapeleka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa mazingira haya sio bure. Kuna haja ya kuendelea kuchunguza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuendelea kuchunguza hata uongozi wa Mkoa kujiridhisha hao

watu walikuwa wapo na mazingira gani hayo ambayo yalikuwa yanatushawishi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Asia Halamga.

**TAARIFA**

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumpa Taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Bilakwate. Ukienda kule *site* Mwekezaji *CSR* yake ameamua kujenga Kituo cha Polisi ndani ya shamba, lakini hajaamua kujenga zahanati kwa wananchi kule kwenye kijiji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa sababu, sisi tulitegemea Kituo cha Polisi kijengwe kwenye jamii, kisaidie jamii, lakini kimejengwa kwenye eneo ambalo muwekezaji anadai ni eneo lake. Kwa hiyo, haya mazingira kwa kweli, yanatia aibu na yanafedhehesha kwa viongozi ambao wameaminiwa na Mheshimiwa Rais waende kumsaidia, lakini hawamsaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na naomba sana, namwomba sana Mheshimiwa Rais, mapendekezo yote ayafanyie kazi, ili wananchi wale waweze kupata haki, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Sichalwe.

Mheshimiwa Condester Sichalwe na Wabunge wanaofuata hapo, wawili, watachangia kwa dakika tano, tano. Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia jambo hili muhimu sana.

Nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuunda Kamati hii, ni kamati ambayo imelitendea haki Bunge, imetutendea haki Wanarukwa, imewatendea haki sana wananchi wa Mkoa wa Rukwa, hasa wanaotokea Wilaya ya Sumbawanga Vijijini. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati taarifa inasomwa hapa akili yangu ikawa inafanya rejea. Mwaka 2016 nikiwa Mbunge wa Viti Maalum nilitoa hiyo taarifa hapa Bungeni, malalamiko juu ya manyanyaso ambayo wanapata wale wananchi. Mwaka 2017 wakati nazungumza nikapewa taarifa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwela, 2017. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zimeshafanyika taratibu mbalimbali kwenye eneo lile, tume mbalimbali zikitumia fedha za Serikali ambazo hazikuweza kuleta matokeo chanya mpaka limefika hapa ndani Bunge. Nashukuru kwa namna ambavyo kamati imeenda kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa. Wamefanya kazi kwa kujituma na wamekuja kuleta matokeo ya kile ulichowaagiza, kwa ulivyowaamini na wao imani hiyo wameilinda, wameleta hicho kitu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na athari ambazo zimezungumzwa hapa ikiwemo unyanyasaji kwa wanawake na wananchi wa maeneo yale kuanzia mwaka 2014 mpaka 2017 nilikuwa naishi kwenye hayo maeneo. Natambua tuna kiasi cha kusema hapa ndani Bungeni, nakubaliana na mapendekezo yote ya kamati, lakini naendelea kulishauri Bunge lako, hatua stahiki zichukuliwe kwa kwenda kufanya tathmini ya kina na uchunguzi wa kina juu ya athari zilizojitokeza katika yale maeneo miaka yote hii mfululizo.

Mheshimiwa Spika, wapo wanafunzi ambao nilikuwa nasoma nao kuanzia 2014, baada ya machafuko yaliyokuwa yanaendelea waliacha masomo, maisha yao yameharibika mpaka leo. Hatuwezi kujua, pengine tungepata Rais kutoka pale, maisha yao yaliishia pale. Ninajiuliza, hivi tumefikaje hapa? Nini kilikosekana miaka yote mpaka leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, nikagundua tulikosa uzalendo kwa wale waliopewa nafasi ya kuaminiwa kumsaidia Mheshimiwa Rais. Malalamiko haya yametolewa ndani ya Bunge zaidi ya mara 17, lakini yamekuja kuonekana na uzito zaidi na Mbunge wa Jimbo wa sasa. Pamoja na nia njema ambayo uliionesha na dhamira hii kwa hatua ambayo tumefikia sasa hivi, Taifa letu hatuwezi kusema hatuwahitaji wawekezaji, tunawahitaji wawekezaji, lakini tunahitaji uwekezaji wa namna gani? (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kinachofanyika leo pale, Serikali inachopata na athari walizopata wananchi ni sawasawa? Athari zilizojitokeza mpaka leo kuna haja ya kuendelea kufikiria kuwa na wawekezaji wa namna hii? Najiuliza, shida ilikuwa ni makubaliano yaliyowekwa kwenye mkataba?

Mheshimiwa Spika, shida ilikuwa kuna jambo lingine lililokuwa nyuma ya kile kilichoandikwa kwenye *documents* zile? Shida ni kuwa mpaka hapa tulipofika ni kwamba viongozi waliokuwepo kipindi chote na hawakujua athari za haya yaliyojitokeza au tuliamua kuweka pamba masikioni?

Mheshimiwa Spika, leo yule ambaye anayeishi na risasi kichwani, tunaweza kuthaminisha na nini kwenye nchi yetu? Yule mama ambaye alibakwa, sijui hata kama walikwenda kupimwa. Inawezekana kuna athari kubwa zaidi ambazo wamezipata; ndiyo maana naendelea kusisitiza kuna haja ya Serikali kwenda kufanya tafiti za kina juu ya athari ambazo zimejitokeza. Hata kama haya ambayo yameelezwa hapa yakithibitika kwamba ni kweli yalifanyika, ni kweli yalitokea, hatua siyo kubatilisha tu. Hatua zichukuliwe kwa wote ambao wamefanya makosa haya kwa mujibu wa sheria zetu za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufanya hivyo wananchi wataendelea kuamini kwamba Serikali imesikiliza na imechukua hatua. Kama wamekwenda wameona makovu, siku ambayo Mbunge wa jimbo anatoa hoja yake hapa ndani tukasimama, yule mgonjwa akawa amekimbizwa Hospitali ya Rufaa Mbeya. Hatua zilizochukuliwa

mpaka leo ukiziangalia angalia unagundua yanaonesha hapo katikati kuna mambo ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba watu wote hawafahamu, kule Rukwa siyo kwamba hatuna wasomi, siyo kwamba wateule wote wa Mheshimiwa Rais waliopo kule hawajui kwamba kulikuwa na shida, kwa nini wamesubiri?

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja tu la kujiuliza, kama mwananchi huyu amepigwa risasi, tena hatua zilianza kuchukuliwa baada ya ripoti kuja Bungeni, waliopo kule wanaohusika na vyombo vya ulinzi ndio wanaanza kuulizwa wakati wao ndio walipaswa watoe taarifa mapema na hatua zichukuliwe kabla ya kuja hapa ndani Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto hii iliyojitokeza katika Shamba la Malonje athari yake ni kubwa kuliko hivi inavyoelezwa. Kuna wakati ulifika ukienda kwenye nyumba wanaume wote wamekimbia. Nini kinatokea? Athari yake siyo kwa ajili ya mama tu. Ndiyo maana nasema kuna wanafunzi niliokuwa nasoma nao mimi waliacha shule. Haki yao ya msingi ya elimu wakanyang'anywa kwa sababu ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuna haja, hatua hii ambayo umeitoa leo, hatua nyingine ziendelee baada ya hapa mapema zaidi. Kama kuna viongozi wameshiriki kwa namna yoyote ile hatua zichukuliwe. Wakati tunakwenda kufikiri kupima upya, tuangalie mazingira ambayo tutaacha wananchi wa eneo lile wakiwa salama. Maisha yetu watu wa Rukwa ni kilimo na ndiyo uchumi wetu. Leo ukiwambia wasilime, unataka wafanye nini? Unataka kuzalisha vibaka mtaani? Maisha ambayo sisi hatukuyazoea. Pamoja na kwamba kuna changamoto kwenye hizo hatua zilizopitiwa hapo, namna ya kuongeza mkataba, mkataba wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hivi nchi yetu mbona ina wanasheria wengi nguli kabisa? Kama shida ilikuwa ni kwenye mkataba, hili si lilikuwa suala la kufanya maamuzi tu. Sasa mpaka athari hizi zimejitokeza,

tunataka nini kingine kijitokeze baada ya haya mambo yaliyotokea Mlonje?

Mheshimiwa Spika, nashauri pamoja na mapendekezo haya ambayo Kamati imeleta, kuna haja sasa wanapokwenda kuchukua hatua yoyote, ushirikishwaji wa jamii ile uwe wa kina. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili wananchi wale wanahitaji kupewa elimu, kama ni uwekezaji wajue wao wananufaika nini na uwekezaji huo na hili jambo limekuwa shida sana kwa Taifa letu. Tunawekeza, wananchi wanaozunguka lile eneo la uwekezaji hawaoni manufaa ya uwekezaji huo. Lazima tujiulize tunawekeza kwa ajili ya nani? Kama ni tunawekeza kwa ajili ya Watanzania, je Watanzania hao wananufaika na huo uwekezaji?

Mheshimiwa Spika, lazima tukae na tuwe tunafikiri tena…

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** …haya matatizo yanayojitokeza leo yatufundishe…

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Felista Njau.

**TAARIFA**

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nilitaka nimpe Taarifa Mheshimiwa Khenani kwamba, pamoja na usaidizi utakaofanyika, tuombe pia wasaidizi wa mambo ya kisaikolojia. Wanawake waliopata shida ya kubakwa na vijana waliopigwa, wapate usaidizi wa kisaikolojia mapema, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea Taarifa hiyo na niendelee kusema, tunapozungumzia suala la ekari 25,000 ni lazima tujiulize ukubwa wa lile eneo pale na idadi ya watu waliopo. Je, kuna haja ya kuendelea kuwekeza kwa namna hiyo? Tunategemea ile jamii itaishije?

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema inayoendelea, niendelee kusema kama watajiridhisha, wakagundua kuna ukiukwaji uliofanyika pale wa kina kabisa, sitegemei kwamba tutaipata faida ya yeye kuendelea kuwa mwekezaji kwenye maeneo haya. Kuna haja ya kufikiri upya, kama bado wanafikiri kuhusu mwekezaji, basi ni tutafute mwekezaji mwingine ambaye hawezi kuleta migogoro kama hii na ataleta mahusiano mazuri kati ya yeye mwekezaji na jamii inayomzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa yote yaliyopendekezwa na Kamati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hawa wanaomalizia, dakika tano kila mmoja. Mheshimiwa Condester Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul, tutamalizia na Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niungane na wenzangu kutumia nafasi hii kukupongeza sana kwa jambo zuri na kubwa ambalo umelifanya la kuunda Kamati hii ya kizalendo. Pia nitumie nafasi hii kuendelea kuwapongeza Wabunge wenzangu ambao walikuwa ni Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wamefanya. Siyo kwamba wamefanya kwa watu wa Jimbo la Kwela (Malonje), wamefanya kwa ajili ya Watanzania wote. Pia, naamini hata Watanzania ambao wanasikia mjadala huu wanaendelea kuwaombea

Mheshimiwa Spika, changamoto kama hii ipo katika maeneo mengi kwenye nchi yetu na katika nyakati tofauti inawezekana Wabunge wamekuwa wakija hapa wakieleza, wakati mwingine

kupuuzwa na kutokusikilizwa. Matokeo yake ndiyo yanaleta madhara makubwa kama haya. Laiti kama Wabunge wangekuwa wakija na kusema changamoto zao hapa na zikachukuliwa harakaharaka na watu wakaacha kulindana, yamkini tungekuwa hatufiki kwenye matokeo kama haya ambayo tunaendelea kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshawahi kusimama hapa Bungeni, juzi tu hapa kwenye Bunge la Bajeti ambapo Waziri akiwa ni Mheshimiwa Jerry Silaa. Nikarejea maneno ya Baba wa Taifa ambayo aliyasema mwaka 1958 na leo narejea tena. Baba wa Taifa alisema hivi:

*"Katika nchi kama yetu ambamo Waafrika ni maskini na wageni ni matajiri kuna uwezekano mkubwa kwamba, mwafrika akiruhusiwa ardhi yake katika miaka 80 au 100 ijayo, ardhi yote ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri na wageni na wenyeji watakuwa watwana, lakini hata kama wageni wasingekuwa matajiri litaibuka tabaka la Watanganyika (ambalo ndilo hawa akina Efatha Ministry) matajiri na wajanja. Tukiruhusu ardhi iuzwe kama njugu, katika muda mchache kutakuwa na kundi dogo la Waafrika wakiwa na ardhi na wasiokuwa na ardhi watakuwa ni wengi ambao watakuwa ni watwana."* Maneno ya Baba wa Taifa yaliyoongelewa mwaka 1958.

Mheshimiwa Spika, wako Watanganyika wenzetu wajanja ambao ndio hao akina *Efatha Ministry*, ambao wameibuka kwa sababu wana misuli na wana pesa wanaendelea kusumbua wenzao.

Mheshimiwa Spika, mfano tu, kama wa sakata hili la Shamba la Malonje; kule Momba kuna mwekezaji mmoja pia ana tabia kama hii hii, anafanya matukio kama haya haya na anaendelea kunyamaziwa. Wanataka kuna siku tuje hapa tuanze kueleza mambo mengi, ameshadhuru watu, watu wameshaumia na wameshateseka. Nafikiri Serikali itumie wakati huu kujifunza kupitia Shamba la Malonje. Kwa maeneo mengi ambayo hayapo hapa

Tanzania na yanapitia changamoto kama hizi na Wabunge wameshawahi kueleza.

Mheshimiwa Spika, halafu tabia ya kuwadhihaki Wabunge, Mbunge akija akiongea hapa wanasema ni mambo ya siasa. Huwa najiuliza Rais anafanya jambo gani? Mheshimiwa Rais wa nchi hii kupatikana na watu wote aliowateua kama Mkuu wa Mkoa na viongozi wote, ni kiongozi wa siasa na ndiyo atatengeneza mfumo tulionao. Bunge tunafanya kazi kwa siasa. Tukija kutetea watu hapa, kwa nini wanaibua maneno ya kusema ni mambo ya kisiasa?

Mheshimiwa Spika, kule Momba kuna huyu mwekezaji anaitwa Jihumbi, ameshawahi kuteka watu zaidi ya watu 50 kijijini. Alivyowateka akawanyang'anya simu na mengine ambayo aliyafanya huko anajua yeye mwenyewe. Yupo tu anaendelea na anaendelea kuchukua ardhi ya kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tufike hatua ambayo wanawake wanabakwa kwenye ardhi ya kwao wenyewe? Halafu ni tabia gani watu waliotunza ardhi yao wenyewe miaka na miaka, wamezaliwa na babu zao wamezaliwa hapo, halafu anakuja mtu mmoja tu eti kwa sababu ni Mtanzania ambaye ni bepari (beberu) anakuja anaanza kuwatesa wenzake, anaangaliwa tu eti kwa sababu ni Mtanzania na anaruhusiwa kumiliki ardhi mahali popote pale.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nafikiri hata hii sheria pia inapaswa kubadilishwa, kwa sababu kusema tu Mtanzania anabidi akamiliki ardhi mahali popote inawatesa baadhi ya watu, inawaumiza na ndiyo matendo kama haya yanaendelea kuja. Nafikiri ni wakati sasa Serikali itumie tukio hili la watu wa Jimbo la Kwela kujirekebisha na kwenye maeneo mengine ili Watanzania wasiendelee kunyanyasika.

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana kwa jambo la kiungwana na Wabunge wenzangu ambao walipata hiyo nafasi Mungu awabariki kwa uzalendo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pauline Gekul atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma na mtoa hoja ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi na nashukuru kwa hizi dakika tano. Naomba niwapongeze Wanakamati kwa taarifa hii nzuri ambayo imemgusa kila mmoja wetu.

Mheshimiwa Spika, Wanakamati ambao wamekwenda *site* wamejionea mambo mengi. Kwa sisi ambao tunasomewa hapa naamini ni mambo machache tu ndio wanayotusomea. Umefanya busara kubwa sana kutuma Kamati hii. Naomba kwa moyo wa dhati tukupongeze kama ambavyo wenzangu wamekupongeza.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye mioyo yetu Wabunge tunatamani Kamati hii ifike kwa kila jimbo ambako migogoro hii ipo. Mimi binafsi natamani Kamati hii iwe endelevu, iende kwenye maeneo yote ambayo matatizo haya yapo. Ni kwa vile tu muda ni mchache, lakini haya ambayo yameelezwa kwenye shamba hili la Malonje na Mheshimiwa Condester amezungumza hapa kwa jimbo lake na maeneo mengine. Naamini kila Mbunge akisimama, ambao wana mashamba haya makubwa ya wawekezaji wanakutana na matatizo haya, ni dhahiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu ni kwamba kazi hii imefanyika chini ya kiti chako na maelekezo yako na Wanakamati wamefanya vizuri. Pia kimsingi wameepukana na rushwa labda na vishawishi kama ambavyo wamesema.

Mheshimiwa Spika, niombe ikupendeze, Wizara ya Ardhi wakae watafakari. Kuna *move* ilikuwa imeanzishwa ya kuhakiki mashamba ya wawekezaji ambayo hayatumiki. Ile *move* naona imeishia hewani. Kuna wawekezaji ambao wanamiliki mashamba, lakini hawafanyi kile ambacho walipaswa kufanya. Nadhani wenzetu wa Wizara ya Ardhi wana Makamishna kila Mkoa, hebu sasa wamalizie pale ambapo kuna kazi ilikuwa imeshaanza ya kuchambua yale mashamba ya wawekezaji ambayo hayatumiki.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwenye nchi yetu kuna wawekezaji wana mashamba lakini hawayatumii ipasavyo. Mimi binafsi jambo hili la Malonje linanigusa kwenye Jimbo langu la Babati Mjini. Kuna Shamba la Dudumera ambalo nimshukuru Mheshimiwa Waziri Lukuvi aliwahi kulitolea maamuzi. Wananchi wa Dudumera lakini na wananchi wa Singu, mashamba mawili haya nimekuwa nikiyasema na natolea mfano. Mheshimiwa Waziri Lukuvi alilitolea maelekezo Shamba la Singu kwamba wananchi wapewe ekari 829, lakini mpaka leo hakuna maamuzi, mpaka leo yaliyoagizwa hayatekelezwi. Katika shamba hili kulikuwa na maelekezo ya Wizara, lakini kule chini kwenye mikoa maamuzi haya hayafanyiwi kazi, wananchi wanateseka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi langu kutoka moyoni hii kazi iliyofanyika ni kubwa na ni nzuri. Hebu tuombe sasa iwe ni *wakeup call* kwa ajili ya maeneo yale ambayo kazi hii haijahitimishwa ili wale wananchi wapate haki kwa sababu huu unyanyasaji wa kupiga wananchi risasi siyo jambo jipya, lipo katika mashamba haya. Wawekezaji kutokufanya uwekezaji siyo jambo jipya. Nadhani huu mzigo Waziri wa Ardhi sasa akae chini na achukue *data* ya maeneo yote ili waweze kuona nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kauli imezoelekea, tuwe wakweli. Mbunge anaposema matatizo ya wananchi wake anaonekana mchochezi. Mimi binafsi nilishawahi kuitwa mchochezi. Unapokwenda *site* unachukua maumivu ya wananchi, unayapeleka kwenye Serikali, Mbunge anaonekana mchochezi. Pia, baadhi ya viongozi hawa wamekuwa wakirudia kauli hizi hizi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu viongozi wa aina hii wachunguzwe. Mtu anasema nilikuwa nimekaa na mwekezaji lakini kwenda kwa wananchi ambao Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amempa dhamana hiyo kwamba nenda ukanisaidie kwenye mkoa huu na kwenye wilaya hiyo, hakai na wananchi. Yuko tayari kukaa na mwekezaji kunywa chai, halafu mwananchi ambaye kupitia Mbunge au Diwani akiomba kwamba wananchi watendewe haki, Diwani anaitwa mchochezi, Mbunge anaitwa

mchochezi, lakini mtu yuko tayari kukaa na huyo mwekezaji na hakai na wananchi.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza kabisa nianze kwa kukupongeza kwa maamuzi yako magumu ya kuunda hii Kamati na kwa kweli Kamati imetutendea haki kama Wabunge. Nimpongeze sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Manya kwa kuiongoza Kamati ambayo kwa kweli kwa wale tuliokuwemo toka mwaka 2015 hili suala la Malonje siyo geni na lilimwondoa Malocha. Pia hata Mbunge aliyepo kama Bunge na Serikali hawatamsaidia na huyu watamla kichwa. Tunapambana na watu *ma-giant*, lazima tuwaambie ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuchukue maamuzi magumu, najua ameitwa mchochezi, lakini mimi kama Musukuma namwona ndiye atakuwa Mbunge wa kudumu pale kama Bunge na Serikali litaamua kumsaidia kwenye hili suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ni nzuri sana, Kamati imefanya kazi nzuri na sisi Wabunge ambao hatukwenda kule tumeona taarifa ni nzuri. Nilikuwa najaribu kuona, wakati Mheshimiwa Profesa Manya anawasilisha, Wabunge majirani zangu kama nane hapa walikuwa wanatiririsha machozi, hiyo ni kuonesha kwamba kweli watu wengi wameguswa na suala hili.

Mheshimiwa Spika, najaribu kujiuliza kwa nini tunawaficha hawa watu kwa kutowataja. Kwa sababu Kamati inajaribu kuingia halafu inatoka. Sijui kama kuna sababu za kisheria zinazotukinga kuwataja. Yaani kuwaweka wazi wale viongozi wa mkoa ambao walifika mahali *waka-mislead* Kamati kwamba nendeni huku halafu Kamati nayo ikajiongeza kwenda kuona hayo mashambulizi yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kama itakupendeza kabla hujalihoji Bunge, tungetamani kuwajua ili tuisaidie Serikali. Saa nyingine tusioneane aibu kwa sababu hawa ni viongozi wamepelekwa kwa ajili ya kumsaidia Rais kusimamia wale wananchi na wala siyo kusimamia wawekezaji. Wawekezaji wanakuja baada ya kuwa wananchi wamekaa vizuri. Kama utaratibu utakuruhusu ni vizuri tukawajua ili kama itawezekana tuweze kushughulika nao.

Mheshimiwa Spika, najaribu kujiuliza, hata kabla ya maazimio na hatua za Kiserikali tumeoneshwa mtu amekata mtu masikio, amepigwa risasi, mwingine ana risasi kichwani na viongozi wapo na waliotoa hizo *PF3* wapo. Hivi hawa viongozi wanaotakiwa kupelekwa kushtakiwa wakiwa madarakani ni akina nani kama siyo hao walioko huko mikoani? Inawezekanaje mpaka Kamati ikatuletea hizi taarifa? Ina maana wao hawajawahi kuyaona haya mambo? Maana yake wao wamefunga mipaka ya wananchi kuwaona wao, lakini ni rahisi wao kwenda kuwaona wawekezaji. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali isiache kwa kweli hii taarifa ikapita hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua Bunge tutatoa maamuzi lakini Serikali tunaihitaji; Mama tunafanya kazi ya kukusaidia, tunaomba atushike mkono kwenye hili. Ingekuwa mimi ni msaidizi wake wa karibu, leo hii tungekuwa tunamaliza hapa na karatasi wanazo mkononi. Haiwezekani tunafumba macho, tunasema tusitaje mtu. Efatha anajulikana ni nani, huyu ni kiongozi na ni taasisi inashughulika na imani za kiroho. Ina kampuni ya ulinzi, inafundisha miezi mitatu, hao wanaofundishwa wanakwenda kupewa bunduki wanatungua risasi tuh tuh! Kwa jina la Yesu! Aah, hapana! Haiwezekani! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwenyeji kidogo Nairobi. Haya mambo yalianza kimzaha kimzaha hivi Shakahola, msipite huku, mkipita huku tuh! Kwa jina la Yesu! Anasema eneo la dini, walichokwenda kukikuta ndicho hicho. Kama haya wameyaona machache, wale waliojitokeza kuwaambia, je, wale ambao walikufa wakazikwa bila ninyi kuwaona?

Mheshimiwa Spika, sasa ni vizuri Serikali iwe *serious*. Hili suala limechukua muda mrefu na watu wamekwishajulikana na hizi Imani, Mungu anisaidie tu niendelee kubaki kwenye Roma kwa kweli. Naona kama tunataka kuingia kwenye majaribu. Wiki jana tu hapa tumefukuza kiboko ya wachawi huku tena tunaibuka na *Efatha*…

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli tufike mahali tulimalize hili suala…

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, sijui ni nani alikuwa anasema Taarifa kabla kengele haijagonga. Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mzungumzaji kwamba, tusisahau suala la watu kuuawa katika ardhi yao ndani ya Tanzania, nina imani kama kuna mtu alilia nadhani huyo amenifuata mimi. Mheshimiwa umenifuata mimi na ufuate mfano wangu!

Mheshimiwa Spika, kama ni kulia mimi nimelia, kama ni kudhalilishwa, mimi nimedhalilishwa, lakini imani haikuhusika. Nimewahi kusema *there is the problem of governance* ina-*centre* kwenye *governance*.

Mheshimiwa Spika, nikueleze *dwell around the governance, issue* ipo kwenye *governance,* hawa ambao hawatimizi wajibu ni *governance* haina mahusiano yoyote na dini. Sikupenda kuzungumza hili, nimelia mpaka ofisini kwako sikuja na tasbihi au na

rozali au na maji ya kukanyaga ni *governance,* yaani *governance,* huyu amelia kufikia mimi huyu? Aah! *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma unaipokea taarifa hii?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naipokea.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema hivi, mimi ni mkopaji wa mabenki lazima niwe wazi, kama *valuation* imetoa milioni 600 baada ya mwaka mmoja hujaendeleza chochote ukapata bilioni tatu, *it means valuation* yake ilienda bilioni tano na kitu, sasa huyu aliyeipitisha shilingi milioni 600 akaja akapitisha na ya bilioni tano..

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, kuna kitu gani jamani au…

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma naona kuna taarifa mbili unataka kupewa na muda wako ulikuwa umeshaisha, nilimsikia Mheshimiwa Kigwangalla kwanza kabla yao. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, jambo analoliongelea la *valuation* ni katika mambo muhimu sana yaliyopelekea sisi kutoa hayo mapendekezo, sasa nimeona nisiliache likapita hivi hivi niliweke sawa, kwamba paliuzwa bila *valuation* kufanyika, paliuzwa bila mipaka ya shamba kuhakikiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa sababu napiga mambo ya kidaktari, kwa hiyo naipokea taarifa ya daktari mwenzangu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na, naunga mkono hoja ya Kamati. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kuna taarifa nyingine, Mheshimiwa Flatei Massay.

**TAARIFA**

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Musukuma pamoja na mchango wake mzuri, *valuation* isingeweza kufanyika kwa sababu upo msamiati unasema "penye uzia penyeza rupia". Kwa hiyo hicho kisingeweza kufanyika kwa sababu rupia ilipenya. Ahsante. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema Kamati imefanya kazi nzuri Mheshimiwa Spika wetu umefanya kazi nzuri na Bunge lako hatutakuangusha kwenye maamuzi. Baada ya maamuzi yetu tunaiomba Serikali inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan, wasomi na wataalam wako wengi mtaani, iondoe wote kule ipeleke wapya.*(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum, Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA – MWENYEKITI WA KAMATI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja ambayo imeletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Nitambue kwamba hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 14 na kwa kadri ya michango ya Wajumbe wote walikuwa wana-*support* mapendekezo ya Kamati Maalum.

Mheshimiwa Spika, nianze pale ambapo Mheshimiwa Musukuma ameongea habari ya *valuation,* kusema ukweli pendekezo letu la kwanza linatokana na mtiririko wa mapungufu katika manunuzi na mauzo ya Shamba la Malonje.

Mheshimiwa Spika, kwanza Baraza la Mawaziri maelekezo yake kwa Mkoa wa Rukwa yalikuwa ni shamba hili ligawanywe katika vipande vya hekta 50 na wapewe wafugaji wadogo wadogo. Maelekezo ilikuwa ni kugawa katika hekta 50 na iwapo Mkoa ungepata changamoto yoyote katika kushughulikia jambo hili walikuwa wameelekezwa waweze kurejea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mchakato wote wa kulipata shamba una mapungufu makubwa ambayo ndiyo yamepelekea Kamati yako Maalum kufikia pendekezo lake la kwanza. Kwa sababu Mkoa badala ya kwenda kupima shamba hili kwa hekta 50, 50 badala yake wakatangaza tangazo la ekari 3,000 kuuza na baada ya tangazo hili kutolewa, mwekezaji akapendekeza yeye mwenyewe kwamba atahitaji 10,000.

Mheshimiwa Spika, Mkoa ukamkubalia kumuuzia 10,000, Kamati yako ilipotamani kupata *valuation report,* tathmini haikupatikana, sasa milioni 600 ilipatikanaje? Haikujulikana badala yake yaonekana kabisa kwamba mkoa ulikaa na mwekezaji wakapanga mezani hatimaye wakafikia bei ya milioni 600 na mchakato huo unapata kasoro zaidi pale ambapo shamba linakubaliwa kwamba hekta 10,000 zitauzwa, lakini upimaji haukufanywa kabla, kwa maana ya kwamba upimaji umekuja baada ya mauzo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa hayo mapungufu hayawezi yakahalalisha yale yote yaliyokuja kuendelea na iwapo matokeo yake yangekuwa bora basi tungesema mapungufu haya yamejijenga, lakini mapungufu haya yanatoa matokeo ambayo ni mabaya kwa sababu mchakato tangu mwanzo ulikuwa umekosewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa manunuzi yamefanyika, upimaji ukaja baadaye, lakini Kamati yako pia ikagundua kwamba ukubwa wa shamba ulipokuwa umekabidhiwa kutoka Wizara ya Mifugo ilikuwa ni ekari 37,000 (hekta 15,000) lakini inapokuja sasa kwenye hali halisi baada ya mwekezaji kupewa 10,000 ambazo zilipimwa *post*-manunuzi, zinabaki 3,400 peke yake badala hata ya zile 5,000, kwa maana ya kwamba hata kama makadirio yalikuwa ni kwamba wananchi wapate hekta 5,000 bado walipata 3,400 na ukiondoa zile za Gereza la Mollo wakaja kuishia kupata 2,600.

Mheshimiwa Spika, wale wa Halmashauri ya Sumbawanga *DC*. walipendekeza kwamba basi hivi vitalu 51 vilivyopatikana wapewe wananchi wetu bure kwa sababu hata uwezo wao wa kununua si mkubwa. Jambo hili halikukubalika badala yake vikauzwa na vikauzwa kwa shilingi milioni 2.5, lakini kwa watu ambao ni nje ya wale wananchi wanaozunguka vijiji. Kwa hiyo, watu wa Mjini Sumbawanga, wafanyabiashara na viongozi wa Serikali pamoja, kitu ambacho Kamati ilisikitika kidogo niki-*point out* kwamba hata baada ya mwekezaji kuwa amepata hekta10,002 bado katika vile vitalu pia anaonekana akiwa ananunua na vitalu, rekodi hizo zipo na zilitia mashaka juu ya mchakato mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mchakato huu wa manunuzi ulikosewa na baada ya hapo, mkataba pamoja na hati ya umiliki ya mwekezaji ilikuwa ni kufuga, nakumbuka kile kipengele ni kifungu cha sita na saba cha ule mkataba, ambao kimsingi kwa tathmini ya Kamati ulikuwa ni mkataba ambao nao haukidhi viwango vya mkataba.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 na 7 kinasema ni kwa ajili ya kufuga na malisho kama dhamira ya kwanza ya Baraza la Mawaziri kuashiria kwamba haya mambo yalijulikana Mkoani pale ndiyo maana yanaingia kwenye mkataba na hati ya umiliki, lakini mwekezaji anafuga kidogo, Kamati mtakumbuka tulikuta ng'ombe wasiozidi 200, walisema ni 140 hivi na hii ni miaka 17 ya ufugaji. Hata kama huwa wanauza na kula nyama, lakini ng'ombe 170 na kama dhamira ilikuwa ni kufuga, sasa wakafuga na hati ya umiliki na

mkataba wa mauziano ukarejea dhamira ya Baraza la Mawaziri. Kwa maana ya kwamba haya mambo yalijulikana lakini badala yake kilimo kikatiliwa mkazo. Serikali ikaacha kufuatilia utekelezaji wa mkataba, mwekezaji akaendelea na kilimo.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Kamati inakazia tu kusema kwamba inawezekana baada ya kugundua kwamba masharti ya mkataba hayatekelezeki vizuri, mwaka 2021 Hati ikaongezea kilimo, mifugo pamoja na upandaji miti ili sasa mambo yawe halali, lakini hiyo hata kama imefanyika mwaka 2021 ni baada ya miaka 14 baadaye. Kwa hiyo masharti ya mkataba hayakutekelezwa na Serikali haikumsimamia vizuri.

Mheshimiwa Spika, nirejee kusema kwamba pendekezo la Kamati la kwanza ambalo ni kubatilisha, Serikali ibatilishe umiliki wa Shamba lote la Malonje ikiwa na maana ya Shamba la Efatha pamoja na mashamba yanayozunguka vikiwemo vitalu 51.

Mheshimiwa Spika, wazo hili siyo jipya, wazo hili na dhamira hii ilishakuwepo mwaka 2015 ambayo ilikuwa ni kubatilisha shamba hili, lakini kama ambavyo taarifa yetu imesema ni kweli kwamba kukaingiwa na utendaji mbaya upande wa Serikali kwa sababu Kamishna wa Ardhi ndiye aliyepaswa kushtakiwa, lakini akashtakiwa Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Manispaa naye akaingia hati ya maridhiano huku akijua kwamba siyo mwenye ardhi! Kilichokuwa na sintofahamu kubwa ni pale yule aliyetia saini kusema kwamba hii si saini yangu kwa maana ya kwamba hati hiyo imegushiwa. Pia kimekuwa ndiyo kigezo nakumbuka barua ziliandikwa nyingi kuelekeza kwamba mwekezaji asisumbuliwe na asibugudhiwe baada ya ile Hati ya Maridhiano.

Mheshimiwa Spika, mambo haya ndiyo yaliyoipelekea Kamati yako kwamba tunaona mapungufu makubwa upande wa mwekezaji, lakini pia na upande wa Serikali wa jinsi ambavyo mgogoro huu umekuwa ukishughulikiwa. Kwa hiyo kwa sababu Wajumbe wote waliochangia wamekubaliana na mapendekezo ya

Kamati naweka msisitizo kwamba pendekezo letu la kwamba shamba hili libatilishwe umiliki wake liendelee kusimama.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ijue kwamba ina sababu ya kutokukubaliana na ile amri ya Mahakama kwa sababu kuna kughushi pale ndani na kwa hiyo inaweza ikafanya marejeo kwa sababu mhusika Kamishna wa Ardhi siye aliyeshtakiwa badala yake alishtakiwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, tumesisitiza pia habari ya kusimamia Kanuni za Ardhi, lakini pia na usimamizi wa kampuni za ulinzi nchini, maana tumegundua kwamba kampuni zaweza zikatoa mafunzo tena ya kutumia silaha za moto kwa watu wake na hao wakaenda kutekeleza bila kuwa na weledi wa mafunzo ya mgambo wala JKT vitu ambavyo ndivyo vigezo halisi vya wanaopaswa kuajiriwa katika kampuni binafsi za ulinzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo na ufafanuzi huo naliomba Bunge lako sasa likubali kupokea taarifa ya Kamati Maalum iliyoundwa kuchunguza mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo kikiwemo Kijiji cha Sikaungu katika Jimbo la Kwela.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mwenyekiti ahsante sana kwa kuhitimisha hoja hiyo na sasa Waheshimiwa Wabunge kama ilivyo ada naona Mheshimiwa Waziri umesimamisha kisemeo, unataka kuzungumza kabla sijahoji Bunge au baada ya kuhoji Bunge? Nitakupa nafasi unataka kuzungumza baada au kabla?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Baada.

**SPIKA:** Baada ya kulihoji Bunge?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Ndiyo.

**SPIKA:** Sawa, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumesomewa hapa taarifa, tena ngoja nisimame hapa kuweka msisitizo ili wasiwepo wanaotembea tembea.

Waheshimiwa Wabunge, tumesomewa hapa muhtasari wa taarifa ya Kamati Maalum ya Bunge na sasa kwa sababu mmeshaunga mkono naelekea kuwahoji lakini kabla sijawahoji lazima Mwenyekiti ametueleza vizuri hapa mwishoni mambo tunayohojiwa, lakini taarifa hii inayo mapendekezo yote ya Maazimio ya Bunge, kwamba Serikali itakuwa inaambiwa kitu gani cha kwenda kufanya.

Waheshimiwa Wabunge, katika haya maazimio, hili azimio la kwanza:-

(a) linasema Serikali ibatilishe umiliki wa Shamba lote la Malonje (Shamba la Efatha) na mashamba yanayolizunguka vikiwemo vitalu 51 kwa kuzingatia sheria na maslahi ya umma.

(b) Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote nane vinavyozunguka shamba pamoja na Gereza la Mollo, utakaobainisha mahitaji ya ardhi pamoja na matumizi ya ardhi hiyo; na

(c) Serikali ilipime shamba hilo na kuligawa upya kwa wahusika ambao ni wanavijiji, Gereza la Mollo, Mwekezaji (Efatha *Church*) na wenye vitalu kwa kuzingatia: -

(i) Mahitaji halisi ya ardhi kwa wanavijiji;

(ii) Uwezo wa Mwekezaji;

(iii) Uwezo wa Wenye vitalu; na

(iv) Mahitaji ya Gereza la Mollo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hapa kwenye (b) kabla Bunge halijaazimia kwa sababu tukishaazimia tena ni maelekezo kwa upande wa Serikali, kinazungumzia kuhusu Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote nane. Hili sina hakika kisheria kama ni Serikali inatengeneza ama ni vijiji huwa vimepewa mamlaka ya kutengeneza yale matumizi bora ya ardhi. Sasa nataka tusaidiane ili Azimio letu hili likae vizuri, tusije tukawa tumeielekeza Serikali ikatengeneze matumizi bora, mpango wa matumizi kwenye ardhi wakati wenye mamlaka hayo ni vile vijiji vyenyewe. Kwa hiyo, lazima hili tuwe tumeliweka sawa ili Azimio la Bunge likae vizuri.

*(Hapa Mhe. Hawa s. Mwaifunga alikuwa akizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Kuna mtu namsikia hapa amekazana kweli na Tume ya Mipango sijui kama kule vijijini ile Tume ndiyo inazunguka kote? Mheshimiwa Hawa una uhakika na unachokisema ama unachangia tu? Kwa hiyo, tusaidiane hasa Wizara ya Ardhi, kama hili mnalijua ili Bunge tutengeneze vizuri azimio letu tunavyoiambia Serikali. Sasa nimemwona Mheshimiwa Kigwangalla amesimama.

Mheshimiwa Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naona ulikuwa umeshatoa maelekezo kwa Wizara ya Ardhi, lakini tuliweka pendekezo hilo kwa msingi kwamba huwa kuna mpango shirikishi wa matumizi bora ya ardhi, ambao huwa unaongozwa na Sheria ya *Land Planning* ambapo kule kwenye ile sheria inaanzishwa *Land Planning Commission,* Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi. Kwa hiyo, ule mpango unasimamiwa tu na wataalam,

lakini wananchi wanashirikishwa katika kufanya maamuzi juu ya namna ya kupanga.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Ngoja kwanza, sasa hapo unasema inapanga Serikali wananchi wanashirikishwa, mimi ninachokifahamu ndiyo maana nataka tuliweke sawa, ninachokifahamu ni wananchi wanapanga matumizi bora ya ardhi yao, mimi najua ni wananchi lakini kama tunajua, kuna chombo kingine mahali kinachowapangia wanakijiji ndiyo tuweke hapa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria unachokisema ndiyo sahihi, kwa maana kwamba, mipango ya matumizi bora ya ardhi ni zao la kijiji chenyewe. Kijiji ndiyo kinakaa kinajipangia na ndiyo maana mwisho wa siku anaye-*approve* ni Mkutano Mkuu wa Kijiji. Jukumu la Serikali kwenye jambo hili ni kutoa uwezeshaji. Hata tume inachofanya ni kutoa uwezeshaji wa kitaalam na ushauri kwa wananchi, lakini mwenye mamlaka ya kupanga ni kijiji chenyewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nami nilikuwa najua hivyo. Sasa kama hivyo ndivyo, hapa inaposomeka; "Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote" hapa vijiji vinaondoka. Nataka kufikiri hivi, Kamati yetu ilikusudia kwamba, Kamati iandae mpango wa matumizi bora ya hilo shamba litakalobatilishwa. *(Makofi)*

Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye hilo shamba ambalo (a) imependekeza kubatilisha. Hivyo ndiyo ama sivyo? Kwa sababu ni mapendekezo ya Kamati. Sasa hapa kama niko sahihi haya maneno mengine huku mbele tunaweza

tukayaweka vizuri, lakini tunataka mpango bora kwenye lile shamba, kwa sababu tukiingiza tu hapa vijiji, hii siyo Serikali inayotengeneza mpango bora. Tusije tukaleta tena mkanganyiko mwingine.

Mheshimiwa Mhandisi Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, tunashukuru kwa kutusaidia. Kimsingi hapo tuliona kwamba kuna eneo ambalo ni la mwekezaji, yaani tukili-*consider* lile shamba zima la Malonje, lile la awali kabla ya kugawanywa na kuuzwa, tunalo eneo lile la mwekezaji na tunalo eneo lile la vitalu 51 ambalo kutokana na hawa wanavijiji sasa na hao vijiji na wenyewe ambao tumesema kwamba katika tafsiri wanavijiji wanasema kwamba, "Mipaka yetu ni mpaka kule", ambako ni ndani ya lile shamba na wale wenye shamba wanasema; sisi mipaka yetu ni kule kwa wale wananchi kwa sababu hiki kijiji ni jina tu.

**SPIKA:** Sawa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, sasa kwa misingi hiyo kwa sababu tayari kunakuwa na *overlapping* ya *ideas* na ndiyo eneo lenye mgogoro. Kwa hiyo, shida yetu sisi tupate huo ufumbuzi katika kukamilisha hili.

**SPIKA:** Sawa, sasa kwenye hoja hii ili Bunge tufanye maamuzi nilisema kipindi kile cha kuchangia, ardhi ambayo iko kwenye mipaka ya vijiji, jina lolote itakayoitwa, ardhi iliko kwenye mipaka ya vijiji kwa sasa tusiiguse hapa, tushughulike na ile ambayo imeleta hii shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Stella Manyanya, hoja yako imeeleweka lakini tukigusa kule tutaleta mchanganyiko wa mambo. Nataka nimuulize Mheshimiwa Mbunge wa Kwela. Likiitwa Shamba lote la Malonje, linahusisha na hivi vitalu 51 au likiitwa Shamba la Malonje linahusisha tu shamba lile la hekta 10,000?

**MHE. DEUS C. SANGU - NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Hivyo vitalu vinavyoelezwa vilitolewa vikagawiwa kwa maana walinunua watu wengine. Kwa hiyo, vilitoka kwenye shamba.

**SPIKA:** Kwa hiyo, ukisema Shamba la Malonje lazima useme, Shamba la Malonje pamoja na vitalu?

**MHE. DEUS C. SANGU - NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, na hivyo vitalu.

**SPIKA:** Ambapo nafikiri hapa kwenye namba moja imewekwa sawa. Sasa badala ya kutumia neno ikiwemo inabidi tuandike na mashamba, ngoja, imesema; "Serikali ibatilishe umiliki wa shamba lote la Malonje, Shamba la Efatha na mashamba yanayozunguka ikiwemo vitalu" kuna mahali ambapo shamba linazunguka hilo Shamba la Malonje ambalo haliko kwenye vitalu, yaani hili eneo linapwaya au hakuna?

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA – MWENYEKITI WA KAMATI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ukiacha Gereza la Mollo shamba lote hili linazungukwa na hivyo vitalu.

**SPIKA:** Sawa. Kwa hiyo, tutakuwa sahihi tukisema, "Serikali ibatilishe umiliki wa Shamba lote la Malonje na vitalu 51 kwa kuzingatia, badala na mashamba, maana tusije tukaingiza tena mgogoro mwingine, kukaenda kuguswa na mahali ambapo sipo, Kamati niko sahihi? Kwa hiyo, tunafuta haya mashamba, tunasema na vitalu.

Haya sasa twende hapa kwenye (b), Mwenyekiti nimeeleweka nilichosema? Ili tufanye marekebisho hapa badala ya; "Iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi," sisi tuseme; "Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika yale yanayotokana na ile (a)."

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA – MWENYEKITI WA KAMATI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tukifanya hivyo tutakuwa sawa lakini lengo letu hapa ni kwamba tunapofanya mpango mpya wa matumizi ya ardhi maana yake tuzingatie mahitaji ya vijiji vinavyozunguka tunapokuwa tunafanya *plan* upya kwa sababu wao wana mipaka yao inayoingiliana na shamba, lakini mwekezaji naye anaingiliana nao. Kwa hiyo, tunaposema kuwahusisha ni kwa sababu tu wao nao wawe sehemu ya kuona kwamba mahitaji yao ni yapi? Kama (c) ina-*take care* basi tunaweza tukaenda na hiyo *proposal* yako.

**SPIKA:** Hii (c) nayo tutaifikia lakini kwanza tumalize (b). Hii (b), "Tuondoe ardhi katika vijiji" kwa nini? Kwa sababu vile vijiji si vina ile mipaka na Serikali kwa maelezo mliyoyasema kwenye hii taarifa mmesema hivi: "Ile ardhi iliyoko kwenye mipaka ya vijiji ambayo iko sehemu ya shamba ni sehemu ya *general land*" si ndiyo wamesema hivyo? Kwamba ina watu, haina au iko wazi, wao si wamesema ni *general land* lakini iko kwenye mipaka ya vijiji? Kwa sasa hivi sisi tusizungumzie mipaka ya vijiji, vijiji vibaki vile vilivyo.

Serikali ile ardhi yao ambayo inaitwa *general land* iliyoko huko kijijini, maadam hapa mwanzo tumesema kwa kuzingatia sheria na maslahi ya umma, wao watatazama namna bora ya kuiweka, lakini haitakuwa tena sehemu; yaani sisi hatuwezi kuihamisha matumizi kutoka *general* kwenda *village land,* kwa sababu hayo ni mabishano ambayo tunaweza kubishana kwenye tafsiri. Ili ya kwetu hapa ikae vizuri tuweke hii ya (b) iwe ni Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo ambayo yanahusiana na hiyo (a) hapo juu, si ndiyo? Kwa hiyo, hii sehemu yote inakuwa inaondoka.

Labda kama tunataka kuacha hili neno, "Utakaobainisha mahitaji ya ardhi pamoja na matumizi bora ya ardhi", lakini tutakuwa tumeshajirudia maana tumeshasema matumizi bora hapo mwanzo. Mwenyekiti sijui kama unasoma na mimi hapo, hapa tunasoma sote eeh?

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA – MWENYEKITI WA KAMATI MAALUM:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo lote kama lilivyotajwa kwenye (A), si ndiyo?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, samahani.

**SPIKA:** Naam, nani anasema? Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiria tuweke, tukitambua hilo eneo kwa kuzingatia mipaka kabla halijauzwa itakuwa imesaidia?

**SPIKA:** Eneo gani Mheshimiwa?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, hilo eneo la Shamba la Malonje, tukilitaja kwamba kwa kutumia mipaka kabla halijauzwa?

**SPIKA:** Kwa sababu tunataka mgogoro uishe kabisa na tumesema mgogoro ulianza tangu kipindi cha ukoloni na tumesomewa historia. Kwa hiyo, hata tukisema kabla haijauzwa huyu mwekezaji ameenda juzi tu, lakini hoja zimeanza huko miaka ya 1930.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 wakati linauzwa.

**SPIKA:** Mwaka 2007, hata wakati halijauzwa si kulikuwa na mgogopro, ama sijasikia vizuri kwenye Taarifa yenu? Ni kwamba hata kabla kulikuwa na migogoro. Kwa hiyo, hata tukisema turudi, yaani...

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla umesimama.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, Shamba la Malonje ni tafsiri ambayo inawekwa kwa shamba lote ikihusisha na vile vitalu 51 vilivyopo na ikihusisha na shamba ambalo linajulikana kama Gereza la Mollo; hilo ndiyo Shamba la Malonje. Kwa hiyo, hiyo tafsiri inayowekwa hapo juu inamaanisha hivyo, shamba lile lote na vile vitalu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lile pendekezo la pili la namna ya kuweka ile *statement* ya *land use,* pamoja na maelezo mazuri aliyoyatoa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi ambayo nakubaliana nayo, pengine tupendekeze tu Serikali isimamie hilo zoezi la kufanya mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye hivyo vijiji. Sababu ni nini? Ili kutatua mgogoro kwa ujumla wake hatupaswi kuishia hapo, vile vijiji ni lazima vipimwe upya ili ardhi yao ijulikane.

Mheshimiwa Spika, pia, shamba lipimwe upya...

**SPIKA:** Mheshimiwa ngoja. Hapo kwenye vijiji hebu tupaache. Si ni sawa na ambavyo Serikali ina mamlaka ya kufuta vijiji? Hilo sisi tuliondoe Bungeni kwa sasa, kwa sababu tukiazimia hivyo kwamba na vijiji vikapimwe maana yake Serikali ni lazima iende ikafanye hivyo. Hilo tuwaachie wao kwa sababu ni jambo la kiutendaji.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, ninyi si ndiyo mmeenda kule? Leo wananchi walioko kule wasikie Bunge linasema vijiji vipimwe upya? Wakati mnasema hata walivyopewa zile 3,000 walisema hatuoni mnachotupa kwa sababu ni sehemu ya vijiji vyetu. Tutaleta mkanganyiko zaidi.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa uzoefu wangu kwenye mambo ya kutatua migogoro ya ardhi kama kuna *element* moja ya mgogoro utaiacha nyuma, mgogoro hautoisha *once and for all,* kwa sababu...

**SPIKA:** Uzuri vijiji si vina vyeti? Ngoja nikuulize wewe kwa sababu ni sehemu ya Kamati. Vile vijiji vina hati za kuanzishwa? Vinayo, kwa hiyo, mipaka yake ni ile ramani mliyotuonesha?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, vijiji vina hati ya usajili ya TAMISEMI.

**SPIKA:** Mipaka yake inajulikana kwenye hizo hati?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, pia vina ramani.

**SPIKA:** Mipaka yake ipo?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, vina ramani ambayo inaonesha *coordinates* za mipaka.

**SPIKA:** Ambazo hizo *coordinates* zipo?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, zipo.

**SPIKA:** Ninyi mmeziona?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Ndiyo maana nasema, vijiji vile vipo na viendelee kuwepo. Ardhi inaitwaje na Serikali hilo siyo suala letu, kwa sababu tukitaka kuingia huko saa hizi hatutakuwa tunamaliza mgogoro, tunaanzisha mwingine tena. Yaani huu mgogoro lazima tuanzie mahali. Maadam tumesema vijiji nane vipo, vilikuwepo na vina hati, Serikali inasema ardhi aliyopewa mwekezaji imeingia na huku kwa sababu huku ni *general land,* lakini na wao wanakubali kwamba iko ndani kwenye ardhi ya vijiji; vijiji kama ramani zao zilivyo mpaka sasa ziachwe hivyo. Tushughulike na vitalu 51 na Shamba la Malonje.

Haya mjumbe mwingine wa Kamati tumalize hili jambo jamani.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuweka *clear* na Mwenyekiti pamoja na wajumbe wengine ni mashahidi, hatukujadili sisi kufuta vijiji; hatukujadili hayo kabisa na wala hatukusema kwamba kuna kupima vijiji upya. Sidhani kama ndiyo

ilikuwa malengo na maazimio ya Kamati labda inawezekana tu ni langu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, sasa ngoja nisome hapa. Naona kuna Wabunge wawili ambao siyo wana Kamati wamesimama. Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mgogoro huu pamoja na kutogusa vijiji kama unavyosema lakini kuna sheria mbili hapo zimeingiliana. Sheria ya Vijiji na ile Sheria ya Ardhi, ile *general land.* Sasa pale ili uweze kuutatua mgogoro huo vizuri ni lazima kwanza kubainisha ipi inaangukia kwenye *general land* na ipi inabaki kwenye vijiji na mipaka yake.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye ramani tuliyopewa vijiji vile mipaka yake inaingia mpaka kwenye *general land.* Kwa hiyo, habari ya kufuta...

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa tusaidie, kwa sababu aliyeingiza ile mipaka ya vijiji kule kwenye *general land* ni nani?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ni wapimaji wakati wanampa mtu shamba.

**SPIKA:** Wapimaji ambao ni Serikali?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, eeh maana yake...

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Unaendelea kuongea? Haya endelea.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema, kwa sababu kosa limefanyika toka mwanzo ni wazi lazima shamba lote lile lifutwe wakiwemo na watu ambao wanakaa.

**SPIKA:** Ngoja, vile vijiji sasa hivi tukisema vijiji nane; je ni sehemu ya hilo shamba?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, vijiji ni kuhakiki tu mipaka yake wakati vinasajiliwa kama vijiji bila kuathiri, kwa sababu vilisajiliwa kama vijiji.

**SPIKA:** Aliyevisajili vijiji ni nani?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ni Serikali.

**SPIKA:** Ni Serikali?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Aliyempa mwekezaji ni nani?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ni Serikali.

**SPIKA:** Sasa mwanakijiji anakosa gani?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ili umalize kisheria, kwa sababu tayari kuna mgongano wa sheria katika kutoa ardhi ile. Kwa hiyo, ili uweze kuwatendea haki wanakijiji lazima zile sheria mbili zilizogonganishwa katika upimaji zirekebishwe kwenye ardhi yenyewe kwa sababu pale kuna aliyetangulia. Vijiji vilitangulia kabla ya shamba au shamba lilitangulia...

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mabula nilisema tangu mwanzo, hoja ya *village land* na *general land* tukiileta hapa ni hoja ambayo tutabishana kwenye tafsiri, kwa nini? Kwa sababu mimi nijuavyo *village land* ni *village land* na sheria ndivyo inavyosema.

Wewe uliingizaje huko kitu kinaitwa *general land*? Hata kama hiyo *general land* haiwezi kuning'inia mahali. Yaani ile *general land* lazima iwe kama ni kwenye manispaa au kijiji lakini inaitwa *general land*. Wewe mpimaji ukiwa unajua kabisa kwamba kule kuna mgogoro wa tangu mkoloni ukaamua kupima na vijiji ukavipa na *general land,* kwa nini usiiweke kwenye shamba ambalo sasa hivi ndiyo *general land? (Makofi)*

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema ifutwe ili kuanza upya katika kuthibitisha tu kile kijiji; kijiji hakifutwi...

**SPIKA:** Ndiyo tunasema hivi, Bunge halitaki kujielekeza kwenye kushughulika na mipaka ya vijiji.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, sawa.

**SPIKA:** Tunataka vijiji vikae vile vilivyo. Sisi tushughulike na hoja iliyo mbele yetu sasa. Tukienda na huko kwenye vijiji hatutamaliza hili jambo, kwa nini? Kwa sababu tayari kule kuna taharuki. Sasa tena na sisi Bunge tuingie kwenye...*(Kicheko)*

Naona Wabunge wengi zaidi mmesimama na wengine wanasheria, haya ninyi mtakuwa wa mwisho jamani, tumalize hoja hii. Ninyi mliosimama simameni hivyohivyo, Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, sitaenda kwenye *technicalities,* lakini msingi wa hoja ambayo Kamati yako imefanyia kazi ni hekta 10,002; huo ndiyo msingi wa hoja. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani kwamba chochote kile tunachokiamua kijikite ndani ya msingi wa hoja; tusiende nje wala tusirudi ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama katika hizo 10,000 *plus* 002 kuna vijiji kule ndani, ni suala tu la kutoa maelekezo kwamba, hali iliyokuwepo itaendelea, wananchi wabaki kama walivyo wakati utatuzi wa mgogoro unafanyika kwa sababu ukizungumza kama ni *forgery* kwa

maelezo ya Mwenyekiti inazungumzia 10,000 *plus* mbili, kama shughuli nyingine ambazo zinaendelea zinahusu 10,000 *plus* mbili. Kwa hiyo, nadhani tuji-*confine* pale ambapo Kamati imefanyia kazi na kama kuna...

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kama kuna maelekezo mengine yoyote ya kiutawala ili kuzuia taharuki huko *then* maelekezo yatoke. Kwa hiyo, nilikuwa nataka tu tusijichanganye. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, tuji-*confine* ndani ya hoja ambayo imefanyiwa uchunguzi, utafiti na vitu vinavyofanana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi siyo mjumbe wa Kamati, lakini kuna *issue* ya kisheria hapa watu huwa wanachanganya. *Definition* ya *village land includes unused land* lakini iko ndani ya vijiji. Sasa watu wengine huwa wanasema hiyo ni *general land, but it is not general land; general land* ni kitu kingine tofauti. Ardhi imegawanyika mara tatu; kuna *general land, village land* na *reserved land.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwenye *definition* ya ardhi ya vijiji ukisema *village land includes unused parts of village land,* ambayo watu wengine ndiyo wanatumia *loosely* kama ni *general land.* Siyo *general land* kwa maana hiyo. Kwa hiyo, haiwezekani kuwa na *general land* kwenye ardhi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa tunavyoona hapa ukiangalia hii ripoti ya Kamati *page 15, unless* Kamati watuambie. Unajua kijiji kinaweza kikawa kimesajiliwa na inawezekana wametengeneza ramani, lakini

hawana *village land certificate*. *Village land certificate* inapatikana pale ambapo *boundaries* zake ziko *clear*.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mchoro hapa kwenye *page* hiyo ya Kamati inaonekana kuna mwingiliano wa ardhi inayoitwa ya vijiji na shamba hili. Kama ndivyo maana yake kuna *contestation* hapa. Wanachosema wanakijiji kwamba ndiyo mwisho wa ardhi yetu wao wanavyofahamu *on the ground* ni ndani ya shamba, kama ndivyo; na kama vijiji havina hati maana yake ili huu mgogoro utatulike vizuri ni lazima kwanza tuanze ku-*identify boundaries* za vijiji halafu sehemu itakayobaki ndiyo shamba hilo la...

**SPIKA:** Ngoja ngoja, ambazo zipo?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, zipo.

**SPIKA:** *Boundaries* zipo na wana vyeti?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, *yes*.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Kama zipo maana yake ardhi ya kijiji, lakini pia wanachosema Kamati *unless* kama tutapata tofauti kwamba, hata hilo eneo lililobaki bado wanataka kijiji wapate sehemu kama sehemu ya wadau na wao waongezewe baadaye, si ni kweli?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana yake kama leo vijiji vina maeneo yao na hekta 5,000 lakini kwenye eneo lililobaki ambalo labda ni 4,000 wanatarajia 1,000 irudi tena kijijini maana yake eneo la kijiji litaongezeka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita nadhani ufafanuzi wako sehemu ya kwanza unatupeleka sehemu sahihi. Kwa maana ya kwamba, kwa sasa hivi, hii ramani uliyoisema hapa, vijiji hivi kuingiliana na shamba, hiyo hoja ya vijiji kuingiliana na shamba kwanza vijiji tuvitoe, kwanini? Kwa sababu shamba si lipo tu huko hata ambalo haliko

kwenye vijiji? Kwa hiyo, maadam vijiji vina hati *(certificates)*, jina lolote lile, vijiji tuviondoe ili tushughulike na hili shamba sasa.

Maelezo kwa sasa hivi ni kwamba hili shamba la hekta 12,000 ni kwamba lenyewe limeingia vijijini na siyo vijiji vimeingia kwake. Ili tukae sawa ni kwamba hili shamba limeingia vijijini. Vijiji pale panapoishia kwa sasa paishie pale, huku kulikobaki ndiko tunataka Serikali ikakufanyie kazi kwa sababu ndiko ambako hizi changamato zinazojitokeza, zinaanzia hapo. Huku kwingine watu wamekamatwa wamefanya nini, hiyo tunamaliza leo hapa. Haya mengine tunayowashauri ni yale sasa ya nje ya vijiji ili twende vizuri, maana la sivyo tutaleta changamoto huko vijijini.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, sawa. Kama nimeelewa sawasawa, hii sehemu nyekundu yote ndiyo ardhi ya vijiji? Ikitoka vijiji havina tena *claim* kwenye eneo lililobaki. Kama ndivyo…

**SPIKA:** Sasa, ndiyo hatutaki uweke hilo neno havina *claim*. Ndiyo maana ya hili pendekezo kwamba ile ardhi waweke mpango wa matumizi bora, kwa sababu ardhi haiongezeki lakini watu wanaongezeka na wameongezeka, si ndiyo?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ni sawa.

**SPIKA:** Sasa ukisema tena hawana *claim* tunarudi pale pale.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nilitaka niulize ili tuweke sawa.

**SPIKA:** Haya, hawana lakini ufafanuzi…

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ukweli vijiji kwa maana ya eneo lao litoke halafu lililobaki sasa ambalo nafikiri ndiyo ripoti ya Kamati, kwamba, baada ya vijiji kutoka kwa mujibu wa hiyo *red line then* eneo lililobaki ndiyo hii ripoti ya Kamati inahusu mapendekezo hayo, siyo ardhi za vijiji.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangalla, hili inabidi lifungwe na naamini tutaelewana vizuri tu wala msiwe na wasiwasi, Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hapa kuna ardhi ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 na nyingine ipo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.5, zote za mwaka 1999. Sasa, hii *general land,* ambayo sasa kwa mujibu wa mapendekezo ya Kamati nadhani tuko kwenye mwelekeo sahihi, kwamba tu-*deal* na *general land*, ile ya kijiji ibaki kwa sababu kama Serikali bado hawana nafasi ya kuingia kwenye ardhi ya kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tubaki na mtazamo wa *general land* ambayo ipo chini ya Wizara ya Ardhi. Ndiyo maana hiyo *general land* hata ikifutwa bado ya vijiji ilishatangazwa kuwa ipo kwa mujibu wa Sheria Na.4 siyo Sheria Na.5 tena. Kwa hiyo, utaratibu hata hizo hati zikifutwa maana yake inapaswa irejeshwe, sasa mrejesho ukoje? Yaani irudi tena kuwa chini ya kijiji ili kusudi kijiji wawe na mamlaka nayo baada ya ufutwaji huo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, kama ilivyo sasa, tuendelee na hizo hekta 10,000 na hivyo vitalu kama mapendekezo ya Kamati, lakini baada ya kufutwa sasa Serikali Kuu ijiondoe kwenye mamlaka ya umiliki ya hiyo *general land*, irejeshe kwenye vijiji ili sasa vijiji waanze mpango wa matumizi bora ya ardhi na wao wawe *facilitators,* ahsante.

**SPIKA:** Hayo yote tayari yako kwenye (a) Serikali ibatilishe umiliki wa Shamba lote la Malonje na vitalu 51 kwa kuzingatia sheria na maslahi ya umma, si ndiyo iko hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa mwisho kuzungumza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa

Spika, nakushukuru. Kwanza tukubaliane, kwamba hakuna mgogoro kuhusu mipaka ya vijiji na kwa sababu hakuna mgogoro kuhusu mipaka ya vijiji, hili wazo la kufuta vijiji unalitoa wapi? Hii ardhi ni kweli ni ardhi ya jumla kwa maana ya *general land* lakini tunakubaliana kwamba hakuna ardhi inayoelea angani. Kila ardhi ina-*fall* kwenye eneo fulani lililomegwa kama eneo la kiutawala. Hili shamba linapita kwenye maeneo ya kiutawala ya vijiji zaidi ya hivyo nane, lakini tunacho-*deal* nacho hapa na chenye mgogoro mbele yetu ni hili shamba.

Mheshimiwa Spika, hili azimio la kwanza (a) ndilo linalomaliza kazi. Tunabatilisha milki ya shamba hili, haya mengine yatakuja kufanyika kwa utaratibu unaofuatia, lakini hakuna sehemu yoyote kwenye mgogoro huu na sisi tumeshughulika nao, kwamba eti kuna mgogoro wa mpaka kati ya kijiji kimoja au na shamba au na kitu gani. Kwa hiyo, huwezi kuvigusa vijiji hapa. Tukabatilishe shamba ambalo ndilo lenye mgogoro, baada ya hapo, upangaji, ugawaji, utoaji, utategemea taratibu nyingine za kisheria kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ushauri.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tulikubaliana huyo atakuwa mzungumzaji wetu wa mwisho. Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ili kuondoa mgogoro huo nashauri (b) itoke yote. (a) ibaki kama kawaida, Serikali ibatilishe, (b) itoke kwa sababu hii (b) ndiyo inasema inaondoa mpango wa matumizi wakati vijiji vipo vimeshajipangia, vina utaratibu wake. Hii (b) ikitoka yote maana yake hii (c) itaelekeza sasa baada ya kutengua, utaratibu utaanza upya wa kuja kupima hilo shamba na kuligawa upya kwa wahusika ambao ni wadau wote. Kwa hiyo, nadhani hii (b) ikitoka mtiririko utaenda vizuri.

**SPIKA:** Haya, Mwenyekiti, hapa kuna mawazo ya aina mbili. Kwanza, ni ile (a) tumeshakubaliana, (b) Serikali iandae mpango wa

matumizi bora ya ardhi katika eneo lote kama lilivyotajwa kwenye aya (a), hiyo ni ya pili. Sasa, ukishaiweka hii ya pili, ukienda (c) inasema, Serikali ilipime shamba hilo na kuligawa upya kwa wahusika, hapa inaanza kutaja ni nani na kitu kama hicho.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, hili nalo kwa mwongozo wenu wa Kamati ili tuweze kuhoji vizuri Bunge, tukishasema Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo lote kama ilivyotajwa, si ndiyo wataandaa hapa uwekezaji, hapa vitalu, hapa sijui wanakijiji wapewe, si ndiyo watafanya hivyo? Hii (c) inakuwa na kazi gani? Kwa sababu hapa hii (c) ni kama tunaielekeza sasa Serikali kwamba mkishapima mkawagawie hawa. Je, Serikali ikienda huko ikagundua hivi vitalu havikuwa na tija poyote? Labda mahitaji halisi ya ardhi kwa wanavijiji wameshaona wamekubaliana wataendaje yaani hii (c) inakuwa na shughuli gani? *(Makofi)*

Wajumbe wote wa Kamati hii inawahusu. Tukisharekebisha hapa kwenye (b) kwa maneno namna tulivyoweka kwamba Serikali ikaandae sasa mpango wa matumizi bora ya ardhi kulingana na ile ardhi ya kwenye (a) hii (c) bado inakuwa na kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wajumbe wako watatu wamesimama wakusaidie. Mheshimiwa Ester Bulaya halafu naelekea huku. Mheshimiwa Ester Bulaya halafu Mheshimiwa Manyanya na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati, *yes,* lakini kama naelewa *point* yako, kwamba sisi kama Kamati, Bunge limepitisha maazimio ya kubatilisha hili shamba sisi tunapaswa kuishia hapo. Kuhusiana na kwenda kugawa na taratibu nyingine ambazo zinatakiwa kufuata sasa ni kazi ya Serikali. Nimeanza kukuelewa kwamba sisi tulipaswa kuishia kwenye azimio la kubatilisha pekee. Sasa, Serikali ndiyo ina jukumu la kwenda kuangalia yale maelekezo yote, *I mean* zile *technicalities* na kuangalia ule ushahidi na vielelezo kuanzia mwanzo wa ugawaji wa shamba mpaka sasa hivi *and then* wao wenyewe ndiyo wataamua wanaligawaje.

Mheshimiwa Spika, nimeiona hiyo *point* yako kwamba sisi tulitakiwa kuishia kwenye hili azimio la kwanza *and then* hayo masuala ya ugawaji linawahusu wenyewe wanaokwenda kutekeleza na siyo sisi tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hapa naomba Waheshimiwa wabunge waelewe, si kwamba Kamati tunashindana au tunatofautiana ila tu kama hivi ilivyotokea. Kuna baadhi ya siku Mheshimiwa Ester alikuwa na msiba kwa hiyo kuna mengine tuli-*discuss* pengine hakutusikia. Suala ni hivi, tulikuwa tumeona mwenendo mzima wa namna shamba lilivyouzwa, halikuweza ku-*consider* wadau wengine muhimu. Hata lengo la mjadala huu ni kuweka amani na kuhakikisha kwamba wadau wote muhimu wanafikiriwa. Kamati haikuona kwamba inamfukuza huyu au inafanya nini, inahitaji kuleta amani na kuhakikisha kwamba wadau wote wafikiriwe kwa haki.

**SPIKA:** Sasa, hii tusaidie jambo moja.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA– MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Ni nani anatoa taarifa? Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi naona unataka kumpa taarifa, unasemaje?

**TAARIFA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe mzungumzaji, Mheshimiwa Manyanya taarifa. Pamoja na hiyo nia nzuri ambayo inawezekana ndiyo ilikuwa nia ya Kamati, lakini utakapobatilisha; suala la kubatilisha miliki ni suala la kisheria, unayembatilishia miliki atakuwa na haki zake za kisheria na

kuwa mwekezaji ndiko kumemfanya akahusika kwenye jambo hilo. Ukishabatilisha miliki unamhitaji tena kama mdau na yeye anawekwa kwenye orodha mpaka Serikali inaelekezwa kwamba miongoni mwa watu wa kwenda kupewa ni pamoja na huyu ambaye tumeshambatilishia miliki, ndiyo changamoto inapokuja. Kwa hiyo nadhani ni vizuri tukabatilisha halafu Serikali kwa taratibu zake kwa utaratibu unaofaa ikaendelea kuona nani anastahili kulingana na mahitaji yaliyopo na watu waliokuwa na uhitaji wa ardhi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya malizia.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nadhani hatutofautiani sana, la msingi sisi tunaelewa na tunakubali kwamba mwekezaji na yeye ni mdau muhimu, atakachopewa kama haki yake, apewe sifuri, moja, kumi, lakini wakati huo ndilo litakalokuwa limeonekana lakini atakuwa amefikiriwa na ikaonekana kwamba anastahili hiki. Anachostahili ni hicho kitakachokuwa kimeonekana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya, hii ya pili inasema, Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo lote kama lilivyotajwa kwenye aya (a). Serikali ikienda kufanya huo mpango ikaamua hata wewe upewe pale, kuna sehemu, itakuwa ina kosa? Kwa sababu hili ni jambo la kiutendaji, yaani sisi Bunge tunataka kuingia kwenye utendaji? Kwa sababu sisi tunatoa maamuzi makubwa makubwa yale, hayo madogo madogo tunaiachia yenyewe ili ikienda ikikosea inakuja tena hapa. Sasa sisi tukiituma kazi kwamba kampe moja, mbili, tatu, watasema Bunge mlielekeza na sisi tumetekeleza. Je, hao watu kama hawakufanya sasa sisi Serikali tutawaulizaje?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, labda hapo tulipata utata kwa misingi kwamba, kama ulivyosema, Serikali inaweza kwenda kuamua kadri itakavyoona, lakini sisi tumeona vijiji vina shida halafu ikaamua kwamba Sikaungu hatumpi, Songambele hatumpi…

**SPIKA:** Sawa, twende na hoja yako. Ikishaamua haiwapi si ndiyo itakuja kwetu tutaiuliza mpango mliweka? Sasa tukiamua sisi kawape…

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, basi sawa, naona Waheshimiwa Wabunge watatusaidia sisi zaidi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, neno moja, huku, sekunde moja tu.

**SPIKA:** Leo naona Bunge linataka kuwaka moto. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, halafu tutarejea tena upande huu.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, labda nyongeza tu kwa alichochangia *engineer*. Ni kwamba pamoja na kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi kwenye eneo fulani ile inabainisha tu hii ardhi itakuwa ya hifadhi, hii itakuwa ya kilimo, hii itakuwa ya mifugo, hii ya makazi, huo ndio mpango, lakini suala la kwamba ardhi hii itamilikiwa na nani ni kitu tofauti; ardhi hii atagawiwa nani ni kitu kingine tena.

**SPIKA:** Kwa nini Bunge linataka kuingia kwenye nani atapewa? Hilo tu ndilo swali langu mimi. Yaani kwa nini tuseme akapewe Dkt. Kigwangalla na siyo Dkt. Tulia? Yaani kwa nini tuiambie Serikali hivi? Waheshimiwa Wabunge lazima tuelewe jambo moja, haya ni maazimio ya Bunge. Yakishakuwa ni maazimio ya Bunge ni maelekezo kwa Serikali. Kama ni maelekezo, kwenye hili la nani apewe tunatoa ushauri au tunaielekeza Serikali kwamba lazima hao ndio wapewe. Tukiweka kwenye maazimio maana yake tunaielekeza Serikali nani apewe, ndicho ambacho Bunge tunataka kufanya?

Bunge unaweza kuishauri Serikali kwamba kawape hawa, lakini isipowapa siyo kwamba ni kesi maana si ni ushauri, unaweza kufuatwa au usifuatwe, lakini ukishaweka kuwa ni azimio maana yake ni lazima Serikali ikawape hawa. Sijui tunaelewana Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla? *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakuelewa, naomba nimalizie kusema hivi, ushauri wetu ulijikita kwenye msingi huo wa kwanza, lakini msingi wa pili ilikuwa ni *facts* zilizokuwepo pale uwandani. Kuna watu wanamiliki mashamba, kuna watu wameendeleza, kuna watu wamewekeza, kuna mali pale, vyote hivyo, mwisho wa siku usipotoa ushauri wa namna ambavyo wanaweza wakamaliza huo mgogoro linaweza likabatilishwa lile shamba halafu kesi zikatokea kutokana na watu wana mali zao ziko pale. Kuna uharibifu unaweza ukafanyika, kuna dhuluma inaweza ikafanyika, kwa hiyo sisi tuliona kwamba itakuwa bora tukapendekeza hivi.

**SPIKA:** Sawa. Sasa niwaulize kwa sababu ninyi ndiyo mlikuwepo. Kwa hiyo, kwa hapa tulipo, moja mmesema mahitaji halisi ya ardhi kwa wanakijiji, je, ikitokea ardhi yote ile pamoja na aliyonayo mwekezaji, kwa namna hapa ilivyoandikwa, hao wanakijiji wote wanahitaji, mwekezaji yeye atapewa wapi? Haya, wakati huo huo mmesema, uwezo wa mwekezaji, mwekezaji amejieleza, amekopa, amefanya nini kajieleza, ardhi yote ile anaihitaji kwa kweli kwa uwezo tuliouona, hawa wanakijiji watapewa kutokea wapi na wewe umeielekeza Serikali lazima iwape? Hapa umesema, uwezo wa wenye vitalu, je, ikitokea uwezo wa wenye vitalu lile eneo lote wana uwezo wa kulitumia utafanya nini? Huyu mwekezaji atapewa wapi, wanakijiji watapewa wapi?

Hoja ya kwa nini tunataka kuyaondoa haya kwenye maamuzi ya Bunge au kwenye maelekezo ya Bunge ni kutoa nafasi kwa Serikali kwenda kufanya hiyo tathmini, kuangalia haya kama mambo ya kiutendaji na si mambo ya maelekezo ya Bunge. Sijui kama nimeeleweka? Waheshimiwa Wabunge, tulimalize hili. *(Makofi)*

Haya, kuna mtu hajaongea kabisa leo, Mheshimiwa Rose Tweve.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tumepata maoni mazuri sana kutoka kwenye Kamati, tumesikia

michango mingi tu ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa kwa unyeti wa jambo hili, napendekeza tujipe muda, waende wakalichakate tena kwa sababu hapa inaonekana…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ROSE C. TWEVE:** …Nisikilizeni Waheshimiwa Wabunge, tupate ushauri mzuri kutoka kwa wanasheria, tuna wanasheria wazuri ili tuje na azimio ambalo linaeleweka kwa unyeti wa jambo hili.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Serikali ya mkoa tena, Mheshimiwa Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati, lakini nimekuelewa. Nadhani taarifa ile kubwa ina *details* za kutosha. Sisi tutoe maazimio ya ubatilishaji wa shamba pamoja na ile (d) kama ambavyo tumei-*craft* hapa sasa hivi. Sasa, Serikali kwa kuzingatia *details* zilizoko kwenye taarifa kubwa ndipo itaamua kwamba inatekelezaje, lakini suala la msingi ni lile shamba ambalo lilibinafsishwa ambalo ndilo limepelekea haya yote ambayo yametokea. Kwa hiyo, nakubaliana na pendekezo lako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumefika sehemu nzuri na tumeelewana kwenye hii sehemu ya kwanza ya maazimio, inakuwa; Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ibatilishe umiliki wa shamba lote la Malonje (Shamba la Efatha) na vitalu 51 kwa kuzingatia sheria na maslahi ya umma; na

(b) Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo lote kama lilivyotajwa kwenye aya (a). Hii nyingine (c) inaondoka. *(Makofi)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nina hoja kidogo hapo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba, tumewasikiliza Waheshimiwa Wabunge wakati wanaongea, hasa waliopata nafasi ya kuchangia, wameituhumu Serikali ya Mkoa. Naamini Serikali ya Mkoa ndiyo ilikuwa na *mandate* ya kugawa lile shamba wakati ule, kama ilikuwa sahihi. Sasa, tunaposema Serikali ibatilishe na iangalie utaratibu mzuri wa kugawa tena, mgogoro umekuwepo muda mrefu na inaonekana watu hawa mpaka wamejaribu kurubuni Kamati isifanye kazi. Je, *are we sure* ikiendelea kubaki chini yao walewale ambao wamehusika na ambao wametuhumiwa hapa, *whether* ni wilaya au ni mkoa, haki itatendeka kwa wale wananchi au tutarudi palepale? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, sasa hiyo ni hoja ambayo haitaweza kuingia hapa kwenye Maazimio, lakini ni hoja ya msingi, tutaendelea nayo kwenye kuishauri Serikali. Waheshimiwa Wabunge tumeelewana?

Sasa nitawahoji. Si ndiyo jamani?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, ombi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul ni ombi la kuingiza humo, eeh?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, la Azimio, la kuongezea hapo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. La kwangu ni ombi, kwa kuwa, tuko kwenye haya maazimio na

wenzetu wa kamati wametuletea, nadhani pia, na sisi tunachangia. Nadhani tuongeze Azimio la *General* hapo, *General Provision* kwenye Maazimio hayo ambayo kamati imetuletea kwamba, Serikali kwa ujumla wake sasa itatue migogoro ambayo inafanana na shamba hili baina ya wawekezaji na wananchi na watuletee taarifa hii kabla Bunge hili halijamaliza muda wake. Lilikuwa ni ombi kwako.

**SPIKA:** Haya, nimekusikia, lakini nitaeleza baadaye kidogo kwa nini hatuwezi kuiingiza hapa.

Sasa, Waheshimiwa Wabunge Hoja ilikuwa imeshaungwa mkono na sasa nawahoji, mkiwa mnakijua kilichoandikwa humu ambacho tunahojiana, kuhusu Mapendekezo na Maoni ambayo yako kwenye Taarifa ya Kamati Maalum ya Bunge ya Kuchunguza Mgogoro wa Ardhi kati ya Mwekezaji katika Shamba la Malonje na Wananchi wa Vijiji vinavyozunguka Shamba hilo, wote mmeafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mapendekezo na Maoni ya Kamati Maalum ya Bunge ya Kuchunguza Mgogoro wa Ardhi kati ya Mwekezaji katika Shamba la Malonje na Wananchi wa Vijiji Vinavyozunguka Shamba Hilo Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Hujamaliza nini tena Mheshimiwa?

Waheshimiwa Wabunge, Taarifa hii ambayo ilisomwa kwetu hapa kwa kifupi, kwa upande wa vile vielelezo vyote ambavyo kamati imenikabidhi na Taarifa yao ile kubwa kabisa yenye Taarifa zote ambazo wamezisema hapa kwa urefu zaidi na za ziada ambazo hawakupata nafasi kwa sababu ya muda, wamenikabidhi nami nitaikabidhi Serikali, ili wakaifanyie kazi kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka mwisho, lakini kwa maana ya Maagizo ya Bunge kwa Serikali, ni haya Maazimio ambayo tumehojiana hapa. Sasa,

tulizungumza hilo la kwanza kwa sababu, kuna mengine ambayo pia, ni Maazimio ya Bunge.

Hilo moja ndiyo lilikuwa linahitaji marekebisho kidogo ndiyo maana tulilijadili hilo, lakini yote ni Maazimio ya Bunge. Kwa hiyo, Serikali inapewa hayo, lakini pia, ile Taarifa kubwa kabisa ambayo haikuwekwa hapa mbele yetu tutaikabidhi Serikali na vielelezo vyote.

Kuna Mheshimiwa Mbunge alichangia hapa kuhusu majina ya watu wanaohusika na nini, mbona hawajatajwa hapa? Kwenye ile Taarifa kubwa, taarifa zote zipo na majina ya watu yapo. Siyo kwamba, wanafichwa ni kwa sababu, maneno huwa yanapunguzwa kutajwa hapa mbele kwa hiyo, ndiyo maana wengine wametajwa kwa sababu ya ufupisho wa ile Taarifa, lakini Taarifa Rasmi kubwa kabisa ipo na ina majina ya kila mtu. Naamini Serikali itayafanyia kazi hayo na haya pia, ambayo tumeyaazimia hapa.

La kwanza, ni hili la Mheshimiwa Gekul ambalo alikuwa amependekeza na aliniandikia hapa kwa sababu, Kanuni zetu zinataka mtu akitaka marekebisho kwenye Maazimio yaliyopendekezwa na Kamati aandike na yeye aliandika, lakini pendekezo lake linahusu migogoro iliyoko sehemu nyingine ambayo inafanana na huu mgogoro. Sasa hilo tutaikabidhi Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge ambao kuna changamoto za namna hiyo kwenye maeneo yao, wanaweza kuzungumza na kamati, ili kamati kadiri inavyofanya kazi zake, Serikali inapoenda mbele yake, wataendelea kuifuatilia hiyo migogoro yote. Kwa sababu, hatutaweza kumudu kutengeneza kamati, kwa ajili ya kila mgogoro na tunaamini kwa juhudi mbalimbali zinazoendelea kufanywa na Serikali, migogoro itaendelea kupungua na kisha kumalizika kabisa.

Sasa, pamoja na Maazimio haya ambayo tumeyapitisha kama Bunge na yanaenda kwa upande wa Serikali, kwanza ni muhimu

kufahamu kwamba, kuna hiyo taarifa kubwa ambayo tunawakabidhi Serikali kwenda kuifanyia kazi ambayo imewekwa vielelezo vyote.

Jambo lingine ambalo ni la muhimu ni kwamba, Taarifa ya Kamati imesomwa hapa, ila pia, Waheshimiwa Wabunge wanaruhusiwa kuchangia kadiri waonavyo. Sasa wakati mwingine huwa inaleta mkanganyiko mchango wa Mheshimiwa Mbunge mmoja unaonekana ndiyo Bunge limesema.

Nimeona nitoe huu ufafanuzi, ili isije ikaleta mkanganyiko huko nje ambavyo Mheshimiwa Mbunge mmoja akiwa amezungumza jambo fulani, basi inaonekana ni Bunge limesema. Ni mawazo yake na anaruhusiwa humu ndani, analindwa kabisa na Ibara ya 100 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa, kwa maana ya Taarifa nzima ya Kamati, wote tumeisikia na imeonesha kila mahali ambapo kuna changamoto, upande wa wanavijiji kwa changamoto hizi zilizojitokeza.

Ilitokea upande wa mwekezaji, kuna mtu ameuawa, Kamati imetusomea hapa. Wakati huohuo wanavijiji pia, wamepata madhara makubwa sana kutoka upande wa mwekezaji na kwa muktadha huohuo pia, Kamati yetu imeonesha namna ambavyo Serikali kuna mahali ambapo haikufanya ilivyopaswa kufanya. Sasa kwa sababu nia ni mgogoro kwisha na si kutafuta mchawi yuko sehemu gani, tunaamini kwa mjadala huu ambao umekuwepo hapa Bungeni na Maazimio ambayo Bunge limeyafikia, basi mgogoro huu wa Shamba la Malonje utafika mwisho.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo ni la muhimu kulizungumza ni kwamba, yale tuliyoyasema hapa ndani, Serikali inayachukua, ikafuate utaratibu, ikafuate Sheria, ili tusirudi tena kule ambako tumetoka. Kwa maana hiyo, kile kinachoendelea kule shambani haya maamuzi hakiyazuii, yaani haizuii yule mwenye kitalu kuendelea kuvuna, sijui kama anavuna, kama analima ama kama huyu mwingine anafuga maana yake atafuga mpaka Serikali itakapomaliza huo mchakato na inapaswa kufanya mchakato

ambao hatutarudi tena hapa ndani kwamba, haikufuata utaratibu. Kwa hiyo taratibu zote zitafuatwa na wale wawekezaji walioko kwenye hili shamba wasije wakaona kwamba, basi leo ndiyo mwisho wao wa kuingia na kutoka hapo na mambo kama hayo. Kwa hiyo, nawaomba sana wanavijiji wa vijiji vile nane wanaolizunguka shamba hili, kwa namna ambavyo wamewasikia Waheshimiwa Wabunge hapa ndani, isije ikaleta picha kwamba, sasa lile shamba pengine limerejeshwa wapi? Limeelekea wapi? Hapana.

Shamba lile Bunge limeazimia kwamba, Serikali iweze kuchukua hatua kadhaa, lakini hatua hizo zifuate utaratibu uliopo na pia, zifuate Sheria za nchi. Kwa hiyo, Serikali itakapomaliza mchakato wake, wote tutataarifiwa. Wakati huo, nawaomba kama ambavyo huko nyuma wameendelea kuwa watulivu na wastahimilivu, basi utulivu huo na ustahimilivu uendelee wakati Serikali inaendelea kujipanga kutekeleza maagizo haya ya Bunge.

La mwisho kabisa Waheshimiwa Wabunge, sote tunafahamu, nchi yetu hii haiongezeki ama ardhi haiongezeki, lakini watu tunaongezeka. Kwa hivyo, ni muhimu sana sisi sote kulikumbuka hilo haitawezekana kwamba, kila mahali ambapo kuna ardhi, basi kadiri watu wanavyoongezeka kwamba, ardhi itakuwa inagawanywa kwa ajili ya watu, hapana. Kama kuna mahali ambako Sheria zitakuwa zimefuatwa, watu wamepewa hati zao na ni wawekezaji na wanafanya uwekezaji, maana yake itakuwa hivyo. Hili linamaanisha nini?

Upande wa Serikali kwa sasa tunayo, ukiacha Tume ile ya Upimaji wa Ardhi, ndiyo inaitwa hivyo ama inaitwa jina lingine, lakini Tume hiyo inayoshughulika na Ardhi na majukumu yake, lakini sasa ipo Tume ya Mipango, ile Tume ya Taifa kabisa, lazima sisi wananchi tuwe tunajua kwamba, eneo letu limeishia hapa. Pamoja na kuishia hapa, hakuna namna tutaongezwa kwa sababu, huko kwingine Serikali imepanga kuja kujenga barabara pengine ya njia nane.

Kwa hiyo, ukienda hapo unalima, lakini Serikali kuna muda itajenga barabara pana ya njia nane, lazima kuwe na hiyo mipango. Au kwamba, eneo hili hata kama tunalima sasahivi, lakini Serikali imejipanga huko baadaye kuja kuweka kitu fulani. Hili litatusaidia pia, kama nchi na kujua kwamba, ardhi haiongezeki na hatuwezi kujenga kila mahali, hatuwezi kulima kila mahali na hatuwezi pia, kufuga kila mahali. Kwa sura hiyo, Serikali mkitusaidia hiyo mipango na sisi itakuwa ni kazi yetu kuendelea kuizungumza, ili tusiingie kwenye migogoro hii ambayo inatufanya hata tuko hapa muda huu.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, nilimwomba Mheshimiwa Naibu Waziri aende akafuatilie ni mazingira gani wanaume, wanawake na watoto wanalazwa kwenye wodi moja. Nimeletewa taarifa hapa na hii taarifa inao ushahidi wa picha, maana teknolojia imetusaidia.

Hii taarifa niliyoletewa hapa na huu ushahidi wa picha, unaashiria kwamba, hawa watu hawalazwi wodi moja. Kuna picha hapa imepigwa wodi ya wanaume na kuna picha imepigwa wodi ya wanawake, lakini jambo la msingi ni kwamba, miundombinu kwenye kituo hiki cha afya bado inahitajika. Kwa nini, kwa sababu, watu waoweza kulala kwenye hii iliyoitwa wodi ya wanaume ni wanaume wachache, wanaweza kulazwa wawili kwa wakati mmoja, wakati upande wa wanawake ni watano kwa wakati mmoja na upande wa watoto ni kulaza watoto watatu kwa wakati mmoja. Hili ni jengo la matibabu ya nje ama *OPD* ndiyo linalotumika kulaza hawa wagonjwa, kwa hiyo wodi haipo.

Kwa hivyo, yale maelezo yaliyokuwepo ya kwamba, wanalala wote sehemu moja hilo halipo, hawalali sehemu moja watoto, wanawake na wanaume, lakini wanalala kwa namna ambayo tumeelezwa hapa. Kama nilivyosema, nimeletewa na ushahidi wa picha na sitaki kuamini katika sekunde zile chache vilienda kuchapishwa vibao halafu vikabandikwa kwa sababu, vinaonekana ni vibao vya muda kidogo na hiki ni kituo cha afya.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo taarifa niliyokuwa nimemwambia Mheshimiwa Naibu Waziri akaifuatilie, ameifuatilia na inaonekana watu wanaoweza kulazwa hapo kwenye hicho kituo cha afya kwa wakati mmoja ni watu 10, watano wanawake, wawili wanaume na watoto watatu, lakini ni vyumba tofauti. Hizi siyo wodi ila ni vyumba vile ambavyo vingeweza kutumika, kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa wa nje sasa vinatumika, kwa ajili ya kazi hii. Kwa hiyo, hawalali kwenye wodi moja.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa uvumilivu wenu na Kamati tunawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya. Nilisema ningempa nafasi Mheshimiwa Lukuvi, sasa nimpe hiyo nafasi kisha tutasitisha Bunge. Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye yupo nje ya jengo hili kikazi, lakini kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye bahati njema tunaye humu ndani amesikia tangu mwanzo, napenda niseme kidogo, lakini kabla sijasema naomba kwa uungwana tu, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniwezesha kupata nafasi inayonifanya niseme leo. Namshukuru sana kwa kuniamini na kurudi kwenye kiti hiki ambacho wengi wenzangu mnajua nimekuwa nacho kwa miaka kumi. Najua mnaguna, kwa hiyo mjue kwamba, mi ni mzoefu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie kwamba, kwanza hatua uliyochukua ni njema sana na ya kiungawana na bila shaka Watanzania wote waliosikia watakuwa wamefurahia sana hatua hii. Kwa hiyo, tunakupongeza sana, kama Serikali, kwa hatua hii uliyochukua ya kumaliza mgogoro huu, lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Spika kwamba, siku zote Mheshimiwa Rais amekuwa anathamini na kuheshimu sana maamuzi ya Bunge, mara zote.

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia tu kwamba, sisi wasaidizi wake kwa sababu, kama mnavyomjua Mheshimiwa Rais amekuwa anaheshimu na kusimamia sana kwa dhati kabisa Utawala wa Sheria na Utawala Bora. Kwa sababu hiyo, sisi wasaidizi wake wajibu wetu ni kufanya kazi kwa kutekeleza majukumu yetu kwa maono yake, hadhi na heshima yake na matarajio ya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwaondolee wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika na Watanzania wote wanaosikiliza, hasa Watanzania wanaoishi Mkoa wa Rukwa kwamba, Serikali imesikia na Serikali iko humu ndani. Serikali ni wenzenu kwa sababu, hata Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo msimamizi wa shughuli za Serikali Bungeni. Kwa hiyo, nimesimama hapa kwa heshima na taadhima kwa nafasi uliyonipa kukuhakikishia kwamba, kwa niaba, kama nilivyosema, ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Serikali imesikia Maazimio yote ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nakiri pia kwamba, baadhi ya maelezo yamesemwa hapa, Mheshimiwa Rais ni kweli alikuwa Rukwa kwenye ziara na mimi kama mshauri wake nilikuwa sehemu ya *delegation* hiyo. Ni kweli, haya aliyasikia na ni kweli, alijua kwamba, Mheshimiwa Spika ameunda hiyo Kamati, alisikia. Kwa hiyo, hili ninalolifanya ni kweli, Mheshimiwa Rais alikuwa analijua na ndiyo maana nasimama kwa heshima na taadhima kukuhakikishia kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ina jukumu la kuratibu shughuli zote za Serikali, italifanyia kazi jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, linahusisha sekta nyingi, italiratibu vizuri sana na kuhakikisha Maazimio haya yote yaliyoainishwa na Bunge lako Tukufu yanatekelezwa kwa mujibu wa Sheria. Kwa sababu hiyo, nakushukuru sana, nimesimama kuthibitisha tu, kwamba, Serikali itakuwa tayari na ipo tayari kufanya hivi na sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu, tutahakikisha Serikali kwa umoja wetu tunatekeleza Maazimio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, lazima tutakuja kuripoti mwenendo na *outcome,* yaani mwisho wa kazi hii ambayo tumeelekezwa na Bunge. Hatutasita kutekeleza mambo yote yatakayokuwa yameazimiwa na Bunge pamoja na hili. Kwa hiyo, nakushukuru sana, lakini tunaomba mwendelee kutushauri kwa sababu, nchi hii itajengwa na sisi sote na hasa wawakilishi wa wananchi, ninyi mna wajibu wa kuikumbusha Serikali mambo kadhaa ambayo yamekuwa yanaleta kero kwa wananchi na kuwahakikishia kwamba, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi hii amejipambanua, asingependa wananchi waendelee kuwa na kero huko. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnapoibua kero kama hizi zinaisaidia Serikali na kuikumbusha Serikali ili kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA**: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Unatokea wapi? Nani kasema Mwongozo?

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA**: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 76, kwa kutunza muda naomba nisiisome. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri aliyekwenda kuthibitisha na kuleta picha, lakini nataka nikwambie, kama Mheshimiwa Mbunge ninayetoka Ilemela, kituo kile nilishakitembelea na kwa macho yangu nikayaona. Kabla ya kuuliza swali, nime-*confirm* na Mstahiki Meya ambaye ndiyo kata yake, hakuna wodi ya wanaume, hakuna wodi ya watoto, iliyopo ni wodi moja.

Mheshimiwa Spika, nilishaenda mwenyewe nikakuta wanaume wapo na wanawake wapo na nikaongea na mtu wa kituoni. Sasa hili la kuwaweka watu kwenye chumba ambacho ni cha *OPD* na kuweka vitanda viwili ukaita wodi, hiyo sijui kama imefanyika leo au siku mbili zilizopita, lakini ninachotaka kusema, kwa ridhaa yako, ni

uridhie safari na Waziri mhusika akaone mazingira ya kile kituo halafu alinganishe na picha zilizoletwa hapo kama ushahidi kwamba, ndiyo wako hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwakilishi, ni mtu mzima, siwezi kuleta uongo, *unless* wamehamisha vitanda juzi na lini au leo asubuhi kuweza kufanya zile kuwa wodi na sio wodi. Wodi iko moja tu katika kituo cha afya cha toka mwaka 1999.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, kwa maelezo hayo unayoyatoa ni kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri taarifa aliyoleta hapa ni ya uongo?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA**: Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba, itakuwa ya uongo kwa sababu, hakuna hiyo wodi ya wanaume anayoisema na ndiyo maana amesema wako kwenye…

**SPIKA:** Sawa.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA**: Mheshimiwa Spika, chumba cha *OPD* tangu lini kikatumika kama wodi?

**SPIKA:** Jamani, Waheshimiwa Wabunge, mimi ninayo hapa picha ambayo yuko mdada anachukua dawa na pembeni yake, na ndiyo maelezo niliyonayo hapa, pameandikwa wodi ya wanaume na maelezo yaliyotolewa hapa ni kwamba, hivi ni vyumba vimewekwa vitanda. Kwa sababu hiyo, hicho kituo cha afya hakina wodi, sasa Mheshimiwa anasema wodi ipo ila wanalala wote hawa kwenye wodi moja, hakuna hao waliotenganishwa vyumba.

Si ndiyo Mheshimiwa, nimeelewa vizuri, kwamba, wodi ipo, lakini iko moja na wanalala wote humo.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA**: Mheshimiwa Spika, nimesema wodi iko moja na ilikuwa ni ya wanawake. Mimi nilitembelea pale.

**SPIKA:** Haya.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA**: Mheshimiwa Spika, sema siku zimepita.

**SPIKA:** Sawa, hilo limeshaeleweka.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA**: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kinachofanyika hapa, kama wameandaa hizo wodi ni kwamba, si wodi kama wodi na hazina muda mrefu. Leo asubuhi nimeongea na Meya.

**SPIKA:** We umeenda lini Mheshimiwa, leo asubuhi?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA**: Mheshimiwa Spika, nasema hivi, kama wameandaa hizo wodi hazina muda mrefu kwa sababu, mimi nimeenda miezi kadhaa iliyopita, kama miwili, lakini nimeongea na Mstahiki Meya wa Ilemela ambaye ni Kata yake.

**SPIKA:** Sawa, sasa Waheshimiwa Wabunge, keti Mheshimiwa. Mimi kwa sababu, huwa napenda haki itendeke, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula anasema hizi picha nilizoletewa hapa ambazo zimeandikwa wodi ya wanawake na wodi ya wanaume na nimewapa maelezo kwamba, hizi zilizoitwa wodi wamesema ni vyumba ambavyo kwa sasa vinatoa hiyo huduma.

Mheshimiwa Angeline Mabula amesisitiza kwamba, pale kwenye kituo cha afya iko wodi ya wanawake ambayo wote wanalala humo. Maana yake ni sasa hivi hata tukienda hapo labda watuambie wametengeneza wiki iliyopita, si ndiyo? Ili tumtendee haki Mheshimiwa Mbunge na ili pia, tuitendee haki Serikali kwa maelezo waliyoniletea hapa, Mheshimiwa Angeline Mabula Kanuni zetu zinataka anayesema kwamba, mwingine anasema uongo yeye

ndiye anayepaswa kuthibitisha. Kwa hivyo, wewe Mheshimiwa Mabula niletee tu uthibitisho wa hiyo wodi moja ambayo wanalala hao wote halafu tuanze sasa, upande wa Serikali kwa nini wamelidanganya Bunge? Si tumeelewana Waheshimiwa eeh? Ndiyo Kanuni zetu zinavyosema. Mheshimiwa Mbunge atasimama na atasema Mbunge mwingine anasema uongo, ni kazi yake yeye kuthibitisha kwamba, huyu ndiye anayesema uongo.

Mheshimiwa Naibu Waziri naona unataka kusema jambo, lakini mpe nafasi Mheshimiwa Angeline Mabula aniletee ushahidi. Akishaniletea huo ushahidi tutalijadili hilo jambo kwa sababu, si limetokea hapa ndani kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi litaenda vizuri kabisa.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni, leo.

*(Saa 9.40 Alasiri Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR - KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa mara ya Pili sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria,

Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Mwaluko Aidan Kabudi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza mbele ya Bunge lako Tukufu naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa kuniwezesha kusimama leo mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara yangu ya kwanza tangu nilipoteuliwa na kuapishwa kutumikia nafasi ya Waziri wa Katiba na Sheria tarehe 15 Agosti, 2024.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu na kwa kuona ni vyema nimsaidie katika nafasi hii ya Waziri wa Katiba na Sheria. Namwahidi Mheshimiwa Rais kwamba nitatekeleza majukumu haya aliyonipa kwa nguvu zangu zote, kwa moyo wangu wote na kwa akili zangu zote kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Mawaziri na Manaibu Waziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa namna ya kipekee nimshukuru mtangulizi wangu Balozi Dkt Pindi Hazara Chana, Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani nisipokushukuru wewe binafsi kwa kunipongeza na kwa ushirikiano ambao nimeupata kuanzia kwenye Kamati ya Utawala Katiba na Sheria na sasa katika mkutano huu. Kwa namna ya kipekee nakupongeza wewe binafsi kwa kutekeleza kwa umahiri na ufanisi mkubwa majukumu ya Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*.

Juzi nilipokuona Beijing furaha yangu ilikuwa kubwa sana. Picha ile itunze sana, nakupongeza sana na nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria, kuisimamia na kuishauri Serikali. Aidha, niwashukuru sana kwa ushirikiano mnaonipa, hii ni Wizara yenu wakati wote milango yake ipo wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wanaonipatia toka nilipoteuliwa tena kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Hamza Saidi Johari kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na namwahidi ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu yangu unategemea watendaji walio chini yangu. Kwa namna ya kipekee nimpongeze Ndugu Eliakim Chacha Maswi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kutumika katika nafasi hii na nimtakie mafanikio mema. Aidha, nampongeza Dkt. Franklin Jasson Rwezimula, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na kuipongeza Manejimenti yote ya Wizara na watumishi wote kwa ushirikiano wanaonipa kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliletea Taifa letu maendeleo makubwa na

kutekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo na kuboresha huduma mbalimbali ikiwemo elimu, afya, maji na kadhalika. Mengi yamefanyika chini ya uongozi wake na sote ni mashahidi wa jitihada anazochukua katika kuiongoza na kuitangaza nchi yetu kimataifa ili kuendelea kuwaletea maendeleo wananchi wote kwa ujumla bila kusahau falsafa yake ya *4R* (Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Ujenzi Upya) ambazo zimekuwa nguzo muhimu katika kuimarisha utawala wa sheria na utawala bora nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024)* ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, napenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu mbele ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ushauri huo muhimu wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayopendekezwa kurekebishwa kupitia Muswada huu kama ulivyowasilishwa Bungeni ni Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania. Madhumuni ya Muswada huu yanalenga kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zilizobainika katika utekelezaji wa masharti ya Sheria hii ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa shule kutoa mafunzo ya kozi nyingine maalum za mafunzo ya sheria hiyo ni pamoja na kuondoa sharti la kila mhitimu wa shahada ya sheria kulazimika kupitia na kufaulu masomo ya sheria kwa vitendo hata kama hakusudii kufanya kazi za uanasheria katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu mbili ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya

utangulizi yanayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali yanapendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu marekebisho yanayopendekezwa katika vifungu mbalimbali vya Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha watu wanaosimamiwa na Sheria hiyo. Aidha, inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho. Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka tafsiri ya neno "mafunzo maalum" kwa lengo la kuhakikisha hakuna tashwishwi katika kuelewa dhana hiyo kama inavyopendekezwa katika Muswada. Aidha, kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupanua wigo wa majukumu ya Shule ya Sheria Tanzania ili kujumuisha jukumu la kutoa mafunzo maalum katika Sekta ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa sharti la majukumu ya wakurugenzi kuainishwa katika kanuni na badala yake kuainishwa katika muundo wa utumishi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa Sheria inazingatia nyaraka sahihi zinazoainisha majukumu ya wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9(2) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumwondoa Mkuu wa Shule kuwa Katibu wa Kamati ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Mitihani na badala yake kumweka Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na mafunzo kuwa katibu. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuimarisha ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hiyo kwa kuwa Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na mafunzo ndiye mwenye jukumu mahsusi la kusimamia masuala ya mafunzo na mitihani katika Shule ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9(4) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha muda wa ujumbe wa wajumbe wa Kamati ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Mitihani. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa muda wa wajumbe

kuhudumu unatamkwa bayana katika Sheria. Aidha, Kifungu kipya cha 13A kinapendekezwa kuongezwa ili kutambua katika Sheria nafasi ya Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na Mafunzo na Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na Utawala. Marekebisho haya yanalenga kutambua nafasi hizi muhimu katika uongozi wa Shule ya Sheria ambazo kwa sasa hazijatambuliwa katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho, kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kuhusu sifa za wanafunzi wanaoweza kudahiliwa kwa ajili ya mafunzo maalum. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa sifa za wanafunzi zinabainishwa wazi katika mtaala wa mafunzo husika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubadili muundo wa Bodi ya Shule ya Sheria ili kujumuisha wajumbe wa taaluma nyingine muhimu ambao si wanasheria. Kifungu hicho pia kinarekebishwa ili kuongeza uwakilishi wa taasisi zinazotoa mafunzo ya sheria na zinazosimamia mafunzo ya sheria katika ngazi zisizo za shahada na wadau wengine wa sheria. Aidha, kifungu kidogo cha tatu (3) kinaainisha mamlaka ya uteuzi ya wajumbe wa Bodi ambao hawaingii kwa nafasi zao za madaraka.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 17 pia kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha kuwa wajumbe wa Bodi watalipwa posho kadri itakavyoamuliwa na Msajili wa Hazina. Lengo la marekebisho haya ni kutambua nafasi ya Msajili wa Hazina katika kuamua kiwango cha posho na stahiki za wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024)* na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MAELEZO YA MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (MB) WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA SHULE YA SHERIA TANZANIA WA MWAKA 2024 (THE LAW SCHOOL OF TANZANIA (AMENDMENT) BILL, 2024) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza mbele ya Bunge lako tukufu, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa kuniwezesha kusimama leo mbele ya Bunge lako tukufu kwa mara yangu ya kwanza tangu nilipoteuliwa na kuapishwa kutumikia nafasi ya Waziri wa Katiba na Sheria tarehe 15 Agosti 2024.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu, na kwa kuona ni vyema nimsaidie yeye na Serikali yetu katika nafasi hii ya Waziri wa Katiba na Sheria. Namwahidi Mheshimiwa Rais kwamba nitatekeleza majukumu haya aliyonipatia kwa nguvu zangu zote, kwa moyo wangu wote na kwa akili zangu zote kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru na kuwapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Mawaziri na Manaibu Waziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ya kipekee

nimshukuru mtangulizi wangu Balozi. Dkt Pindi Hazara Chana (Mb) Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani nisipokushukuru wewe binafsi kwa kunipongeza na kwa ushirikiano ambao nimeupata kuanzia kwenya kamati ya Utawala Katiba na Sheria na sasa katika mkutano huu. Kwa namna ya kipekee, nakupongeza wewe binafsi kwa kutekeleza kwa umahiri na ufanisi mkubwa majukumu ya Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria, kuisimamia na kuishauri Serikali. Aidha, niwashukuru sana kwa ushirikiano mnaonipa, hii ni Wizara yenu wakati wote milango yake ipo wazi.

Mheshimiwa Spika, Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (ndc.) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaonipatia toka nimeteuliwa tena kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Nichuke fursa hii pia kumpongeza Mhe. Hamza Saidi Johari kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kumteuwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mwahidi ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa majukumu yangu unategemea watendaji waliochini yangu. Kwa namna ya kipekee nimpongeze Ndugu Eliakim Chacha Maswi Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kutumika katika nafasi hii na nimtakie mafanikio mema. Aidha, nampongeza Dkt Franklin Jasson Rwezimula Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na kuipongeza Manejimenti yote ya Wizara na watumishi wote kwa ushirikiano wanaonipa kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliletea Taifa letu maendeleo makubwa na kutekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo na kuboresha huduma mbalimbali ikiwemo Elimu, Afya, Maji. Mengi yamefanyika Chini ya uongozi wake na sote ni mashahidi wa jitihada anazochukua katika kuiongoza na kuitangaza Nchi yetu kimataifa ili kuendelea kuwaletea maendeleo wananchi wote kwa ujumla bila kusahau falsafa yake ya 4R Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga Upya ambazo zimekuwa nguzo muhimu katika kuimarisha utawala wa sheria na utawala bora nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 (The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024) ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb) pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayopendekezwa kurekebishwa kupitia Muswada huu kama ulivyowasilishwa Bungeni ni Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania. Madhumuni ya Muswada huu yanalenga kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zilizobainika katika utekelezaji wa masharti ya Sheria hii ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa shule kutoä mafuzo ya kozi nyingine maalum za mafunzo ya sheria pamoja na kuondoa sharti la kila muhitimu wa shahada ya sheria kulazimika kupitia na kufaulu masomo ya sheria kwa vitendo hata kama hakusudii kufanya kazi za uwanasheria katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu mbili ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali yanapendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu marekebisho yanayopendekezwa katika vifungu mbalimbali vya Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha watu wanaosimamiwa na Sheria hiyo. Aidha kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka tafsiri ya neno "mafunzo maalum" kwa lengo la kuhakikisha hakuna tashwishwi katika kuelewa dhana hiyo kama inavyopendekezwa katika Muswada.

Aidha, kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupanua wigo wa majukumu ya Shule ya Sheria Tanzania ili kujumuisha jukumu la kutoa mafunzo maalum katika Sekta ya sheria. Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa sharti la majukumu ya Wakurugenzi kuainishwa katika kanuni na badala yake kuainishwa katika muundo wa utumishi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa Sheria inazingatia nyaraka sahihi zinazoainisha majukumu ya Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9(2) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumuondoa Mkuu wa Shule kuwa Katibu wa Kamati ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Mitihani na badala yake kumuweka Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na mafunzo kuwa katibu. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuimarisha ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hiyo kwa kuwa Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na mafunzo ndiye mwenye jukumu mahsusi la kusimamia masuala ya mafunzo na mitihani katika Shule ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9(4) kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha muda wa ujumbe wa wajumbe wa Kamati ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Mitihani. Lengo la

marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa muda wa wajumbe kuhudumu unatamkwa bayana katika Sheria. Aidha, kifungu kipya cha 13A kinapendekezwa kuongezwa ili kutambua katika Sheria nafasi ya Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na Mafunzo na Naibu Mkuu wa Shule anayehusika na Utawala. Marekebisho haya yanalenga kutambua nafasi hizi muhimu katika uongozi wa Shule ya Sheria ambazo kwa sasa hazijatambuliwa katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kupitia Jedwali la Marekebisho, kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kuhusu sifa za wanafunzi wanaoweza kudahiliwa kwa ajili ya mafunzo maalum. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa sifa za wanafunzi zinabainishwa wazi katika mtaala wa mafunzo husika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubadili muundo wa Bodi ya Shule ya Sheria ili kujumuisha wajumbe wa taaluama nyingine muhimu ambao si wanasheria. Kifungu hicho pia kinarekebishwa ili kuongeza uwakilishi wa taasisi zinazotoa mafunzo ya sheria na zinasimamia mafunzo ya sheria katika ngazi zisizo za shahada na wadau wengine wa sheria. Aidha, kifungu kidogo cha tatu (3) kinaainisha mamlaka ya uteuzi ya wajumbe wa Bodi ambao hawaingii kwa nafasi zao za madaraka.

Pia kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha kuwa wajumbe wa Bodi watalipwa posho kadiri itakavyoamuriwa na Msajili wa Hazina. Lengo la marekebisho haya ni kutambua nafasi ya Msajili wa Hazina katika kuamua kiwango cha posho na stahili za wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 (The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024) na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, NAOMBA KUTOA HOJA.

**PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (MB.) WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania ya Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, utangulizi, maelezo ya awali na hadidu za rejea. Kwa mujibu wa Kanuni ya 95(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Nne, Kikao cha Kumi na Tatu kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 15 Februari, 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyotekeleza jukumu la uchambuzi wa Muswada; Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya mikutano ya kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearings*) kuanzia tarehe 15-16 Agosti, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 22 Agosti, 2024, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha

rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada; Kamati ilichambua Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 ukiwa umegawanyika katika sehemu kuu mbili kwa lengo la kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hiyo na kuboresha masharti yanayopendekezwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inaundwa na Ibara ya 1 inayoelezea jina fupi la Muswada na inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria hiyo. Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Ibara ya 2 hadi 8 ya Muswada huu.

Mhshimiwa Spika, maudhui ya marekebisho ya Sheria hii; wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu pamoja na maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria, Kamati ilibaini changamoto na mapungufu katika Ibara mbalimbali zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 3 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 5 kinachochainisha majukumu ya Shule, kwa kuongeza aya mpya ya ‘k’ inayoipa shule ya sheria jukumu la kuendesha mafunzo mengine yoyote mahsusi katika sekta ya sheria. Lengo linalokusudiwa ni kuongeza wigo wa mafunzo yanaweza kutolewa na Shule ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 7 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 15 kinachoanzisha Bodi ya Uongozi ya Shule kwa kukifuta na kukiandika upya kifungu kidogo cha kwanza. Marekebisho yanayopendekezwa yanahusisha:-

(a) Kuongeza idadi ya wajumbe kutoka sita hadi tisa nje ya Katibu. Lengo ni kufikia idadi inayotakiwa kwa mujibu wa

maelekezo ya Serikali na *NACTIVET* pamoja na kuhusisha makundi tofauti tofauti kuwa sehemu ya Bodi ya Shule;

(b) Kumwondoa Mjumbe kutoka Taasisi ya Msaada wa Kisheria miongoni mwa wajumbe wa Bodi hiyo;

(c) Kumwondoa Jaji Kiongozi na badala yake kumweka Msajili wa Mahakama ya Rufani;

(d) Kubadili Mtiva wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es salaam kuwa Mtiva wa Kitivo cha Sheria au Amidi wa Shule Kuu ya Sheria kutoka Taasisi yoyote ya Elimu ya Juu. Lengo hapa ni kuongeza wigo wa Taasisi za Elimu ya Juu zinazoweza kutoa mjumbe na kutambua mabadiliko yaliyofanyika katika baadhi ya vyuo ambavyo havina Vitivo vya Sheria bali Shule za Shule;

(e) Kubadili Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika kuwa Mjumbe mmoja kutoka Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili wa Tanganyika. Lengo ni kuruhusu kuteuliwa ama Rais wa Chama au kiongozi mwingine wa Chama ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Uongozi;

(f) Kuwaongeza Mkurugenzi anayehusika na masuala ya huduma za sheria kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Mjumbe kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Shule, Mjumbe anayewakilisha Chama cha Mawakili wa Serikali, Mjumbe anayewakilisha wanafunzi na Mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wahitimu wa shahada ya fedha, mipango, rasilimali watu au utawala. Lengo likiwa ni kuwahusisha wafanyakazi, wanafunzi, Wizara inayosimamia shule na watu wengine wasio wanasheria kushiriki katika Bodi ya Uongozi wa Shule; na

(g) Kumpa Waziri jukumu la kuteua wajumbe wote isipokuwa wale wanaoingia kwa nafasi zao waliotajwa kwenye kipengele cha (a) hadi (c) za kifungu kinachopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitolea maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya ibara ya 3 ya Muswada; Kamati ilishauri kuwepo na tafsiri mahususi ya maneno "*Specialized Training*" ili mawanda ya mafunzo yanayotarajiwa kutolewa yakafahamika. Aidha, Kamati ilishauri kuweka bayana sifa za wanafunzi wa mafunzo mahsusi. Serikali iliieleza Kamati kuwa marekebisho yatafanyika kwenye Kifungu cha 11 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) kitakachoelezea sifa hizo. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Ibara ya 7 ya Muswada; Kamati ilikuwa na maoni kuwa kwenye marekebisho ya Kifungu cha 15 kinachohusu Wajumbe wa Bodi ya Shule ya Sheria, Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika abaki kama mjumbe na kuingia kwa nafasi yake, pamoja na Mjumbe mwingine kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika miongoni mwa wanachama wa chama hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilieleza kuwa kwa namna Bodi ya Shule ya Sheria ilivyo, Bodi hiyo itakuwa na Mawakili watatu ambao ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwakilishi kutoka Chama cha Mawakili wa Serikali na Mwakilishi kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika ambaye ni wanachama wa chama hicho. Aidha, ilielezwa kuwa Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika kwa nafasi yake tayari ni Mjumbe katika baadhi ya bodi na majopo ya kitaaluma ikiwepo Bodi ya Ithibati ya Wapatanishi na Usuluhishi, Bodi ya Parole, Bodi ya Uongozi ya Chama cha Mawakili Tanganyika *(University of Dar es Salaam School of Law Board)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilieleza kuwa, yapo maelekezo ya Msajili wa Hazina yanayokataza mtu mmoja kuwa mjumbe wa bodi

zaidi ya tatu hivyo marekebisho haya yanalenga kuendana na miongozo ya Serikali. Kwa msingi huo, utaratibu unaopendekezwa unatoa nafasi kwa Wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Chama cha Mawakili Tanganyika kupendekeza jina watakaloona linafaa miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, Kamati bado inadhani upo umuhimu wa Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika na mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa Wanachama wa Chama hicho, kuwepo kwenye Bodi ya Shule ya Sheria. Kwa muktadha huo, Kamati imeandaa Jedwali la Marekebisho ya Sheria linalozingatia maoni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia, ilipendekeza Mjumbe anayependekezwa kutoka miongoni mwa wahitimu wa Shahada ya Fedha, Mipango, Rasilimali Watu au Utawala awe na uzoefu kwenye maeneo hayo usiopungua miaka mitatu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho ya kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, shukrani; napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu, ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba orodha ya Wajumbe wa Kamati hii iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upekee Kamati inampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa ushirikiano mkubwa alioupatia Kamati. Kipekee Kamati inamshukuru kwa ushirikiano wake aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Mbunge, Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana na inampongeza kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri

wa Maliasili na Utalii, Kamati inamtakia utendaji mwema katika majukumu mapya aliyopangiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inampomngeza na kumshukuru Mheshimiwa, Jumanne Abdallah Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kwa ushirikiano alioupatia Kamati. Kamati pia inampongeza Ndugu Eliakim Chacha Maswi kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria. Kipekee Kamati inamshukuru kwa ushirikiano wake aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ya Katiba na Sheria Ndugu Mary Gaspar Makonda na inampongeza kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma. Aidha, Kamati inawashukuru Watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Kamati kuhusu hoja, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

# MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHULE YA SHERIA TANZANIA WA MWAKA 2024 *[THE LAW SCHOOL OF TANZANIA (AMENDMENT) BILL, 2024]* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

---

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024)*.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na nne kikao cha kumi na tatu kwenye Bunge la 12, tarehe 15 Februari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya Mhe. Balozi

Dkt Pindi Hazara Chana aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mikutano ya Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearings*) kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 16 Agosti, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa kuzingatia maoni ya Wadau. Mnamo tarehe 22 Agosti, 2024 Kamati ilikutana na Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024)* ukiwa umegawanyika katika sehemu mbili (2) kwa lengo la kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hiyo na kuboresha masharti yanayopendekezwa katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inaundwa na Ibara ya 1 inayoelezea jina fupi la Muswada na inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Ibara ya 2 hadi Ibara ya 8 ya Muswada huu.

## 2.2 Maudhui ya Marekebisho ya Sheria hii

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika Ibara mbalimbali zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 3 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 5 kinachochainisha majukumu ya Shule, kwa kuongeza aya mpya ya (k) inayoipa shule ya sheria jukumu la kuendesha mafunzo mengine yoyote mahsusi katika sekta ya sheria. Lengo linalokusudiwa ni kuongeza wigo wa mafunzo yanaweza kutolewa na Shule ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 7 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 15 kinachoanzisha Bodi ya uongozi ya Shule kwa kukifuta na kukiandika upya kifungu kidogo cha (1). Marekebisho yanayopendekezwa yanahusisha;

a) Kuongeza idadi ya wajumbe kutoka sita (6) hadi Tisa (9) nje ya Katibu. Lengo ni kufikia idadi inayotakiwa kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali na NACTIVET pamoja na kuhusisha makundi tofauti tofauti kuwa sehemu ya Bodi ya Shule;

b) Kumuondoa Mjumbe kutoka Taasisi ya Msaada wa Kisheria miongoni mwa wajumbe wa Bodi hiyo;

c) Kumuondoa Jaji Kiongozi na badala yake kumuweka Msajili wa Mahakama ya Rufani;

d) Kubadili Mtiva wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es salaam kuwa Mtiva wa Kitivo cha sheria au Amidi wa Shule Kuu ya Sheria kutoka Taasisi yoyote ya Elimu ya Juu. Lengo hapa ni kuongeza wigo wa Taasisi za Elimu ya Juu zinazoweza kutoa mjumbe na kutambua mabadiliko yaliyofanyika katika baadhi ya Vyuo ambavyo havina Vitivo vya Sheria bali Shule za Shule;

e) Kubadili Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika kuwa Mjumbe mmoja kutoka Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili wa Tanganyika. Lengo ni kuruhusu kuteuliwa ama Rais wa Chama au kiongozi mwingine wa Chama ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Uongozi;

f) Kuwaongeza Mkurugenzi anayehusika na masuala ya huduma za sheria kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Mjumbe kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Shule, Mjumbe anayewakilisha Chama cha Mawakili wa Serikali, Mjumbe anayewakilisha Wanafunzi na Mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wahitimu wa shahada ya Fedha, Mipango, Rasilimali Watu au Utawala. Lengo likiwa ni kuwahusisha wafanyakazi, wanafunzi, Wizara inayosimamia Shule na watu wengine wasio wanasheria kushiriki katika Bodi ya Uongozi wa Shule.

g) Kumpa Waziri jukumu la kuteua wajumbe wote isipokuwa wale wanaoingia kwa nafasi zao waliotajwa kwenye (a) hadi (c) za kifungu kinachopendekezwa.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitolea

maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.1.1 Marekebisho ya Ibara ya 3 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishauri kuwepo na tafsiri mahususi ya maneno "*Specialized Training*" ili mawanda ya mafunzo yanayotarajiwa kutolewa yakafahamika. Aidha, Kamati ilishauri kuweka bayana sifa za Wanafunzi wa mafunzo mahususi. Serikali iliieleza Kamati kuwa marekebisho yatafanyika kwenye kifungu cha 11 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) kitakachoelezea sifa hizo. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.1.2 Marekebisho ya Ibara ya 7 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikuwa na maoni kuwa kwenye marekebisho ya kifungu cha 15 kinachohusu wajumbe wa Bodi ya Shule ya Sheria Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika abaki kama mjumbe na kuingia kwa nafasi yake, pamoja na Mjumbe mwingine kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika miongoni mwa wanachama wa chama hicho. Serikali ilieleza kuwa kwa namna Bodi ya Shule ya Sheria ilivyo Bodi hiyo itakuwa na Mawakili watatu ambao ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwakilishi kutoka Chama cha Mawakili wa Serikali na Mwakilishi kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika ambae ni wanachama wa Chama hicho.

Aidha, ilielezwa kuwa Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika kwa nafasi yake tayari ni mjumbe katika baadhi ya bodi na majopo ya kitaaluma ikiwepo bodi ya ithibati ya wapatanishi na wasuluhishi, bodi ya parole, Bodi ya Uongozi ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Univeristy of Dar es Salaam School of Law Board (UDSol). Serikali ilieleza kuwa yapo maelekezo ya Msajili wa Hazina yanayokataza mtu mmoja kuwa mjumbe wa bodi zaidi ya tatu hivyo marekebisho haya yanalenga kuendana na miongozo ya Serikali. Kwa msingi huo, Utaratibu unaoopendekezwa unatoa nafasi kwa

wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Chama cha Mawakili Tanganyika kupendekeza jina watakaloona linafaa miongoni mwao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati bado inadhani upo umuhimu wa Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika na Mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa Wanachama wa Chama hicho kuwepo kwenye Bodi ya Shule ya Sheria. Kwa Muktadha huo, Kamati imeanda Jedwali la Marekebisho ya Sheria inayozingatia maoni hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipendekeza mjumbe anaependekezwa kutoka miongoni mwa wahitimu wa shahada ya Fedha, Mipango, Rasilimali Watu au Utawala awe na uzoefu kwenye maeneo hayo usiopungua miaka mitatu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe

10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Aidha kwa upekee Kamati inampongeza na kumshukuru Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb) kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa ushirikiano mkubwa alioupatia Kamati. Kamati inamuahidi ushirikiano uliotukuka. Pia Kamati inaendelea kumshukuru Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb) Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kiupekee Kamati inamshukuru kwa ushirikiano wake aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb) na inampongeza kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Kamati inamtakia utendaji mwema katika majukumu mapya aliyopangiwa.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

## 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mb)
**MJUMBE WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
27 Agosti, 2024

**SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti kwa wasilisho hilo.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Edward Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na tumshukuru Mwenyezi Mungu ametupatia afya njema na tupo hapa salama.

Mheshimiwa Spika, tumpongeze Profesa Kabudi kwa kuteuliwa na kuaminiwa, nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria. Hawa wote ni wapya tunawapongeza sana na kuwashukuru kwa kazi ambayo mmekuwa mnafanya na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia walimu wangu wa *Law School*. Mimi na wewe tumekutana *Law School,* nilikuwa mwanafunzi wa kwanza wa *Law School.* Kwa hivyo, kwa kweli kwa kutambua kazi walizokuwa wanafanya walimu wangu wote wale nawapongeza sana, akiwepo Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vifungu vinavyobadilishwa ni vichache sana, vipo kama saba tu, lakini nia ni kuleta majawabu kwa changamoto ambazo Shule ya Sheria Tanzania imekuwa ikipitia. Ninaambiwa tangu sisi tupite huko karibu miaka 16 iliyopita hivi na siku hizi kuna *cohort* naambiwa zipo mpaka 40. Kuna wanafunzi wengi sana hapa wa *Law School* wamepita *Law School.* Kwa kweli wakati tunaanza sisi na matarajio yetu, tulikuwa tunatamani *Law School of* Tanzania kama ilivyo kwenye dira yake kwamba, iwe ni taasisi ama kituo bora cha utoaji wa mafunzo ya uanasheria wa vitendo Barani Afrika. Hiyo ndio imekuwa *dream* yetu. Kwa kweli mabadiliko haya huenda ikatusaidia twende huko kwa sababu inatibu baadhi ya changamoto zilizokuwepo kama alivyosema Mwenyekiti wetu wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka *Law School of Tanzania* ilivyoanza mara ya kwanza 2007 sheria ilivyopita, ilimfanya kila mtu ambaye ni *graduate* wa sheria uhitaji ku-*practice* ama utake, upende usipende, ilikuwa ni lazima uende *Law School of* Tanzania ambayo si sawa. Nadhani mantiki yake ilikuwa ni ku-*replace* ile *oral exam* ya zamani ambayo kimsingi ilikuwa ni ya wale ambao walikuwa wana-*practice*. Pia, kwa sababu kulikuwa na kusudi lingine kubwa ukilinganisha wale ambao walikuwa wana-*appear* kwenye ile mitihani ya *oral* ambayo mtu anaweza akafaulu kwa dakika 30 ama saa moja.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sheria baada ya watu ku-*graduate* kwenye shule zetu mbalimbali za sheria mnapita sehemu moja mnapikwa hivi ili mtengenezwe kwa ajili ya soko huko duniani, nadhani ndiyo ilikuwa mantiki yake. Kwa hivyo, marekebisho ya Kifungu cha Ibara ya Pili ya Muswada ambayo inarekebisha ni kujaribu kuondoa hilo sharti kama alivyoeleza Mjumbe wetu wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa marekebisho yaliyopo sasa itakuwa siyo lazima, itakuwa kwa wale tu ambao wana-*practice* ambao ni Mawakili wa Kujitegemea, Mawakili wa Serikali na Mahakimu ambao kwa kweli ndiyo wana-*practice*. Kuwe kuna

ulazima wao waende huko, lakini mwingine ambaye anataka tu kuwa *Lawyer* wa *any house lawyer* ambaye hahitaji ku-*practice* wala kwenda mahakamani isiwe lazima, kwa sababu hii sheria ilikuwa inafanya *LLB degree* ionekane kwamba ni *incomplete*. Ukimaliza *LLB* ama *degree* yako ya *sheria* ikawa ni *incomplete* mpaka uende *Law School of* Tanzania. Kwa hiyo, kuondoa sharti hilo limefungua sasa fursa kutokuwalazimisha wale wengine. Kwa hiyo, marekebisho hayo kwa kweli yatatibu changamoto ambayo imekuwepo kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyingine ni ibara ya 3 ambayo inabadilisha kifungu cha 5 kama walivyosema, inaipa *Law School of* Tanzania ambayo dira yake ilikuwa ni kubwa sana. Kama tunataka kufanya iwe ni *center of excellence,* ni lazima iwe na jukumu zaidi ya lile la ku-*train* wanafunzi wa Shule ya Sheria Tanzania. Iweze kutoa *specialized courses* kama *paralegal* na wengine, kwa sababu wakifanya hivyo watafanya chuo kama *course* zake zikiwa nzuri hata watu kutoka nchi zingine wanaweza kuja *Law School of* Tanzania na wakajifunza halafu tukawa tume-*achieve* ile *dream* yetu ya kuwa *a center of excellence in Africa.* Haiwezi kuwa *center of excellence in Africa* kama hakuna wanafunzi kutoka vyuo vingine kuja kwenye *Law School of Tanzania.*

Mheshimiwa Spika, kama mantiki tulimaanisha iwe ni Tanzania basi tungeandika kwenye dira kwamba tunataka iwe ni *center of excellence* kwa masuala ya kisheria Tanzania, lakini tulikuwa na *a bigger dream* na ili iweze kufanya hivyo ndiyo maana mabadiliko hayo kifungu cha tano inawezesha *Law School of Tanzania* kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia, kama walivyosema wengine kuongeza sasa *structure* kidogo kama hawa *Deputy Principals*, pia marekebisho ya sheria, unajua ilivyoundwa hii sheria Kifungu cha 5 cha sheria mama katika kutengeneza sasa ile *governing board, assumption* ilikuwa ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam peke yake ndiyo ina-*exist,* lakini sasa tuna vyuo vingi sana. Kwa hiyo, kuendelea kusema *Dean School of Law University of Dar es Salaam* ilikuwa siyo

*fair.* Kwa hiyo, kuondoa hili na kusema mwakilishi anayetokana na *faculties of law* kutoka vyuo vingine inafanya iwe *broad* zaidi. Kwa hiyo, ilikuwa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo kuhusu kifungu ambacho hasa Kamati ilileta jedwali na ambalo naona pia Serikali imeleta jedwali hapa. Tumekubaliana kwamba kumwacha *President* wa *Tanganyika Law Society* kuwa kwenye *governing council* ya *Law School of Tanzania.* Tukiheshimu *Tanganyika Law Society* hakuna *a better respect* kuliko kwenda na mtu ambaye ni *President* wa *society,* tena ambaye anachaguliwa na wanasheria wote wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kwa kweli niishukuru Serikali, Profesa Kabudi kwamba baada ya Kamati, imeleta jedwali wamekubali kwa sababu kiukweli Chama cha Wanasheria wa *Tanganyika Law Society* ni chombo muhimu sana kwetu sote na kwa sababu tunataka *Law School* iwe na wanasheria wengi sana. Siyo vibaya wakaanza kumjua *President* wao. Pia, tupate *contribution* ya *Tanganyika Law Society* kupitia kwa Rais wao. Ile ya kumleta tu *member* mwingine ilikuwa ni ku-*belittle Tanganyika Law Society*. Kwa hiyo, kwa kweli Serikali na Kamati tupo *at per* kwamba, abaki kwa cheo chake na kwa heshima ya *Tanganyika Law Society*. Kwa hiyo, hapo hakuna *controversy* kubwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni la jumla sasa Profesa Kabudi, tulitegemea sana hiki chuo isiwe tu ni *another theoretical college* kama zilivyo nyingine huko, tunataka tuone *practice* zaidi ili tuandae wanasheria ambao ni *competitive* na ambao wanaweza kwenda mahakama yoyote hapa duniani na wakaonesha *excellence* zao kwa mafunzo ambayo wanapata kwenye Shule ya Sheria. Ili kufikia lengo hilo lazima *somehow* hii *Law School of Tanzania* iwe *autonomous* kidogo.

Mheshimiwa Spika, unajua hatuwezi kuwa *center of excellence* kama hatuna uhuru kupitia chuo hiki cha kuwaleta wataalamu wote Afrika ambao ni wazuri, wawe wanatembelea shule hii na kutoa

*courses* mbalimbali. Tukifanya hivyo ndiyo tunaelekea huko kuwa kituo bora cha utoaji wa mafunzo ya wanasheria kwa vitendo na tukajulikana Afrika. Kwa hivyo hii shule *the more autonomous it becomes* inasaidia sana. *Principal of Law School* leo wanaweza wakakaa wakaleta *the best lawyers* wawa-*train* Mawakili wetu hawa, kwa hiyo tukielekea huko nadhani itajenga aina ya taasisi ambayo tunaitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku hizi naambiwa *University* of Dar es Salaam pia wanaitwa ni *Law School.* Sijui ile *faculty of law* naambiwa na yenyewe siku hizi inaitwa *Law School.* Sasa, *maybe* ili kuondoa hii *confusion* kwamba, *Law School of Tanzania University of Dar es Salaam, faculty of law* na nyingine kuitwa *faculties of law, maybe* twende *direction* waliyoichukua Uganda ya kutengeneza taasisi ambayo inaitwa *Law Development Center* kama ilivyo kwenye dira.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. Nalishawishi Bunge tupitishe sheria hii kwa haraka na kwa sauti kubwa sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi. Mtoa hoja ajiandae.

**MHE SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Binafsi kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Palamagamba Aidan Kabudi kwa kupewa nafasi tena na kuaminiwa kwa mara nyingine, kupata nafasi ya kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mheshimiwa Rais hajakosea, hongera sana Mheshimiwa Profesa kwa uteuzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nitumie fursa hii nimpongeze Mwalimu wangu alikuwa akinifundisha chuoni, alikuwa akinifundisha Sheria ya *International Laws,* Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari, hongera sana kwake kwa kupata uteuzi huu wa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, una-*deserve,* tangu akiwa mwalimu

kule chuoni, lakini baadaye akawa *DG* wa masuala ya mambo ya ndege, pia leo amekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tumeungana na yeye ndani humu Bungeni. Hapo zamani alikuwa mwalimu na mimi mwanafunzi na leo mwalimu na mwanafunzi wote tupo mjengoni humu, hongera sana. Kwa hiyo, matunda yanaonekana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie fursa hii kwenye haya maboresho ya sheria ya Shule ya Sheria. Niwapongeze Wizara pamoja na taasisi zake kuwa *flexible* katika kuboresha hii sheria na vifungu mbalimbali kuhusiana na Shule ya Sheria, kama ambavyo watangulizi walivyoelezea. Pamoja na mabadiliko ambayo yameletwa hapa kwenye huu Muswada wa Waziri Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, pia kwenye Kamati yetu tume-*debate* kwa muda na tunamshukuru Mheshimiwa Palamagamba Kabudi kwa kuwa *flexible* kukubaliana, pia kwenda pamoja na mawazo ya Kamati, hasa vifungu mbalimbali ambavyo tumekuwa tukivipitia kwa pamoja na kukubaliana kwa pamoja, hasa kuangalia vifungu vya sheria katika Shule ya Sheria, kifungu cha 4, 5, 8, 9, 11 pia 15 ambacho kinaunda Wajumbe wa Bodi kama ambavyo tulijadili kwa pamoja kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, tumeona ule Muundo wa Bodi na wakati mwingine tulikuwa tunafikiria au wanafikiria kumwondoa labda yule Rais wa *TLS,* lakini baada ya *debate* kubwa pamoja, tukakubaliana tumwache Rais wa *TLS* kwa sababu hakuna sababu za msingi za kumwondoa na kwa sababu bodi yenyewe inajumuisha wataalam wa sheria ambao pia wapo ambao wanatoka Serikalini, Wizarani pia na Msaidizi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wadau wengine kwa pamoja. Tunaamini kabisa kwamba, uwepo wake utaleta ufanisi katika kuhakikisha kwamba Shule ya Sheria inaimarika zaidi.

Mheshimiwa Spika, tumekubalina pia na baadhi ya vifungu hasa katika kitengo kile cha kuongeza *Dean of Students* kutoka katika *recognized high institution* au *college* ambayo inahusika na masuala ya kisheria. Maana yake hapo mwanzo walikuwa

wanamaanisha moja kwa moja *University of Dar es Salaam* na kwa sasa hivi kwa sababu nchi yetu pia Mheshimiwa Profesa na Spika wa Bunge, sasa hivi Tanzania tumekuwa na vyuo vingi sana ambavyo kimsingi na vyenyewe vinatoa masuala haya yanayohusu sheria.

Mheshimiwa Spika, zamani tulikuwa tuna chuo kimoja *University of Dar es Salaam,* lakini leo tunavyo vyuo kama *University of Dodoma,* tunacho chuo kule Mwanza na maeneo mbalimbali, zaidi ya vyuo kumi vikitoa elimu ya sheria. Kwa hiyo, kuna haja ya *Dean of Students* kutoka katika maeneo mbalimbali wakawa na usawa wa pamoja katika kupata uteuzi kushiriki katika muundo wa hii shule, kuwa Wajumbe wa Bodi katika Shule ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi binafsi napongeza Wizara kwa kuwa na utayari na kukubaliana na maoni ya Kamati kwamba, hawa Wajumbe wawepo. Pia, wale ambao wanatambuliwa kwa nafasi zao wawepo, pia kumpa nafasi Waziri kuteua baadhi ya Wajumbe kutoka katika taasisi nyingine ambazo hazihusiani na masuala ya sheria. Kwa hiyo, binafsi ninaipongeza Wizara na Kamati kwa kazi nzuri tuliyoifanya kwa muda wa wiki mbili tulizokuwepo hapa Bungeni kwa ajili ya kuchakata kupitia Kamati yetu ya Katiba, Utawala na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi nikupongeze kwa kunipatia nafasi ya kuingia kwenye hii Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. Naanza kuelewa vifungu mbalimbali kwa hivyo, masuala ya sheria hapo awali nilikuwa nimeshayasahau, lakini ameanza kunirudisha shule kwa kuanza kupitia kifungu kimoja baada ya kingine, nimeanza kuwa mbobezi kwenye masuala haya ya Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja na naunga mkono Muswada uliowasilishwa hapa na Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Kunambi na mtoa hoja ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nianze na shukrani. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais hasa katika mabadiliko mbalimbali anayoyafanya kwenye Taifa letu hasa yahusuyo sheria.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa *Professor* Kabudi kwa kupata dhamana hiyo tena ya kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Pia, nampongeza Mwanasheria wa Serikali mteule; siyo tu mteule, sasa ana-*practice* yuko hapa ndani. Nampongeza sana kaka yangu na kwa kweli nikimtazama ni kijana anaishiaishia lakini tunaamini kwamba ana *fresh mind in a changing world*. Kwa hiyo, Bunge letu litanufaika sana na uwepo wake hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najielekeza katika maeneo mawili; eneo la kwanza, ni eneo la marekebisho ya Kifungu cha pili ambacho chenyewe kinapendekezwa kurekebishwa ili kubaini watu wanaosimamiwa na sheria hiyo. Hapo awali ni kweli ilikuwa ni takwa la kisheria kwamba kijana au mtu yeyote aliyehitimu mafunzo ya sheria Shahada ya Kwanza, analazimika kupita Shule ya Sheria. Siyo wote wanapenda kuwa Mawakili, siyo wote wanapenda kuwa Mahakimu, siyo wote wanapenda kuwa Majaji na siyo wote wanapenda kuwa Mawakili wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi nchi yetu iko miongoni mwa nchi 56 katika *Commonwealth Countries*; miongoni mwa nchi ambazo zipo kwenye nchi za Jumuiya ya Madola, nchi 56. Nchi zote za Jumuiya ya Madola tunafuata sana mfumo wa sheria unaotumika kule Uingereza.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Uingereza wana makundi mawili kwenye sheria; wana *Barrister na Solicitor*. *Barrister* yeye kazi yake ni kwenda Mahakamani, anafanya kazi kama Wakili lakini *Solicitor* yeye anaweza kufanya kazi ya kuandaa tu nyaraka za kisheria lakini pia anaweza kuwa hata *Legal Officer*.

Mheshimiwa Spika, sasa, leo hii tunaona kitendo cha takwa la kisheria kwamba lazima mtu aliyehitimu Shahada ya Sheria apite

*Law School*. Kwa kweli kuna baadhi ya watu hawakutendewa haki. Mwingine anasoma sheria angependa kuwa *Legal Officer*. Sasa, si lazima sana, sasa naona mabadiliko haya yanakwenda kupanua wigo mkubwa katika tasnia hii ya sheria.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka ni-*complement* mchango wangu ni eneo la marekebisho ya Kifungu cha tano kinachopanua wigo wa majukumu na kuongeza jukumu la kutoa mafunzo maalum ya sheria. Eneo hili naomba niseme kidogo; tunavyoona sasa Shule ya Sheria inakwenda kutoa mafunzo maalum, nadhani pia itakuwa fursa ya Serikali hasa ukizingatia masuala ya Haki Jinai na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, juzi tunafahamu mwaka 2003 tuna Waraka Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.1 wa Mwaka 2023 uliotolewa tarehe 30 Oktoba, 2023, kuhusu matumizi ya madaraka ya ukamataji wa watuhumiwa. Nadhani semina ambazo zinatolewa kwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa hazitoshi. Sasa, hili eneo ambalo linaenda kutoa mafunzo maalum, Serikali nayo ingetumia fursa hii kupeleka Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya mara tu wanavyoteuliwa waende kwenye mafunzo maalum na siyo semina.

Mheshimiwa Spika, maana yake leo hii tunashuhudia mambo haya bado yanaendelea ya ukiukwaji wa Haki Jinai, mathalani jana jioni pale Jimboni kwangu Mlimba. Majira ya Saa 12 Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro akimuagiza Mheshimiwa *DC* wa Kilombero kwenye mkutano wa hadhara akamate wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa wamekamatwa wananchi 11 wakiwemo wananchi wanne, Mheshimiwa Diwani, Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kata na Mtendaji wa Kijiji; mpaka sasa wako ndani. Sasa, nadhani kuna kila sababu sasa Wakuu wa Mikoa wa namna hii na Wakuu wa Wilaya wa namna hii wapelekwe shule hii mara tu programu itakapoanza, waende wafundishwe.

Mheshimiwa Spika, siyo tu semina, wapewe mafunzo maalum ya namna gani ya kutafsiri sheria ili wajue mipaka yao ya majukumu. Mathalani, unaona Mkuu wa Wilaya anatembea na Kamati ya Ulinzi na Usalama. Ukimwangalia *DSO* ana kazi yake, *OCD* ana kazi yake. Sasa, jambo hili Mkuu wa Wilaya wa namna hii akipata elimu ambaye anapenda kutembea na Kamati ya Ulinzi na Usalama kila eneo itasaidia utawala bora na haki jinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itoshe tu kusema na kabla sijahitimisha, kesho asubuhi mara tu ya kipindi cha maswali na majibu, kwa sababu nikiona wale wananchi hawajatolewa na kwa sababu wamekamatwa bila *justification* yoyote, nitakuja hapa na Hoja ya Dharura Bungeni juu ya vitendo vinavyofanywa vya ukiukwaji wa haki jinai vya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Mkuu wa Wilaya ya Kilombero na baada ya hapo na tuseme tu kwa dhati. Vitendo vimekuwa vikiigharimu sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuna Kesi moja ya Madai Na.4 ya mwaka 2020 ambayo Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aliyekuwa anaitwa Onesmo Buswelu, alishtakiwa na alihukumiwa kwa kesi ya madai na Serikali ikaingia kulipa shilingi milioni 90 na yeye akalipa shilingi milioni 10 kwa sababu tu ya uzembe wa Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sasa, hili eneo linasaidia kwenda kutoa mafunzo mahususi kwa viongozi wa namna hii ili Serikali isiendelee kupata hasara. Hata hivyo, watu wangu wamekusudia majira ya kesho nao wanakusudia kuwashtaki viongozi hawa kwa Katibu Mkuu Kiongozi lakini pia watakwenda Mahakamani kufungua Shauri ya Jinai dhidi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Mkuu wa Wilaya ya Kilombero ili vitendo hivi vikome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nitaungana na wananchi wangu kuwatetea mpaka mwisho. Ahsante sana na Mungu akubariki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Kabudi (mtoa hoja) aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania Amendment Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge watatu wamechangia Muswada huu; Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Seif Said Khamis Gulamali wa Manonga na Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mbunge wa Mlimba.

Mheshimiwa Spika, maoni yaliyotolewa na wachangiaji wa Muswada huu ni muhimu sana katika kuendelea kuimarisha Shule ya Sheria Tanzania na Kamati imefanya kazi kubwa katika kuuboresha Muswada huu. Kuhusu kutamkwa kwa Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika, Jedwali la Marekebisho ya Serikali limefanya hivyo na ningependa kufafanua kwamba, toka mwanzo halikuwa lengo la Serikali kumwondoa. Tulisema anaweza kuwa Mjumbe yeyote wa *Governing Board* ya *Tanganyika Law Society*, tukiamini kwamba ukienda *by construction* Rais yumo kwenye *statutory interpretation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapotunga sheria wakati mwingine *clarity* ni muhimu. Kwa hiyo, ninataka niweke wazi kabisa, Rais wa *Tanganyika Law Society* hakuwa ameondolewa. *By construction* alikuwemo lakini tumeona tuliweke wazi na ndiyo maana *Schedule of Amendment* sasa tumemtaja. Kwa kufanya hivyo sasa tumeongeza; badala ya kuwa Mtiva au Amidi wa Kitivo cha Sheria au Shule ya Sheria, sasa wamekuwa wawili. Mmoja atatoka kwenye Kitivo au Shule ya Chuo cha Umma na mwingine ama kwenye Kitivo au Shule ya Chuo Kikuu Binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo naomba niliweke hivi, *Dean* au Amidi au Mtiva wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliwekwa siyo tu kwa sababu nyingine. Sibadili msimamo lakini napenda tuelewe; katika mila, desturi na kunga za vyuo vikuu duniani, vyuo vikongwe vinapewa hiyo heshima siyo kwa sababu

vingine siyo vyuo. Vyote ni vyuo lakini viko vyuo ambavyo kwa mila, desturi na kunga, kwa Kilatini vinaitwa *Primus Inter Pares (First Among Equals)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda mijadala mingine inapokihusisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo au sasa Shule Kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kifahamike kuwa chenyewe ni *Primus Inter Pares (First Among Equals)*. Kwa kufanya hivyo hakidhalilishi kabisa vyuo vingine. Ili kuondoa tashwishwi na ili kuondoa hofu tumeona tuweke hivi lakini nimelisema hili ili tujue mila na desturi. Kwa mujibu wa Bunge hili msimamo wa Serikali ni huo, sasa tutakuwa na wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni mengine tumeyachukua yale ya jumla na naamini yatatusaidia kwa kadri tunavyoweza. Ni kweli kabisa Shule ya Sheria Tanzania tayari inatoa mafunzo kwa *Paralegals* kwa mujibu wa Sheria ya Msaada wa Kisheria Sura ya 21 ya Sheria za Tanzania. Tayari Shule ya Sheria inatoa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye mambo ya usuluhishi *(Arbitration)* na tayari pia inatoa mafunzo kwa niaba ya *Tanganyika Law Society* kwenye mambo ya *CLE*.

Mheshimiwa Spika, wazo alilolitoa Mheshimiwa Kunambi la kuongeza wigo au la kuongeza uga wa ambao watahusika na chuo hicho, kuhusisha hao wengine ambao uliwataja nalo litafikiriwa kwa sababu chuo hiki lengo lake ni hilo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri. Tumepokea maoni mazuri ambayo yanalenga kuboresha, siyo tu Muswada huu hata masharti mengine ya Sheria Mama. Kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi kwamba, suala la marekebisho ya sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo linamhusu kila mmoja wetu katika Bunge hili na ni jambo endelevu. Ndiyo maana kila mwaka Serikali inakuja na Muswada wa aina hii ili kuboresha masharti ya sheria zetu na kuzifanya ziendane na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania Amendment Bill, 2024)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jedwali la Serikali inaonyesha kuna Kifungu kipya *immediately* baada ya Kifungu cha pili. Kifungu Kipya cha tatu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hii ndiyo ya hiyo *specialized training* siyo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Tumeiweka kule kwenye tafsiri, halafu pia iko hapa kwenye Kifungu cha tatu, tumeongeza hiyo (k) kwenye ule mlolongo wa *functions* za majukumu ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kule kwenye Kifungu cha pili tumetoa tafsiri nini maana ya *specialized* kama Kamati ilivyopendekeza na hapa kwenye (k) sasa tumeweka Kifungu chenyewe.

**MWENYEKITI:** Sawa; sasa, nataka kuelewa hizi *specialized trainings* zinazofanywa na *Law School* ili ziweze kutofautishwa na zinazofanywa na vyuo vingine, si lazima ziwe zina uhusiano na huko ku-*practice law*? Kwa sababu la sivyo vyuo vikuu vinavyofanya hizi *specialized courses* zitakuwa na utofauti gani yaani na *Law School*? La sivyo na chenyewe kitajigeuza kuwa kama vyuo vingine wakati chenyewe ni maalum kwa ajili ya *practice*. Ama?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *course* hizi ni zile ambazo kwa mfano sasa shule inatoa *course* ya *Paralegals* ambayo siyo Shahada lakini pia inatoa mafunzo haya ya *Arbitration* ambayo siyo shahada na hii ya *Paralegals* inasimamiwa na *NACTE*. Ndiyo maana kwenye bodi tumemwongeza mtu wa *NACTE*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawatatoa shahada lakini ni mafunzo maalum ambayo ni *tailor made bespoke* ukiondoa hiyo ya *Paralegal*. Kwa mfano sasa *CAG* alihoji kwamba mnatoa haya mafunzo lakini hamjayaonyesha. Wakili Mkuu wa Serikali ameomba *special course* kwa ajili ya *Arbitration* kwa watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizo ndiyo *specialized course* ambazo tumekuwa tukiziendesha na *CAG* aliona ni vyema hiyo *function* alishauri tuilete. Kwa hiyo, hawatatoa shahada zozote za *degree*, hapana. Ni *course* za muda mfupi ambazo zina malengo maalum na siyo shahada ya vyuo vikuu.

**MWENYEKITI:** Sikusudii kwamba ziwe shahada; swali langu ni kwamba, yaani tutazitofautishaje? Kwa mfano hii ya *Paralegal* ni kabisa, kwa sababu hawa si wana-*practice law*? Hata kama siyo watu ambao wana-*degree* lakini wana-*practice law*. Kwa hiyo, wakifundishwa na *Law School* na kwa sababu ile ni Shule ya Vitendo, inakuwa ni sawa kwa sababu wanachotenda ni sheria.

Sasa, kama tukiiweka hivi tulivyoweka; je, wakija kuanzisha kitu kingine ambacho siyo cha hawa ambao wana-*practice law*? Kwa maana hii iliyowekwa hapa, nataka tu kuelewa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa. Lengo lilikuwa linalenga hizi *course* ambazo tunazitoa kwa *Tanganyika Law Society*, kwenye *CLE* na *course* ambazo tunazitoa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, labda jinsi ya kukiweka ambazo zote zinaongeza ufanisi wa wao katika ku-*practice law* watu wa Tanganyika *Law Society*, Mawakili na wale wa Wakili Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, ndilo lilikuwa ambalo linafanya hivyo. Ndiyo maana kwenye *amendment* hiyo ili kuweza kuleta labda maana, tunaweza tukasema *Specialized Training means Practical Training*. Kule kwenye *definition* ili ku-*capture* hiyo ili kweli ilenge *practical*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kule kwenye *definition* tuseme *Specialised Training means Practical Training* ili ku-*capture* hiyo kwamba, hapa tunakwenda kwenye *Practical Training*. Ukiona inafaa tuweke hivyo ili liondoe huo uwazi ambao baadaye unaweza ukaleta maana nyingine. Tuongeze neno '*Practical*' ili li...

**MWENYEKITI:** Nafikiri iwekwe hivyo kwa sababu la sivyo *Law School* itaondoka kwenye lengo lake. Lengo lake kuu na lenyewe litaanza kutengeneza hiyo *tailor courses* halafu sasa tutajikuta kwamba imeacha ile *core function* yake.

Likiongezwa hilo neno Waheshimiwa Wabunge litatuondoa kwenye mazingira ya hiki chuo kujigeuza na chenyewe kinaweza kutoa kila *course*. Lazima iwe ina uhusiano na kile ambacho ndiyo shughuli yao mama. Kwa hiyo, nafikiri kama ulivyopendekeza kule kwenye *definition* iwekwe hiyo *Practical Training*.

Kifungu Kipya cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha tatu cha zamani kabla ya hicho kipya.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa tutawauliza hivyo hivyo halafu baadaye tutakuja kubadilisha namba kwa pamoja.

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5

**MWENYEKITI:** Hiki kifungu cha 5 anachohojiwa; samahani Waheshimiwa Wabunge, tuvumilie kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunapata mkanganyiko kidogo hapa kwenye hizi *schedules* za *amendments* zilizoletwa. Sasa hivi tupo kwenye kifungu cha 5 cha huu Muswada. Hiki kifungu cha 5 ukisoma kinasema, "*The Principal Act is amended in section 9A in subsection (1) by deleting*

*(d) and substituting it with one member representing faculties*. Hiki si ndicho ambacho sasa hivi huku mbele kimekuja kurekebishwa, lakini hapa hakijarekebishwa.

Huku mbele kwenye kifungu cha 7 kinasema *two Dean of the Faculties of Law or Schools of Law*, sasa kabla hakijarekebishwa cha 7, si inabidi kirekebishwe hicho cha 5? Maana cha 5 kikipitishwa na hii ya mmoja halafu huku wawili tutawawekaje? Hebu nisaidieni kama mimi ndiye niliyechanganya hapa mbele ama imesahaulika kubadilishwa hii ya tano.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona...

**MWENYEKITI:** Hii ya tano hapa kwenye (a), (i), (d) inasema *one member*, sasa huku mbele tutakujaje kurekebisha kwenye cha 7.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hiyo ...

**MWENYEKITI:** Ama imesahaulika.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tulichanganya namba kwa sababu ya kuandika. Hiyo ya *one member* ilikuwa inahamia kwenye kifungu cha 9 cha sasa, anarudi tena *clause 7*. Hayo ya *one member* yalikuwa yanaingia kwenye *clause 7* ya Muswada wa awali. Sasa kwenye *clause 7* ya Muswada wa mapendekezo ndiko tunakofanya mabadiliko haya yanayoleta *one member*. Kwenye cha 5 inarudi kwenye zile *functions* za *school* na cha 6 ina-*deal* na kitu kingine, kwa hiyo nadhani tu ...

**MWENYEKITI:** Ngoja niitazame vizuri hapa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *clause 5* ina-*amend section 11*.

**MWENYEKITI:** Ile *Principal Act* unayo hapo Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ninayo.

**MWENYEKITI:** Hebu twende kwenye *section* 9.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *section* 9 ndiyo ina-*deal* na ....

**MWENYEKITI:** *Examination Committee*.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Examination Committee*, ambapo hapa tunapendekeza kwamba pawe na *one member representing Faculties of Law or Schools of Law from recognize higher education institutions* na ndiyo tunapendekeza kwenye hiyo na 9*(1)*. Halafu 9*(2)* tunapendekeza sasa kumuwndoa *Principal* na kumweka *Deputy Principal* kwenye kuwa *secretary* wa hiyo *committee*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kwenye hii 9 mnapunguza idadi ya hawa wanaotoka kwenye *faculties*?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ndiyo badala ya *two* anakuwa *one*.

**MWENYEKITI:** Anakuwa *one*?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Aaa, sawa. Halafu ndiyo mnamwongeza huyu wa *vocational training*.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ndiyo, ndiyo tunamwongeza huyu hapa.

**MWENYEKITI:** Ana-*replace* huyo mmoja, wengine wanaendelea.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwongeza *one member* kutoka *NACTE*. Kwa hiyo walikuwa wawili sasa leo wapo, *one representing private university* tumemwondoa, tumewa-*merge* wote wawili, halafu tumemwongeza sasa *one member from institution for recognition of technical and vocational training, accredited training*. Kwa hiyo hawa ndiyo wajumbe sasa.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa swali langu; huyu ameletwa kwa ajili ya ile *specialized course* ambayo ipo kwa ajili ya *paralegals*, si ndiyo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, kwa ajili ya *paralegals*.

**MWENYEKITI:** Sasa hizi *specialized courses* si zitakuwa nyingi nyingi pale? Yaani kwa sababu hawa ni *examination* ya *the entire Law School*, ambayo *principal objective* ya kuanzishwa kwake ni ku-*train lawyers* wanaokwenda kwenye *practice*, huyu wa *NACTIVET* anakuja kwa ajili ya *in specialized course* ya hawa *paralegals*.

Najaribu kuwaza tija ya huyu wa *NACTIVET* anayekuja kwa ajili tu ya hii *specialized course* ya hawa *paralegals,* lakini hii ni bodi ambayo inashughulika na lile jambo kubwa zaidi ya hii shule ambayo kwa kweli ni ku-*train* hawa *lawyers*, anapunguzwa *dean* kwa ajili ya *NACTIVET* ambao ni *specialized course* na ni ya muda?

Kamati, maana nisimshikilie bango tu Mheshimiwa hapa, Kamati huyu *NACTIVET* anaingia kwa ajili ya *specialized course* moja na wakija wale wengine wa *arbitration* na wenyewe tunaongeza *member* humu?

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ambayo sisi tulitaka Serikali itoe ilikuwa ni kwamba ni

kuwa *specific* na kutoa ufafanuzi kwamba hiyo *specialized training* itakuwa inahusu nini na kwa hiyo mfano waliotoa na walisema watarekebisha kwenye kifungu cha 11 katika kuongeza kifungu kidogo cha (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo haya marekebisho waliyowasilisha ndiyo waliona kwamba ndiyo wanayotaka kufanya katika eneo la *specialized training*.

**MWENYEKITI:** Jamani Mheshimiwa Waziri mimi ni mwalimu wangu kama ambavyo mimi ni mwalimu wa watu kadhaa humu ndani. Hata hivyo mimi nafikiri bado wale *Deans* wawili; tutakuja bado kwenye hoja ya wawe nani; lakini wale *Deans* wawili ukiangalia *primary role* ya *Law School* huwezi kum-*replace Dean* na mtu wa *NACTIVET* ambaye anakuja kwa ajili ya *specialized course* kwa ajili ya hawa *paralegals*.

Kama ni lazima wakati wa ku-*handle* mtihani wa hawa *paralegals* huyu awe *invitee,* tunaweza kuweka hapa *provision* ambayo hii *committee*, kwa sababu ni *committee* ya mitihani, kule kwenye bodi ni suala lingine lakini hii ni *committee* ya mitihani. Huyu wa *NACTIVET* kwa nini asiwe *invited* wanaposhughulika na mitihani inayowahusu, kwa sababu mengine hayamhusu. Ili wale *Deans* wabaki kwa sababu hii inahusu *practical legal training examinations* za hawa *lawyers* ambao huyu *NACTIVET* anakuja kwa ajili ya jambo moja tu linalomuhusu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja tunaipata kabisa ya umuhimu wa hawa *Deans* wawili au hawa wawakilishi wa *Public* na *Private Universities*. Sasa wewe ndiye mwalimu wangu wa kanuni, ninaona umuhimu na naona umuhimu pia wa hata huyu bado kubaki mtu wa *NACTE*, sasa kama tunaruhusiwa tukawaweka hawa wawili *plus* yeye, kwa sababu hii *committee* haina mpaka wa namba; na atakachosaidia, kwa sababu wenzetu wa *NACTE* wana-*deal* na, wao ni *competency based* na *Law School* ni *competency based,* kwa hiyo anaweza

bado akatajirisha mijadala ya mle, lakini nakubali kabisa hoja yako tukawa na hawa wawili *plus* yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui katika ngazi hii kikanuni ikiruhusiwa sisi tunakubali, tunaafiki upande wa Serikali kuwa na mwakilishi mmoja wa *Public Universities*, mwakilishi mmoja wa *Private Universities* na huyu mjumbe mmoja kutoka *NACTE*. Hili kweli *Deans* wawepo katika bodi hii muhimu sana ya mitihani, hii ni bodi muhimu sana ya mitihani na ni vizuri wote wakawakilishwa, sisi turadhi kuwaweka wote, kwa sababu tupo kwenye ngazi ya kutunga sheria na hili ni wazo zuri.

**MWENYEKITI:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge, haya marekebisho yanayopendekezwa hapa, kwa sababu hii inahusu mitihani na ukizungumzia mitihani nadhani wote tunaelewa hapa tumeshapata kuwa wanafunzi. Kwa hiyo wale *Deans* wawili wabaki kwa kweli, wabaki na alikuwa anauliza Mheshimiwa hapa mimi ndiye mwalimu wa kanuni kwa kweli, mwalimu wa kanuni. Hizo kanuni kwa sababu zimenipa mimi mamlaka siyo Mbunge mwingine, kwa hiyo haina changamoto, hii kule tumeongeza lile neno *practise*, hapa hawa *Dean* wawili wabaki aongezwe huyo mtu wa *NACTIVET* kwa sababu yeye anakuja kushughulika na jambo moja tu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hapa kabla hatujavuka kwanza, hiyo ilikuwa ngazi ya kwanza. Ngazi ya pili, hii (d) hii bado, yenye *two members representing faculties of Law over credited universities in Tanzania* kama ambavyo imerekebishwa hapa sasa hivi. Ni *faculties of Law or Schools of Law, whatever the name*. *Issue* ya, waheshimiwa wajumbe hapa Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja wakati wa Bunge siyo kwenye Kamati, ameeleza kuhusu mabadiliko ambayo wabunge baadhi yenu hapa mmeyapongeza ya kuondoa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenye hii Shule Kuu ya Sheria, kwamba sasa hivi vyuo vipo vingi.

Huyu mmoja kutokea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, huyu mwingine ndiye atokee penginepo, kwa nini? Si kwa sababu mimi nimetoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni kama hoja zingine tu

ninazozileta hapa. Jamani dunia nzima sisi ndio tutakuwa wa kwanza. Sisi ndio tutakuwa wa kwanza kusema kwamba hatutambui tofauti za vyuo, hakuna huo utaratibu na ndiyo maana kila mwaka unakwenda unarudi Afrika nzima huwa wanaorodhesha, cha kwanza ni kipi, kipi kimekuwa huko. *(Makofi)*

Hata hapa nchini si huwa vinaorodheshwa, si lazima kinachotajwa kiwe chuo kila siku, lakini lazima ule utambuzi uko dunia nzima, wala si hoja ya usawa, yaani kwenye hoja ya namna hii huwa hakuna usawa. Tunataka hapa kutengeneza hoja kwamba tumetengeneza usawa wa kila mtu yupo sawa, hakuna usawa wa sura hiyo. Sasa tukisema kwamba kwa kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pengine kinawatazama wengine vipi, hakuna kumtazama, ni sawa tu na mtu aliyesoma *Havard,* si lazima atasema amesoma *Havard*? Kwa nini anajitaja kila saa *Havard,* yaani hata kama hutaki kasoma *Havard*, hata kama wewe unaona mnalingana akili zenu, lakini yeye ndiyo kasoma *Havard* wewe hukusoma. *(Makofi)*

Sasa lazima tuweke hayo mazingira, yaani tusijitoe sisi kwamba jamani sisi, hapana. Ni kweli vyuo vipo vingi lakini pamoja na wingi huo nafasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam bado ipo pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa umesimama, sasa hapa unajua nipo kwenye kutumia *veto* kwa sababu hamna marekebisho yaliyoletwa hapa, sasa sijajua kama unataka kushirikiana na mimi kwenye kutumia *veto* ama unataka kufanyaje? Nakupa nafasi halafu tunasonga kwenye hili. *(Kicheko)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nataka kusema tu kwamba, kwa sababu tunaandika sheria na tumeshaandika vizuri sana na kwa sababu yule anaye-*appoint actually* ni Waziri; hatafungwa akifanya hivyo lakini kwenye kuandika tumeandika vizuri sana.

**MWENYEKITI:** Uzuri wake hoja ilikuwa ni ya Kiti, kwa hiyo hoja ya Kiti kidogo itapata changamoto. Inaweza kuja kufanywa huko

baadaye kwa sababu nyingine, lakini kwa ngazi hii, kama nilivyosema leo siyo siku ya kutoa mafunzo kuhusu jambo hili, lakini huko duniani mlikonituma pia mlishanituma huko zamani na kodi zenu na nini tushazunguka sana huko. Kwa hiyo dunia ndivyo inavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, nimesema leo siyo siku ya kutoa mafunzo tutatoa siku nyingine. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri kwenye hili kwa kweli halitakaa sawa, kufikiri kwamba kwa kutunga sheria ya namna hii ndiyo tunafanya sawa hapana kwa sababu na sisi tunajifunza kwa wenzetu na tunaona kwa wenzetu pia. Haitaonekana vizuri tukitunga sheria kama vile tupo kwenye *vacuum*. Kwa hiyo nafikiri maelezo ya Waziri yakiungana na haya, imeeleweka Waheshimiwa Wabunge? Kwa hiyo wajumbe bado watakuwa wawili, mmoja atatoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na huyo mwingine atakapotoka popote ataungana. Si tumeelewana? *(Makofi)*

Wengine mnapiga makofi, wengine hampigi, lakini huo ndio uhalisia, si mmetutuma duniani jamani kujifunza, ndiyo haya haya tunajifunza au ni pamoja na haya. Ahsante sana.

Sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali umekaa na Mheshimiwa Waziri hapo, tusaidiane. Hapa kwa sababu tumeshakubaliana kwamba hawa wajumbe wanabaki na kwa sababu uandishi wa yale maneno madogo madogo ile *Laws Revision Act* inampa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama kuna mahali neno litakuwa limepungua; lakini hapa yarejeshwe yale maneno yaliyokuwa yanasomeka mjumbe kutoka, sijui ataitwa *dean* au chochote, mimi sijui. Huku nimeona mtiva na amidi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyokumbuka niliporudi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuombwa kuwa Katibu wa Baraza la Chuo nilipeleka pendekezo kwenye Baraza la Chuo, kwamba kila mtu ni mkuu, mkuu. Mkuu wa Idara, Mkuu wa Kitivo, Mkuu wa Shule. Kwa hiyo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ndio ukongwe huo, tukawaomba watu wa BAKITA

(Baraza la Kiswahili Tanzania), Baraza la Kiswahili Zanzibar na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu, kuja na maneno mapya. Kwa hiyo istilahi mpya ni kama ifuatavyo; *Dean of Faculty*, *faculty* ni kitivo na kitivo ni neno tumelitoa kwa lugha ya kisambaa, Kikamba na Kipare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukasema Mkuu wa Kitivo anaitwa Mtiva, lakini Mkuu wa Shule anaitwa Amidi na Mkuu wa Idara anaitwa Mudiri na *Principal* wa *College* anaitwa Rasi na *college* inaitwa Ndaki.

**MWENYEKITI:** Sawa, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumeelewana vizuri, hiki kifungu cha 5 cha kwenye ibara kinachorekebisha kifungu cha 9, hapa ambapo panasomeka *one member representing faculties of law*, itasomeka; *Dean of University of Dar es Salaam*, halafu na mwingine ili wawili wote wawepo hapa, halafu ndiyo anafuata huyo wa *NACTIVET*, imeeleweka?

Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 5 kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu Kipya cha 6

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 6 kilichopendekezwa na Serikali. Waheshimiwa Wabunge, kifungu kipya kinahusu mabadiliko kwenye kifungu cha 11 cha ile sheria mama na kinazungumzia sifa za wale wanafunzi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7

**MWENYEKITI:** Kamati nadhani marekebisho yenu ndiyo aliyachukua Mheshimiwa Waziri? Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hilo kulikuwa na marekebisho ya mapendekezo ya Kamati, lakini kwa maboresho ambayo tunaona Serikali imekuja nayo maana yake wametanua wigo wa uwakili, kwa hiyo tunaungana nayo kama walivyorekebisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hiki si ndicho kinachohusu *membership* ya bodi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maelekezo siyo maelekezo, yale maamuzi tuliyoyafanya ya kutaja *University of Dar es Salaam Schools of Law* hapa ndipo mahali pake pia.

**MWENYEKITI:** Sasa hapa kwa sababu, ulikuwa umeshaweka *to Dean of Faculties of Laws or Schools of*. Kwa hiyo, inakuwa moja, *University of Dar es Salaam* anaongezeka na huyo mwingine.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa.

**MWENYEKITI:** Sasa kulikuwa na ile hoja ya *President* of *Tanganyika Law Society* ametajwa moja kwa moja halafu…

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongeza *member* mmoja ambaye yeye hana *Degree* ya Sheria, lakini anaweza kuwa na *Degree* katika mambo ya *Finance, Planning, Human Resources* au *Administration,* huyo naye ni mpya tumemuongeza.

**MWENYEKITI:** Hii kwenye Muswada inasomeka *Deputy Attorney General* si ndio?

*Registrar of the Court of Appeal Director responsible for legal services from the Ministry Responsible for legal affairs, Dean of,* hii ndio umeleta wawili. Kwa hiyo, hapa ndio wanaingia wale wawili, *one member from the Governing Council of Tanganyika Law Society* hapa ndio anaitwa *President,* si ndio? Kwenye marekebisho mbona ilikuwa inasomeka (*d)* wakati (*d)* huku inahusu *Dean?* Unayo yale marekebisho yako Mheshimiwa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo. Baada ya ile (*c)* ya *Director responsible for legal services from the Ministry responsible for legal affair (d)* sasa ndio inamwingiza huyu *President of Tanganyika Law Society* na yule *one member* wa *governing council* bado tena anabaki. Kwa hiyo, *TLS* inakuwa na *President,* lakini pia, itakuwa na *one member* kutoka kwenye *Governing Council*. Kwa hiyo, *TLS* watakuwa na Wajumbe wawili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Na huyu wa *Public Bar Association* anaondoka au anakuwepo kwenye *(g)* kwenye Muswada?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *Public Bar Association* ya ma-*State Attorney. Yeah,* huyo sasa naye anabaki.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, anabaki anakuwepo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio anaingia.

**MWENYEKITI:** Sasa kama huku huyu anaitwa *one member representing the Public Bar Association* hawa hawana kiongozi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wana *President.*

**MWENYEKITI:** Na wenyewe wana *President?*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio wana *President*.

**MWENYEKITI:** Sasa, kama kwa sababu wao siyo sawa na *Law Society,* lakini kama na wao wana kiongozi kachaguliwa, si ndio aje huyohuyo, ama? Kwa sababu, lazima twende.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo ni sahihi. *Yes,* maadamu tumebadilisha kule kwa *Tanganyika Law Society* hivyohivyo kimantiki na hapa.

**MWENYEKITI:** Utungaji wa Sheria huwa unaenda ni mserereko ama inaitwaje?

Sawa, sasa turudi hapa kwenye (*e) one member,* baada ya kumtaja tayari Rais wa *TLS* hapa kwenye *one member from the Governing Council of Tanganyika Law Society* kwa sababu, Rais yule wa *TLS* ndio Mwenyekiti wa ile *Governing Council.* Huyu *member* ni lazima atoke kwenye *Governing Council?* Hebu Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa marekebisho yaliyoletwa na kamati sisi tumesema akiwepo *President* pale awepo, ni muwakilishi tu anayetokana na *Tanganyika Law Society.* Kwa hiyo, siyo tena *member of the Governing Council* kwa sababu, hii ndio ilikuwa *original position.*

**MWENYEKITI:** Najaribu kuwaza hivi kwa sababu, yule *President* yeye tayari ni *member* wa *Governing Council by virtual of his position,* lakini pia, ndio Mwenyekiti. Sasa huyu akisema *one member from the, one member from* wao wanaweza kwa sababu, anaye *appoint* ni Waziri anaweza akatoka mle kwenye *governing,* lakini pia, anaweza kutoka nje kulingana na mambo yanavyokuwa, si mambo samahani pengine watu.

Kwa mfano, sasa hivi Rais wa *TLS* pengine ni mwanaume na anatafutwa wanamke, pengine sijui, mwenye sifa tofauti na Rais na

kule kwenye *Governing Council* akawa haonekani. Kwa nini, asiweze kutafutwa nje ya *Governing Council?*

Kwa sababu, tayari Rais anatoka *Governing Council* na yeye ndio Mwenyekiti, ili kutoa huo mwanya maadamu Wajumbe wawili wanatokea *TLS?* Ama mimi ndio peke yangu, jamani na mimi ni Wakili, maana watu wanaweza… *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaafiki kabisa, hiyo ni sahihi kwamba, tuondoe ile *the Governing Council* iwe *to one member from Tanganyika Law Society.*

**MWENYEKITI:** Eeh, kwa sababu, tayari Rais anakuwa ametajwa na yeye anatoka kwenye *Council.* Kwa hiyo, hapa walikuwa wameleta, Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria katika marekebisho yake ya mwanzoni waliitaja hii ya *President* ambayo tayari Serikali imeleta, lakini walileta pia, hii ya ku-*substitute* hii ya *one member from the governing of the Tanganyika Law Society* na kuleta iwe *one member representing Tanganyika Law Society*. Kwa sababu, hii nyingine *President* wa *Tanganyika Law Society* anaingia *by virtual of his position,* lakini huyu mwingine anakuja, kwa ajili ya maslahi ya *Tanganyika Law Society*. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wajumbe, hii ndio mmeongezea iwe *three years' experience?* Kwa sababu, ilikuwepo tangu mwanzo, Mheshimiwa Waziri? Hii *7(1)(i) one member who possesses at least,* kwa hiyo, marekebisho ni kwenye *experience?*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti*, yes.* Ndio.

**MWENYEKITI:** Sawa. Waheshimiwa Wajumbe, Kifungu cha saba pamoja na marekebisho ya Serikali na marekebisho yaliyoingizwa baadaye baada ya marekebisho ya Serikali na marekebisho ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa ajili ya kuongeza yule *member* wa kubadilisha badala ya kuwa

*member* wa *Council* kuwa, *member* wa *Tanganyika Law Society* yanaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutakuwa na *renumbering* baada ya kupisha vifungu hivyo kutoka Kifungu cha 3 hadi kifungu cha 8. Sasa vitakuwa kifungu cha 4 hadi 10.

**MWENYEKITI:** Marekebisho ya namba kwenye hivi Vifungu yanafikiwa?

*(Marekebisho ya Namba ya vifungu vilivyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa hoja, Taarifa.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria ya Tanzania wa Mwaka 2024, *The Law School of Tanzania Amendment Bill 2024,* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024, *The Law School of Tanzania Amendment Bill 2024,* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Sasa baada ya kufanya hilo Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji, kama ilivyo ada kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania Amendment Bill 2024)*. Wote mmeafiki. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho ya Sheria katika Sheria ya Shule ya Sheria ya Tanzania kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamebainika wakati wa utekelezaji wa masharti ya Sheria hiyo *(A Bill for an Act to Amend The Law School of Tanzania Act in order to address various challenges observed in its implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 (The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024] Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa Mara ya Tatu na kwa utaratibu wetu, maana yake ni sisi tumeshamaliza kazi yetu ya kutunga Sheria hii ambayo ni ya Marekebisho na kwa sababu, kama ilivyoelezwa kwamba, kulikuwa na changamoto ya utekelezaji wa Sheria ambayo tuliitunga hapo awali, basi tumefanya hayo marekebisho ili utekelezaji uwe na tija zaidi.

Sasa baada ya hatua hii ya Kusomwa Mara ya Tatu tutampelekea Mheshimiwa Rais ili na yeye aweze kufanya kwa sehemu yake kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na akishafanya hivyo, Waheshimiwa Wabunge, basi tutaweza kuwapa taarifa kama ilivyo ada. Kwa hivyo, nitangaze rasmi kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania (Amendment) Bill, 2024),* umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na

kwa kweli na Watendaji wote wa Shule Kuu ya Sheria. Shule ya Sheria tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa Sheria hii.

Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana kwa ushiriki wenu na Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya ya kuishauri Serikali mpaka imekuja na marekebisho hayo mbalimbali ambayo yanaufanya Muswada wetu huu uwe na tija zaidi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri, Makamu Mwenyekiti, Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa ushirikiano wako wewe pamoja na mtangulizi wako, ambaye ndio Muswada huu ulianzia kwake, lakini tunakushukuru kwa ushirikiano uliotoa kwa Kamati kwa kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.33 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 28 Agosti, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*